

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 16 Mei, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatoo Asubuhi)*

#### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Tano, leo ni Kikao cha Ishirini na Tisa tangu tumeanza. Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:**

#### TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina taarifa mbili muhimu, taarifa ya kwanza, ningependa leo kuwajulisheni kuhusu hatua iliyofikiwa katika ukaguzi wa hesabu za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, wengi tumezoea kuiita Ofisi ya CAG kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa kifungu cha 46(1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma, Sheria Namba 11 ya mwaka 2008, Hesabu za CAG yaani za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi zinapaswa kukaguliwa angalau mara moja kwa mwaka na kwamba Bunge kuititia Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) huwa lina jukumu la kuteua Mkaguzi wa kukagua hesabu za ofisi hiyo. Kwa maneno rahisi, Bunge ndiyo tunatafuta Mkaguzi wa Nje ambaye ndiye anakagua hesabu za Ofisi ya CAG.

Kwa hiyo, kazi hiyo ilishafanyika huko nyuma na Kampuni ya Mkaguzi inayoitwa *EK-Mangesho and Company* ilikwishakupatikana na imefanya kazi hiyo ya ukaguzi na imetuletea taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za ofisi hiyo.

Nimeona niwajulisheni ili muweze kufahamu katika hesabu zilizowekwa mezani wakati ule hesabu za Ofisi ya CAG mwenyewe huwa haziwekwi mezani pale, utaratibu wake ni huu ninaoueleza ambao kuna kuwa na *External Auditor* anakagua, nawataarifu sasa Bungeni kwamba nimeshapokea taarifa hiyo na nimeshaipitia, kuna mambo, lakini utaratibu ni kwamba tunapeleka kwenye Kamati ya PAC sasa.

Kwa hiyo, kwa kuzingatia Sheria ya Ukaguzi hiyo, naipeleka taarifa hii kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ili walipitie na kuichambua na mara watakapomaliza kazi hiyo ya uchambuzi watawasilisha uchambuzi huo kwangu na mengine yatakayofuata yatakuwa wakati huo utakapokuwa umewadia, ni kuwataarifuni tu kwamba katika masuala ya ukaguzi, hakuna ambaye anabaki, na hakuna anayejikagua mwenyewe, ila watu wanaangalia wenzao.

Waheshimiwa Wabunge la pili, tunao Wawakilishi wetu katika Mabunge mbalimbali ambao baadhi yao tumewachagua ndani ya Bunge. Tuna wawakilishi ambao tunawapeleka katika Bunge la SADC, SADC PF, Wabunge wenzetu wako hapa, kuna Wawakilishi tunawapeleka kwenye Bunge la PAP (*Pan African Parliament*), Bunge la Afrika. Tuna Wawakilishi huwa tunawapeleka kwenye ACP EU (*African Caribbean Pacific*) na EU, na pia kuna Wawakilishi tunawapeleka kwenye Bunge linaitwa Great Lakes (IGLSA)Bunge la Maziwa Makuu.

Wawakilishi hawa, tunawachagua watuwakilishe katika Mabunge hayo na wamekuwa wakifanya kazi nzuri, lakini katika uwakilishi wa Bunge la Afrika, kumejitokeza matatizo makubwa, hasa kwa Mheshimiwa Stephen Masele.

Kuna matatizo makubwa sana ya kinidhamu, ambayo nisingependa kuyafafanua leo muda hautoshi, lakini tumelazimika kumtafuta Mheshimiwa Masele kumrudisha nyumbani, kuanzia Jumatatu, badala yake amekuwa akionesha kugoma na hata jana kwenye Bunge hilo, *clips* zinaonesha zimerushwa, baada ya kumwandikia kwamba arudi nyumbani ili aje ahudhurie kwenye Kamati ya Maadili hapa, amekuwa akilihutubia lile Bunge akisema japo ameitwa na Spika lakini ameambiwa na Waziri Mkuu a-disregard wito wa Spika, aendelee tu na mambo yake kule, kitu ambacho ni uongo na kutudhalilisha kama nchi, ni kiongozi ambaye amekuwa akifanya mambo ya hivyo hovyo, na ndio maana tumemuita kidogo kwenye Kamati ya Maadili, atufafanulie, huenda labda yuko sahihi, lakini kwa mtazamo wetu amekuwa akifanya mambo ambayo ni hatari kubwa ikiwemo kugonganisha mihimili, anapeleka kwenye Mhimili wa Serikali juu kabisa, maneno mengi ya uongo na ushahidi upo na kulidhalilisha Bunge, ni kiongozi amejisahau, hajui hata anatafuta kitu gani. Ukiacha hizo vurugu ambazo hivi sasa zinazoendelea kwenye Bunge lake huko, ambazo anaziongoza ye ye mwenyewe ni vurugu kubwa, hilo halituhusu sana, sisi tunamuita kwa ajili ya mambo ya hapa nyumbani ya utovu wa nidhamu.

Sasa kwa kuwa tumekuwa tukimuita tangu jumatatu, hataki kurudi, ningependa kulifahamisha Bunge hili kwamba kwa niaba yenu na kwa mamlaka niliyonayo basi, nimemwandikia barua Rais wa PAP ya kusitisha uwakilishi tuliompatia Mheshimiwa Masele katika Bunge la PAP hadi hapo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itakapokamilisha uchunguzi wa tuhuma dhidi yake na kukamilisha taarifa yake.

Kwa hiyo, kwa muda (*temporarily suspension*) ya Mheshimiwa Masele kuwa Mbunge wa Bunge la Afrika hadi hapo tutakapomalizana naye hapa na hapa kuna Kamati mbili zinamsubiri, Kamati Maalum hii ya Bunge ya Maadili, lakini pia Kamati ya Maadili ya Chama chake nayo kuna mambo inamuhitajia, kuja kuyajibu hapa nyumbani.

Kwa hiyo, kuanzia sasa yeye siyo Mbunge wa Bunge hilo tena, hadi tumalize masuala ya hapa nyumbani, ndiyo tutaamua wenyewe, mambo haya huwa tunaamua wenyewe, tunaendeleaje kuanzia hapo.

Katibu!

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KWASILISHA MEZANI**

**SPIKA:** Hati za Kuwasilisha Mezani, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Ooh! Samahani, tuna Waziri wa Kilimo kwanza, samahani sana, Waziri wa Kilimo, ulikaa mbali bwana, Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Bashungwa tafadhali, Innocent.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, naomba nikuite uweke mezani hati zako.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi, tunakushukuru.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, tafadhali. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa.

**MHE. BONNAH M. KALUWA - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa bajeti, majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mbunge wa Segerea. Sasa naomba nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzania Bungeni hukusu Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Mheshimiwa Joseph Selasini, tafadhal!

**MHE. JOSEPH R. SELASINI - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KUHUSU WIZARA YA ULIZNI NA JESHI LA KUJENGTAIFA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Wizara ya Ulizni na Jeshi la Kujenga Taifa juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Selasini. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI-KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, swali la kwanza linaelekea Ofisi ya Mheshimiwa Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Sabreena Gabriel Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kwa niaba yake Mheshimiwa Susan.

Na. 239

### **Hitaji la Mashine ya Utra Sound Kituo cha Afya Ujiji**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA (K.n.y MHE. SABREENA H. SUNGURA) aliuliza:-**

Kituo cha Afya Ujiji kinahudumia zaidi ya wakazi 20,000 lakini kituo hicho hakina mashine ya *ultrasound*.

Je, ni lini Serikali itapeleka mashine ya *ultrasound* katika kituo hicho?

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa, majibu ya swali hilo, vituo vya afya vinatakiwa viwe na *ultrasound*? Karibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) Alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI), naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/19, Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji imeidhinisha kiasi cha Shilingi 15,475,254.28 kupitia Mradi wa Malipo kwa Ufanisi (*Result Based Financing*) kwa ajili ya ukarabati wa chumba kitakachotumika kwa huduma za mionzi na shilingi 45,000,000.00 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa *ultrasound*. Fedha hizo zimepelekwa MSD kwa ajili ya taratibu za ununuzi wa kifaa hicho. Kwa sasa huduma ya *Ultrasound* inapatikana katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Maweni na Hospitali Teule ya Manispaa ya Baptist.

**SPIKA:** Mheshimiwa Susan, swalii la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nipate kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa suala la *ultrasound* katika vituo vya afya au Hospitali za Wilaya na Halmashauri, ni suala kubwa sana na halipatikani maeneo mengi nchini Tanzania na hii inaathiri kina mama na wanaokwenda katika Hospitali hizo kuangalia hali zao za kiafya hasa katika suala la tumbo.

Je, ni lini sasa Serikali itaweka mkakati kupeleka *ultrasound* kwenye vituo vyote vya afya nchini Tanzania na Hospitali za Wilaya ili wanawake wapate huduma hizo katika hospitali nchini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mlimba, Kituo cha Afya cha Mlimba kina *ultrasound* na mfuko wa Jimbo nilichukua nafasi mimi kumpeleka kwa kuomba na *DMO* kwenda kumsomesha mtaalam ambaye amesharudi na huduma hii inapatikana Kituo cha Afya cha Mlimba, lakini kuna Kituo cha Afya cha Mchombe, hakina *ultrasound*.

Je, nini kauli ya Serikali kupeleka *ultrasound* katika Kituo cha Afya cha Mchombe, ndani ya Jimbo la Mlimba? (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na Serikali inatambua umuhimu wa uwepo wa kifaa cha *ultrasound* na ndiyo maana katika vituo vyote vya afya ambavyo tunavijenga, tayari fedha tulishapeleka *MSD* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kituo cha afya vinavyokamilika vinakuwa na vifaa ikiwa pamoja na *ultrasound*.

Mheshimiwa Spika, na kwa mfano, katika swali la msingi la Kituo cha Afya cha Ujiji, tayari fedha imepelekwa na fedha hiyo imepelekwa tarehe 29 Aprili uliopita na baada ya wiki tatu, katikati ya mwezi Juni, tayari *ultrasound* itakuwa imefika.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swalii lake la pili, hicho kituo cha afya ambacho anakisema cha Mchome, naamini ni miiongoni mwa vituo vyatya afya ambavyo tayari tumeshapeleka fedha *MSD*, kwa hiyo, tukishamaliza kipindi cha maswali na majibu, ni vizuri tukakutana na Mheshimiwa Mbunge ili tutazame wao lini wanatarajia kupata *ultrasound*.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea, niwataarifu tu kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu yuko katika kazi maalum Dar es Salaam na kwa maana hiyo, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe yuko pale kama kiaongozi wa shuguli za Serikali humu Bungeni. (*Makofii*)

Kwa hiyo, wale wenye mambo ya kiserikali, mnaweza mkamuona pale ili kuweza kupata ushirikiano, lakini pia nimuombe radhi Mheshimiwa Bonnah, nilimtamka kama Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, nimearifiwa kwamba kuna mabadiliko. Sasa anaitwa Mheshimiwa Bonnah Kamoli. (*Makofii*)

Mheshimiwa Bonnah tuwekee *spellings* vizuri tu, ni Kamori, Kamoli au? Tuwekee vizuri.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naitwa Bonnah Kamoli.

**SPIKA:** Ni "L"? Kamoli!

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** "L" Kamoli *yah*.

**SPIKA:** Ahsante sana. Bonnah Kamoli, tafadhalini, baada ya hapo, nimekuona Mheshimiwa Grace Kiwelu swalii la nyongeza.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi, Kituo cha Afya cha Pasua kilichopo Manispaa ya Moshi nacho kina tatizo la *ultrasound*, lakini pamoja na *mortuary*. Je, ni lini Serikali itapeleka *ultrasound* na kujenga hicho chumba cha kuhifadhindugu zetu waliotangulia mbele ya haki? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu la swali hilo kwa vituo vya afya nchi nzima. Mheshimiwa Naibu Waziri, Josephat Sinkamba Kandege, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimetoa majibu katika swali la msingi, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba maeneo yote ambayo vituo vya afya vinajengwa, vinakuwa ni vituo vya afya ambavyo vinakamilika kwa maana ya kuwa na watalaamu lakini pia kuwa na vifaa vya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa katika swali lake anaongelea Kituo cha Afya ambacho kinaitwa Pasua kiko Moshi na anasema kuna haja ya kuwepo *mortuary* lakini pia na uwepo wa *ultrasound*. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hakuna kituo cha afya hata kimoja ambacho tungependa kikawa kituo cha afya nusu, tungependa vituo vya afya vyote vikamilike, ni vizuri tukaelezana tatizo ni nini na hasa ukizingatia kwamba, hata kwa Halmashauri ya Moshi, mapato yake ya ndani yapo ya kutosha kabisa. Kwa hiyo, ni suala tu la mipango tujue nini kifanyike kwa haraka ili wananchi waweze kupata huduma hizo.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaelekeea Wizara ya Viwanda na Biashara Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, Mbunge wa Muheza, tafadhalii, uliza swali lako.

Na. 240

### **Sera ya Kufungua Viwanda vya Zao la Chai**

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB** Aliuliza:-

Sera ya Serikali ya Viwanda kuhusu zao la chai hairuhusu wakulima wa chai kufungua viwanda wenyewe ili kuiongeza thamani chai hivyo kufanya Kampuni ya *East Usambara Tea Co. Ltd. (EUTCO)* iliyoko Amani - Muheza kuathirika.

Je, kwa nini Serikali isiiondoe sera ambayo haiendani na sera ya viwanda nchini?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, *Engineer Stella Manyanya*, tafadhalı.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mbunge wa Muheza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuanzisha viwanda vya chai unafanyika kwa kufuata Sheria ya Chai Na. 3 ya mwaka 1997 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2009 na Kanuni za Chai za mwaka 2010. Kwa mujibu wa sheria na kanuni, mwombaji wa leseni ya kuanzisha kiwanda cha kusindika majani mabichi au kuchanganya chai anatakiwa kukidhi vigezo vinavyotakiwa. Mnyororo wa uzalishaji wa zao la chai unahusisha hatua mbili ambazo ni usindikikaji wa majani mabichi ili kuzalisha cha kavu na uchanganyaji na uwekaji wa chai kwenye vikasha kwa ajili ya kuuzwa sokoni.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *East Usambara Tea Company Limited (EUTCO)* ni mionganı mwa wakulima wakubwa wa chai hapa nchini yenye viwanda vitatu vya kusindika majani mabichi ya chai ikiwa ni hatua ya awali ya kuongeza thamani kwenye zao la chai kwa ajili ya kuza kwenye soko la nje na kwenye viwanda vya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha. Kampuni hiyo iliomba leseni ya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha ikiwa ni hatua ya pili ya kuongeza thamani kwenye zao la chai.

Mheshimiwa Spika, kutokana na sheria ya chai, kampuni ilitakiwa kuanzisha kampuni tanzu kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo kama ambavyo imeainishwa na sheria husika ya kuchanganya na kufunga chai kwenye vikasha. Kwa utaratibu wa sasa hakuna kampuni ambayo imezuiwa kuchanganya na kufunga chai kupitia kampuni tanzu.

Mheshimiwa Spika, lengo la Sera ya Maendeleo Endelevu ya Viwanda ni kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Souka, hata hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa hivi sasa Bodi ya Chai inafanya mapitio ya kanuni zake kuhusiana na suala zima la usindikaji majani mabichi ya chai. Kazi hii inafanywa kwa kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali, na ni matarajio yangu kuwa suala hilo litapatiwa ufumbuzi katika mchakato huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab swali la nyongeza tafadhalii!

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii ya *East Usambara Tea Company Limited (EUTCO)*ni kampuni kubwa sana pale Muheza ambayo inalima chai na inasindika chai, sasa kampuni hii imekuwa inapeleka chai hii baada ya kuisindika kwenye mnada kule Mombasa na kule Mombasa baada ya kununua wanafanya *packaging* na kurudisha tena hapa nchini kuanza kuuza na hii wanaifanya kwa sababu ya kuzuiwa kupata kibali cha kuanzisha kampuni hiyo ya *packaging* na *blending*.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza kutoa ukaamuru sasa hivi kampuni hiyo iache kupeleka chai hiyo ambayo imesindikwa hapa nchini kwenye mnada Mombasa?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa sababu umesema, hakuna kampuni ambayo imekatazwa kufanya *blending* na *packaging*, ningependa uwaandikie barua kampuni hii ili waanzе kutengeneza, waandae kiwanda cha kufanya kazi hiyo ya *blending* na *packaging*. Nakushukuru. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi, majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Viwanda na Biashara, *Engineer Stella Manyanya*, tafadhal!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, kwanza nikubaliane na mtazamo wake Mheshimiwa Balozi Adadi na nilipotembelea Muheza pia tuliweza kutembelea eneo hili na nikaona kwamba ni kweli ni kampuni kubwa ambayo inafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kama ambavyo nimeeleza hapo awali, kama ni masuala ya kanuni, inabidi lazima yapitiwe na kufanyiwa marekebisho, lakini wakati huo huo, napenda pia kumsisitiza mwenye kiwanda kwamba anao uwezo wa kuanzisha hii kampuni tanzu ambayo itawezesha kuongeza thamani mpaka hatua za mwisho kupitia uzalishaji wa mashamba yake na hatua za awali ambazo anazifanya kwa sasa.

Kwa hiyo, nipende tu kuwataka wenyewe mashamba wote wa chai, sisi Tanzania tunahamasisha viwanda, na tungependa ajira zipatikane kupitia mlolongo mzima wa thamani katika nchi yetu. Kwa hiyo, wachukue hizo hatua lakini wakati huo tunaendelea kufanyia marekebisho ya kanuni na sheria ili kuwezesha wadau hawa kushiriki vizuri katika shughuli hii ya uongezaji thamani chai.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mbunge aliomba muwaandikie barua, mfanye hivyo! Maana yake wakifanya tu kinyemela kama hizo kanuni zinakataza si watakuwa wamekosea. Hili naongezea tu Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa sababu kama kweli tunalazimika tuipeleke chai yetu Mombasa itakuwa haipendezi. Kwa hiyo, tujaribu kuangalia hili katika azma ya Serikali ya awamu ya tano ya viwanda, nafikiri tunakubaliana na majibu yako, tufanye hizo *blending* na kadhalika hapa nchini.

Nilikuona Mheshimiwa Mwambe, nani mwingine mkulima wa chai huko, na Mheshimiwa Chumi.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, suala hili la chai, linafanana kabisa na suala ambalo liko kwenye mikoa inayolima korosho. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mlolongo huu wa kuongeza thamani ya mazao na mwaka kama utakumbuka Mheshimiwa Waziri alipokuja kwenye Kamati yetu ya viwanda na bishara walileta pale ndani wakasema wanafanya utafiti namna ya kuongeza thamani kwenye kochoko ambayo inazalisha nipa ili kuwaongezea mapato wakulima kwa maana ya gongo...

**SPIKA:** Kochoko ndiyo nini?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, kochoko ni zile washi zinazotokana baada ya mavuno ya korosho, wakulima huwa wanazitupa lakini wengine huwa wanaziua na wanatengeneza gongo na inafahamika na kwamba kongo si pombe haramu isipokuwa namna inavyotengenezwa.

Sasa nataka nimuulize Mheshimiwa utafiti huo ambaa ulikuwa unafanywa na Chuo cha Kilimo cha Naliendele umefikia wapi mpaka sasa hivi ili wakulima waweze kujipatia kipato cha ziada kutokana na mazao yao ya shambani? Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Siju kama swali hilo lina Waziri wa Viwanda na Biashara, nadhani zaidi liko kwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, ngoja utasaidiwa na Waziri wa Kilimo tafadhali, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tafadhali.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyyoatoa, pia nichukue nafasi hii kumpongeza ndugu yangu Mheshimiwa Mwambe kwa jinsi ambavyo ameendelea kufuatilia suala hili la korosho.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Chuo chetu kupyitia tawi letu la Naliendele tumefanya utafiti wa kina na tumebaini kwamba kuna mazao mengi tunayoweza kuzalisha kutokana na korosho ikiwemo *juice* na ikiwemo mvinyo maalum ambao unatokana na haya mabibo ya korosho na tumetoa maagizo kwenye tawi letu sasa hivi kujenga kinu cha kuweza kuchakata hiyo ili tuweze kuzalisha mvinyo pamoja na *juice* ambayo tutaiiza hapa nchini na hivi itaongeza thamani na kuongeza mapato yanayotokana na zao la korosho.

Mheshimiwa Spika,kwa hiyo Mheshimiwa Mwambe awe na subira baada ya muda mfupi tu atakiona kile kiwanda kikiwa kimejengwa pale na kuweza kuchakata hiyo, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwambe gongo bado ni haramu hapa nchini. Mheshimiwa Chumi tafadhalii nilikuona.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunionna na kunipa nafasi. Sera tunayoenda nayo sasa tunaelekea katika uchumi wa viwanda, ili tuweze kuwa na uchumi wa viwanda lazima tuhakikishe viwanda vinapata malighafi ipasavyo. Katika Mji wa Mafinga kuna Kiwanda cha Pareto hata hivyo kumekuwa na walanguzi ambao wanununa maua ya pareto na kuyasafirisha kwenda nje ya nchi hivyo kusababisha kiwanda kukosa malighafi.

Serikali inatuambia nini katika kudhibiti walanguzi ambao wanababisha Kiwanda cha Pareto Mafinga kukosa maua? (Makof)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ameeleza changamoto inayopatikana katika Kiwanda cha Pareto cha Mafinga, changamoto hizo pia zipo katika maeneo mengine ya kuhitaji

malighafi nchini kama kwenye maeneo ya ngozi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, changamoto iliyopo ni kwamba unakuta kiwanda kinahitaji kipate hizo malighafi lakini baadhi ya viwanda utakuta kwamba vinanunua malighafi kwa bei ndogo sana kiasi kwamba mkulima anakuwa ahapendi kupeleka hiyo malighafi katika kiwanda kama hicho. Lakini wakati huo hivyo viwanda vinahitaji malighafi hiyo kwa bei ndogo labda kutokana na uwezo wake mdogo wa kifedha hasa katika hatua za awali za ujenzi wa kiwanda.

Kwa hiyo, sisi tunafikiria kama Serikali tunaowajibu sasa wakuingilia kati kuona kwamba viwanda viweze kupata malighafi hizo kwa kusaidiwa na Serikali lakini wakati huo mkulima na ye ye aweze kupata bei inayostahili kutokana na kazi aliyofanya. Kwa hiyo, tumeanza kufanya kazi masuala hayo katika baadhi ya viwanda na tunaamini kwamba kuna hatua stahiki zitachukuliwa kwa viwanda maalum ambavyo vinatumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini.

**SPIKA:** Njombe kuna kilimo kikubwa sana cha chai Mheshimiwa Neema Mgaya nilikuona. (*Makofi*)

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, sisi watu wa Mkoa wa Njombe ni wakulima wazuri wa kilimo cha chai tangu enzi ya ukoloni, nilitaka kujua.

Ni lini Serikali itawasaidia wakulima wadogo wadogo wa kilimo cha chai ndani ya Mkoa wa Njombe na Mikoa mingine kuanzishia viwanda vidogo vidogo vya kuchakata chai ili kukuza thamani ya chai ile na kuweza kuuliza kwa bei nzuri kwenye kiwanda vikubwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Umesikia swali hilo limepigiwa makofi sana, ni kweli kilimo cha chai kimeongezeka sana katika Mkoa wa Njombe, viwanda vidogo vidogo, majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Viwanda na Biashara.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kwamba wakulima wa Njombe, kwanza nipongeze jitihada ambazo zimeshafanyika na vilevile nipongeze kiwanda cha Unilever ambacho tayari kimeshaanza kuchukua chai ya wakulima wanjombe pamoja na inayozalishwa na hao wenyewe. Lakini wakati huo nimepata barua kutoka kwa chama cha Ushirika cha Muvyulu cha Njombe kule Lumbembe ambao nao wanaona kuna changamoto ziko pale kuhusiana na kiwanda ambacho kilianzishwa toka mwaka 1969 na kimekuwa hakijaweza kuendelea na uzalishaji kama ilivyokusudiwa.

Kwa hiyo, tutakapotembelea maeneo hayo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo naamini tutapata hatua nzuri zaidi za kuwasaidia wananchi wa Njombe.

**SPIKA:** Ahsante sana tuendelee Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Kilimo swali linaulizwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijiji.

Na. 241

### **Mradi wa Umwagiliaji Bonde la Mto Mkomazi**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Wananchi wa Tarafa ya Mombo wamekuwa na hitaji la kuwa na skimu kubwa ya umwagiliaji katika Bonde la Mto Mkomazi na mara kadhaa viongozi wa Serikali wamekuwa wakitoa ahadi ya kukamilisha jambo hilo.

Je, ni lini Serikali itatekeleza mradi wa umwagiliaji katika Bonde la Mto Mkomazi?

**SPIKA:** Majibu ya Serikali kuhusu swali namba 241 Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba, Naibu Waziri Kilimo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Timotheo Mnzava Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijiji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 1980 Serikali kuititia na washirika wa maendeleo, yaani Wakala wa Ushirikiano wa Kitaalam wa kimataifa wa Serikali ya Ujeruman (Germany) Agency for Technical Cooperation Limited ulifanya upembuzi yakinifukwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Mkomazi katika tarafa ya Mombo, Halmashauri ya Korogwe. Hata hivyo taarifa ya upembuzi yakinifu na usanifu zilibaini kuwa ujenzi wa bwawa hilo ungesababisha kuongezeka kwa maji katika Ziwa Manga na kupelekea kuzama kwa Kijiji cha Manga Mikocheni pamoja na mashamba ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo katika mwaka 2014/2015 wataalam wa Ofisi ya Kanda ya Umwagiliaji ya Kilimanjaro walifanya mapitio ya upembuzi yakinifu upya na usanifu wa kina uliofanywa katika eneo hilo kwa lengo la kuepusha uwezekano wa kufurika kwa Ziwa Manga, kuzama kwa Kijiji ca Manga Mikocheni na mashamba ya wakulima kutokana na ujenzi wa bwawa hilo. Mapitio hayo yalibaini uwezekano wa ujenzi wa bwawa na mradi wa umwagiliaji katika eneo hilo bila kuathiri wakazi wa eneo hilo. Mapitio ya usanifu huo yalibaini kuwa ujenzi wa bwawa pekee utagharimu shilingi bilioni 1,543,736,877.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika mchakato wa kufanya ukaguzi na tathmini ya kina ya miradi yote ya umwagiliaji nchini ili kufanya uhakiki wa eneo la umwagiliaji kwa lengo la kubaini ubora wa miradi, thamani ya fedha, gharama za miradi na mahitaji halisi ya sasa ya kuboresha, kuendeleza na kuongeza miradi mipya ya umwagiliaji. Aidha, baada ya tathmini hiyo Serikali itaendelea kutafuta fedha ndani na nje ya nchi ili kuhakikisha mabwawa na skimu za umwagiliaji nchini ikiwemo mradi wa umwagiliaji katika

Bonde la Mkomazi zinaendelezwa na kuwanufaisha wananchi wa Mombo na taifa kwa ujumla.

**SPIKA:** Mheshimiwa muuliza swali.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara kwenye hili na anazungumza eneo ambalo analifahamu. Pamoja na majibu yake mazuri ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza mradi huu ulibuniwa muda mrefu sana na ni mradi ambao una uwezo wa kuhudumia eneo kwa maana hekta karibu zaidi ya hekta 5000 na tathmini ambayo unasema ilifanyika ya usanifu uliofanyika ulifanyika muda mrefu.

Je, Serikali iko tayari sasa kuharakisha mapitio ya usanifu upya ili kujua gharama halisi kwa mazingira tuliyokuwanayo sasa na kwa namna ya kutekeleza mradi huu?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili tunayo Skimu ya Songea na Makalala kule Magoma, lakini pia skimu ya Kwamkumbo pale Mombo ambapo wananchi wamekuwa wakiathirika wakati mvua maji yakiwa mengi yanaenda kwenye mashamba ya wakulima na kuharibu mazao na kusababisha hasara kubwa.

Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari, kuwatuma wataalam wa umwagiliaji waende kwenye maeneo haya na kuona namna ya kutatua changamoto hizi za wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Omary Tebweta Mgumba tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, swalii lake la kwanza anataka kufahamu Serikali kuharakisha mchakato wa kuweza kupitia upya

tathmini ya mradii huu. Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tangu siku zile nilivyofika mimi katika bonde hili na kufika bwawa lile tayari tushawaelekeza viongozi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro wanalfanya tathmini upya bwawa lile ili kujua gharama halisi na kuanza utekelezaji kwa mipango ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu athari ya mafuriko katika skimu hizi tatu alizozitaja za Skimu ya Songea na Makalala, kwamba nitumie nafasi hii kwanza kuwaelekeza Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Kanda ya Kilimanjaro kwenda haraka katika mabwawa haya kufanya tathmini na kuona namna gani tunaweza kujenga miundombinu ile yamatuta kwa ajili ya kukinga mafuriko ya athari ya mabwawa haya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafumu kule mwisho kabisa, uliza swali lako.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, bonde la Mto Manonga kama lilivyo bonde la mto Mkomazi kuna Skimu ya Umwagiliaji ya Ijurubi, ambayo ilijengwa miaka ya 1980 lakini sasa hivi ilibebwa na maji wakati wa msimu wa mvua uliopita. Naiomba Serikali basi kama inaweza kwenda kuifufua hiyo skimu ili wananchi wa eneo hilo waendelee na kilimo cha mpunga, lakini pia skimu zingine ambazo za namna hiyo zilizoachwa kama kule Kibaha Vijiji na sehemu zingine ziangaliwe zote ili ziweze kufufuliwa, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante majibu ya swali hilo kwa skimu zote za umwagiliaji Tanzania, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru, kwanza ombi lake la kwenda kufanya ukarabati mkubwa kwenye skimu hii ya Ijurubi kwanza tunalipokea, lakini nichukue nafasi hii kuwaeleza Wabunge wote skimu ziko nyingi sana katika Taifa hili, tuna eneo zaidi la hekta milioni 29 zinatafaa kwa umwagiliaji na mpaka sasa miaka 58 tumeendeleza hekta 4,75,000 tu. Kwa

hiyo, tukitumia au tukitegemea skimu hizi zote kuendeleza kwa kupata pesa za kibajeti tutachelewa sana, sisi kama Serikali na ndiyo maana tulianzisha benki ya mkakati ya Maendeleo Benki ya Kilimo kwa ajili ya kuendeleza miradi mikubwa hii.

Kwa hiyo sasa hivi Benki ya Maendeleo ya Kilimo itapita kila Halmashauri ambayo iliyokuwa na eneo hili la umwagiliaji kwa ajili ya skimu zingine tuziendeleze kwenye kilimo cha kibashara kwa ajili ya kupata mikopo yenye riba nafuu ili badala ya kusubiri hela za kibajeti ili tuweze kuendeleze skimu hizi kwa muda mfupi Tanzania nzima.

**SPIKA:** Ahsante kwa sababu ya muda tunaendelea na swalii la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda uliza swalii lako tafadhalii, Mbunge wa Kondoaa Mjini.

Na.242

### **Mradi wa Kilimo ch Umwagiliaji-Kijiji cha Mongoroma**

**MHE. EDWIN M. SANNDA** aliuliza:-

Halmashauri ya Mji wa Kondoaa imewasilisha andiko la Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji katika Kijiji cha Mongoroma, Kata ya Serya takribani miaka mitatu sasa, eneo la ekari 3,000 limetengwa kwa ajili ya mradi huo utakaonufaisha takribani wananchi 12,000.

Je, ni lini Serikali italeta fedha hizo ili mradi huo uanze?

**SPIKA:** Majibu ya swalii hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo kuhusu umwagiliaji pale Kondoaa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika,kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Jimbo la Kondoaa Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2010/2011 Serikali kupitia Idara iliyokuwa ya Umwagiliaji chini ya Wizara ya Kilimo ilitumia shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuendeleza miradi ya umwagiliaji ya Kisese, Kidoka na Mongoroma Serya katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa wakati huo. Kati ya fedha hizo shilingi 143,265,000 zilitumika kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika mradi wa Mongoroma Serya uliopo katika Kata ya Serya. Kazi zilizofanyika ni pamoja na upimaji wa sura ya ardhi, usanifu wa kina matayarisho ya gharama za ujenzi, tathmini ya rasilimali maji, tathmini ya awali ya mazingira, utafiti wa udongo na masuala ya jamii.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bwawa la Mongoroma Serya ulibaini kuwa bwawa hilo lingegharimu shilingi bilioni nne kwa wakati huo. Aidha, bwawa hilo lingekuwa na uwezo wa kumwagilia zaidi ya hekta 3,000 na kunufaisha zaidi ya wakulima 12,000 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, matumizi ya binadamu, unyweshaji wa mifugo na wanyamapori pamoja na ufugaji wa samaki katika vijiji vya Mongoroma, Serya na Munguri.

Mheshimiwa Spika, Serikali iko katika mchakato wa kufanya tathmini ya kina kwa miradi yote ya umwagiliaji nchini ili kubaini thamani ya fedha, ubora wa miradi na mahitaji halisi ya uboreshwaji, uendelezwaji na kuchagua miradi michache kwa utekelezaji wa ujenzi kwa miradi yenye tija, matokeo na manufaa makubwa kwa wakulima na Taifa kwa ujumla. Aidha, baada ya tathmini hii na kutegemea upatikanaji wa fedha Serikali itahakikisha bwawa hilo na skimu zingine zitajengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sannda tafadhali nilikuona.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nitumie fursa hii kushukuru majibu ya Serikali sambamba na hayo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, namba moja, ni miaka tisa sasa toka tumeingiza zaidi ya milioni 143 kwenye mradi huu na

hakuna ambacho kimeweza kuwa *realized* mpaka leo. Ukichukua faida ambazo tungezipata kwa mradi ule watu 12,000 kunufaika tungekuwa tu kwa mwaka tunapata zaidi ya bilioni 50; mpaka leo tunazungumzia miaka tisa tungekuwa tumetengeneza zaidi ya bilioni 500, ukiangalia hii *opportunity cost* peke yake acha *multiplier effect* kipindi cha uchumi wa viwanda na mazao ambayo yangetokana na matokeo yale ya pale kwenye mradi ule tungekuwa tumepeiga hatua kubwa sana kwa wananchi wa Kondoaa.

Je, ni lini sasa Serikali itafikia hatua ya kuweza kufanya hii tathmini ya kina na hatimaye kufanya hii tathmini ya kina na hatimaye kukamilisha mchakato mradi huu utekelezwe? la kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili ili Mheshimiwa Naibu Waziri uweze kujiridhisha na fursa iliyoko kule fursa kubwa sana.

Ni lini sasa mimi na wewe na pamoja na wataalam wako tutaongozana tuende pale Mongoroma tukaone nini kinaweza kikafanyika kwa haraka zaidi? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili muhimu Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo, Mheshimiwa Mgumba tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza anataka kujua kwamba huu mradi umechukua muda mrefu zaidi ya miaka tisa na hela pale tumeshawekeza ni lini sasa kwamba tumeanza kuuharakisha huu mchakato.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kwanza kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge pamoja na kwamba sijafika katika mradi huu, lakini viongozi wetu, Wahandisi wetu wa Kanda ya Umwagiliaji Kanda ya Dodoma tayari wako kwenye mchakato wa kuufanya tathmini ya kina ili kubaini gharama halisi za sasa badala hizi za miaka kumi iliyopita ili kuingiza katika mpango kabambe wa umwagiliaji ambao

tumeuhaulisha ile Sera ya mwaka 2013 kwa hii ambayo Sera Mpya ya mwaka 2018 mradi huu pia tunaenda kuutekeleza na tathmini itafanyika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili kama nilivyojibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Kafumu kwamba mradi mbadala au njia mbadala ya kutekeleza miradi hii mikubwa ni kutumia Benki ya Maendeleo ya Kilimo kwa sasa hivi kwa sababu tunaondoka kwenye kilimo kile cha kujikimu tuko kwenye kilimo cha kibashara. Kwa hiyo, lazima sasa tuwekeze ndiyo maana tumewaletea benki hii yenye riba rafiki kwa wakulima ili kuenda kuendeleza miradi mikubwa kama hii kwa sababu ile ni benki ya kimkakati.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili niko tayari baada ya bajeti yetu inayoanza kesho tarehe 17 Mei na kumalizika tarehe 20 Mei tuonane tupange ikiwezekana tarehe 21 na 22 Mei mimi na wataalam wangu tuko tayari kufika Kondoa ili kuliangalia.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, uliza swalii lako.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye kuleta matumaini kuhusiana na miradi hii ya umwagiliaji. Lakini pamoja na pongezi hizo mimi naomba niulize swalii dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, iko miradi ya kilimo cha umwagiliaji ambayo ilikuwa inaendelea katika Mkoa wetu wa Ruvuma ikiwemo mradi wa kilimo cha umwagiliaji uliopo Legezamwendo, Misyaje na baadhi ya vijiji vingine. Miradi hii imesimama kwa ajili ya kukosa pesa na nina uhakika tayari miradi hii ilishaanza. Kuendelea kuchelewa kupeleka pesa maana yake ni kuongeza gharama za mradi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha tunapeleka pesa katika miradi hii ili kukamilisha? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Kilimo tafadhali

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, nashukuru, ni kweli kwamba kuna miradi mingi ambayo imeanza kujengwa na haijamalizika mpaka sasa na labda nilitaarifu Bunge lako rasmi; baada ya Tume hii ya Taifa ya Umwagiliaji kurudi Wizara ya Kilimo tuliweza kupita katika scheme karibuni zote nchini ili kuzingalia na namna gani na wataalam wetu na hiyo pia ndani ya Serikali kama mnakumbuka siku tatu zilizopita Mheshimiwa Waziri Mkuu amewasimamisha zaidi ya Wakurugenzi saba kwa ajili ya kupisha uchunguzi tufanye tathmini ya kina kuangalia matumizi ya fedha kwa sababu pesa zillkwenda nydingi, lakini matumizi yalikuwa ni mabovu sana.

Kwa hiyo siyo kila mradi ukikwama kumalizika ni kwa sababu kwamba pesa zilikosekana, lakini baada ya hiki chombo tulichounda sasa hivi, Tume tuliyouna sasa hivi kwenda kuchunguza mapungufu hayo ya ubora wa miradi, thamani ya miradi baadae tutakuja na taarifa rasmi na kujipanga namna gani tutakwenda kumaliza mradi huu.

**SPIKA:** Twende swali la mwisho kwa siku ya leo Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto swali litaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Kaliua, Mheshimiwa Magdalena Sakaya tafadhali.

Na. 243

### **Sera ya Kutoa Huduma za Afya Bure**

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA** aliuliza:-

(a) Je, ni lini Serikali itatekeleza kwa ukamilifu Sera ya Afya ya kutoa huduma za afya bure kwa wanawake

wajawazito, watoto chini ya miaka mitano pamoja na wazee wenye umri zaidi ya miaka 60?

(b) Mwaka 2014 Serikali ilianza utaratibu wa kuwapatia wazee vitambulisho kwa ajili ya matibabu bure kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali. Je, ni Wilaya ngapi zimekamilisha zoezi hilo muhimu ili kuokoa maisha ya wazee yanayopotea kwa kukosa huduma za afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mbunge wa Kaliua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya jitihada katika kutoa huduma bora za afya na zenyekufikiwa na watu kwa kuandaa sera na miongozo na kusimamia utekelezaji wake. Katika kutoa huduma hizi, Serikali imekuwa ikiyapa kipaumbele makundi maalum kama vile wajawaziti, watoto chini ya miaka mitano, wazee wasio na uwezo na wenye ulemavu ambaao kwa namna moja au nyingine hawawezi kuijishughulisha na shughuli za kiuchumi na kujipatia kipato kwa kuanzisha sera za matibabu bila malipo kwa makundi hayo. Tangu kuanzishwa kwa sera hii Serikali imekuwa ikisimamia kwa ukaribu kuhakikisha inatekeleza ipasavyo na watoa huduma katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada hizi ambazo Serikali imekuwa ikizifanya katika kuwapatia makundi haya matibabu bure, bado kumekuwa na changamoto katika utekelezaji wa sera hii kutokana na kuongezeka kwa magonjwa na idadi ya watu walio katika makundi maalum. Hali hii inasababisha watoa huduma kuwa na idadi kubwa ya watu walio katika makundi maalum wakati rasilimali kwa ajili ya kuwashudumia ni ndogo.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali iko katika hatua ya maandalizi ya mkakati wa

ugharamiaji wa huduma za afya ambao lengo lake ni kuibua vyanzo mbalimbali vya mapato kwa ajili ya kugharamia huduma za afya kwa maana ya *health care sector financing*. Moja ya vyanzo vilivypendekezwa katika mkakati huo ni uanzishwaji wa Bima ya Afya moja (*Single National Health Insurance*) ambayo uchangajikatika bima hiyo itakuwani ya lazima kwa wote walio na uwezo wa kuchangia. Kulingana na tafiti zilizofanywa, njia hii itasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza rasilimali fedha katika sekta ya afya na kuweza kugharamia makundi maalum yatakayohitaji msaaha wa kulipia huduma za afya. Mkakati huu unataraja kukamilika na kuanza kutekelezwa mapema mara baada ya taratibu za Serikali za kufanya maamuzi zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa maagizo kwa watoa huduma watenge madirisha maalum kwa ajili ya kuwashumia wazee na Halmashauri ziwatambue na kuwapa kadi za wazee kwa ajili ya matibabu. Hata hivyo utekelezaji wa utaratibu huu umekuwa na changamoto ambapo takribani asilimia 40 tu za Halmashauri zote zimeweza kutekeleza agizo hilo. Natoa rai kwa Halmashauri zote nchini kutekeleza agizo la Serikali la kutoa vitambulisho kwa Wazee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Magdalena Sakaya tafadhali uliza swali lako.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekiri changamoto kubwaya utekelezaji wa Sera hii ya kutoa huduma bure kwa makundi haya maalum ikiwemo wajawazito, watoto chini ya miaka mitano, wazee wanaozidi umri wa miaka 60 ambao hawana uwezo lakini pia makundi ya watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hii makundi haya yanateseka sana kupata huduma maeneo mbalimbali na wengi kiukweli wanapoteza maisha. Leo maeneo ya vijijini, Wilayani huko wanaandikiwa barua

kwenye Ofisi ya Mkuu wa Wilaya watembee mitaani wanaomba misaada ili waweze kutibiwa kwahiylo Serikali ione changamoto kubwa hii iliyopo.

Mheshimiwa Spika, napenda kujuu, Serikali imekuja na mkakati wa kuweza kuwepo hii huduma ya kuweza kutoa bima kwa wote sasa hawajasema *specific* ni lini itakamilika. Wanasema mpaka mchakato wa Serikali kutoa maamuzi. Hebu muone umuhimu ni lini sasa, naomba *commitment* hapa Bungeni ni lini mchakato huu utakamilika ili mfuko huu uweze kuwa na fedha ya kutosha makundi haya yatibiwe yaweze kupona kwa kuwa wengi wanapoteza maisha?

Mheshimiwa Spika, Iakini tangu Serikali imetoa agizo kwenye Halmashauri zetu ni miaka zita sasa na Mheshimiwa Waziri kwenye majibu yake ni asilimia 40 tu wametekeleza, kwa hiyo bado wazee wengi hawajapewa vitambulisho, hawapati huduma za fya kwenye madirisha maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali, siyo kutoa tu rai, Serikali sasa naiomba leo iweze kutoa tamko hapa Bungeni, itoe *deadline* ni lini ambapo vitambulisho hivi vikamilike na wale Halmashauri ambazo hazijakamilika kwa wakati waweze kupewa adhabu ili wazee hawa ambao wametumikia Taifa hili wapate huduma za afya bure waweze kuishi. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante kwa maswali yako mazuri. Jamani msisitizo ni wazee wasiojiweza maana wako wazee wengine ndiyo kwanza wanachumbia, sasa hawa hawahusiki. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhalii. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Magdalena Sakaya alitaka *commitment* ya Serikali kwamba ni lini utaratibu au mchakato huu wa Bima ya Afya kwa wananchi wote utakamilika; nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ifikapo Bunge la Septemba Serikali tutaleta Muswada wa Bima ya Afya kwa wananchi wote ndani ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, Iakini ameuliza swlai la pili kuhusiana na wazee na lini mchakato huu tuweze kutoa tamko; mimi naomba niseme tu kama ifuatavyo; nchi yetu sasa hivi inaendelea kupata neema na wastani wa Matanzania sasa hivi kuishi ni iaka 64 kwamba tunategemea kwamba na tunatarajia kama kila mtu atatunza afya yake vizuri tunatarajia tu kwamba atafika miaka 64, kwa hiyo umri huu unazidi kuongezeka na iddai ya watu hawa wanazidi kuongezeka ambao wanazidi miaka 60. Kwa hiyo, hatuwezi tukasema wkamba tutatoa ukomo kwamba ifikapo kesho wazee wote wa miaka 60 wawe wamepata vitambulisho.

Kwa hiyo mimi niendelee kusositiza tu kwamba Serikali imeshatoa maagizo kwa Halmashauri zote na hili ni agizo la Serikali wanatakiwa waendelee kuwatambua wazee na waendelee kuwapatia vitambulisho wale wazee ambao hawna uwezo wa kugharamia matibabu.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Kemilembe Lwota uliza swalo lako.

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli suala hili la matibabu bure limekuwa na changamoto kubwa sana mpaka kuna baadhi ya vituo na hospitali wakina Mama wajawazito wanambiwa waende na mabeseni, pamba na hata mikasi.

Je, ni lini Serikali sasa itaona umuhimu wa kuweka angalau fedha kidogo za kuchangia akina mama wajawazito ili waweze kupata huduma bora? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sera ya Afya ya mwaka 2007, huduma kwa ajili ya akina mama

wajawazito ni bure na sisi kama Seriakli tumekuwa tunaendelea kuwekeza sasa hivi takribani akina mama milioni mbili wanajifugua kwa mwaka ndani ya nchi yetu na sisi kama Serikali kupitia Bajeti hii ya dawa, vifaatiba na vitendenishi tumejaribu sana kuhakikisha vifaa vya kujifungulia vinakuwepo, tumehakikisha kwamba chanjo kwa ajili ya watoto tunakuwa nazo, dawa zote za muhimu kwa maana dawa za kupunguza upungufu wa damu kwa akina mama yale madini ya *iron* pamoja na *phera sulfate* pamoja na *folic acid* tunakuwa nazo, dawa za kuongeza uchungu *oxytocin* tunakuwa nazo na dawa za kupunguza kifafa cha mimba tunakuwa nazo. Kwa hiyo, ni sehemu chache sana ambazo tunapata malalamiko kama hayo na mimi kama Naibu Waziri nimetembelea sehemu mengi sana basi ni sehemu nyingi vifaa vya kujifungulia tunavyo na sisi kama Serikali tunavyo kupitia Bohari yetu ya madawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Same Mashariki lina tatizo kubwa sana la huduma za afya. Kituo kilichokuwa kimeitwa Kituo cha Afya Vunta kwenye Tarafa ya Mamba Vunta ilikuwa ni ghala la mazao kikapandishwa hadhi lakini hakina hadhi hata ya kuwa *dispensary*, Tarafa ya Gonja haina hata zahanati wala kituo cha afya cha serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kuiomba Serikali kwamba kwa muda mrefu nimeenda kuongea na Serikali kuhusu kuboresha angalau basi Hospitali ya Gonja Bombo ambayo Serikali kupitia KKKT wanasaidia watu wa Tarafa hii ya Gonja na ya Mamba Vunta kupata huduma katika hospitali hii.

Je, ni lini Serikali itapeleka angalau Madaktari basi wakasaidie kuboresha huduma hii ili akina mama wajawazito wasife wakitembea umbali mkubwa zaidi ya kilometra 15 mpaka 30 kufuata huduma katika Tarafa ya Ndungu ambayo

kituo kipo bondeni na Tarafa hizi zote kubwa ziko milimani ambapo hata barabara zetu ni mbaya sana?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Afya umesikia *terrain*ya huko milimani Upareni huko sijui kama umewahi kufika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuboresha sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuunga mkono juhudzi za wananchi pale ambapo wanaanzisha ujenzi wa maboma ya zahanati Serikali kupitia Halmashauri imekuwa ikichangia kukamilisha yale maboma lakini sambamba na hilo tumefanya maboresho makubwa sana ya vituo vya afya takribani kati ya vituo zaidi ya 500 ndani ya nchi yetu, zaidi ya 300 na tumeweza kuvifanyia maboresho kuweza kutoa huduma za dharura za kumtoa mtoto tumboni.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, Serikali katika mwaka huu wa fedha mabao unakwisha tumejielekeza nguvu katika kujenga hospitali za Wilaya 67 na lengo ni kusogeza hizi huduma za fya karibu zaidi na wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo, katika maeneo ambapo hatuna Hospitali za Wilaya tumekuwa tunafanyakazi kwa karibu sana na hizi hospitali ambazo ziko katika taasisi za kidini ambazo kwa jina zimekuwa zinaitwa *DDH* na tumekuwa tunawapatia rasilimali fedha kwa ajili ya dawa pamoja na watumishi. Kwa hiyo, sisi tuko tayari kama Serikali tukipata maombi mahususi kuhusiana na hii Hospitali ya *DDH* ambayo nimekuwa nimeiongelea kama kuha hitaji la rasilimali watu tuko tayari kuweza kushirikiana nao kwa ajili ya lengo la kutoa huduma kwa wananchi wa Same Mashairiki.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge leo ni Wizara ya siku moja kwahiyio inabidi tuangalie muda kidogo, mtuwie radhi kidogo kwa maswali ya nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, leo tunao wageni 80 wa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kusema ukweli Waheshimiwa Wabunge leo Jeshi liko hapa.

Nawashukuru sana Jeshi kwa kuja kushirikiana na sisi siku ya leo ambapo baadae kidogo Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa atatutolea hoja hapa kwa ajili ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2019/2020.

Kwa hiyo tunayo timu ambayo ningependa kuitambulisha, naomba Waheshimiwa Wabunge amba hamuufahamu muwe makini kidogo niwatambulishemmoja mmoja katika wale Maofisa Wakuu.

Kwanza Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Florens Turuka. Karibu sana, karibu sana. (*Makofi*)

Namleta kwenu Waheshimiwa Wabunge, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Jenerali Venance Mabeyo. Karibu sana *General*, karibu sana mionganoni mwetu. (*Makofi*)

Nawaletea Mnadhimu Mkuu wa Jeshi Yacoub Mohamed. (*Makofi*)

Nawaletea Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Martin Busungu. (*Makofi*)

Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Nchi Kavu, Meja Jenerali George Msongole. (*Makofi*)

Mkuu wa Kamandi ya Jeshi la Anga, Meja Jenerali George Ingram. Ahsante. (*Makofi*)

Mkuu wa Jeshi la Wanamaji, *Rear Admiral* Richard Makanzo. (*Makofi*)

Mkuu wa Kamandi ya Makao Makuu ya Jeshi, Meja Jenerali, Shariff Othman. (*Makofi*)

Mkuu wa Tawi la Tiba Jeshini, Meja Jenerali Denis Janga. (*Makofi*)

Mkuu wa Utumishi Jeshini, Meja Jenerali Blasius Masanja. (*Makofi*)

Kamishna wa Utafiti na Maendeleo ya Jeshi, Meja Jenerali Ramadhani Mlangira. (*Makofi*)

Mdhibiti Mkuu wa Jeshi, Meja Jenerali Mathew Mkingule. (*Makofi*)

Mkuu wa Shirika la Mzinga, Meja Jenerali Shija Makona. (*Makofi*)

Mkuu wa Shirika la Nyumbu, Meja Jenerali Anselm Bahati. (*Makofi*)

Jaji, Wakili Mkuu Wizarani, Meja Jenerali Kaisi Njelekela. Wengine mtashangaa hii kule Mahakama pia ya Kijeshi, kwa hiyo ndio maana kuna mambo haya. (*Makofi*)

Mkuu wa Mipango na Maendeleo Jeshini, Brigedia Jenerali Fulgence Msafiri. (*Makofi*)

Mkuu wa Jeshi la Akiba, Brigedia Jenerali Ismail Ismail. (*Makofi*)

Mkuu wa Usalama na Utambuzi Jeshini, Brigedia Jenerali Julius Mbwelo. (*Makofi*)

Mkuu wa Tawi la Ugavi na Uhandisi Jeshini, Brigedia Jenerali Paul Simuli. (*Makofi*)

Kamanda wa Bridei Zanzibar, Brigedia Jenerali Fadhili Nondo. (*Makofi*)

Kamishina wa Sera na Mipango, Ndugu Egbert Ndauka. (*Makofi*)

Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii Jeshini, *Lieutenant Colonel Sophia Hassan. (Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Mnamuona alivyokaa sawasawa? Hakuna kucheka wala kutabasamu. (*Kicheko*)

Mkaguzi Mkuu wa Nje wa Wizara, Ndugu Fortunatus Donge. Ahsante sana makamanda wetu. (*Makofi*)

Wameambatana na Wakuu wa Idara na Vitengo na Maafisa Wakuu na Viongozi wa Chama cha Wafanyakazi (*TUGHE*) kwa hiyo mtakubaliana nami kwamba Jeshi liko hapa leo. Kwa hiyo, wale wanaonisumbuaga sumbuaga jamani Jeshi liko hapa leo, nategemea na uchangiaji wetu utazingatia hilo kwamba Jeshi lipo. Tunawapenda sana, tunawapongeza kwa kazi nzuri, karibuni sana, Bunge liko na Jeshi maana hilli ni Jeshi la Wananchi, tunawapenda sana. (*Kicheko*)

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni 90 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira ambao ni wanafunzi 84 na walimu sita kutojs shule ya Sekondari ya Maria De Mathias iliyoko Mkoani Dodoma wakiongozwa na Sister Mary Malele. Maria De Mathias wako wapi? Mnawaona watoto walivyopendeza hao, shule za Dodoma hizo karibuni sana walimu na wanafunzi kutoka Maria De Mathias na hongereni sana. (*Makofi*)

Wageni 32 wa Mheshimiwa Emmanuel Papian ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Kiteto Mkoana wa Manyara wakiongozwa na Mheshimiwa Lairumbe Mollel, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto, Madiwani wa Kiteto karibuni sana, karibuni majirani hamuwezi kufiti inafika hapa bila kufika Kongwa kwa hiyo karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Vedastus Mathayo ambaye ni jamaa yake kutoka Musoma Mkoani Mara Ndugu James Makanya popote pale ulipo Makanya karibu. (*Makofi*)

Wageni 60 wa Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wanaosomea Sayansi ya Tiba kutoka pale UDOM wakiongozwa na Ndugu Veronica Nelson, *UDOM* karibuni sana. (*Makofii*)

Wanakwaya 37 kutoka kikundi cha kwaya ya Jimbo la Mwakaleli Kanisa la KKT Dayosisi ya Konde, wale wa Mwakaleli ohoo karibuni sana kutoka kule Konde, karibuni sana wanakwaya. (*Makofii*)

Wananchi wanne waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya kujifunza wakiongozwa na Ndugu Peter Maganga, karibuni sana wale wageni wetu kutoka huko mlikotoka. (*Makofii*)

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

**SPIKA:** Ahsante kabla ya kumuita Mheshimiwa Waziri kusoma hotuba yake naomba nimuite Mheshimiwa Mwenyekiti Zungu ili aendelee na shughuli za hapa mezani.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Wizara hii ni siku moja tu leo, mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuendelea kutupa uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa Bungeni leo hii kujadili hotuba ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Aidha, nitumie fursa hii kwa moyo wa dhati kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Pia niwashukuru Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungani wa Tanzania kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayoyatoa katika kufanikisha utendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza kwa weledi Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje ya Ulinzi na Usalama inayoongozwa na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa ushauri na ushirikiano mnaotupatia katika kusimamia utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifanikiwa kutembelea baadhi ya miradi na kutoa ushauri kwa maeneo yenye changamoto ili yaweze kupatiwa ufumbuzi. Vilevile Kamati ilioita ushauri na maoni wakati ikichambua taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuandaa mpango wa bajeti hii ninayowasilisha leo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na wenzangu kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako tukufu, familia na wananchi wote wa Jimbo la Korogwe Kijijiini kwa kuondokewa na mpendwa wetu Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijiini kuititia Chama cha Mapinduzi. Vilevile natoa pole kwa wananchi walipatwa na majanga pamoja na kufikwa na misiba ya ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali ya ajili ikiwemo ya kuzama kwa vivuko, kuzama kwa kivuko cha MV Nyerere katika Ziwa Victoria Wilayani Ukerewe tarehe 20 Septemba, 2018 ambapo wananchi wapatao 224 walipoteza maisha.

Pia natoa pole kwa Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa msiba wa watumishi 12 waliofariki kwa ajali ya gari Mkoani Morogoro. Aidha, natoa pole kwa Mheshimiwa Japhet Hasunga Waziri wa Kilimo kwa msiba wa watumishi watano waliofariki Mkoani Singida ambapo wote kwa ujumla walikuwa wakitekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi na Maafisa Askari, Watumishi wa Umma na familia za wanajeshi walipoteza maisha wakitekeleza jukumu ya ulinzi wa amani hadi kufikia mwezi Aprili 2019, wanajeshi watano walipoteza maisha, wawili katika Jamhuri uya Kidemokrasia ya Kongo na watatu Jamhuri ya Afrika ya Kati,

Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dira, dhima na majukumu ya Wizara; dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuendelea kwa taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha amani na usalama wa Taifa letu. Vilevile dhima ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina yoyote kutoka ndani na nje ya nchi na kuhakikisha kuwa Mamlaka na maslahi ya Taifa yanakuwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufanikisha dira na dhima malengo makuu ya Wizara yameendelea kuwa yafuatayo:-

- (a) Kuwa na Jeshi dogo lenye wataalam dhana na vifaa vya kisasa;
- (b) kuendelea kuwajengea vijana wa kitanzania ukakamavu, maadili mema, Utaifa, moyo wa uzalendo na uwezo wa kujitegemea;
- (c) Kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali za uhaulishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;
- (d) Kuwa na Jeshi imara la akiba;
- (e) Kusaidia mamlaka za kiraia katika kukabiliana na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha maslahi ya Taifa, maisha, amani na utulivu nchini; na
- (f) Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyiningine duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama; wakati wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ilitoa maoni na ushauri kwa Wizara yaliyokusudia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuriarifu Bunge lako tukufu kuwa maoni, ushauri na maaazimio yaliyotolewa yalifanyiwa kazi na Wizara na taarifa yake iliwasilishwa kwa Kamati tarehe 28 Machi, 2019. Aidha, Wizara imezingatia hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wakati wa mjadala katika kuandaa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2019/2020 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa llani ya uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015/2020 na mpango wa pili wa maendeleo wa Taifa wa miaka mitano, 2016/2017 hadi 2020/2021; Wizara imeendelea kutekeleza llani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020 sambamba na Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano na utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara. Maelekezo ya llani kwa Wizara yameainishwa katika Ibara ya 146 ambayo ni haya yafuatayo:-

- (a) Kuviwezesha vyombo vyao ulinzi na usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na fedha;
- (b) Kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vyao ulinzi na usalama;
- (c) Kuweka mazingira mazuri yanayoliwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa mujibu wa sheria;
- (d) Kushirikiana na Umoja wa Mataifa na Umoja wa Afrika katika shughuli za ulinzi wa amani kwenye nchi mbalimbali duniani ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za ulinzi wa amani na kushirikiana na Mataifa mengine na asasi za Kimataifa katika kupambana na uhalifu unaovuka mipaka hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji fedha,

biashara haramu ya madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Wizara imeendelea kutekeleza llani kwa ufanisi, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi yameainishwa katika kiambatisho namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya nchi yetu; hali ya usalama wa mipaka; hali ya usalama wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari katika kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 hakuna matukio ya kuhatarisha usalama wa nchi yaliyopotiwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kutekeleza majukumu yake ya ulinzi wa mipaka kwa weledi na umakini ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. Hata hivyo zipo baadhi ya changamoto kwenye maeneo mbalimbali ya mipaka zinazohitaji kushughulikiwa ili kuboresha udhibiti wa mipaka na kuimarisha usalama wa nchi yetu. Changamoto hizo zimeainishwa katika aya ya 16 ukurasa namba tisa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu kwa pamoja na nchi husika zimeendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo. Mathalani katika mpaka wa Kaskazini tunapopakana na nchi za Kenya na Uganda, Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na mazungumzo na nchi tunazopakana ili kutatua changamoto za wafugaji haramu wanaotafuta malisho na maji, wahamiaji haramu, uwekaji wa alama za mipaka zilizoharibiwa na uwekaji wa alama mpya za mipaka katika maeneo yanayohitaji kuwekewa alama hizo ili kuimarisha ulinzi wa mpaka wetu wenye urefu wa kilometra 5401. Maelezo ya kina kuhusu hali ya mipaka yetu yameelezwa katika aya ya 18 hadi 25 ukurasa namba 10 hadi 13 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tishio la ugaidi; ugaidi wa kimataifa umeendelea kuwa tishio la usalama duniani, kuendelea kuwepo kwa makundi ya *Al Shabaab*, *Al Qaeda*, *Boko Haram* na *Islamic State* kunafanya matishio ya ugaidi kusambaa kila kona ya dunia. Vitendo vya kigaidi vinavyofanywa na kundi la *Sunna-wal-Jamaa* katika Jimbo la Cabo Delgado Kaskazini mwa Msambiji vinaweza kuhatarisha usalama katika maeneo ya Kusini mwa nchi yetu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama limeendea kufuatilia viashiria na matishio ya kigaidi yanayoweza kutoka hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa kundi la *Al Shabaab* ambalo limeendelea kufanya mashambulizi katika nchi jirani ya Kenya ni changamoto kwa Tanzania, hata hivyo Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya ulinzi na usalama vinaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa salama. Vilevile wito wangu kwa Watanzania ni kuendelea kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi na usalama mara wanapobaini watu ambao mienendo yao ni ya mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019; makadirio ya makusanyo ya maduhuli; mwaka wa fedha 2018/2019 Wizara ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 75,420,100 kutoka katika mafungu yake matatu yaani Fungu 38 Ngome shilingi 17,317,100; Fungu 39 JKT shilingi 56,903,000 na Fungu 57 Wizara shilingi milioni 1,200,000. Kufikia mwezi Machi, 2019 mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 66,469,557 sawa na asilimia 88.13 ya makadirio. Fungu 38 Ngome ililikusanya jumla ya shilingi 22,719,557 kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na Kamisheni ya Uwakala wa Bima unaofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Fungu 39 JKT ililikusanya shilingi 42,750,000 kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni, mazao ya bustani, mazao ya mifugo na mazao ya shamba. Fungu 57 Wizara ililikusanya kiasi cha shilingi 1,000,000 ambazo zimetokana na kodi ya pango la kantini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya shilingi 1,910,722,891,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo shilingi 1,676,722,891,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 234 bilioni ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu umeoneshwa katika kiambatisho namba mbili ukurasa wa 53 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 fedha iliyopokelewa ilikuwa ni shilingi 1,610,411,417,602.2 sawa na asilimia 84.28 ya bajeti. Kati ya fedha hizo shilingi 1,446,309,579,339.62 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 164,101,338,262.58 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kiasi kilichopokelewa hadi mwezi Aprili, 2019, umeainishwa katika kiambatisho namba tatu ukurasa wa 54 hadi 55 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za matumizi ya kawaida kiasi cha shilingi 1,313,755,685,669.62 zimetumika kulipa mishahara na posho mbalimbali za maafisa, askari, vijana wa mujibu wa sheria na wa kujitolea. Vilevile fedha hizo zimetumika katika shughuli za kijeshi na kiulinzi katika nchi za Kikanda yakiwemo mazoezi, mafunzo na *operation* za kijeshi. Aidha, sehemu ya fedha hizo zimetumika kugharamia huduma ya afya kwa wanajeshi, kulipa sehemu ya madeni ya wazabuni wanaotoa huduma na kuhamasisha wanajeshi na watumishi wa umma kwenda Dodoma, usafirishaji na uhifadhi wa korosho na uendeshaji wa ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi 164,101,338,262.58 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kupitia mafungu yake matatu. Fedha hizo zimetumika kulipia ununuzi wa dhana na vifaa vya kijeshi, uwekaji wa umeme kwenye minara ya mawasiliano salama jeshini na kulipia mifumo ya ujenzi wa mundombinu ya maji safi na maji taka. Fedha hizo pia zimetumika kununua ardhi kwa ajili ya matumizi ya kimkakati ya Jeshi katika maeneo ya

Kakonko, Kigoma na kulipia fidia katika eneo la Rasi Mshindo Lindi, kuboresha mfumo wa ulinzi wa anga, kukamilisha ujenzi wa ukarabati wa mahanga ya askari na vijana, ujenzi wa jengo la utawala Kambi Mpya ya JKT Kibiti Pwani na ujenzi wa miundombinu ya wezeshi kwa ajili ya Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Ofisi ya Wizara Mtumba na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa Dodoma.

Vilevile fedha hizo zimetumika katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule na vyuo vya kijeshi. Aidha fedha hizo zimetumika kununulia malighafi kwa ajili ya kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi katika Shirika la Mzinga pamoja na kuendeleza shughuli za utafiti na uhaulishaji wa teknolojia katika Shirika la Nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafanikio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019; matumizi katika shughuli za kawaida, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Wizara imefanikiwa kulipa mahitaji na huduma muhimu ikiwemo mishahara na posho za maafisa, askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma. Aidha, kwa kutumia fedha hizo majukumu yaliyotekelze wa ni pamoja na yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo na mazoezi ya kijeshi; Wizara kuititia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika shule na vyuo vya kijeshi ndani ya nchi. Mafunzo yametolewa katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi, Chuo cha Ukamanda na Unadhimu, Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi - TMA, Chuo cha Mafunzo Maalum ya Kijeshi - CTC Mapinga, Chuo cha Usalama na Utambuzi wa Kijeshi Tanzania, Shule ya Kijeshi ya Mafunzo ya Anga (*Military School of Information and Communication Technology*), Shule ya Mafunzo ya Awali - RTS, Shule na Vyuo vingine vya kijeshi. Pia wanajeshi wetu wamehudhuria kozi za kijeshi katika nchi mbalimbali zikiwemo Afrika ya Kusini, Bangladesh, Burundi, Canada, China, Ghana, Kenya, India, Jamaica, Nigeria, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Oman, Rwanda, Uingereza, Uganda, Urusi, Zambia, Zimbabwe, Ujerumani, Sri Lanka, Uhlanzi, Saudia Arabia na Ufaransa.

Mafunzo hayo yameliwezesha Jeshi kuongeza uwezo wake wa kiutendaji na utayari kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 Jeshi lilifanikiwa kufanya mazoezi mbalimbali ya Kitaifa na ya Kimataifa yafuatayo:-

(i) *Exercise ushirikiano imara; zoezi lilifanyika Mkoani Tanga kuanzia tarehe 5 hadi 21 Novemba, 2018, lengo kuu likiwa ni kuwajengea washiriki uwezo na uelewa unaofanana katika kupanga na kutekeleza majukumu yanayohusu operesheni za ulinzi wa amani, kupambana na ugaidi na uharamia pamoja na kukabiliana na hatari zinazotokana na maafa. Nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilishiriki isipokuwa Sudan ya Kusini.*

(ii) *Zoezi la utulivu wa Afrika IV, zoezi hili lilifanyika nchini Uganda kuanzia tarehe 27 Agosti hadi tarehe 3 Septemba, 2018 chini ya Umoja wa Afrika katika mpango maalum wa kujenga uwezo wa kuitikia kwa haraka majanga yanapotokea (*African Capacity for Immediate Response to Crisis*). Lengo kuu lilikuwa ni kuwaandaa maafisa, wanadhimu wa ngazi za kati na ngazi za chini kuwa tayari kufanya kazi maazimio mbalimbali ya Umoja wa Afrika katika kutuliza migogoro na kukabiliana na majanga yanapotokea kwa nchi wanachama.*

(iii) *Exercise UMODZI; zoezi hili liliendeshwa chini ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, lilifanyika nchini Malawi kuanzia tarehe 01 hadi tarehe 16 Oktoba, 2018 lengo kuu lilikuwa ni kuleta uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa maazimio mbalimbali kukabiliana na machafuko.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana; Jeshi la Kujenga Taifa limeendelea kutoa mafunzo kwa vijana wa kujitolea na wa mujibu wa sheria ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na kuwapa mafunzo ya stadi za kazi na stadi za maisha. Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 jumla ya vijana 19,895 wa mujibu wa sheria walipatiwa mafunzo kwenye kambi

mbalimbali za jeshi la kujenga Taifa nchini. Kati ya vijana waliopata mafunzo 13,308 ni wa kiume na 4,587 ni wa kike. Aidha, vijana wa kujitolea wapatao 21,966 wameendelea na mafunzo katika kambi mbalimbali nchini ambapo kati yao wanaume ni 15,507 na wa kike 6,459.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mafunzo ya Jeshi la Akiba; katika mwaka wa fedha wa 2018/19 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limetoa mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa wananchi katika ngazi ya awali. Jumla ya wananchi 23,255 wamepata mafunzo hayo katika mikoa yote ya Tanzania Bara kati yao waanchi 20,816 ni wa kiume na 2,439 ni wa kike. Idadi hiyo, ni sawa na asilimia 149 ya lengo lilokusudiwa la kutoa mafunzo kwa Wananchi 15,600 katika kipindi husika. Hili ni ongezeko la wahitimu 4,239 ukilinganisha na jumla ya Wananchi 19,016 waliopata mafunzo ya aina hiyo mwaka wa fedha wa 2017/18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa kiulinzi na kijeshi na nchi nyingine; ushirikiano kati ya Tanzania na nchi nyingine katika masuala ya kiulinzi na kijeshi umeendelea kuimarika; nchi yetu kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa, hususan katika *operation* ya ulinzi wa amani chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa ili kuleta amani usalama, utengamano kwenye nchi zenyenye migogoro na machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepeleka maafisa maaskari wa kulinda amani katika maeneo ya Darfur – Sudan, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Lebanon.

Pia kuna maafisa wanadhimu na makamanda wanaoshiriki kwenye *operations* za ulinzi wa amani katika nchi za Sudan, Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Mkutano wa Kimataifa wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wetu wanatekeleza majukumu yao kwa mafanikio makubwa pamoja na kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazojitokeza wakati wa ulinzi wa amani. Mnamo tarehe 12 Novemba, 2018 huku Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Brigedi Maalum inayoundwa na vikosi vya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika ikiwa katika *operation ilishambuliwa* na kundi la ADF katika maeneo ya Ngadi, Mangoko na Kashinga yaliyoko karibu na Mji wa Beni. Katika shambulio hilo askari watano waliuawa, mmoja akiwa Mtanzania na wanne wakiwa askari wa Malawi. Vilevile tarehe 10 Disemba, 2018 Kikundi cha Jeshi letu kikiwa katika doria karibu na eneo la Kiteule cha Simulike kilishambuliwa na waasi wa Kundu la ADF ambapo askari mmoja alipata majeraha. Pia kikosi chetu kikiwa katika jukumu la ulinzi wa amani huko Afrika ya Kati kilishambuliwa na waasi wa Kundu la Siriri ambapo askari wetu mmoja aliuawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2018/19 Serikali kupitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imekamilisha taratibu za kuridhia mkataba wa kimataifa wa kukataza utengenezaji, utumiaji, ulimbikizaji na usambazaji wa silaha za kibaiolojia na sumu kwa mwaka 1972. Mkataba huo umeridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 15 Novemba, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano wa jeshi na mamlaka za kiraia; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kusaidia mamlaka za kiraia wakati wa maafa. Hii ni pamoja na kushiriki katika uokoaji wa watu na mali zao katika Kivuko cha MV Nyerere kilichozama tarehe 20 Septemba, 2018 katika Wilaya ya Ukerewe, Mkoani Mwanza. Vilevile Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilisafirisha misaada ya kibinadamu tani 14 za mchele na tani 16 za dawa kwa walioathirika na Tufani Idai katika nchi za Msumbiji na Zimbabwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania inashiriki katika ujenzi wa *Standard Gauge Railway*, ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba – Dodoma,

vituo vya umahiri vya madini katika maeneo ya Dodoma, Bukoba, Musoma, Handeni, Songea, Bariadi na Mpanda. Aidha, JWTZ limeshiriki kikamilifu katika shughuli za usafirishaji na ulinzi wa korosho katika mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeshiriki katika kuhamisha Serikali kwa kusafirisha samani za ofisi na nyaraka kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Serikali kuhamia Makao Makuu ya nchi, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kuitia Shirika la Mzinga imeendelea kusimamia zana na silaha zinazomilikiwa na mashirika ya meli zinazofanya kazi nchini ili kuzuwia matumizi mabaya ya silaha. Jukumu hilo limekuwa likitekelezwa sambamba na utunzaji wa silaha zinazomilikiwa na meli kutoka nje ya nchi mara zinapotia nanga kwenye bandari yetu. Vilevile Shirika la Mzinga limeendelea kuagiza na kusambaza baruti zinazotumika katika ujenzi pamoja na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za afya na tiba; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa maafisa, askari, vijana wa JKT, watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla. Pamoja na upatikanaji wa huduma hizo kwa wanajeshi, takwimu hizi zinazonesha kuwa asilimia 50 ya wanaopata huduma katika hospitali zilizo chini ya jeshi ni raia. Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha huduma za afya ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali Kuu ya Jeshi – Lugalo, Hospitali za Kanda, Vituo vya Afya na Zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mionganoni mwa vifaa tiba vinavyonunuliwa ni pamoja na mashine za *Dialysis*, *CT Scan* na *Ultra Sound* ambazo zimefungwakatika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Vilevile ujenzi wa Hospitali ya Jeshi ya Kanda – Arusha umekamilika na hospitali hiyo iliyokabidhiwa kwa Serikali tarehe 06 Mei, 2019 na Serikali ya Ujerumanii

imewekewa vifaa vya kisasa vya matibabu. Aidha, vituo hivyo vya tiba vimeendelea kushiriki katika kampeni mbalimbali za afya nchini, pia Wizara imeendelea na utaratibu wa kuanzisha bima ya afya kwa wanajeshi, ili kuwezesha wanajeshi na familia zao kupata huduma bora na za uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi katika shughuli za maendeleo; katika mwaka wa fedha wa 2018/19 shughuli za maendeleo zilizoteklezwa ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha mtandao wa mawasiliano salama jeshini; Wizara imefanikiwa kupanua wigo wa mawasiliano salama jeshini kwa kuunganisha mawasiliano mtandao katika Mkoa wa Tanga. Kwa sasa mawasiliano yanapatikana katika maeneo ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tanga na Zanzibar. Wizara inaendelea na mpango wa kupeleka mawasiliano hayo katika mikoa iliyopo Kanda ya Kusini, Magharibi, Ziwa na Kaskazini. Vilevile Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati imekamilisha tathmini ya kufikisha miundombinu ya umeme kwenye kanda hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhibiti uvamizi wa maeneo ya jeshi, upimaji na ulipaji fidia; katika kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi Wizara kuititia vikosi, vyuo na shule za kijeshi imeendelea kupanda miti, kusimika nguzo na kuweka mabango ya ilani na kufanya doria za mara kwa mara kwenye mipaka ya vikosi. Aidha, Wizara imeweza kulipa sehemu ya gharama ya kununua eneo lilioko Kakonko kiasi cha shilingi milioni 550 na kulipia fidia eneo la Rasi Mshindo kiasi cha shilingi 3,500,697,801 ili kupisha maeneo hayo kwa ajili ya matumizi ya jeshi. Serikali inaendelea na uhakiki wa maeneo mbalimbali, ili kuweza kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha miundombinu ya kimkakati ya Jeshi; Serikali imeendelea kuliimarisha jeshi kwa kununua vifaa na zana za kijeshi, kuboresha ulinzi wa anga kwa kufanya ukarabati wa mfumo wa rada na ukarabati wa mahanga ya ndege. Vilevile Serikali imeweka mfumo wa ulinzi

kwenye miundombinu ya kimkakati ya jeshi na ununuzi wa vifaa vya mfumo wa malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwendelezo wa kutekeleza agizo la Serikali la kuhamia Dodoma, Wizara imekamilisha ujenzi wa ofisi zake katika Mji wa Serikali Mtumba. Vilevile Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaendelea na taratibu za ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Kikombo. Pia Jeshi la Kujenga Taifa limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa – Chamwino na linaendelea na ujenzi wa ofisi nydingine za idara mbalimbali. Aidha, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na ujenzi na ukarabati wa kambi mbalimbali zikiwemo Kibiti – Pwani, Makuyuni – Arusha, Mpwapwa na Makutupola – Dodoma, Itaka – Songwe, Milundikwa na Luwa – Rukwa, Bulombora – Kigoma, Mbweni – Dar es Salaam, Nachingwea – Lindi, Mafinga – Iringa na Maramba – Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yanayosimamiwa na Wizara; Shirika la Uzalishaji Mali la JKT; SUMA JKT limeendelea kutekeleza shughuli zake za kibiashara kupitia sekta ya kilimo na ufugaji, ujenzi kupitia kampuni yake tanzu ya ujenzi, viwanda kikiwemo Kiwanda cha Ushonaji, Kiwanda cha Kuchakata Nafaka kilichopo Mlale, Kiwanda cha Samani – Chang’ombe, Kiwanda cha Maji – Mgulani na Kiwanda cha Kuchakata Kokoto. Aidha, shirika linaendesha shughuli mbalimbali za kibiashara ambazo ni huduma ya ulinzi binafsi inayotolewa na Kampuni Tanzu ya Ulinzi - *SUMA JKT Guard*, uuzaaji na usambazaji wa matrekta na zana za kilimo, huduma za chakula na kumbi za mikutano na kampuni tanzu ya kukusanya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SUMA JKT Guard Limited* hutoa huduma ya ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa mwaka wa 2018/2019 kampuni imefanikiwa kuongeza huduma za ulinzi kwa taasisi za Serikali 27 na kampuni binafsi sita, hivyo, kwa sasa kampuni ina malindo 360 kwa taasisi za Serikali, kampuni binafsi na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii ya ulinzi imeendelea kutoa ajira na kuchangia kupunguza tatizo la ajira nchini, hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya vijana 8,528 wameajiriwa. Aidha, kampuni imefanikiwa kununua magari matano ya doria ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji kampuni imekusudia kuimarisha shughuli zake kwa kuendelea kununua vitendea kazi vipyta ikiwemo vifaa vya kupambana na moto na uokoaji, vifaa vya kuhakikisha usalama katika usafirishaji fedha na magari ya kusafirisha wagonjwa ili kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT kupitia Kampuni ya Ujenzi imekamilisha ujenzi wa ofisi za Wizara sita katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Wizara hizo ni Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Katiba na Sheria, Mifugo na Uvuuvi, Maliasili na Utalii na Kilimo na Maji. Vilevile linatekeleza ujenzi katika Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Chuo Kishiriki cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia linatekeleza ujenzi wa Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa, *Dealers House* na *One Stop Centre* katika mgodi wa *Tanzanite*, Mererani na vituo vya umahiri vya madini katika mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Dodoma, Simiyu, Kagera na Tanga. Aidha, SUMA JKT imehusika katika ujenzi wa Ofisi za Halmashauri za Wilaya ya Kahama, Mpanda, Songwe na Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda SUMA JKT limeendelea kuimarisha viwanda vyake vikiwemo Kiwanda cha Ushonaji – Mgulani ambacho kimeanza kushona sare za wanajeshi ili klupunguza gharama ya kuagiza sare hizo nje ya nchi kwa siku zijazo. Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi – Mlalakuwa ambacho huuza bidhaa zake kwa maafisa na maaskari wa JWTZ, walinzi wa *SUMA JKT Guard*, mgambo na kampuni binafsi za ulinzi. Kiwanda cha Samani – Chang’ombe ambacho hutengeneza samani za aina mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kimeuza bidhaa hizo kwa taasisi mbalimbali za Serikali, ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Bima Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mamlaka ya

Chakula na Dawa Tanzania Kanda ya Mbeya na kampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vingine ni Kiwanda cha Kuchakata Kokoto na Kiwanda cha Kuchakata Nafaka – Mlale, Songea ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani 20 za unga wa mahindi kwa siku na kimeanza kusambaza bidhaa zake kwenye Vikosi vya Jeshi na matarajio ni kusambaza katika maeneo mengine ya mkoa wa Ruvuma. Kiwanda hicho kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 8 Aprili, 2019. Vilevile SUMA JKT ina kiwanda cha kutengeneza maji ya kunywa yanayotambulika kwa jina la *Uhuru Peak* ambacho huzalisha lita 12,000 kwa siku na husambaza maji hayo katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT limeendelea kutekeleza miradi ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mbegu bora, ufugaji na uvuvi. Vilevile shirika linajihuisha na shughuli za ufugaji wa samaki katika mabwawa na vizimba katika Kambi ya Rwanakoma – Mara, ufugaji wa nyuki katika Vikosi vya Kanemba – Kigoma na Msange, Tabora. Pia mbegu bora za mpunga na mahindi huzalishwa katika vikosi vya Chita – Morogoro, Itende – Mbeya na Mlale – Ruvuma. Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 Shirika limefanikiwa kulima jumla ya ekari 4,779 ambapo ekari 2,779 ni za mahindi, ekari 1,500 za mpunga, ekari 500 za alizeti na ekari 200 za mbogamboga na matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki matrekta 100 yameingizwa nchini na shirika, ili kutekeleza azma ya matumizi ya zana za kisasa kwenye sekta ya kilimo, kati ya matrekta hayo 34 yameuzwa. Shirika linaendelea kuzifanyia kazi changamoto za urejeshaji wa madeni kwa wakati kutokana na wateja waliokopeshwa matrekta na zana. Hata hivyo hadi kufikia Machi, 2019 mradi ulikuwa unadai washitiri wake kiasi cha shilingi 35,294,530,089 ambayo sehemu kubwa yakiwa ni madeni ya awamu ya kwanza ya mradi. Jitihada za kukusanya madeni kutoka kwa washitiri wanaodaiwa wakiwemo vipngozи wa Serikali, Wabunge, watumishi wa

umma na watu binafsi zinaendelea kufanyika; katika kipindi cha Mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 madeni ya matrekta yenyе jumla ya shilingi 733,707,979 yalikusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mzinga; katika mwaka wa fedha 2018/2019 Shirika la Mzinga limeendelea kutekeleza shughuli za uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo ya msingi na ya kiraia. Shirika limefanya utafiti wa malighafi zinazopatikana hapa nchini ili zitumike katika uzalishaji wa mazao ya msingi. Vilevile shirika limefanya tafiti mbalimbali zikiwemo utafiti wa mashine inayotumia vumbi la mbaо kuzalisha mkaа, mashine ya kusindika uyoga, utafiti wa tela la kubeba abiria kwenye pikipiki, utafiti wa uzalishaji wa malighafi ya *Gilding Metal Clad Sheet* na *Brass Sheet*. Aidha, shirika limekarabati zana na vifaa vya kijeshi, pia limeendelea na utengenezaji wa samani za nyumbani na maofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Kampuni Tanzu ya Shirika la Mzinga (*Mzinga Holding*), shirika limeshiriki katika ujenzi wa ofisi za Wizara nne katika Mji wa Serikali, Mtumba – Dodoma. Wizara hizo ni Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu, Uwekezaji na Bunge, Wizara ya Madini, Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Vilevile Shirika la Mzinga limeendelea na ujenzi wa ukumbi wa mikutano pamoja na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Mji Mdogo Makambako – Njombe, ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo – Mbeya na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi – Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumbu linaendelea kutoa mchango wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa kushiriki katika maandalizi ya vifaa na zana za kijeshi kwa ajili ya vikosi vya ulinzi wa amani kwa kukarabati magari ya kivita, kutengeneza matela ya kubeba maji na mafuta, vitanda vya kulalia askari, mahema na majiko ya medani. Vilevile shirika limeshiriki katika matengenezo ya mashine na mitambo kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Ulinzi la

Wananchi wa Tanzania na kukarabati miundombinu ya taasisi mbalimbali za Serikali na utengenezaji wa vipuri vyatia aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha utafiti kuhusu utengenezaji wa gari la zimamoto na uokoaji na uzoefu waliouopata hapo awali katika utengenezaji wa magari ya zimamoto, shirika limeanza kazi ya kutengeneza magari hayo kwa ajili ya matumizi katika viwanja vyatia ndege na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha wa 2018/2019 shirika limeendelea kutekelza agizo la Serikali liliolitaka jeshi letu kuongoza katika uanzishwaji wa viwanda nchini. Katika kuhakikisha kuwa shirika linaendeleza kutekeleza majukumu ya msingi ya kuanzishwa kwake yameandalwa mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa miaka 10 yaani 2018/2019 hadi 2027/2028 wa kuliimarishe shirika, ili liweze kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini. Mpango huu uko katika hatua za kuridhiwa na Serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2018/2019 shirika limekarabati baadhi ya miundombinu ya majengo na mitambo iliyopo ili kuongeza ufanisi na kukuza uwezo wa uzalishaji. Vilevile limenunua mashine kwa ajili ya kiwanda kipyaa cha kutengeneza *air cleaners, oil/nna fuel filters* za magari. Pia shirika limefunga mashine ya kutengeneza misumari ya ukubwa mbalimbali na mashine ya kudarizi vyeo na nembo za kijeshi pamoja na ununuzi wa malighafi zake. Aidha, shirika limenunua mitambo mipya kwa ajili ya kuboresha karakana za kukereza, kukata, kuunga vyuma na usubiaji. Maboresho haya yataliingizia shirika mapato na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za utekelezaji wa mpango wa bajeti katika mwaka wa fedha wa 2018/2019; Wizara katika kutekeleza bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 imekutana na changamoto mbalimbali,

kubwa ikiwa ni ufinyu wa ukomo wa bajeti ambapo kiasi kilichoidhinishwa cha shilingi 1,910,722,891,000 hakikidhi mahitaji halisi. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa zimetumika kulipia mikataba michache ya ununuzi wa zana na utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo. Hali hii imesababisha Wizara kutoweza kutekeleza mipango yote iliyojiwekea katika mwaka wa fedha wa 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azma ya uimarishaji na uanzishaji wa viwanda vipyta jeshini; zipo changamoto za uchakavu wa miundombinu ya viwanda ikiwemo karakana, maabara, barabara, mitambo na majengo. Aidha, karakana nyingi zinatumia teknolojia zilizopitwa na wakati na kuna upungufu wa wataalam wa kuendesha mitambo hususan katika Mashirika ya Mzinga na Nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiriana na changamoto hizo, Wizara imekutana na wazabuni mbalimbali ili kuweka utaratibu wa kulipa madeni hayo. Vilevile Wizara imefanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la kupitia, kujadiliana na kukubaliana kuhusu utaratibu wa kulipa madeni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yaliyo chini ya Wizara yameandaa mipango ya maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu ili kutatua baadhi ya changamoto. Shirika la Nyumbu limeandaa mpango wa miaka kumi wa kuliimisha ambapo upo katika hatua ya kuridhiwa na Serikali. Shirika la Mzinga nalo limeandaa/limeendelea kutekeleza mpango mkakati wa miaka mitano yaani 2017/2018 hadi 2021/2022.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT linakabiriwa na changamoto ya washitiri kutolipia huduma kwa wakati na kuzalisha madeni kwa shirika ambayo yanakwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali na malengo ya shirika. Hivyo, SUMA JKT limeendelea na juhudi mbalimbali za kukusanya

madeni ikiwemo kwa kutumia kampuni ya ukusanyaji madeni na mnada ya SUMA JKT (*SUMA JKT Auction Mart*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020; mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika mwaka wa fedha 2019/2020 unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa jeshi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na dira na dhima. Hivyo Wizara imeadhimia kutekeleza majukumu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulipatia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajeshi ili kuliongezea uwezo na weledi wa kiutendaji kiulinzi na kivita, kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma, kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, umoja wa kitaifa, uzalendo na stadi za kazi, kuendeleza tafiti na uhaulishaji wa teknolojia kwa kuimarisha na kuanzisha viwanda kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia, kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, kikanda na nchi moja moja katika nyanja za kijeshi na kiulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufanya upimaji, uthamini na ulipaji fidia wa ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya jeshi, kuendelea kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura pale inapohitajika, kuendelea kuendesha mafunzo na mazoezi kwa Jeshi la Akiba, kuboresha mawasiliano salama jeshini kwa ajili ulinzi wa Taifa, kujenga maghala ya kuhifadhia silaha na zana za kijeshi, kulipa stahili mbalimbali za maafisa, askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma na kukamilisha Sera ya Ulinzi wa Taifa, mwongozo wa viwanda jeshini na mpango wa maendeleo wa miaka kumi wa kuliimarisha Shirika la Nyumbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani; napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu mbalimbali kwa

michango waliyoitoa katika kutayarisha makadirio haya. Nawashukuru Dkt. Florens Turuka - Katibu Mkuu, Jenerali Venance Mabeyo - Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Luteni Jenerali Yacoub Mohamed - Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Meja Jenerali Martin Busungu - Mkuu wa Jeshi la Kujenga la Taifa, Wakuu wa Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Matawi, Idara na Vitengo, Maafisa, Askari na watumishi wa umma kwa kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Bi. Immaculate Peter Ngwale, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye amestaafu utumishi wa umma kwa mujibu wa sheria. Kwa niaba ya Wizara tunamshukuru sana kwa kuitumikia Wizara kwa ufanisi na mafanikio, ni imani yetu kuwa ushirikiano huo tulloupata kutoka kwake ataendelea kuutoa huko alipo kwa maslahi ya Taifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ni matumaini yangu kuwa tutaaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Serikali napenda kuzishukuru Serikali za nchi mbalimbali, mashirika na wahisani kwa ushirikiano walioipatia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wahisani hao ni pamoja na Canada, China, India, Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uturuki.

Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladesh, Ghana, Indonesia, Israel, Jamaica, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Misri, Morocco, Nigeria, Oman, Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Sri Lanka, Uholanzi, Uingereza, Urusi na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020; makadirio ya mapato; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa linatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 81,104,000 kutoka katika mafungu yake matatu; ambapo Fungu 38 - Ngome linakadirisha kukusanya shilingi 20,001,000, Fungu 39 - JKT shilingi 59,903,000 na Fungu 57 - Wizara shilingi 1,200,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida na maendeleo; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 1,854,037,343,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo ili iweze kutekeleza majukumu yake katika mwakaa fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,726,037,343,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 128,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo kwa kila fungu ni kama ifuatavyo:- Fungu 38 – Ngome matumizi ya kawaida shilingi 1,406,726,908,000; matumizi ya maendeleo ni shilingi 6,000,000,000 jumla ni shilingi 1,412,726,908,000.

Fungu 39 – JKT matumizi ya kawaida 300,035,425,000; matumizi ya maendeleo shilingi 2,000,000,000, jumla shilingi 302,035,425,000.

Fungu 57 – Wizara, matumizi ya kawaida 19,275,010,000, matumizi ya maendeleo 120,000,000,000, jumla shilingi 139,275,010,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makof)*

HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. HUSSEIN ALI MWINYI (MB.),  
WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA AKIWASILISHA  
BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupidisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.
2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingu wa rehema, kwa kuendelea kutupa uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa Bungeni leo kujadili Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Aidha, nitumie fursa hii kwa moyo wa dhati kumshukuru **Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa kuendelea kuniamini kuiongoza Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Pia, ninawashukuru **Mhe. Samia Suluhu Hassan**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na **Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wao makini na maelekezo wanayoyatoa katika kufanikisha utendaji wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu ulinzi wa nchi yetu.
3. **Mheshimiwa Spika**, naomba pia kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza kwa weledi Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama inayoongozwa na **Mhe. Azzan Mussa Zungu (Mb.)**,

kwa ushauri na ushirikiano inayonipatia katika kusimamia utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kamati ilifanikiwa kutembelea baadhi ya miradi na kutoa ushauri kwa maeneo yenye changamoto ili ziweze kupatiwa ufumbuzi. Vile vile, Kamati ilitoa ushauri na maoni wakati ikichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, ambayo yamesaidia kwa kiasi kikubwa katika kuandaan Mpango na Bajeti hii ninayowasilisha hapa leo.

4. ***Mheshimiwa Spika***, naomba pia nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa katika chaguzi ndogo kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amba ni: Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara, Mbunge wa Jimbo la Ukonga; Mhe. Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Jimbo la Monduli; Mhe. Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Jimbo la Liwale; Mhe. Mhandisi Christopher Kajoro Chizza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu; Mhe. James Kinyasi Millya, Mbunge wa Jimbo la Simanjiro; Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe; Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti; Mhe. Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini; Mhe. Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Jimbo la Temeke; Mhe. Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini; na Mhe. Dkt. John Pallangyo, Mbunge Mteule wa Arumeru Mashariki.

5. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwapo- ngeza Mhe. Angellah Jasmine Kairuki (Mb.), Mhe. Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga (Mb.), Mhe. Prof. Palamagamba Aidan Kabudi (Mb.), Mhe. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Mhe Joseph George Kakunda (Mb.) na Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga (Mb.) kwa kuteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania kuwa Mawaziri kuongoza Wizara mbalimbali. Pia, nawapongeza Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb.), Mhe. Constantine John Kanyasu (Mb.), Mhe. Mwita Mwikabe Waitara (Mb.) na Mhe. Innocent Luga Bashungwa (Mb.) kwa kuteuliwa kuwa Naibu Mawaziri katika Wizara mbalimbali.

Sambamba na pungezi hizi, nawatakia kila la heri katika utekelezaji wa majukumu muhimu ya kuwatumikia Watanzania na Taifa kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika**, naomba kuungana na wenzangu kutoa salamu za pole kwako, Bunge lako Tukufu, familia na wananchi wote wa Jimbo la Korogwe Vijijini, kwa kuondokewa na mpendwa wetu **Mhe. Stephen Hilary Ngonyani**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini kupitia Chama cha Mapinduzi.

7. **Mheshimiwa Spika**, vile vile, natoa pole kwa wananchi waliopatwa na majanga, pamoja na kufikwa na misiba ya ndugu, jamaa na marafiki kutokana na matukio mbalimbali ya ajali ikiwemo ya kuzama kwa kivuko cha MV. Nyerere katika Ziwa Victoria Wilayani Ukerewe tarehe 20 Septemba, 2018 ambapo wananchi wapatao **224** walipoteza maisha. Pia, natoa pole kwa Mhe. William Vangimembe Lukuvi (Mb.), Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Watumishi **12** waliofariki kwa ajali ya gari Mkoani Morogoro. Aidha, natoa pole kwa Mhe. Japhet Ngailonga Asunga (Mb.), Waziri wa Kilimo kwa watumishi **5** waliofariki mkoani Singida, ambapo wote kwa ujumla walikuwa wakitekeleza majukumu ya ujenzi wa Taifa.

8. **Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee natoa pole kwa Mheshimiwa Rais na Amiri Jeshi Mkuu, Mkuu wa Majeshi, Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma na familia za Wanajeshi waliopoteza maisha wakitekeleza jukumu la Ulinzi wa Amani. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2019 Wanajeshi **watano (5)** walipoteza maisha; **wawili (2)** katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na **watatu (3)** Jamhuri ya Afrika ya Kati. Naziombea roho za marehemu wote zipumzike mahali pema peponi.

## **DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA**

9. **Mheshimiwa Spika**, Dira ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni kuendelea kuwa Taasisi iliyotukuka ya kulinda na kudumisha Amani na Usalama wa Taifa letu. Vile vile, **Dhima** ya Wizara ni kuendelea kulinda Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania dhidi ya adui wa aina ye yote kutoka ndani na nje ya nchi na kuhakikisha kuwa Mamlaka na Maslahi ya Taifa yanakuwa salama.

**10. *Mheshimiwa Spika***, katika kufanikisha **Dira** na **Dhima**, Malengo Makuu ya Wizara yameendelea kuwa yafuatayo:

- (a) Kuwa na Jeshi dogo lenye wataalam, zana na vifaa vya kisasa;
- (b) Kuendelea kuwajengnea vijana wa Kitanzania ukakamavu, maadili mema, utaifa, moyo wa uzalendo, na uwezo wa kujitegemea;
- (c) Kujenga uwezo katika tafiti mbalimbali za uhawilishaji wa teknolojia kwa matumizi ya kijeshi na kiraia;
- (d) Kuwa na Jeshi imara la akiba;
- (e) Kusaidia mamlaka za kiraia katika kukabiliana na athari za majanga na matukio yanayoweza kuhatarisha maslahi ya Taifa, maisha, amani na utulivu nchini; na
- (f) Kudumisha amani na usalama kwa kushirikiana na nchi nyingine duniani.

#### **UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BUNGE NA USHAURI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA**

**11. *Mheshimiwa Spika***, wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilipokaa na kujadili Makadirio ya Mapato, Mpango na Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ilitoa maoni na ushauri kwa Wizara yaliyokusudia kuboresha utendaji na utekelezaji wa majukumu yake.

**12. *Mheshimiwa Spika***, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, maoni, ushauri na maazimio yaliyotolewa yaliifanyiwa kazi na Wizara na taarifa yake iliwasilishwa kwa Kamati tarehe 28 Machi, 2019. Aidha, Wizara imezingatia hoja mbalimbali

zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati wakati wa mjadala katika kuandaa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 ninayowasilisha leo hapa Bungeni.

**UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI YA MWAKA 2015-2020 NA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17 – 2020/21)**

13. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015-2020 sambamba na Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na utekelezaji wa majukumu mengine ya Wizara. Maelekezo ya Ilani kwa Wizara yameainishwa kwenye Ibara ya 146, ambayo ni:

- (a) Kuviwezesha Vyombo vya Ulinzi na Usalama kwa kuviongezea rasilimali watu na fedha;
- (b) Kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya Ulinzi na Usalama; liwezesha Jeshi la Kujenga Taifa kuimarisha mafunzo kwa vijana wanaojiunga kwa hiari na wale wanaojiunga kwa Mujibu wa Sheria;
- (d) Kushirikiana na Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Afrika (AU) katika shughuli za Ulinzi wa Amani kwenye nchi mbalimbali duniani, ili majeshi yetu yaendelee kupata uzoefu na mbinu za kisasa za Ulinzi wa Amani; na
- (e) Kushirikiana na Mataifa mengine na Asasi za Kimataifa katika kupambana na uhalifu unaovuka mipaka hasa ugaidi, uharamia, utakatishaji wa fedha, biashara haramu ya madawa ya kulevyta na usafirishaji haramu wa binadamu.

14. *Mheshimiwa Spika*, napenda kularifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeendelea kutekeleza Ilani kwa ufanisi. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi yameainishwa katika **Kiambatisho Na. 1.**

## **HALI YA ULINZI NA USALAMA WA MIPAKA YA NCHI**

### **(a) Hali ya Usalama wa Mipaka**

15. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama wa mipaka yetu kwa ujumla imeendelea kuwa shwari. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 hakuna matukio ya kuhatarisha usalama wa nchi yалиорипотиwa baina ya nchi yetu na nchi tunazopakana nazo. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) limeendelea kutekeleza majukumu yake ya ulinzi wa mipaka kwa weledi na umakini ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa salama. Hata hivyo, zipo baadhi ya changamoto kwenye maeneo mbalimbali ya mipaka zinazohitaji kushughulikiwa ili kuboresha udhibiti wa mipaka na kuimarisha usalama wa nchi yetu.

16. ***Mheshimiwa Spika***, mionganoni mwa changamoto hizo ni uharibifu wa alama za mipaka ya nchi. Aidha, kuendelea kuwepo kwa migogoro na viashiria vya machafuko ya ndani katika baadhi ya nchi tunazopakana nazo, imekuwa sababu mojawapo inayochangia wakimbizi na wahalifu kuingia nchini. Changamoto nyingine ni wafugaji kutoka baadhi ya nchi tunazopakana nazo kuendelea kuingiza mifugo nchini kwa kisingizio cha kutafuta malisho na maji. Vilevile, nchi yetu imeendelea kukumbwa na tatizo la usafirishajji haramu wa binadamu na wahamiaji haramu kutoka nchi mbalimbali. Baadhi ya wahamiaji haramu wamekuwa wakijihuisha na uhalifu.

17. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali yetu kwa pamoja na nchi husika zimeendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo. Mathalan, katika Mpaka wa Kaskazini tunakopakana na nchi za Kenya na Uganda, Serikali kuititia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, imeendelea na mazungumzo na nchi tunazopakana nazo ili kutatua changamoto za wafugaji haramu wanaotafuta malisho na maji, wahamiaji haramu, uwekaji wa alama za mipaka (boundary pillars) zilizoharibiwa na uwekaji wa alama mpya za mipaka katika

maeneo yanayohitaji kuwekwa alama hizo ili kuimarisha ulinzi wa mpaka wetu wenye urefu wa Kilomita **5,401**.

### ***Mpaka wa Mashariki***

**18. Mheshimiwa Spika**, Mpaka wa Mashariki una urefu wa Kilomita **1,424** ambapo Tanzania inapakana na Bahari ya Hindi. Hali ya usalama katika mpaka huu ni shwari. Changamoto zilizopo ni pamoja na; uvuvi haramu katika Bahari ya Hindi, biashara za magendo na kutumika kama mapitio ya wahamiaji haramu, usafirishaji wa madawa ya kulevyia na usafirishaji haramu wa binadamu. Hata hivyo, matukio hayo yameendelea kupungua. Kuanzia Julai, 2018 hadi Aprili, 2019 hakuna tukio la kihalifililioripotiwa. Hali hii imetokana na kufanyika kwa doria za pamoja katika Eneo Tengefu la Kiuchumi (Exclusive Economic Zone – EEZ) kati ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na taasisi nyingine za Serikali.

### ***Mpaka wa Kaskazini***

**19. Mheshimiwa Spika**, mpaka huu una urefu wa kilomita **1,221** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Kenya na Uganda. Hali ya usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Hata hivyo, katika eneo la mpaka huu kuna changamoto ya kuingizwa mifugo kutoka nchi jirani kwa ajili ya kutafuta malisho na maji bila kufuata sheria na taratibu. Aidha, yapo matukio ya wafanyakibashara wanaojihuisha na biashara za magendo mpakani. Mikutano ya pamoja baina ya nchi za Tanzania na Uganda inaendelea kufanyika ili kutatua changamoto hizi.

**20. Mheshimiwa Spika**, Katika mpaka wa Tanzania na Kenya, changamoto kubwa iliyoponi uwazi wa mpaka (porous border) kwenye Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Tanga unaotoa mwanya kwa wahalifu kuingia nchini na kuhatarisha usalama wa nchi. Pia, mpaka huu umeendelea kukabiliwa na changamoto ya usafirishaji haramu wa binadamu kuingia Tanzania kutoka nchi za Eritrea, Ethiopia na Somalia.

21. **Mheshimiwa Spika**, katika eneo la Ziwa Victoria kumekuwa na vitendo vya kihalifu vinavyotishia usalama wa Watanzania wanaofanya shughuli za uvuvi. Hata hivyo, vitendo hivyo vimeendelea kudhibitiwa kwa kutumia Kiteule cha Jeshi la Wanamaji Musoma Mkoani Mara na kuanzisha kingine kipyta katika Kisiwa cha Magafu Mkoani Geita.

***Mpaka wa Magharibi***

22. **Mheshimiwa Spika**, mpaka huu una urefu wa kilomita **1,220** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Burundi, Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Hali ya ulinzi na usalama katika mpaka huu ni shwari. Changamoto katika mpaka huu ni eneo la Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kuendelea kukumbwa na matukio ya uvunjifu wa amani kutokana na mapigano na mauaji. Kundila Waasi la *Allied Democratic Forces* (ADF), limeendelea kufanya mashambulizi dhidi ya Burugedi Maalum (Force Intervention Brigade – FIB), inayoundwa na vikosi vya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, katika eneo la Mji wa Beni.

23. **Mheshimiwa Spika**, katika mpaka wa Tanzania, Burundi na Rwanda hali ya usalama ni shwari na imeendelea kuwa ya kuridhisha na hakuna taarifa za matukio dhahiri ya kuhatarisha usalama wa nchi yetu.

***Mpaka wa Kusini***

24. **Mheshimiwa Spika**, mpaka huu una urefu wa kilomita **1,536** ambapo Tanzania inapakana na nchi za Msambilji, Malawi na Zambia. Hali ya ulinzi na usalama katika mpaka huu kwa ujumla ni shwari. Changamoto zilizopo ni pamoja na maeneo mengine ya mpaka kuwa wazi, ujenzi holela wa makazi na kuwepo kwa matukio ya uhalifu yenye mwelekeo wa kigaidi hususan Kaskazini mwa Msambilji. Kundi la kigaidi la *Al Sunnah wal Jamaah*, linaendelea kufanya uhalifu nchini Msambilji katika Wilaya ya Nangane, Jimbo la Cabo Delgado. Vikao baina ya Mawaziri wa Ulinzi wa nchi ya Tanzania na Msambilji vimeendelea kufanya ikiwa ni juhudhi na mwendelezo wa ushirikiano katika kupambana na vitendo hivyo viovu.

25. ***Mheshimiwa Spika***, hali ya usalama wa mpaka wa Tanzania na Malawi imeendelea kuwa shwari na hakuna tishio la wazi dhidi ya nchi yetu. Changamoto ya mpaka katika Ziwa Nyasa linaendelea kufanyiwa kazi. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Nje, na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inaendelea kutumia njia za kidiplomasia ili kulipatia suala hili ufumbuzi wa kudumu. Pamoja na hali hiyo, wananchi wa pande zote mbili wanaendelea na shughuli zao bila bugudha yoyote. Vile vile, kwa upande wa mpaka wa Tanzania na Zambia kwa ujumla hali ni shwari, ingawa tatizo la ujenzi holela wa makazi umeendelea kulikabili eneo hilo.

**(b) Tishio la Ugaidi**

26. ***Mheshimiwa Spika***, ugaidi wa kima-taifa umeendelea kuwa tishio la usalama duniani. Kuendelea kuwepo kwa makundi ya *Al-Shabaab*, *Al-Qaeda*, *Boko Haram* na *Islamic State* kunafanya matishio ya ugaidi kusambaa kila kona ya Dunia. Vitendo vya kigaidi vinavyofanywa na kundi la *Al Sunnah wal Jamaah* katika Jimbo la Cabo Delgado Kaskazini mwa Msumbiji, vinaweza kuhatarisha usalama katika maeneo ya Kusini mwa nchi yetu. Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kwa kushirikiana na Vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama limeendelea kufuatilia viashiria na matishio ya kigaidi yanayoweza kutokea hapa nchini.

27. ***Mheshimiwa Spika***, kuwepo kwa kundi la *Al-Shabaab* ambalo limeendelea kufanya mashambulizi katika nchi jirani ya Kenya ni changamoto kwa Tanzania. Hata hivyo, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama vinaendelea kuhakikisha kuwa Tanzania inakuwa salama. Vilevile, wito wangu kwa Watanzania ni kuendelea kutoa taarifa kwa Vyombo vya Ulinzi na Usalama mara wanapobaini watu ambao mienendo yao ni ya mashaka.

**UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA  
2018/2019**

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli**

28. ***Mheshimiwa Spika***, Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara

ilikadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 75,420,100.00** kutoka katika mafungu yake matatu ya Fungu 38-NGOME **Shilingi 17,317,100.00**, Fungu 39-JKT **Shilingi 56,903,000.00** na Fungu 57-Wizara **Shilingi 1,200,000.00**.

29. **Mheshimiwa Spika**, kufikia Mwezi Machi, 2019 mafungu hayo yalifanikiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 66,469,557.00** sawa na **asilimia 88.13** ya makadirio. Fungu 38 - NGOME, lilikusanya jumla ya **Shilingi 22,719,557.00** kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na kamisheni ya Uwakala wa Bima unaofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. Fungu 39 - JKT lilikusanya **Shilingi 42,750,000.00** kutokana na uuzaaji wa nyaraka za zabuni, mazao ya bustani (mboga mboga na matunda), mazao ya mifugo na mazao ya shamba. Fungu 57 - Wizara, lilikusanya kiasi cha **Shilingi 1,000,000.00** ambazo zimetokana na kodi ya pango la Kantini.

#### **Matumizi ya Kawaida**

30. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa iliidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 1,910,722,891,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu yake matatu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,676,722,891,000.00** nikwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 234,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa bajeti kwa kila fungu umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 2**.

31. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi kufikia mwezi Aprili, 2019 fedha iliyopokelewa ilikuwa ni **Shilingi 1,610,411,417,602.20** sawa na **asilimia 84.28** ya bajeti. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,446,309,579,339.62** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 164,101,838,262.58** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kiasi kilichopokelewa hadi mwezi Aprili, 2019 umeainishwa katika **Kiambatisho Na. 3**.

32. **Mheshimiwa Spika**, fedha za matumizi y a kawaida kiasi cha **Shilingi 1,313,755,685,669.62** zimetumika

kulipa mishahara na posho mbalimbali kwa Maafisa, Askari, Vijana wa Mujibu wa Sheria na wa Kujitolea. Vilevile, fedha hizo zimetumika katika shughuli za kijeshi na kiulinzi katika nchi za Kikanda yakiwemo mazoezi, mafunzo na operesheni za kijeshi. Aidha, sehemu ya fedha hizo zimetumika kugharamia huduma ya afya kwa wanajeshi, kulipa sehemu ya madeni ya wazabuni wanaotoa huduma na kuhamisha Wanajeshi na watumishi wa Umma kwenda Dodoma, usafirishaji na uhifadhi wa korosho na uendeshaji wa ofisi.

**33. *Mheshimiwa Spika*, jumla ya Shilingi 164,101,838,262.58** zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo kupitia mafungu yake matatu. Fedha hizo zimetumika kulipia ununuzi wa zana na vifaa vya kijeshi, uwekaji wa umeme kwenye minara ya mawasiliano salama Jeshini na kulipia mifumo na ujenzi wa miundombinu ya maji safi na maji taka. Fedha hizo pia zimetumika kununua ardhi kwa ajili ya matumizi ya kimkakati ya Jeshi katika maeneo ya Kakonko (Kigoma) na kulipia fidia katika eneo la Ras Mishindo (Lindi); kuboresha mfumo wa ulinzi wa anga, kukamilisha ujenzi na ukarabati wa mahanga ya Askari na vijana, ujenzi wa jengo la utawala Kambi mpya ya JKT Kibiti (Pwani) na ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa, Ofisi za Wizara Mtumba na Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (Dodoma). Vilevile, fedha hizo zimetumika katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule na vyuo vya kijeshi. Aidha, fedha hizo zimetumika kununulia malighafi kwa ajili ya kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi katika Shirika la MZINGA pamoja na kuendeleza shughuli za utafiti na uhawilishaji wa teknolojia katika Shirika la NYUMBU.

#### **MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

##### **Matumizi katika Shughuli za Kawaida**

**34. *Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara imefanikiwa kulipa mahitaji na huduma muhimu ikiwemo mishahara na posho kwa Maafisa, Askari, Vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na Watumishi wa

Umma. Aidha, kwa kutumia fedha hizo majukumu yaliyotekelawa ni pamoja na:

***Mafunzo na Mazoezi ya Kijeshi***

35. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara, kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, imeendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika shule na vyuo vya kijeshi ndani ya nchi. Mafunzo yametolewa katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Chuo cha Ukamanda na Unadhimu (CSC-Duluti), Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi (TMA), Chuo cha Mafunzo Maalum ya Kijeshi (CTC – Mapinga), Chuo cha Usalama na Utambuzi cha Kijeshi Tanzania (TDIC), Shule ya Kijeshi ya Mafunzo ya Anga (SKUA), *Military School of Informationand Communication Technology* (MSICT), Shule za Mafunzo ya Awali (RTS – Kihangaiko), shule na vyuo vingine vya Kijeshi. Pia, Wanajeshi wetu wamehudhuria kozi za kijeshi katika nchi mbalimbali ziklwemo; Afrika Kusini, Bangladesh, Burundi, Canada, China, Ghana, Kenya, India, Jamaica, Nigeria, Marekani, Misri, Morocco, Msumbiji, Oman, Rwanda, Uingereza, Uganda, Urusi, Zambia na Zimbabwe, Ujeruman, Sri Lanka, The Netherlands, Saudi Arabia na Ufaransa. Mafunzo hayo yameliwezesha Jeshi kuongeza uwezo wake wa kiutendaji na utayari kivita.

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/2019, Jeshi liliyanikiwa kufanya mazoezi mbalimbali ya kitaifa na ya kimatalifa yafuatayo:

(i) ***Ex-Ushirikiano Imara (FTX-2018)***: zoezi liliifanyika Mkoani Tanga kuanzia tarehe 5 hadi 21 Novemba, 2018. Lengo kuu likiwa ni kuwajenyea washiriki uwezo na uelewa unaofanana katika kupanga na kutekeleza majukumu yanayohusu operesheni za ulinzi wa amani, kupambana na ugaidi na uharamia pamoja na kukabiliana na hatari zinazotokana na Maafa. Nchi zote za Jumuiya ya Afrika Mashariki zilishiriki isipokuwa Sudan Kusini.

(ii) ***Utulivu Afrika IV (CPX - 2018)***: zoezi hili liliifanyika nchini Uganda kuanzia tarehe 27 Agosti hadi 03 Septemba, 2018, chini ya Umoja wa Afrika katika Mpango Maalum wa

Kujenga Uwezo wa Kuitikia kwa Haraka Majanga yanapotokea (**African Capacity for Immediate Response to Crises - ACIRC**). Lengo kuu likiwa ni kuwaandaa Maafisa Wanadhimu wa ngazi za kati na ngazi za chini kuwa tayari kufanya kazi maazimio mbalimbali ya Umoja wa Afrika katika kutuliza migogoro na kukabiliiana na majanga yanapotokea kwa nchi wanachama.

(iii) **Ex - UMODZI (CPX)**: zoezi hili lililoendeshwac h i n i ya Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika lilifanyika nchini Malawi kuanzia tarehe 01 hadi 16 Oktoba, 2018. Lengo kuu likiwa ni kuleta uelewa wa pamoja katika utekelezaji wa maazimio mbalimbali ya kukabiliiana na machafuko.

#### *Mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa Vijana*

37. **Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) limeendelea kutoa mafunzo kwa vijana wa Kujitolea na wa Mujibu wa Sheria ili kuwajengea ukakamavu, uzalendo, umoja wa kitaifa na kuwapa mafunzo ya stadi za kazi na stadi za maisha. Katika mwaka 2018/2019 jumla ya vijana **19,895** wa Mujibu wa Sheria walipatiwa mafunzo kwenye kambi mbalimbali za Jeshi la Kujenga Taifa nchini. Kati ya vijana waliopata mafunzo **15,308** ni wa kiume na **4,587** ni wa kike. Aidha, vijana wa kujitolea wapatao **21,966** wameendelea na mafunzo katika kambi mbalimbali nchini ambapo kati yao wa kiume **15,507** na wa kike **6,459**.

#### *Mafunzo ya Jeshi la Akiba*

38. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limetoa mafunzo ya Jeshi la Akiba kwa Wananchi katika ngazi ya awali. Jumla ya Wananchi **23,255** wamepata mafunzo hayo katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Kati yao, Wananchi **20,816** ni wa kiume na **2,439** ni wa kike. Idadi hiyo ni sawa na **asilimia 149** ya lengo lilitokusudiwa la kutoa mafunzo kwa Wananchi **15,600** katika kipindi husika. Hili ni ongezeko la wahitimu **4,239** ukilinganisha na jumla ya Wananchi **19,016** waliopata mafunzo ya aina hiyo mwaka 2017/2018.

***Ushirikiano wa Kiulinzi na Kijeshi na Nchi Nyingine***

39. ***Mheshimiwa Spika***, ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi nyingine katika masuala ya kiulinzi na kijeshi umeendelea kuimarika. Nchi yetu kuptitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania imeendelea kushirikiana na Jumuiya za Kikanda na za Kimataifa, hususan katika Operesheni za Ulinzi wa Amani chini ya Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa, ili kuleta Amani, usalama na utengamano kwenye nchi zenyenye migogoro na machafuko. Serikali imepeleka Maafisa na Askari wa kulinda amani katika maeneo ya Darfur – Sudan, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Lebanon. Pia, kuna Maafisa Wanadhimu na Makamanda wanaoshiriki kwenye Operesheni za ulinzi wa amani katika nchi za Sudan, Sudan Kusini, Lebanon, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika, Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Mkutano wa Kimataifa wa Nchi za Ukanda wa Maziwa Makuu (International Conference on Great Lakes Region - ICGLR).

40. ***Mheshimiwa Spika***, Wanajeshi wetu wanatekeleza majukumu yao kwa mafanikio makubwa pamoja na kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazojitokeza wakati wa Ulinzi wa Amani. Mnamo tarehe 12 Novemba, 2018 huko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Burugedi Maalum (Force Intervention Brigade) inayoundwa na vikosi vya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ikiwa katika Operesheni, ilishambuliwa na Kundi la ADF katika maeneo ya Ngadi, Mangoko na Kasinga yaliyopo karibu na Mji wa Beni. Katika shambulio hilo, Askari **watano (5)** waliuawa, mmoja akiwa Mtanzania na **wanne (4)** wakiwa Askari wa Malawi. Vilevile, tarehe 10 Desemba, 2018 Kikundi cha Jeshi letu kikiwa katika doria karibu na eneo la Kiteule cha Simulike, kilishambuliwa na waasi wa kundi la ADF ambapo askari mmoja alipata majeraha. Pia, Kikosi chetu kikiwa katika jukumu la Ulinzi wa Amani huko Jamhuri ya Afrika ya Kati kilishambuliwa na waasi wa Kundi la Siriri ambapo Askari wetu mmoja aliuawa.

41. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Serikali kuptitia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa

imekamilisha taratibu za kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kukataza Utengenezaji, Utumiaji, Ulimbikizaji na Usambazaji wa Silaha za Kibaiolojia na Sumu wa mwaka 1972. Mkataba huu umeridhiwa na Bunge lako Tukufu tarehe 15 Novemba, 2018.

### *Kiraia*

**42. *Mheshimiwa Spika*,** katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeendelea kushiriki katika shughuli mbalimbali za kusaidia Mamlaka za Kiraia wakati wa maafa. Hii ni pamoja na kushiriki katika uokoaji wa watu na mali zao katika kivuko cha MV Nyerere Kilichozama tarehe 20 Septemba, 2018 katika Wilaya ya Ukerewe Mkoani, Mwanza. Vile vile, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lilisafirisha misaada ya kibinadamu **Tani 14** za mchele na **Tani 16** za dawa kwa walioathirika na **Tufani Idai** katika nchi za Msumbiji na Zimbabwe.

**43. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, inashiriki katika ujenzi wa *Standard Gauge Railway*, ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba (Dodoma), Vituo vyta Umahiri vya Madini katika maeneo ya Dodoma, Bukoba, Musoma, Handeni, Songea, Bariadi na Mpanda. Aidha, JWTZ limeshiriki kikamilifu katika shughuli za usafirishaji na ulinzi wa korosho katika Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma na Pwani.

**44. *Mheshimiwa Spika*,** Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, limeshiriki katika kuhamisha Serikali kwa kusafirisha samani za ofisi na nyaraka kutoka Dar es Salaam kwenda la kuhamia Makao Makuu ya Nchi Dodoma.

**45. *Mheshimiwa Spika*,** Wizara, kupitia Shirika la Mzinga, imeendelea kusimamia zana na silaha zinazomilikiwa na mashirika ya meli zinazofanya kazi nchini ili kuzuia matumizi mabaya ya silaha. Jukumu hilo limekuwa likitekelezwa sambamba na utunzaji wa silaha zinazomilikiwa na meli kutoka nje ya nchi mara zinapotia nanga kwenye bandari zetu. Vilevile, Shirika la MZINGA limeendelea kuagiza na kusambaza baruti zinazotumika katika ujenzi

pamoja na uchimbaji wa madini.

### ***Huduma za Afya na Tiba***

**46. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutoa huduma za matibabu kwa Maafisa, Askari, Vijana wa JKT, Watumishi wa Umma na wananchi kwa ujumla. Pamoja na upatikanaji wa huduma hizo kwa Wanajeshi, takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 50 ya wanaopata huduma katika hospitali zilizo chini ya Jeshi ni raia.

**47. *Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kuboresha huduma za afya, ikiwa ni pamoja na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kwa ajili ya Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo, Hospitali za Kanda, Vituo vya Afya na Zahanati. Miongoni mwa vifaa tiba vilivyonunuliwa ni pamoja na mashine za *Dialysis, CT Scan na Ultra Sound* ambazo zimefungwa katika Hospitali Kuu ya Jeshi Lugalo. Vile vile, ujenzi wa Hospitali ya Jeshi ya Kanda Arusha umekamilika na Hospitali hiyo iliyokabidhiwa kwa serikali tarehe 6 Mei, 2019 na serikali ya Ujerumani imewekewa vifaa vya kisasa sana vya matibabu. Aidha, vituo hivyo vya tiba vimeendelea kushiriki katika kampeni mbalimbali za afya nchini. Pia, Wizara inaendelea na utaratibu wa kuanzisha Bima ya Afya kwa Wanajeshi ili kuwezesha wanajeshi na familia zao kupata huduma bora na za uhakika.

### ***Mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza***

**48. *Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza na kusimamia mikakati ya kupambana na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, kwa kutoa elimu ya jinsi ya kujikinga ili kuzuia maambukizi mapya na kupunguza vifo vitokanavyo na UKIMWI. Wizara imekuwa ikihimiza upimaji wa hiyari kwa Maafisa, Askari, Watumishi wa Umma na Vijana wa JKT. Aidha, kwa wale ambao wamethhibitika kuwa wameambukizwa Virusi vya UKIMWI wamekuwa wakipatiwa dawa za kufubaza Virusi, katika Vituo vya Huduma na Matibabu vilivyo katika Hospitali Kuu za

Kanda. Pia, Vituo hivyo hutoa huduma kwa wananchi wengine wanaoishi maeneo yaliyo karibu.

**49. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza maagizo ya **Mhe. Samia Suluhi Hassan, Makamu wa Rais**, kuhusu ushiriki wa Watumishi wa Umma katika mazoezi, Wizara imekuwa ikishiriki katika bonanza za michezo mbalimbali zinazoandaliwa na Wizara na Taasisi nyingine ili kujenga afya na kinga ya mwili. Aidha, upimaji wa hiari wa magonjwa yasiyoambukiza ikiwemo Kisukari na Shinikizo la Damu kwa Watumishi wa Umma umeendelea kufanyika, ambapo mwezi Februari, 2019 watumishi wa Wizara waliopo Dodoma walipima afya zao kwa hiari.

#### *Utawala Bora*

**50. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutekeleza kwa vitendo dhana ya utawala bora, kwa kuweka mifumo ya upimaji matokeo ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara, kuhakikisha Kamati ya Bajeti na Kamati ya Ukaguzi ya Wizara zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria. Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma wameendelea kuhimizwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya utendaji kazi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku. Katika utekelezaji wa dhana ya ushirikishwaji, mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi ilifanyika na kujadili masuala muhimu ya Kiutendaji, Kiutumishi, Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

#### *Utunzaji wa Mazingira*

**51. Mheshimiwa Spika**, katika kushiriki utunzaji wa mazingira, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea kutunza mazingira katika maeneo yanayozunguka Vikosi vya Jeshi kwa kupanda miti katika maeneo yake ikiwemo eneo la Wizara Mtumba, Dodoma ambapo miti 400 imepandwa. Zoezi hili limekuwa likiendelea katika vikosi mbalimbali vya Jeshi.

**52. Mheshimiwa Spika**, Wizara kupitia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa imeanza

kutumia gesi ya kupikia ikiwa ni nishati mbadala katika baadhi ya kambi na itaendelea kutumia nishati hiyo katika kambi nyingine. Vile vile, kufuatia mafanikio yaliyopatikana kutokana na uhawilishaji wa teknolojia uliofanywa na Shirika la NYUMBU wa kutengeneza *mobile field kitchens* ambayo hutumika na vikosi vyetu wakati wa ulinzi wa amani katika nchi mbalimbali, hivi sasa Jeshi limeanza kutumia majiko hayo wakati wa mazoezi ya medani ili kulinda na kuhifadhi mazingira. Pia, Shirika limetengeneza mashine za kutengeneza mkaa kwa ajili ya matumizi ya majumbani kwa kutumia vumbi linalotokana na makaa ya mawe zenye uwezo wa kuzalisha **tani 2** kwa saa.

### **Matumizi katika shughuli za Maendeleo**

53. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018 / 2019, shughuli za maendeleo zillizoteklezwa ni zifuatazo:

#### ***Kuimarisha Mtando wa Mawasiliano Salama Jeshini***

54. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imefanikiwa kupanua wigo wa mawasiliano salama Jeshini kwa kuunganisha mawasiliano ya mtando katika mkoa wa Tanga. Kwa sasa mawasiliano yanapatikana katika maeneo ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tanga na Zanzibar. Wizara inaendelea na mpango wa kupeleka mawasiliano hayo katika Mikoa iliyopo Kanda ya Kusini, Magharibi, Ziwa na Kaskazini. Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati imekamilisha tathmini ya kufikisha miundombinu ya umeme kwenye kanda hizo.

#### ***Kudhibiti Uvamizi wa Maeneo ya Jeshi, Upimaji na Ulipaji Fidia***

55. **Mheshimiwa Spika**, katika kudhibiti uvamizi wa maeneo ya Jeshi, Wizara kupitia vikosi, vyuo na shule za kijeshi, imeendelea kupanda miti, kusimika nguzo, kuweka mabango ya ilani na kufanya doria za mara kwa mara kwenye mipaka ya vikosi. Aidha, Wizara imeweza kulipa sehemu ya gharama ya kununua eneo lilitopo Kakonko (Kigoma) kiasi cha **Shilingi 550,000,000.00** na kulipia fidia eneo

la Ras Mishindo (Lindi) kiasi cha **Shilingi 3,005,697,801.00** ili kupisha maeneo hayo kwa ajili ya matumizi ya Jeshi. Serikali inaendelea na uhakiki wa maeneo mbalimbali ili kuwezesha ulipaji wa fidia.

### *Kuimarisha Miundombinu ya Kimkakati ya Jeshi*

56. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuliimarisha Jeshi kwa kununua vifaa na zana za Kijeshi, kuboresha ulinzi wa anga kwa kufanya ukarabati wa mfumo wa Rada na ukarabati wa mahanga ya ndege. Vile vile, Serikali imeweka mifumo ya ulinzi (CCTV) kwenye miundombinu ya kimkakati ya Jeshi, na ununuzi wa vifaa vya mfumo wa malipo.

57. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwendelezo wa kutekeleza agizo la Serikali la kuhamia Dodoma, Wizara imekamilisha ujenzi wa Ofisi zake katika Mji wa Serikali (Mtumba). Vile vile, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania linaendelea na taratibu za ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (Kikombo). Pia, Jeshi la Kujenga Taifa limekamilisha ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (Chamwino) na inaendelea na ujenzi wa Ofisi nyingine za Idara mbalimbali. Aidha, Wizara kupitia Jeshi la Kujenga Taifa imeendelea na ujenzi na ukarabati wa kambi mbalimbali zikiwemo: Kibiti (Pwani); Makuyuni (Arusha); Mpwapwa na Makutupora (Dodoma); Itaka (Songwe); Milundikwa na Luwa (Rukwa); Bulombora (Kigoma); Mbweni (Dar es Salaam); Nachingwea (Lindi); Mafinga (Iringa) na Maramba (Tanga).

### **MASHIRIKA YANAYOSIMAMIWA NA WIZARA**

#### *Shirika la Uzalishaji Mali la JKT (SUMAJKT)*

58. ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT limee- ndelea kutekeleza shughuli zake za kibiaшara kupitia sekta ya kilimo na ufugaji; ujenzi kupitia Kampuni yake Tanzu ya Ujenzi (National Service Construction Company); Viwanda vikiwemo Kiwanda cha Ushonaji (National Service Garment Factory), Kiwanda cha Kuchakata Nafaka kilichopo Mlale (Songea), Kiwanda cha Samani Chang'ombe, Kiwanda Cha Maji Mgulani na

Kiwanda cha Kuchakata Kokoto (SUMAJKT ANIT ASFALT). Aidha, Shirika linaendesha shughuli mbalimbali za kibiashara ambazo ni: huduma ya ulinzi binafsi inayotolewa na Kampuni Tanzu ya Ulinzi (SUMAJKT Guard Ltd); Uuzaji na Usambazaji wa Matrektta na Zana za Kilimo; Huduma za Chakula na Kumbi za Mikutano (SUMAJKT Recreation and Catering Services) na Kampuni Tanzu ya Kukusanya Madeni (SUMAJKT Auction Mart).

59. ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT Guard Ltd, hutoa huduma ya ulinzi katika Ofisi za Serikali, Mashirika ya Umma na Sekta Binafsi. Kwa mwaka 2018/2019, Kampuni imefanikiwa kuongeza huduma za ulinzi kwa Taasisi za Serikali **27** na Kampuni Binafsi sita **(6)**. Hivyo, kwa sasa Kampuni ina malindo **360** kwa Taasisi za Serikali, Kampuni Binafsi na watu binafsi.

60. ***Mheshimiwa Spika***, Kampuni hili ya ulinzi imeendelea kutoa ajira na kuchangia kupunguza tatizo la ajira nchini. Hadi kufikia Machi, 2019 jumla ya vijana **8,528** wameajiriwa. Aidha, Kampuni imefanikiwa kununua magari matano ya doria ili kuendelea kuimarisha utendaji kazi. Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, Kampuni imekusudia kuimarisha shughuli zake kwa kuendelea kununua vitendea kazi vipyta vikiwemo; vifaa vya kupambana na moto na uokoaji, vifaa vya kuhakikisha usalama katika usafirishaji fedha na magari ya kusafirishia wagonjwa ili kuongeza tija kwa Shirika.

61. ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT kupitia Kampuni ya Ujenzi limekamilisha ujenzi wa Ofisi za Wizara sita (6) katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma. Wizara hizo ni: Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Katiba na Sheria; Mifugo na Uvuvi; Maliasili na Utalii; Kilimo; na Maji. Vile vile, linatekeleza ujenzi katika Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, Chuo Kishiriki cha Elimu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DUCE) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, linatekeleza ujenzi wa Shule ya Sekondari Benjamin Mkapa, *Dealers House* na *One Stop Centre* katika migodi ya Tanzanite – Mirerani na Vituo vya Umahiri vya Madini (Minerals Centres of Excellence) katika Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Dodoma, Simiyu, Kagera na Tanga. Aidha, SUMAJKT imehusika katika ujenzi wa Ofisi

za Halmashauri za Wilaya ya Kahama, Mpanda, Songwe na Bunda.

**62. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza Azma ya Serikali ya kuwa nchi ya uchumi wa viwanda, SUMAJKT limeendelea kuimarisha viwanda vyake vikiwemo: Kiwanda cha Ushonaji-Mgulani (National Service Garments Factory) ambacho kimeanza kushona sare za Wanajeshi ili kupunguza gharama za kuagiza sare hizo nje ya nchi kwa siku zijazo; Kiwanda cha Bidhaa za Ngozi (SUMAJKT Leather Products) – Mlalakuwa JKT, ambacho huuza bidhaa zake kwa Maafisa na Askari wa JWTZ, Walinzi wa SUMAJKT Guard Ltd, Mgambo na Kampuni Binafsi za Ulinzi. Kiwanda cha Samani-Chang'ombe (Chang'ombe Furniture Factory) ambacho hutengeneza samani za aina mbalimbali, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kimeuza bidhaa hizo kwa Taasisi mbalimbali za Serikali, ikiwa ni pamoa na Mamlaka ya Bima Tanzania, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania - Kanda ya Mbeya na Kampuni Binafsi.

**63. *Mheshimiwa Spika*,** viwanda vingine ni Kiwanda cha Kuchakata Kokoto (SUMAJKT ANIT ASFALT) na Kiwanda cha Kuchakata Nafaka - Mlale (Songea) ambacho kina uwezo wa kuzalisha tani **20** za unga wa mahindi kwa siku na kimeanza kusambaza bidhaa zake kwenye Vikosi vya Jeshi na matarajio ni kusambaza katika maeneo mengine ya Mkoa wa Ruvuma. Kiwanda hicho kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 08 Aprili, 2019. Vile vile, SUMAJKT ina Kiwanda cha kutengeneza maji ya kunywa yanayotambulika kwa jina la *Uhuru Peak* ambacho huzalisha **lita 12,000** kwa siku na *husambara* maji hayo katika baadhi ya maeneo ya Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar.

**64. *Mheshimiwa Spika*,** SUMAJKT limee- ndelea kutekeleza miradi ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, mbegu bora, ufügaji na uvuvi. Vile vile, Shirika linajihusisha na shughuli za ufügaji wa samaki katika mabwawa na vizimba katika kambi ya Rwanakoma (Mara), ufügaji wa nyuki katika Vikosi vya Kanembwa (Kigoma) na Msange (Tabora). Pia,

mbegu bora za mpunga na mahindi huzalishwa katika vikosi vya Chita (Morogoro), Itende (Mbeya), na Mlale (Ruvuma). Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shirika limefanikiwa kulima jumla ya ekari **4,779** ambapo ekari **2,779** ni za mahindi, ekari **1,500** za mpunga, ekari **500** za alizeti na ekari **200** za mbogamboga na matunda.

65. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki, matrekta **100** yameingizwa nchini na Shirika ili kutekeleza azma ya matumizi ya zana za kisasa kwenye sekta ya kilimo. Kati ya matrekta hayo, **34** yameuzwa. Shirika linaendelea kuzifanyia kazi changamoto za urejeshwaji wa madeni kwa wakati kutoka kwa wateja waliokopeshwa matrekta na zana. Hata hiyo, hadi kufikia Machi, 2019 mradi ulikuwa unadai washitiri wake kiasi cha **Shilingi 35,294,530,089.00** ambayo sehemu kubwa yakiwa ni madeni ya awamu ya kwanza ya mradi. Jitihada za kukusanya madeni kutoka kwa washitiri wanaodaiwa wakiwemo Viongozi wa Serikali, Wabunge, Watumishi wa Umma na watu binafsi zinaendelea kufanyika. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 madeni ya matrekta yenye jumla ya **Shilingi 733,707,979.00** yalikusanya.

66. **Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa taarifa kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shirika limefanikiwa kuanzisha Kampuni ya Ukusanyaji Madeni na Mnada (SUMAJKT Auction Mart) ili kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa madeni. Hadi kufikia Machi, 2019 Kampuni imekusanya madeni ya Matrekta yenye jumla ya **Shilingi 330,000,000.00** kati ya madeni ya mradi wa matrekta yaliyokusanya. Pia, Kampuni imekusanya kiasi cha **Shilingi 1,543,620,000.00** cha madeni ya Kampuni ya Ulinzi ya SUMAJKT Guard Ltd. Vilevile, SUMAJKT Auction Mart imepata kazi kutoka Taasisi mbalimbali za kifedha ya kukusanya madeni yenye thamani ya **Shilingi 25,000,000,000.00** na kufanikiwa kulipwa kamisheni ya **Shilingi 294,808,630.07** kutokana na kazi hizo.

#### *Shirika la MZINGA*

67. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shirika la MZINGA limeendelea kutekeleza shughuli

za uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo ya msingi na ya kiraia. Shirika limefanya utafiti wa malighafi zinazopatikana hapa nchini ili zitumike katika uzalishaji wa mazao ya msingi. Vile vile, Shirika limefanya tafiti mbalimbali zikiwemo: utafiti wa mashine inayotumia vumbi la mbao kuzalisha mkaa, mashine ya kusindika uyoga, utafiti wa tela la kubeba abiria kwenye pipipiki, utafiti wa uzalishaji wa malighafi ya *Gilding Metal Clad Sheet* na *Brass Sheet*. Aidha, Shirika limekarabati zana na vifaa vya kijeshi. Pia, limeendelea na utengenezaji wa samani za nyumbani na maofisini.

**68. *Mheshimiwa Spika*,** kupitia Kampuni Tanzu ya Shirika la MZINGA (MZINGA Holding Co. Ltd), Shirika limeshiriki katika ujenzi wa Ofisi za Wizara nne (4) katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma, Wizara hizo ni: Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu, Uwekezaji na Bunge; Madini; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Vile vile, Shirika la MZINGA limeendelea na ujenzi wa Ukumbi wa Mikutano pamoja na Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi (Mtwara), ujenzi wa Ofisi ya Halmashauri ya Mji Mdogo Makambako (Njombe), ujenzi wa Jengo la Utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo (Mbeya) na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Ikungi (Singida).

**69. *Mheshimiwa Spika*,** Shirika la MZINGA linaendelea kutekeleza jukumu la kikanuni la kusimamia zana na silaha zinazomilikiwa na makampuni ya ulinzi ambayo yanatoa huduma za ulinzi kwenye meli za kibiashara zinazoingia ndani ya mipaka ya nchi yetu. Aidha, meli ambazo hazitii n a n g a katika bandari yetu kutokana na muda mfupi wa meli hizo kukaa katika eneo letu hukaguliwa na kuhakikiwa zana na silaha zilizonazo. Pia, kwa meli ambazo zinatia nanga katika bandari yetu kwa muda wa zaidi ya saa 24 hukaguliwa na zana huhifadhiwa na kurejeshwa kwenye meli masaa machache kabla ya kuondoka kwa meli hizo. Kazi hii inafanyika ili kudhibiti matumizi mabaya ya zana na silaha hizo.

**70. *Mheshimiwa Spika*,** katika kutekeleza azma ya Serikali

ya kujenga uchumi wa viwanda, Shirika limenunua malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya msingi. Aidha, Mpango Mkakati wa Shirika wa Miaka Mitano (2017/18 - 2021/22) unakusudia kupanua wigo wa uzalishaji wa mazao ya kijeshi. Pia, Shirika limepanga kuanzisha kiwanda cha kutengeneza baruti na kupanua mradi wa kutengeneza mashine ndogo ndogo kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali kuongezea thamani ya mazao ya kilimo na misitu.

***Shirika la NYUMBU***

71. ***Mheshimiwa Spika***, Shirika limeendelea kutoa mchango wa kupunguza matumizi ya Serikali kwa kushiriki katika maandalizi ya vifaa na zana za kijeshi kwa ajili ya vikosi vyta ulinzi wa amani, kwa kukarabati magari ya kivita, kutengeneza matela ya kubeba maji na mafuta, vitanda vyta kulalia askari, mahema na majiko ya medani. Vile vile, Shirika limeshiriki katika matengenezo ya mashine na mitambo kwa ajili ya matumizi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na kukarabati miundombinu ya taasisi mbalimbali za Serikali na utengenezaji wa vipuri vyta aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda.

72. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kukamilisha utafiti kuhusu utengenezaji wa magari ya zimamoto na uokoaji na uzoefu waliopata hapo awali katika utengenezaji wa magari ya zimamoto, Shirika limeanza kazi ya kutengeneza magari hayo kwa ajili ya matumizi katika viwanja vyta ndege na Halmashauri.

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2018/2019 Shirika limeendelea kutekeleza agizo la Serikali liliolitaka Jeshi letu kuongoza katika uanzishwaji wa viwanda nchini. Katika kuhakikisha kuwa Shirika linaendelea kutekeleza majukumu ya msingi ya kuanzishwa kwake, yameandaliwa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2018/19-2027/28) wa kuliimarisha Shirika ili liweze kushiriki katika maendeleo ya uchumi wa viwanda nchini.

Mpango huu uko katika hatua za kuridhiwa na Serikali kwa ajili ya kuanza utekelezaji.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Shirika limekarabati baadhi ya miundombinu ya majengo na mitambo iliyopo ili kuongeza ufanisi na kukuza uwezo wa uzalishaji. Vile vile, limenunua mashine kwa ajili ya kiwanda kipyä cha kutengeneza *air cleaners, oil and fuel filters* za magari. Pia, Shirika limefunga mashine ya kutengeneza misumari ya ukubwa mbalimbali na mashine ya kudarizi vyeo na nembo za kijeshi pamoja na ununuzi wa malighafi zake. Aidha, Shirika limenunua mitambo mipya kwa ajili ya kuboresha karakana za kukereza, kukata, kuunga vyuma na usubiaji. Maboresho haya yataliingizia Shirika mapato na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa kuagiza bidhaa hizo kutoka nje ya nchi.

#### **CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

75. **Mheshimiwa Spika**, Wizara katika kutekeleza bajeti yake kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 imekutana na changamoto mbalimbali, kubwa ikiwa ni ufinyu wa ukomo wa bajeti, ambapo kiasi kilichoidhinishwa cha **Shilingi 1,910,722,891,000.00** hakikidhi mahitaji halisi. Aidha, fedha za maendeleo zilizotolewa kwa kiasi kikubwa zimetumika kulipia mikataba michache ya ununuzi wa zana na utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo. Hali hii imesababisha Wizara kutoweza kutekeleza mipango yote iliojiwekea katika mwaka 2018/2019.

76. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya uimarisaji na uanzishaji wa viwanda vipyä Jeshini, zipo changamoto za uchakavu wa miundombinu ya viwanda ikiwemo; karakana, maabara, barabara, mitambo na majengo. Aidha, karakana nyingi zinatumia teknolojia zilizopitwa na wakati, na kuna upungufu wa watalaam wa kuendesha mitambo, hususan katika Mashirika ya MZINGA na NYUMBU.

77. **Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto hizo Wizara imekutana na Wazabuni mbalimbali ili kuweka utaratibu wa kulipa madeni hayo. Vile vile, Wizara imefanya mazungumzo na Wizara ya Fedha na Mipango kwa lengo la

kupitia, kujadiliana na kukubaliana kuhusu utaratibu wa kulipa madeni husika.

78. ***Mheshimiwa Spika***, Mashirika yaliyo chini ya Wizara, yameandaa mipango ya maendeleo ya muda wa kati na muda mrefu ili kutatua baadhi ya changamoto. Shirika la NYUMBU limeandaa Mpango wa Miaka Kumi (2018/19 – 2027/28) wa kuliimarisha ambao upo katika hatua ya kuridhiwa na Serikali. Shirika la MZINGA nalo limeendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Miaka Mitano (2017/18 – 2021/22).

79. ***Mheshimiwa Spika***, SUMAJKT lina- kabiliwa na changamoto ya washitiri kutolipia huduma kwa wakati na kuzalisha madeni kwa Shirika ambayo yanakwamisha utekelezaji wa miradi mbalimbali na malengo ya Shirika. Hivyo, SUMAJKT limeendelea na juhudi mbalimbali za kukusanya madeni ikiwemo kwa kutumia Kampuni ya Ukusanyaji Madeni na Mnada ya SUMAJKT (SUMAJKT Auction Mart).

#### **MPANGO NA MWELEKEO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

80. ***Mheshimiwa Spika***, Mpango wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, unakusudia kuimarisha utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa Jeshi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na Dira na Dhima. Hivyo, Wizara imeazimia kutekeleza majukumu yafuatayo:

(a) Kulipatia Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania vifaa na zana bora pamoja na kutoa mafunzo kwa wanajeshi ili kulingezea uwezo na weledi wa kiutendaji, kiulinzi na kivita;

(b) Kuboresha mazingira ya kazi, makazi na kuimarisha upatikanaji wa huduma stahiki na mahitaji ya msingi kwa wanajeshi na watumishi wa umma;

(c) Kuwapatia vijana wa kitanzania mafunzo ya ukakamavu, umoja wa kitaifa, uzalendo na stadi za kazi;

- (d) Kuendeleza tafiti na uhawilishaji wa teknolojia kwa kuimarisha na kuanzisha viwanda kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi ya kijeshi na kiraia;
- (e) Kuimarisha ushirikiano na Jumuiya za Kimataifa, Kikanda na nchi moja moja katika nyanja za Kijeshi na Kiulinzi;
- (f) Kufanya upimaji, uthamini na ulipaji fidia ya ardhi katika maeneo yaliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya Jeshi; Kiraia katika kukabiliana na majanga na dharura pale inapohitajika;
- (h) Kuendelea kuendesha mafunzo na mazoezi kwa Jeshi la Akiba;
- (i) Kuboresha mawasiliano salama Jeshini kwa ajili ya ulinzi wa Taifa;
- (j) Kujenga maghala ya kuhifadhia silaha na zana za kijeshi;
- (k) Kulipa stahili mbalimbali za maafisa, askari, vijana wa Jeshi la Kujenga Taifa na watumishi wa umma; na
- (l) Kukamilisha Sera ya Ulinzi wa Taifa, Mwongozo wa Viwanda Jeshini na Mpango wa Maendeleo wa Miaka Kumi (2018/19-2027/28) wa kuliimarisha Shirika la NYUMBU.

## **SHUKRANI**

**81. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watu mbalimbali kwa michango waliyotoa katika kutayarisha Makadirio haya. Nawashukuru Dkt. Florens M. Turuka, Katibu Mkuu; Jenerali Venance S. Mabeyo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi; Luteni Jenerali Yacoub H. Mohamed, Mnadhimu Mkuu wa Jeshi; Meja Jenerali Martin S. Busungu, Kamandi, Wakuu wa Mashirika, Wakuu wa Matawi, Idara na Vitengo, Maafisa, Askari na Watumishi wa Umma kwa kuhakikisha kuwa Wizara inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

82. **Mheshimiwa Spika**, napenda nitumie fursa hii kumshukuru **Bibi Immaculate Peter Ngwalle**, aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambaye amestaafu Utumishi wa Umma kwa mujibu wa Sheria. Kwa niaba ya Wizara tunamshukuru sana kwa kuitumikia Wizara kwa ufanisi na mafanikio. Ni imani yetu kuwa ushirikiano huo tulipata kutoka kwake ataendelea kuutoa huko aliko kwa maslahi ya Taifa.

83. **Mheshimiwa Spika**, vile vile, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa wapiga kura wangu wa Jimbo la Kwahani kwa kuendelea kunipa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yangu. Ni matumaini yangu kuwa tutaendelea kushirikiana zaidi kwa manufaa ya Jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

84. **Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Serikali napenda kuzishukuru Serikali za nchi mbalimbali, Mashirika na Wahisani kwa ushirikiano walioipatia Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Wahisani hao ni pamoja na Canada, China, India, Marekani, Ufaransa, Ujerumanu na Uturuki. Aidha, tunazishukuru nchi rafiki kwa ushirikiano wao katika shughuli zetu za kiulinzi. Nchi hizo ni pamoja na Bangladeshi, Ghana, Indonesia, Israel, Jamaica, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Misri, Morocco, Nigeria, Omani, Umoja wa Falme za Kiarabu, Saudi Arabia, Sri Lanka, The Netherlands, Uingereza, Urusi na nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

#### **MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

##### ***Makadirio ya Mapato***

85. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2019/2020, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatarajia kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 81,104,000.00** kutoka katika mafungu yake matatu; ambapo Fungu 38-NGOME linakadiriwa kukusanya **Shilingi 20,001,000.00**, Fungu 39-

JKT Shilingi 59,903,000.00 na Fungu 57-Wizara Shilingi 1,200,000.00.

*Matumizi ya Kawaida na Maendeleo*

86. *Mheshimiwa Spika*, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,854,037,343,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, ili iweze kutekeleza majukumu yake katika Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,726,037,343,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 128,000,000,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo kwa kila Fungu ni ufuatao:

**Fungu 38 – NGOME**

Matumizi ya		
Kawaida	Shilingi	1,406,726,908,000.00
Matumizi ya		
Maendeleo	Shilingi	6,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	1,412,726,908,000.00

**Fungu 39 – JKT**

Matumizi ya		
Kawaida	Shilingi	300,035,425,000.00
Matumizi ya		
Maendeleo	Shilingi	2,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	302,035,425,000.00

**Fungu 57 – Wizara**

Matumizi ya		
Kawaida	Shilingi	19,275,010,000.00
Matumizi ya		
Maendeleo	Shilingi	120,000,000,000.00
Jumla	Shilingi	139,275,010,000.00

**MWISHO**

87. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa Hoja.

## **WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.**

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa kusoma vizuri na kwa muda, hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Msemaji wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Bunge, Mheshimiwa Mwambalaswa.

**MHE. VICTOR K. MWABALASWA - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza kabisa kwamba taarifa hii yote iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowasilishwa mezani mapema leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa leo ni siku ya kujadili bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hili kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoliwezesha Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na vyombo vingine vya ulinzi na usalama nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 6(3)(c)cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ni mojawapo ya Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii nyingine zikiwa

ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Aidha, kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimezipa Kamati za Kisekta ikiwemo Kamati hii jukumu la kushughulikia bajeti za Wizara inazozisimamia. Kufuatia jukumu hili, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 28 Machi, 2019 ili kuchambua bajeti ya Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti,kwa utaratibu wa Kibajeti, Wizara hii ina jumla ya Mafungu matatu yafuatayo:-

- (i) Fungu 38 - Ngome;
- (ii) Fungu 39 - Jeshi la Kujenga Taifa; na
- (iii) Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina bajeti za mafungu yote matatu na matokeo ya uchambuzi yanaonekana katika sehemu ya tatu na ya nne ya taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulisaidia Bunge lako tukufu kufuutilia ipasavyo utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu nne zifuatazo: -

- (i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na
- (iv) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa

fedha 2018/2019; Kamati ilikagua mradi mmoja unaohusu Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (*National Defence Headquarters*) chini ya Fungu 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili kwa kina taarifa kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa kabla ya ziara na baadae ilitembelea eneo la mradi lillipo Kikombo, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, mradi huu utakatekelezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, utajengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Watu wa China ambapo Serikali ya Tanzania itagharamia ujenzi wa miundombinu wezeshi ya utekelezaji wa mradi huo. Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019, mradi huo ulipelekewa shillingi billioni tano nje ya bajeti kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu ya Makao Makuu ya Jeshi.

Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa mradi huu na kutoa fedha za kugharamia ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019; kutohana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa mradi unaotekeliza chini ya Fungu 38 pamoja na maelezo ya Serikali kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mafungu yote matatu ya Wizara hii, nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizo unaridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019; Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa lilipokea fedha zote zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ambayo ina tija kwa Taifa katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa na utekelezaji wa mpango wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Taarifa hiyo ilijumuisha mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu bajeti hiyo kama inavyoelezwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019; uchambuzi wa Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulilenga kulinganisha makusanyo ya mapato na lengo la makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za matumizi mengineyo (*OC*), fedha za mafunzo ya vijana kwa mujibu wa sheria kwa Fungu 39 - JKT na fedha za maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji wa mapato. katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 75,420,100 kwa mafungu yote matatu kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani, mifugo na mazao ya shamba na kodi ya pango. Makadirio haya yalikuwa ni ongezeko la asilimia saba ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ya shilingi 67,706,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa hiyo hadi kufikia mwezi Februari, 2019, jumla ya shilingi 60,119,557 sawa na asilimia 79.71 ya makadirio zilikuwa zimekusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la shilingi 2,199,315 sawa na asilimia 3.6 ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa kipindi kama hiki mwaka 2018.

Kamati inapongeza juhudzi za Wizara katika kukusanya mapato ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kama inavyoonekana katika chati Na. 1 katika ukurasa wa tano wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01 katika ukurasa wa 5 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi zaidi, Kamati illinganisha mchango wa kila fungu katika makadirio na kuoanisha na mchango wa kila fungu katika makusanyo kama inavyoonekana katika chati Na. 2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makusanyo hayo ikiwemo ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi kilichokusanywa unaonekana katika ukurasa wa sita na saba wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila fungu ikilinganishwa na kiasi kilichokusanywa kwa kila fungu, uliiwezesha Kamati kubaini kuwa vyanzo vya uhakika vya mapato vimeiwezesha Wizara hii kuwa na mwenendo mzuri wa makusanyo. Kwa mwenendo huo, ni dhahiri kuwa lengo la makusanyo litakuwa limefikiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha kutoka hazina. Bunge lako tukufu limekuwa likiishauri Serikali kila Mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Serikali. Naomba kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019 zimetolewa kwa kiasi cha kuridhisha ingawa yapo baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kupelekewa fedha zaidi kama itakavyooneshwa katika sehemu ya nne ya taarifa hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ililinganisha uwiano wa bajeti za mafungu hayo na uwiano wa fedha zilizopokelewa kwa mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 2 katika ukurasa wa nane wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia ipasavyo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 - Ngome ikiwa ni asilimia 71.8 ya bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na fungu hilo ni asilimia 72.1 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi kufikia mwezi Machi, 2019. Kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa bajeti ya Ngome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinganisho wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na fedha zilizopatikana unadhihirisha masuala yafuatayo:-

(i) Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mafungu yote matatu imepokea shilingi 1,219,754,009,915.95 sawa na asilimia 63.84 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa shilingi 1,098,557,978,379.95 sawa na asilimia 90 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 121,960,712,978.50 sawa na asilimia 10 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

(ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni pungufu ya asilimia 13 ikilinganishwa na fedha zilizotolewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

(iii) Fungu 39 - JKT limepokea shilingi bilioni sita kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

(iv) Fungu 38 – Ngome limepokea shilingi 2,581,352,771, sawa na asilimia 52.57 na Fungu 57 – Wizara limepokea shilingi 112,614,678,765, sawa na asilimia 51.19 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ni dhahiri kuwa Serikali itakamilisha kiasi kilichobaki kwa mafungu haya.

(v) Kati ya shilingi 121,196,031,536 zilizopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, asilimia 93 ya fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57 – Wizara, asilimia tano ni kwa ajili ya Fungu 39 – JKT na asilimia 2 ni kwa ajili ya Fungu 38 – Ngome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila fungu, Fungu 57 – Wizara lilipokea asilimia 51.88, Fungu 39 – JKT lilipokea asilimia 72.13 na Fungu 38 – Ngome lilipokea asilimia 64.17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha, hususan za maendeleo kwa Fungu 39 ni mzuri na unasaidia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa mara nyingine tena, Kamati inampongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuendelea kuimarisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hayo, naomba kulibainishia Bunge lako tukufu kuwa kutolewa kwa fedha zote za miradi ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Fungu 39, ni jambo liliowezesha vijana wengi zaidi (kufikia vijana 19,895) kujunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Idadi hiyo ni ongezeko la vijana 4,858 sawa na asilimia 32.3 ikililinganishwa na idadi ya vijana waliochukuliwa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati; Kamati ilipopitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka 2018/2019, ilitoa ushauri katika maeneo

kumi na moja yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo. Taarifa kuhusu utekelezaji wa maoni yaliyotolewa inaonekana katika ukurasa wa 10 mpaka wa 12 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020; wakati wa kuchambua mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020 Kamati ilibaini kuwa Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika kutekeleza majukumu yake kulingana na dira na dhima yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu matano likiwemo la kuendeza utafiti na teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu ya Wizara hii pamoja na kuwapatia vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, stadi za kazi na kuwajengea uzalendo na umoja wa kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikiaji wa malengo ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamillifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020; kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38, 39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 81,104,000. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 7.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2018/2019. Mchanganuo wa lengo hilo la makusanyo na sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 2. Na Chati Na. 04 ya taarifa hii katika ukurasa wa 13 hadi wa 15 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa lengo la ukusanyaji wa mapato limezingatia uhalisia wa makusanyo yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi; maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Kamati yalionesha kuwa katika mwaka wa fedha 2019/2020, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwaa kwa mafungu yote matatu ni shilingi 1,854,037,343,000. Kati ya fedha hizo shilingi 1,726,037,343,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 128,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi mantiki ya masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia kasma (*items*), vifungu (*subvotes*) na mafungu (*votes*) yote ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, Kamati ilifanya uwiano wa bajeti inayoombwaa na Bajeti Kuu ya Serikali inayopendekezwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo mbalimbali kama inavyoonekana katika ukurasa wa 15 hadi wa 16 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala hayo yaliyobainika yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia randama za mafungu matatu ya Wizara na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mapema leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii na maoni yaliyotolewa na Kamati yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019, sambamba na majadiliano ya kina kuhusu

Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa mwaka wa fedha 2019/2020, ikilinganishwa na dhima ya Wizara ya kulinda mamlaka, maslahi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Moja, Kamati inatambua juhudini kubwa za Serikali katika kugharamia kwanza maeneo ya kimkakati na miradi michache mikubwa. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri kuwa upo umuhimu kwa Wizara hii kuongezewa ukomo wa bajeti kulingana na mahitaji yake halisi.

Pili, Serikali ione umuhimu wa kuongeza kasi ya ulipaji wa madeni ya kimkataba kwa kutenga fedha zaidi kwenye miradi ya maendeleo kwa Fungu 57. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 katika shilingi 112,614,678,765 zilizotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa Fungu 57, shilingi 105,250,720,487 sawa na asilimia 93 ya fedha zillizotolewa, zilitumika kwenye Kulipa madeni ya kimkataba. Kulipa madeni hayo kwa wakati kutaisaidia Serikali kuokoa fedha zinazoongezeka kwa ajili ya malipo ya riba, vilevile kuelekeza fedha nyingine katika maeneo mengine ya maendeleo.

Tatu, Serikali itoe fedha zote za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu 38 kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Fungu hili lilikuwa limepokea shilingi 3,346,304,213 katika shilingi bilioni nane zilizokuwa zimedhinishwa na Bunge sawa na asilimia 41.83.

Nne, sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 38 katika mwaka wa fedha 2019/2020 na kutoa fedha hizo kwa wakati. Pamoja na mambo mengine, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi muhimu ya Jeshi.

Tano, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia mafunzo, mazoezi na shughuli za usalama na utambuzi. Aidha, Serikali iongeze fedha kwa ajili ya kifungu hiki kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kulingana na umuhimu wa shughuli hizo katika ulinzi wa nchi hii.

Sita, Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utunzaji wa zana, magari na mitambo katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Saba, Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili kuboresha mfumo wa mawasiliano salama Jeshini chini ya Fungu 57 na nane, Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya programu za utafiti katika Shirika la Nyumbu na Mzinga. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019, Shirika la Mzinga ilikuwa limepokea shilingi bilioni 1.5 na Nyumbu shilingi bilioni 1.5 sawa na asilimia 10 tu kwa Mzinga na asilimia sita tu kwa Nyumbu ya fedha zilizoidhinishwa kwa kila shirika.

Tisa, Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kufanya tathmini na kulipa fidia katika maeneo yallyotwaliwa na Jeshi. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 asilimia 14.3 tu ya fedha zilizoidhinishwa ndiyo zilitolewa na kumi, Serikali itoe fedha zote zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuboresha makazi ya wanajeshi, chini ya Fungu 57. Hadi kufikia mwezi Machi, 2019 Serikali ilikuwa imetoa shilingi 208,260 tu, sawa na asilimia 1.47 tu ya fedha zilizotengwa. Kumi na moja, pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali katika kukamilisha Sera ya...

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia pamoja na juhudzi zinazofanywa na Serikali katika kukamisha Sera ya Ulinzi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza jitihada katika kukamilisha mchakato huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi

na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi (Mbunge), kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Ndugu Florens Turuka pamoja na watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athumani Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati, Ndugu Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha taarifa hii inakamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, kwa heshima na taadhima, sasa naliomba Bunge lako tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA KUHSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA (FNGU 38, 39, 57) KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019; PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa leo ni Siku ya kujadili Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Kamati yangu kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Mhe. Dkt.

John Joseph Pombe Magufuli kwa jinsi anavyoliwezesha Jeshi letu la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Vyombo vingine vyta Ulinzi na Usalama Nchini katika nyanja zote ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya pongezi hizo, sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 [Kanuni za Kudumu za Bunge], naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na kuikubali, kisha kuidhinisha Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (3)(c) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ni mojawapo ya Wizara tatu zinazosimamiwa na Kamati hii nyininge zikiwa ni Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

Aidha, Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimezipa Kamati za Kisikta, ikiwemo Kamati hii, jukumu la kushughulikia Bajeti za Wizara inazozisimamia. Kufuatia jukumu hili, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ilikutana na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tarehe 28 Machi, 2019 ili kuchambua Bajeti ya Wizara hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa utaratibu wa Kibajeti, Wizara hii ina jumla ya Mafungu matatu (3) yafuatayo:-

- (i) Fungu 38- Ngome;
- (ii) Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa (JKT); na
- (iii) Fungu 57- Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Wizara).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipitia na kuchambua kwa kina Bajeti za Mafungu yote matatu na matokeo ya Uchambuzi yanaonekana katika sehemu ya Tatu na ya Nne ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, pamoja na kuishauri vema Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu kuu nne (4) zifuatazo: -

- (i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

### **2.1 Maelezo kuhusu Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ilio chini ya Wizara mbili kati ya tatu zinazosimamiwa na Kamati hii ikiwemo Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuanzia tarehe 14 hadi 21 Machi, 2019, inayotekelzwa katika Mikoa ya Morogoro na Dodoma.

Kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Kamati ilikagua Mradi mmoja unaohusu Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa (National Defence Headquarters NDHQ) chini ya Fungu 38. Mradi huu ulipelekewa Shilingi **Bilioni 5** nje ya Bajeti kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa miundombinu ya Makao Makuu ya Jeshi. Ili kulisaidia Bunge lako Tukufu kupata sura halisi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, naomba kueleza utekelezaji huo kama ifuatavyo:-

### **2.1.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijadili kwa kina Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Ulinzi wa Taifa kabla ya ziara na baadae ilitembelea eneo la Mradi lililopo Kikombo, Dodoma. Kwa maelezo yaliyotolwa mbele ya Kamati, Mradi huu utakaotekerezwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, utajengwa kwa ufadhili wa Serikali ya Watu wa China ambapo Serikali ya Tanzania itagharamia ujenzi wa miundombini wezeshi ya utekelezaji wa Mradi. Taarifa hiyo ilieleza kuwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Mradi huo ulipelekewa Jumla ya Shilingi **Bilioni 5**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutambua umuhimu wa Mradi huu na kutoa fedha za kugharamia ujenzi wa miundombnu wezeshi kwa ajili ya utekelezaji wake.

### **2.1.2 Maoni ya Jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ziara ya ukaguzi wa Mradi unaotekerezwa chini ya Fungu 38 pamoja na maelezo ya Serikali kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mafungu yote matatu ya Wizara hii, nianze kwa kipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa mwenendo wa upatikanaji wa fedha hizo unaridhisha.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Fungu 39- Jeshi la Kujenga Taifa lilipokea fedha zote zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea kutoa kipaumbele na kuipa uzito unaostahili kibajeti miradi ambayo ina tija kwa Taifa katika sekta hii.

## **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kupokea na kujadili

Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Taarifa hiyo ilijumuisha maeneo Makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati kuhusu Bajeti hiyo kama inavyoelezwa katika taarifa hii.

### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 ulilenga kulinganisha Makusanyo ya Mapato na lengo la Makusanyo hayo, upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa, hususan fedha za Matumizi Mengineyo (OC), fedha za Mafunzo ya Vijana kwa Mujibu wa Sheria kwa Fungu 39-JKT na Fedha za Maendeleo ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, Kamati ilizingatia taarifa mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa kipindi cha Oktoba, 2018 na Januari 2019 pamoja na majadiliano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu na za ziada wakati wa vikao vya Kamati. Naomba kuwasilisha uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

#### **3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu Ukusanyaji wa Mapato**


**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Wizara ilikadiria kukusanya Mapato ya jumla ya Shilingi **75,420,100.00** kwa Mafungu yote matatu (3) kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni, mauzo ya mazao ya bustani, mifugo na mazao ya shamba na kodi ya pango. Makadirio haya yalikuwa ni ongezeko la asilimia 7 ikilinganishwa na Makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ya Shilingi **67,706,000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa hiyo, hadi kufikia Mwezi Februari, 2019, jumla ya Shilingi **60,119,557.00** sawa na

asilimia 79.71 ya makadirio zilikuwa zimekusanywa. Aidha, kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la Shilingi **2,199,315.00** sawa na asilimia 3.6 ikillinganishwa na kiasi kilichokusanywa kipindi kama hiki Mwaka 2018.

Kamati inapongeza juhudzi za Wizara katika kukusanya mapato ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa miaka mitatu mfululizo kama inavyoonekana katika Chati Na. 01.

#### **Chati Na. I- Muonekano wa Ongezeko la Makusanyo kwa kila Mwaka 2016/2017- 2018/2019**




#### **Chanzo: Randama za Wizara ya Ulinzi na JKT 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, vile vile Kamati ilifanya uchambuzi kwa kila Fungu na kubainisha mchanganuo wa makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 01.

#### **Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi zaidi, Kamati ililinganisha mchango wa kila Fungu katika makadirio na kuoanisha na mchango wa kila Fungu katika makusanyo kama inavyoonekana katika chati Na. 2.

Chati Na. 02: Ulinganisho wa mchango wa kila Fungu katika Makadirio na Makusanyo ya Mapato



### Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi unaonesha kuwa: -

- Makusanyo katika Fungu 38 – Ngome yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 22.8 lakini katika utekelezaji Fungu hilo limechangia kwa asilimia 37.37 ya kiasi kilichokusanya.
- Makusanyo ya Fungu 39 –JKT yalikusudiwa kuchangia katika lengo la Wizara kwa asilimia 75, lakini hali halisi imeonesha kuwa makusanyo ya JKT yamechangia kwa asimia 61.13. Katika mchango wa Makusanyo, JKT imekuwa nyuma katika mchango ikilinganishwa na lengo la mchango wake katika makusanyo ya mapato ya Wizara kutoka asilimia 75 hadi asilimia 65.13.
- Makusanyo ya Fungu 57 – Wizara, yalikusudiwa kuchangia kwa asilimia 1.2 kwenye mapato yote ya Wizara, lakini Taarifa ya Makusanyo ilionesha kuwa Fungu 57 limechangia kwa asilimia 1.5 ya kiasi kilichokusanya.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi halisi

kilichokusanya, ulisukuma Kamati kutaka kupata sababu za mwenendo huo wa makusanyo. Kamati ilibaini kuwa chanzo kikuu cha Mapato kwa Fungu 38- Ngome ni mauzo ya nyaraka za zabuni na JWTZ kuwa wakala wa ukusanyaji wa makato ya Bima zinazokatwa na Wanajeshi kutoka Kampuni mbalimbali za Bima.

Vyanzo hivyo vimesaidia Fungu 38- Ngome kukusanya mapato mengi ikilinganishwa na lengo lililowekwa. Aidha, Fungu 39-JKT linategemea makusanyo yanayotokana na mauzo ya nyaraka za zabuni na mauzo ya mazao ya bustani, mifugo na mashamba yanayozalishwa na Jeshi hilo.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile, Fungu 57- Wizara linategemea mapato yatokanayo na Kodi ya pango ya Kantini kwa mto huduma za chakula, jambo linalochangia makadirio ya makusanyo kwa Fungu hilo kuwa chini ikilinganishwa na Mafungu mengine.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho huo wa malengo ya makusanyo kwa kila Fungu ikilinganishwa na kiasi kilichokusanya kwa kila Fungu, uliwezesha Kamati kubaini kuwa vyanzo vya uhakika vya mapato vimewezesha Wizara hii kuwa na mwenendo mzuri wa makusanyo. Kwa mwenendo huo, ni dhahiri kuwa lengo la makusanyo litakuwa limefikiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019.

### **3.1.2 Upatikanaji wa Fedha Kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge lako Tukufu limekuwa likiishauri Serikali kila Mwaka kuhusu umuhimu wa Serikali kutoa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa matumizi ya Serikali. Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali ilizingatia ushauri huo ambapo Fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 zimetolewa kwa kiasi cha kuridhisha ingawa yapo baadhi ya maeneo ambayo yanahitaji kupelekewa fedha zaidi kama itakavyooneshwa katika sehemu ya nne ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujiridhisha na uzito uliowekwa wakati wa utoaji wa fedha kutoka Hazina kama uliendana


na uzito uliokusudiwa na Bunge wakati wa kuidhinisha Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ililinganisha uwiano wa Bajeti za Mafungu hayo na uwiano wa Fedha zilizopokelewa kwa Mafungu hayo. Ulinganisho huo unaonekanaka katika Jedwali Na. 02.

Jedwali Na. 02: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinisha na zilizopokelewa mionganoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57					
Fungu	Kiasi cha fedha	asilimia	Fungu	Kiasi cha fedha	asilimia
38	1,372,232,770,000.00	71.8	38	880,562,850,392.88	72.1
39	299,239,411,000.00	15.7	39	215,832,804,079.57	17.7
57	239,250,710,000.00	12.5	57	124,123,036,886.00	10.2
	1,910,722,891,000.00	100		1,220,518,691,358.45	100

### Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020

Kamati ilitumia Jedwali hilo, kupata Chati Na. 03 iliyotumika mionganoni mwa nyenzo za uchambuzi kama inavyoonekana.

Chati Na. 03: Ulinganisho wa fedha zilizoidhinisha na zilizopokelewa mionganoni mwa Fungu 38, Fungu 39 na Fungu 57



### Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo unaonesha kuwa Serikali ilizingatia ipasavyo uzito uliotolewa na Bunge wakati wa

kuidhinisha Bajeti. Kwa mfano, Bunge liliidhinisha bajeti ya Fungu 38 - Ngome ikiwa ni asilimia 71.8 ya Bajeti ya Wizara na fedha zilizopokelewa na Fungu hilo ni asilimia 72.1 ya fedha zote zilizopokelewa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa hadi kufikia mwezi Machi, 2019. Kwa mwenendo huu, Kamati inaipongeza Serikali kutoa uzito stahiki kwa Bajeti ya Ngome.

**Mheshimiwa Spika**, ulinganisho wa kiasi cha Fedha kilichoidhinishwa na Fedha zilizopatikana unadhihirisha masuala yafuatayo:-

- i) Hadi kufikia Mwezi Machi, 2019 Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu imepokea Shilingi **1,219,754,009,915.95** sawa na asilimia 63.84 ya fedha zillizoidhinishwa. Kati ya fedha zillizopokelewa Shilingi **1,098,557,978,379.95** sawa na asilimia 90 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **121,960,712,978.50** sawa na asilimia 10 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.
- ii) Kiasi kilichopokelewa na Wizara hii kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni pungufu ya asilimia 13 ikilinganishwa na Fedha zillizotolewa katika kipindi kama hicho katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- iii) Fungu 39 - JKT limepokea Shilingi **Bilioni 6** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 100 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.
- iv) Fungu 38 Ngome limepokea Shilingi **2,581,352,771.00** sawa na asilimia 52.57 na Fungu 57 - Wizara limepokea Shilingi **112,614,678,765.00** sawa na asilimia 51.19 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Ni dhahiri kuwa Serikali itakamilisha kiasi kilichobaki kwa Mafungu haya.
- v) Kati ya Shilingi **121,196,031,536.00** zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, asilimia 93 ya Fedha hizo ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara, asilimia 5 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 2 kwa ajili ya Fungu 38- Ngome.

vi) Katika Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Fungu, Fungu 57- Wizara lilipokea asilimia 51.88, Fungu 39- JKT lilipokea asilimia 72.13 na Fungu 38 Ngome lilipokea asilimia 64.17.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na uchambuzi huo, Kamati ina maoni kuwa mwenendo huu wa upatikanaji wa Fedha hususan za Maendeleo kwa Fungu 39 ni mzuri na unasaidia utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kwa mara nyingine tena, Kamati inampongeza Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kwa kuendelea kuimarisha vyombo vyetu nya Ulinzi na usalama.

**Mheshimiwa Spika**, zaidi ya hayo, naomba kulibainishia Bunge lako Tukufu kuwa, kutolewa kwa fedha zote za Miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Fungu 39, ni jambo liliowezesha Vijana wengi zaidi kufikia Vijana 19,895 kujiunga na mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Idadi hiyo ni ongezeko la Vijana 4,858 sawa na asilimia 32.3 ikilinganishwa na idadi ya Vijana waliochukuliwa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

### **3.2 Mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipopitia na kuchambua Mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka 2018/2019, iltoea ushauri katika maeneo kumi na moja yaliyopaswa kuzingatiwa na Serikali kuhusu Bajeti hiyo.

Masuala hayo yalihusu mambo mbalimbali yakiwemo yafuatayo:-

i) Serikali kuongeza Ukomo wa Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa;

ii) Serikali kutoa Fedha zote za Maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 38- Ngome na Fungu 39- JKT kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

- iii) Wizara ifuatilie ulipaji wa madeni sugu ya matrekta ya SUMA JKT na madeni yatokanayo na huduma za Ulinzi kutoka SUMA JKT Guard LTD;
- iv) Serikali iboreshe maslahi ya walinzi wa Suma JKT Guard LTD;
- v) Serikali itoe Fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya Mashirika ya Nyumbu na Mzinga;
- vi) Serikali itoe Fedha kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa kwa matumizi ya Jeshi hususan eneo la Ras Mshindo katika Wilaya ya Kilwa, Mkoani Lindi; na
- vii) Serikali kukamilisha mchakato wa Sera ya Ulinzi.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulialirifu Bunge lako Tukufu kuwa katika masuala yaliyotolewa ushauri, masuala matano (5) yamezingatiwa kikamilifu, masuala mengine matano (5) yanaendelea kuzingatiwa na suala moja (1) halijazingatiwa kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa ushauri uliozingatiwa kikamilifu ni kuhusu Fungu 38- Ngome kupatiwa fedha zote za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Taarifa ya utekelezaji imeonesha kuwa hadi kufikia mwezi Juni, 2018, Fungu hili llipokea Shilingi Bilioni 8 ikiwa ni jumla ya Fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Fungu hilo.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mwengine wa ushauri uliotekelawa ni kuhusu kutoa Fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya malipo ya fidia ya wananchi wa eneo la Ras Mshindo Wilayani Kilwa ambapo jumla ya Shilingi **3,662,108,122.00** zilikuwa zimetengwa tangu Mwaka wa Fedha 2017/2018 lakini hazikuwahi kutolewa.

Kamati ilielezwu kuwa, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Serikali kupitia Hazina imekwishatoa Shilingi **3,005,697,801.00**

kwa ajili ya kuwalipa fidia Wananchi ambao Taarifa zao zilikuwa zimehakikiwa na kuridhiwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa Ushauri ambao unaendelea kutekelezwa ni kuhusu kukamilisha Mchakato wa Sera ya Ulinzi wa Taifa jambo ambalo limekuwa likishauriwa tangu Bunge la Tisa, changamoto ikiwa ni upatikanaji wa maoni kuhusu Sera hiyo kwa upande wa Zanzibar.

Taarifa ya Utekelezaji iliyowasilishwa mbele ya Kamati ilielezwa kuwa tayari Wizara imekwishapokea maoni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wizara inaendelea na hatua za kujumuisha ushauri na maoni mbalimbali ili kupitishwa kwenye ngazi mbalimbali za maamuzi ndani ya Serikali kwa ukamilishwaji wake.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri mwingine unaoendelea kuzingatiwa na Wizara ni kuhusu Ukusanyaji wa madeni sugu kutoka kwa Wizara na Taasisi zinazodaiwa na SUMA JKT GUARD LTD kwa ajili ya huduma ya ulinzi.

Kamati ilielezwa kuwa, Shirika la SUMA JKT lilitumia mbinu mbalimbali katika kukusanya madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuitumia Kampuni ya ukusanyaji madeni ya Shirika (SUMA Auction Mart). Vilevile Shirika limekuwa likisitisha huduma ya ulinzi kwenye Wizara na Taasisi zenye wadaiwa sugu.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na jitihada hizo, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Shirika limeweza kukusanya jumla ya Shilingi **2,693,102,032.00** sawa na asilimia 58 ya deni sugu la jumla ya Shillingi **4,653,907.000.00**.

**Mheshimiwa Spika**, Ushauri ambao haujazingatiwa kikamilifu unahusu Wizara kuongezewa ukomo wa Bajeti kulingana na mahitaji halisi ili kulongezea Jeshi uwezo wa kiutendaji.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukomo huu usiolingana na mahitaji, Wizara imeendelea kulimbikiza madeni ya Wazubuni, kushindwa kulipa fidia Wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, na kushindwa

kugharamia ipasavyo shughuli za utafiti, uhawilishwaji wa teknolojia na uendelezaji wa Viwanda katika Mashirika ya Nyumbu na Mzinga.

Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kuwa, pamoja na ukomo huo wa Bajeti, imeendelea kutumia kiwango kinachotengwa kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanafikiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia Madaraka ya Bunge yaliyoainishwa katika Ibara ya 63 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Kamati inaendelea kusitiza kuwa ushauri ambao haujazingatiwa unapaswa kufanyiwa kazi na kuwa sehemu ya ratiba ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

##### **4.1 Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2019/ 2020**

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii, Kamati ilirejea Hati Idhini ya Mgawanyo wa Majukumu ya Wizara za Serikali, Toleo la tarehe 22 Aprili, 2016 na kuoanisha na malengo ya Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa katika kutekeleza majukumu ya msingi manne yaliyoainishwa katika Hati Idhini, Wizara inalenga kuimarisha utendaji kazi na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake kulingana na Dira na Dhima kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.


**Mheshimiwa Spika**, lengo hili limepangwa kufikiwa kwa kutekeleza majukumu matano likiwemo la kuendeza utafiti na Teknolojia kwa madhumuni ya kuzalisha bidhaa na huduma kwa ajili ya matumizi muhimu ya Wizara hii pamoja na kuwapatia Vijana wa Kitanzania mafunzo ya ukakamavu, Stadi za Kazi na kuwajengea Uzalendo na Umoja wa Kitaifa.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umeonesha kuwa, majukumu yaliyopangwa yatawezesha ufikaji wa malengo ya Wizara hii kwa ufanisi zaidi endapo Serikali itazingatia Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa kutoa Fedha zitakazoidhinishwa na Bunge kwa ukamilifu na kwa wakati.

#### 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mafungu yote matatu (38,39 na 57) inategemea kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 81,104,000.00**. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la asilimia 7.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopangwa kukusanya katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Mchanganuo wa lengo hilo la Makusanyo na Sura ya mchanganuo wake inaonekana katika Jedwali Na. 2. Na Chati Na. 04 hapa chini: -

Jedwali Na. 03: Mchanganuo wa mapato



Chanzo: Randama ya Wizara 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati imebaini mambo yafuatayo:-

- i) Lengo la makusanyo kwa Mafungu yote ya Wizara hii limeongezeka kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na lengo la Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha. Jambo hili ni la kupongezwa kwa sababu lengo hili limekuwa likiongezeka kila Mwaka. Kwa Mwaka 2017/2018 lengo hilo liliongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2016/2017, na Mwaka wa Fedha 2018/2019 liliongezeka kwa asilimia 8 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- ii) Fungu 38 – Ngome linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 25 ambapo Mwaka 2018/2019 lilitegemewa kwa asilimia 23.
- iii) Fungu 39 – JKT linategemewa katika Makusanyo kwa kiasi cha asilimia 74 ambapo Mwaka 2018/2019 lilitegemewa kwa asilimia 75.
- iv) Fungu 57 linategemewa kwa makusanyo kwa kiasi cha asilimia 1.5 wakati Mwaka 2018/2019 lilitegemewa kwa asilimia 1.2.
- v) Kiasi cha Makadirio ya Makusanyo kwa Fungu 57 kinalingana na Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Kamati ilielezwa kuwa lengo hilo limebaki kama liliyvo kwa kuwa Wizara inaendelea kukusanya Mapato kutokana na malipo ya Pango la Kantini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa maelezo hayo, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuzingatia Maoni ya Kamati kuhusu lengo la ukusanyaji wa Mapato kwa kuzingatia uhalsia wa makusanyo yanayopatikana.

#### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwenye Kamati yalionesha kuwa katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inayoombwa kwa Mafungu yote

matatu ni Shilingi **1,854,037,343,000.00** Kati ya Fedha hizo, Shilingi **1,726,037,343,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **128,000,000,000.00** ni kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi mantiki ya Masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya uchambuzi wa makadirio hayo kwa kupitia Kasma (Items), Vifungu (Subvotes) na Mafungu (Votes) yote ikilinganishwa na Bajeti iliyoidhinishwa na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019.

Aidha, Kamati ilifanya uwiano wa Bajeti inayoombwa na Bajeti Kuu ya Serikali inayopendekezwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini mambo yafuatayo: -

- a) Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 imepungua kwa **Shilingi 56,685,548,000** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019. Tofauti hiyo ni pungufu kwa kiwango cha asilimia 3.
- b) Wakati Bajeti Kuu kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa na Waziri wa Fedha tarehe 12 Machi, 2019, imeongezeka kwa asilimia 1.93 Bajeti ya Wizara hii imepungua kwa asilimia 0.6.
- c) Asilimia 7 ya Fedha zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na asilimia 93 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Uwiano huu kwa fedha za Maendeleo umeendelea kupungua kwa miaka miwili mfululizo ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na 2018/2019 ambapo Bajeti ya Maendeleo ilikuwa asilimia 8 na 12.7 mtawalia (**respectively**).
- d) Kiasi cha fedha kinachoombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kimepungua kwa asilimia 45 ikilinganishwa na kiwango kilichotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019. Fedha hizi zimepungua katika Mafungu yote matatu kama ifuatavyo: -

- i) Fungu 38- Pungufu ni Shilingi 2,000,000,000 sawa na asilimia 25;
  - ii) Fungu 39- Pungufu ni Shilingi 4,000,000,000 sawa na asilimia 67; na
  - iii) Fungu 57- Pungufu ni Shilingi 99,975,700,000 sawa na asilimia 45.
- e) Kati ya Shilingi **128,000,000,000.00** zinazoombwa kwa ajili ya kugharamia shughuli za Maendeleo, asilimia 1.6 ni kwa ajili ya Fungu 38- Ngome, asilimia 4.7 ni kwa ajili ya Fungu 39- JKT na asilimia 93.7 ni kwa ajili ya Fungu 57- Wizara.

**Mhesimiwa Spika**, maelezo hayo yametokana na uchambuzi wa Kamati baada ya kupitia Randama za Mafungu matatu ya Wizara na kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

**Mhesimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maelezo hayo yatakayosaidia majadiliano kuhusu hoja iliyowasilishwa na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa mapema leo hii.

## **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mhesimiwa Spika**, kwa kuzingatia taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii na Maoni yaliyotolewa na Kamati yangu kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 sambamba na majadiliano ya kina kuhusu Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 ikilinganishwa na Dhima ya Wizara ya kulinda Mamlaka, Maslahi na Mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kamati inatoa Maoni na Ushauri ufuatao: -

- i) Kamati inatambua juhudni kubwa za Serikali katika kugharamia kwanza maeneo ya Kimkakati na Miradi michache mikubwa. Hata hivyo, Kamati inaendelea kushauri kuwa upo umuhimu kwa Wizara hii kuongezewa Ukomo wa Bajeti kulingana na mahitaji yake halisi.

- ii) Serikali ione umuhimu wa kuongeza kasi ya ulipaji wa madeni ya Kimkataba kwa kutenga Fedha zaidi kwenye Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 57. Kwa Mwaka 2018/2019, kati ya Shilingi **112,614,678,765.47** zilizotengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fungu 57, Shilingi **105,250,720,487.00** sawa na asilimia 93 ya fedha zilizotolewa, zilitumika kwenye kulipa madeni ya Kimkataba. Kulipa madeni hayo kwa wakati kutaisaidia Serikali kuokoa Fedha zinazoongezeka kwa ajili ya malipo ya riba, vilevile kuelekeza fedha nyingine katika maeneo mengine ya Maendeleo.
- iii) Serikali itoe Fedha zote za Maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu 38 kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Fungu hili lilikuwa limepokea Shilingi **3,346,304,213.50** kati ya Shilingi Bilioni 8 zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge sawa na asilimia 41.83.
- iv) Sambamba na ushauri uliotolewa hapo juu, Serikali ione umuhimu wa kuongeza Fedha za Maendeleo zilizotengwa kwa ajili ya Fungu 38 katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 na kutoa Fedha hizo kwa wakati. Pamoja na mambo mengine, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi muhimu ya Jeshi.
- v) Serikali itoe Fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia Mafunzo, Mazoezi na Shughuli za usalama na utambuzi. Aidha, Serikali iongeze Fedha kwa ajili ya kifungu hiki kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kulingana na umuhimu wa shughuli hizo katika Ulinzi wa Nchi.
- vi) Serikali ione umuhimu wa kutoa Fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utunzaji wa zana, magari na mitambo katika Mwaka wa Fedha 2018/2019.
- vii) Serikali ione umuhimu wa kutoa fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili kuboresha mfumo wa mawasiliano salama jeshini chini ya Fungu 57.
- viii) Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya program za Utafiti katika Shirika la Nyumbu na Mzinga. Hadi kufikia

Mwezi machi, 2019, Shirika la Mzinga lilikuwa limepokea Shilingi **bilioni 1.5** na Nyumbu Shilingi **bilioni 1.5** sawa na asilimia 10 tu kwa Mzinga na asilimia 6 tu kwa Nyumbu, ya Fedha zilizoidhinishwa kwa kila Shirika.

ix) Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili ya kufanya tathmini na kulipa fidia katika maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, asilimia 14.32 tu ya Fedha zilizoidhinishwa ndio zilitolewa.

x) Serikali itoe Fedha zote zilizotengwa katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuboresha makazi ya Wanajeshi, chini ya Fungu 57. Hadi kufikia Mwezi Machi, 2019, Serikali ilikuwa imetoa Shilingi **208,260,477.00** sawa na asilimia 1.47 tu ya Fedha zilizotengwa.

xi) Pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali katika kukamilisha Sera ya Ulinzi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuongeza jitihada za kukamilisha mchakato huo.

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard):-

1. Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb, **MwenyeKITI**
2. Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb, **M/MwenyeKITI**
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb
4. Mhe. Mussa Hassan Mussa, Mb
5. Mhe. Prosper J. Mbena, Mb
6. Mhe. Victor Kilasile Mwambalasa, Mb
7. Mhe. Fakharia Shomari Khamis, Mb
8. Mhe. Cosato David Chumi, Mb
9. Mhe. Bonnah Mosses Kaluwa, Mb
10. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb

11. Mhe. Sophia Hebron Mwakagenda, Mb
12. Mhe. Gerson Hosea Lwenge, Mb
13. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
14. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mb
15. Mhe. Joram Ismael Hongoli, Mb
16. Mhe. Zacharia Paulo Issaay, Mb
17. Mhe. Joseph Michael Mkundi, Mb
18. Mhe. Mboni Mohamed Mhita, Mb
19. Mhe. Fatma Hassan Toufiq, Mb
20. Mhe. Sebastian Simon Kapufi, Mb
21. Mhe. Silafu Jumbe Maufi, Mb
22. Mhe. Ruth Hiyob Mollel, Mb
23. Mhe. Janeth Maurice Masaburi, Mb
24. Mhe. Augustino Manyanda Masele, Mb
25. Mhe. Almasi Athuman Maige, Mb
26. Mhe. Dkt. Charles John Tizeba, Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutumia fursa hii kumshukuru Waziri wa Ulinzi na JKT Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi (Mb) kwa ushirikiano wake mzuri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu ya Kikanuni ya Kamati. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu Ndugu Florens Turuka pamoa na Watendaji wote wa Wizara kwa ushirikiano wao.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kwa ufanisi. Aidha, nawashukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athumani Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Bi. Angelina Sanga na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Ramadhan Abdallah na Bi. Grace Bidya wakisaidiwa na Bi. Rehema Kimbe, kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na kuhakikisha Taarifa hii inakamilika kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liipokee Taarifa hii na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Mussa Azzan Zungu, **Mb  
MWENYEKITI**  
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE,  
ULINZI NA USALAMA**  
Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kusoma vizuri sana Mheshimiwa Mwambalaswa, hongera sana. (*Makofii*)

Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Cecil Mwambe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwambe, Msemaji Mkuu kwenye taarifa yako, ukurasa wa kwanza namba tatu, nne, tano..., unakwenda wapi sasa? Haya chukua kalamu.

Namba tatu, nne, tano, sita, na ukija ukurasa wa 26, aya ya 81 mpaka 85 kwa maelekezo ya Kiti hutayasoma, yanakwenda kinyume na Kanuni zetu.

Anza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE K.n.y. MSEMAJI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu maneno ya mwanafalsafa mashuhuri Albert Einstein aliyesema kwamba: "*A permanent peace cannot be prepared by threats but only by the honest attempt to create a mutual trust. However strong national armaments may be, they do not create military security for any nation nor do they guarantee the maintenance of peace.*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo ni kwamba; amani ya kudumu haiwezi kupatikana kwa vitisho, isipokuwa tu kwa jitihada za dhati za kutengeneza mazingira ya kuaminiana. Hata silaha ziwe na nguvu kiasi

gani, haziwezi kulisaidia jeshi kuleta hali ya usalama kwa taifa lolote na pia haziwezi kuwa tegemeo la uhakika la kuleta amani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, umenitaka nisisome vifungu vingine vyat hotuba yetu, lakini ujumbe wetu kimsingi ulikuwa unataka kumkumbusha Mkuu wa Majeshi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** ...asjiiingize kwenye mambo ya kisiasa ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMADI WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo ni kwamba ipo sababu ya msingi ya kutenganisha Jeshi na Polisi. Hii ni kwa sababu moja linapambana na kupigana na maadui wa taifa; na lingine linawahudumia na kuwalinda wananchi. Jeshi linapochukuwa majukumu yote; ya Jeshi na ya Polisi, basi maadui wa taifa hugeuka kuwa wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo, wananchi wanakuwa wahanga wakubwa wa uonevu na ukandamizaji wa kijeshi kwa kuwa huonekana kama maadui wa taifa na pia wanakuwa hawana chombo cha kuwalinda wao na mali zao. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapinga vikali suala la Jeshi letu kutaka na au kujaribu kuingilia masuala ya ndani ambayo kimsingi yako chini ya Jeshi la Polisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi la Wananchi kama kisima cha fikra cha Taifa letu; ukiachilia mbali jukumu la kulinda mipaka ya nchi, Jeshi ndiyo mbadala wa kila kitu nchi inapokuwa kwenye mkwamo (*crisis*). Mbadala huo hauwezi

kutokea kama Jeshi halijawezeshwa kitaaluma na kubobea katika hali ya aina hiyo na utaalami wa kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nchi zilizoendelea, Jeshi ni kitovu cha utafiti na ugunduzi wa teknolojia za hali ya juu. Kwa mfano, kwa mujibu wa Jarida la *Business Insider* la nchini Marekani lilichapishwa mwaka 2014 ni kwamba Wizara ya Ulinzi ya Marekani inahusika na ugunduzi wa karibu vifaa vyote kielektroniki duniani. Akitilia mkazo hoja hiyo, mwanauchumi wa Kiitaliano Mazzucato anaeleza kwamba ili kufikia viwango vya juu vya teknolojia kama vile kwenda mwezini kunahitaji ujasiri wa hali ya juu, uwezo na utayari wa kuwekeza kikamilifu katika maeneo yenye hatari ambayo Sekta Binafsi huwa na woga wa kuyafanya. Lakini badala yake tumeshuhudia Jeshi letu la Tanzania likitumika kufanya mambo ya kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchumi huyu anamalizia hoja yake kwa kusema kwamba Jeshi la Marekani lilikuwa mara nyingi linawekeza katika maeneo hatarishi (*risky areas*), jambo ambalo lilipelekea kuvumbuliwa kwa vifaa vya kielektroniki kama vya *apple* na kadhalika. Matokeo ya jambo hili ni kuzalishwa kwa vifaa vinavyotumika duniani kote ambapo ni vigumu kufikiria dunia hii ingekuwaje bila vifaa hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maoni hayo, ukiachilia mbali teknolojia ya kijeshi (*military technology*) ambayo inatakiwa kuwepo na kuendelezwa nyakati zote ili kuimariswa uwezo wa Jeshi katika mbinu za kivita, Jeshi pia linatakiwa libobee katika teknolojia nyingine kwa maendeleo ya taifa. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kama ilivyoelezwa hapo awali kwamba Jeshi linatakiwa kuwa na uwezo wa kufanya kila kitu nchi inapokuwa kwenye mkwamo. Ni dhahiri kwamba, haliteweza kufanya kila kitu ikiwa halina utaalamu katika kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii la msingi hapa ni je, Serikali imewekeza kiasi gani katika shughuli za utafiti na ugunduzi katika Jeshi letu? Je, bajeti ya maendeleo

inayotengwa inakidhi mahitaji ya kufanya tafiti katika sekta mbalimbali ili kuwezesha ugunduzi na uvumbuzi wa teknolojia mpya katika sekta hizo kwa maendeleo ya nchi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupata majibu ya maswali hayo, inabidi kufanya uchambuzi wa bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT angalau kwa miaka minne iliyopita ili tuone kama kuna jitihada zozote za kulifanya Jeshi letu liwe kisima cha fikra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa bajeti mwaka 2015/2016; toka Serikali hii ya Awamu ya Tano imeingia madarakani mwaka 2016 fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa ni shilingi bilioni 220. Lakini fedha iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2016 ilikuwa ni shilingi bilioni 40 tu, sawa na asilimia 18 tu ya bajeti iliyoidhinishwa na bado tunalitaka Jeshi letu lifanye kazi za ueledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017, Fungu 57 (Wizara) fedha ya maendeleo iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 230; iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2017 ni shilingi bilioni 33.9 tu sawa na asilimia 14.7 tu ya pesa iliyoidhinishwa, na bado tunataka Jeshi letu liwe na weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2017/2018 Fungu 57 (Wizara) fedha iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 205 na hadi kufikia Aprili, 2018, shilingi bilioni 169.786 sawa na asilimia 82.82 ya fedha iliyotengwa ilikuwa imeshatolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengaji wa bajeti ndogo ya maendeleo ambayo hata Mheshimiwa Waziri hapa na ye ye ameilalamikia akitaka Wizara yake iongezewe pesa za maendeleo sambamba na utekelezaji duni wa hiyo pesa inayopelekwa unairudisha nyuma Wizara na unapunguza ufanisi, ubora na tija ya majeshi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali, kwa kadri ileile ambayo inalisifu Jeshi letu kuwa ni imara, lenye weledi na ufanisi mkubwa, basi sifa hizo zionekane kwenye kutenga bajeti ya kutosha ya maendeleo pamoja na mishahara, sambamba na utekelezaji

madhubuti wa bajeti hiyo. Vinginevyo itakuwa tunajipotezea muda tu kwa maneno kumbe hali halisi ni mbaya na hali hii hasa inajitokeza kwa wanajeshi wenyewe vyeo vidogo kwa sababu wanajeshi wenyewe vyeo vikubwa wao maslahi yao yako waziwazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT pamoja na mafungu yake yote yaani Fungu 38 - Ngome na Fungu 39 - JKT inazidi kuwa mbaya kila siku. Kwa mfano fedha za maendeleo zinazoombwa kwa Fungu 57 - Wizara ni shilingi bilioni 120; ikiwa ni pungufu ya bilioni 100 kutoka bilioni 220 zilizotengwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kwa upande wa Fungu 38 - Ngome fedha za maendeleo zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni sita ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni mbili kutoka shilingi bilioni nane iliyotengwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Hali kadhalika bajeti ya maendeleo katika Fungu 39 - JKT imepungua kutoka shilingi bilioni sita mwaka 2018/2019 hadi kufikia shilingi bilioni mbili mwaka 2019/2020 kitu ambacho kinatishia maslahi ya wanajeshi wetu ambao ni walini wa mipaka ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha Serikali kutotekeleza bajeti ya maendeleo ya Wizara hii, sio tu kunalifiedhehesha Jeshi letu, lakini pia kinawaweka wananchi katika hali ya hatari kubwa. Kwa mfano, wote tunafahamu jinsi matukio ya milipuko ya silaha katika maghala ya silaha za milipuko huko Mbagala na Gongo la Mboto – Dar es Salaam, yalivyo sababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa makazi ya wananchi. Katika kukabiliana na hali hiyo, ilitakiwa fedha ya kutosha ya maendeleo itengwe kwa ajili ya ukarabati wa maghala hayo, lakini Serikali haijafanya hivyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyoelezwa hapo awali, kwamba Jeshi ni mbadala wa kila kitu ikiwa nchi iko kwenye mkwamo. Kwa sababu hiyo Jeshi linatakiwa kuwa kisima cha fikra (*think tank*) cha Taifa ili kuliondoa Taifa

kwenye mkwamo ikiwa limekwama. Ili Jeshi liweze kuwa na uwezo huo lazima liwekeze sana kwenye tafiti na kuboea katika kila sekta. Kwa vyovytote vile uwekezaji huo hauwezi kuwa wa shilingi bilioni nane au sita ambazo tumezoea kutenga. Bajeti hiyo ni ndogo mno kuweza kujenga maabara za kisasa zenye vifaa vinavyokidhi teknolojia ya kuwezesha Jeshi kufanya tafiti katika nyanja mbalimbali na kulisaidia Taifa kusonga mbele kiuchumi.

Mhehimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi bajeti ndogo ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT sambamba na utekelezaji duni wa bajeti hiyo haiendani kabisa na azma ya kulifanya Jeshi kuwa kisima cha fikra wala kuwa la kisasa ikiwa pamoja na maslahi za wanajeshi hao kwa sababu kwa muda mrefu sana kumekuwa na malalamiko makubwa hasa kutoka kwa wanajeshi wenye vyeo vya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi; kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma, nyongeza ya mishahara ya kila mwaka (*annual increment*) ni hitaji la kisheria na kikanuni na pia ni kichocheo cha ari ya kufanya kazi kwa bidii zaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaomba Serikali ifikirie na ione namna bora ya kuwaongeza wanajeshi wetu mishahara ili waweze kufanya kazi yao kwa uweledi na bila kuwaonea wananchi ili waweze pia kujingiza kufanya mambo ya kisasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uhalisia huo, zipo taarifa kwamba wanajeshi hawajapata nyongeza ya mishahara kwa ngazi zote tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani. Nyongeza ya mwisho ya mishahara ilifanyika mwaka wa fedha 2015/2016 wakati wa utawala wa Serikali ya awamu ya nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishatoa angalizo kwa Serikali hii kutoa kipaumbele kwa maslahi ya wanajeshi kwa kuwa ni kada ambayo imejitoa kwa gharama ya uhai wao katika kulinda mipaka ya nchi yetu dhidi ya adui yetu kutoka nje na kuhakikisha kwamba taifa lipo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishatoa angalizo kwa Serikali hii kutoa kipaumbele kwa maslahi ya wanajeshi tena wa majeshi yote ikiwemo na Jeshi la Polisi kwa kuwa ni kada ambayo imejitoa kwa gharama ya uhai wao katika kulinda mipaka ya nchi yetu dhidi ya adui yoyote kutoka nje na kuhakikisha kwamba Taifa lipo salama wakati wote. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vema wanajeshi wakaanza kulalamika kuhusu masuala ambayo ni stahiki zao za kisheria. Ni vema Serikali ikatambua hatari ya vyombo vyenye dhamana ya kutunza silaha kuwa sehemu ya walalamikaji. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni lini italipa nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi pamoja na malimbikizo hizokutoka wakati huo posho zilizositishwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia eneo hili si vema wanajeshi wakaanza kulalamika kuhusu masuala ambayo ni stahiki zao za kisheria. Ni vema Serikali ikatambua hatari ya vyombo vyenye dhamana ya kutunza silaha kuwa sehemu ya walalamikaji. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili ni lini italipa nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi pamoja na malimbikizo ya nyongeza hizo toka lilipositisha malipo hayo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho za chakula kwa wanajeshi (*ration allowance*)imegeuzwa kuwa ada ya kulipia mafunzo kwa wanajeshi wanaokwenda mafunzoni. Kwa miaka mingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya wanajeshi wetu ikiwemo posho ya chakula kwa maana ya *ration allowance* pamoja na majeshi mengine ikiwemo Jeshi la Polisi Tanzania. Msingi wa kutetea maslahi ya wanajeshi ni kuwapatia wanajeshi wetu lishe bora na kuwafanya wawe na nguvu ya kuhimili mazoezi na kazi ya kiaskari wanazozifanya. Aidha, lengo lingine ni kuwafanya wawe na utulivu na watuletee utulivu wa ndani ili waweze kufanya kazi yao ya kulinda usalama

wa nchi yetu wakiwa hawana mawazo ya kwamba watakula nini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo ni kwamba posho hii ya chakula hutolewa moja kwa moja kwa askari kila mwezi. Askari anayepokea posho hii huwa na uhuru nayo wa kuitumia kwa namna yoyote ile ikiwa ni pamoja na kuitumia na familia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya posho ya chakula kwa wanajeshi kuwa ndogo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma kumeibuka utaratibu mpya wa kutowalipa moja kwa moja askari wanaokwenda kwenye mafunzo na kozi mbalimbali za kijeshi ikiwemo pamoja na Jeshi la Polisi na badala yake posho hiyo hulipwa moja kwa moja kwenye chuo au taasisi inayotoa mafunzo hayo kwa ajili ya kugharamia chakula atakachotumia mwanajeshi huyo atakapokuwa mafunzoni, hii haikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni sawa na kusema kwamba wanajeshi hao wanaokwenda mafunzoni wanajilipia mafunzo na kozi hizo kwa kutumia posho yao ya chakula jambo ambalo si haki kwao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujuua ni shilingi ngapi katika bajeti ya maendeleo ya Wizara hii iliyyotengwa kwa ajili ya kugharamia mafunzo kwa wanajeshi wetu na kama fedha za mafunzo zipo ni kwa nini kuwalazimisha wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kulipa ile fedha yao ya chakula katika chuo au taasisi inayotoa mafunzo wakati fedha hizo zinaweza kusaidia pia matumizi ya familia zao walizoziacha nyumbani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kutoridhishwa na uamuzi huo wa kulipa fedha zao za chakula kwenye taasisi na vyuo vinavyotoa mafunzo hayo, jambo ambalo hawakushirikishwa kwenye kufanya maamuzi hayo bado chakula wanachopewa kwa siku hakiendani na thamani ya shilingi 10,000 wanayolipa kwa siku kwa ajili hiyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie; licha ya wanajeshi wanaokwenda mafunzo kutoridhishwa na uamuzi huo wa kulipa fedha zao za chakula kwenye taasisi na vyuo zinazotoa mafunzo hayo ambavyo ni vyuo vya kijeshi bado chakula wanachopewa kwa siku hakiendani na dhamani ya shilingi 10,000 wanaolipwa kwa siku kwa ajili ya mafunzo hayo na tukumbuke wanajeshi hao wanapewa mafunzo wengi ni wanajeshi wa vyeo vya chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na madai ya wanajeshi ya muda mrefu ya kuongezewa posho yao ya chakula ili kuweza kumudu gharama maisha ambazo zinaendelea kupanda na kutokana na malalamiko ya kutoridhishwa na uamuzi wa kulipa fedha za chakula kwenye taasisi na vyuo vya mafunzo badala ya kuwalipa moja kwa moja kama ilivyokuwa desturi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali; mosi, kuongeza posho ya chakula kutoka shilingi 10,000 kwa siku ya sasa, hadi kufikia shilingi 15,000 kwa siku ili waweze kumudu gharama za kununua chakula bora. (*Makofii*)

Naomba kurudia eneo hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali; mosi, kuongeza posho ya chakula kutoka shilingi 10,000 kwa siku inayolipwa sasa hadi kufikia shilingi 15,000 kwa siku ili waweze kumudu kununua chakula bora na pesa hiyo tunaomba walipwe moja kwa moja wanajeshi hao na Wizara hii itengeta pesa kwa ajili ya mafunzo hayo pamoja na stahiki zao zingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na nyongeza ya posho hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali vilevile kusitisha mara moja uamuzi wa kulipa fedha za posho ya chakula kwa wanajeshi vyuoni na taasisi zinazotoa mafunzo kwa wanajeshi na badala yake fedha hizo zilipwe moja kwa moja kwenye akaunti za wanajeshi husika ili wawe na uhuru wa kutumia fedha hizo wenywewe. Kumekuwa na malalamiko kwamba hata kantini hizo zinaendeshwa na wakubwa wa maeneo hayo. Sambamba na hilo, Serikali ilihakikishie Bunge hili kuwa, itakuwa inatenga fedha za mafunzo kwa wanajeshi na kwamba itaacha mara moja

kutumia fedha za chakula kwa wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kama ada ya kulipia mafunzo na hii ni kwa majeshi yote yalioko Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, muda wa saa za kazi bado unalalamikiwa Jeshini; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika mwaka wa fedha 2017/2018 ilieleza katika hotuba yake juu ya malalamiko ya wanajeshi kuhusu mabadiliko ya muda wa saa za kazi kutoka saa 9.30 alasiri mpaka saa 12.00 jioni bila kupewa saababu za msingi za mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Waziri mwenye dhamana na wizara ya Ulinzi na JKT alisema kwamba kwa asili ya kazi za jeshi, mwanajeshi anatakiwa kuwa tayari kwa kazi wakati wote. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba wanajeshi wanatakiwa kuwa tayari kwa muda wote kama kuna dharura au hali ya hatari. Lakini katika mazingira ya kawaida ambapo hakuna dharura au tishio la usalama kuwaweka kazini wanajeshi kwa muda wa ziada ni kuwachosha kiasi kwamba hata ikitokea dharura unakuta wamechoka.

Naomba nirudie eneo hili; lakini katika mazingira ya kawaida ambapo hakuna dharura au tishio la usalama kuwaweka kazini wanajeshi kwa muda wa ziada ni kuwachosha kiasi kwamba hata ikitokea dharura unakuta wanajeshi hao wamechoka. Lakini pia kuweweka wanajeshi kazini hadi saa kumi na mbili jioni ni kuwanyima fursa na muda wa kufanya shughuli za kijasiriamali kama vile ufugaji, kilimo cha mbogamboga na biashara ndogondo kujiongezea kipato. Kwa maneno mengine ni kuwaongezea umaskini na msongo wa mawazo kutokana na ukata na tukumbuke wanajeshi hawa ndiyo wanao tutunzia silaha zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefuatilia jambo hilo na kubaini kwamba muda wa kazi bado haujarekebishwa na kwamba bado kuna malalamiko kuhusu suala la muda wa kazi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kurekebisha muda huo ili muda wa kutoka kazini kwa

wanajeshi uwe saa tisa alasiri kama ilivyokuwa awali. Hii itaondoa manung'uniko mionganoni mwa wanajeshi na hivyo kuongeza ufanisi wa jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mizengwe katika upandishwaji wa vyeo kwa wanajeshi wetu; kupandishwa cheo ni stahili ya kisheria kwa mwanajeshi ye yote aliye koto ka ajira hiyo kwa zaidi ya miaka minne na au aliye fuzu mafunzo au kozi inayomfanya awe na sifa za kupanda kutoka ngazi moja ya cheo kwenda nyingine. Pamoja na uhalisia huo, zipo taarifa kwamba kuna mlundikano wa wanajeshi wanaostahili kupandishwa vyeo kutokana na muda waliokaa jeshini zaidi ya miaka minne na wengine wamefuzu kozi zinazowastahili kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa vyeo mpaka sasa. Yapo mazingira ambayo unakuta baadhi ya wanajeshi wamedumu jeshini kati ya miaka mitano mpaka sita lakini hawapandishwi vyeona tukumbuke vyeo vya wanajeshi ndiyo vinavyo *determine* maslahi za watu wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba kulikuwa na wanajeshi 8,000 wali ofuzu kupandishwa vyeo mwezi Desemba, 2018 lakini ni 4,000 tu wali opandishwa vyeo. Hii ina maana kwamba wanajeshi 4,000 wali okuwa na sifa hawakupandishwa vyeo. Mwezi Februari, 2019 wapo wengine waliofuzu na kuwa na sifa za kupandishwa vyeo na mwezi Mei wapo wengine watafuzuna mafunzo hayo hivyo kufanya idadi ya wenye sifa za kupandishwa vyeo kuendelea kuongezeka na hii iko katika majeshi yetu yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifahamike kwamba kutowapandisha vyeo maafisa wa jeshi pamoja na polisi kwa wakati kuna athari za moja kwa moja mosi, kwenye mishahara yao na pili, kwenye pensheni zao. Kwa hiyo, askari aliye paswa kupandishwa cheo miaka miwili iliyopita halafu akaachwa akaja kupandishwa miaka miwili baadaye anakuwa amepunjwa nyongeza yake ya mshahara ambayo ingetokana na cheo hicho na pia mapunjo hayo yanakwenda pia kuathiri pensheni za akari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia eneo hili ifahamike kwamba kutowapandisha vyeo maafisa wa jeshi wakati kuna athari za moja kwa moja mosi, kwenye mishahara yao na pili, kwenye pensheni zao. Kwa hiyo, askari aliypaswa kupandishwa cheo miaka miwili iliyopita halafu akaachwa akaja kupandishwa miaka miwili baadaye anakuwa amepunjwa nyongeza yake ya mshahara ambayo ingetokana na cheo hicho na pia mapunjo hayo yanakwenda pia kuathiri pensheni yake huko mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utata huo wa kuwapandisha vyeo wanajeshi wakiwemo pia na polisi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili kuna wanajeshi wangapi wenyе sifa za kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kuna tatizo gani linalosababisha wanajeshi wasipandishwe vyeo kwa wakati na kama jibu ni bajeti finyu, je, Serikali iko tayari kuwaomba radhi wanajeshi ambao wana sifa za kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa na kuwaahidi kuwalipa malimbikizo ya mishahara ya vyeo vipyta pindi watakapotapandishwa vyeo?

Naomba kurudia eneo hili; aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kuna tatizo gani linalosababisha wanajeshi wasipandishwe vyeo kwa wakati; na kama jibu ni bajeti finyu, je, Serikali iko tayari kuwaomba radhi wanajeshi ambao wana sifa za kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa na kuwaahidi kuwalipa malimbikizo ya mishahara ya vyeo vipyta pindi watakapotapandishwa vyeo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa manunuza ya sare za jeshi uchunguzwe; mionganoni mwa mahitaji ya msingi ya wanajeshi ni pamoja na sare zao za kazi na kutokana pilikapilika za shughuli za kijeshi, sare hizo hazina budi kuendana maumbile yao; na pia kuwa na ubora wa hali ya juu ili ziweze kudumu kwa muda mrefu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba tofauti na wakati wa utawala wa awamu ya nne ambapo sare zilikuwa na ubora wa hali ya juu na pia zilendana na maumbo ya wahusika, sare zilizogawiwa mwaka huu wa 2019 hazina ubora stahiki na pia haziendani na maumbo ya wahusika. Jambo hili limesababisha askari kulazimika kuendelea kutumia sare za zamani ambazo zinaonekana kuwa zina bora kuliko sare mpya. Sare za zamani ziligawiwamara ya mwisho mwaka 2014. (*Makofii*)

Naomba kurudia eneo hili; pia kuna habari zinasema kwamba utawala wa awamu ya nne ambapo sare zilikuwa na ubora wa hali ya juu na pia ziliendana na maumbo ya wahusika, sare zilizogawiwa sasa kwa wanajeshi na majeshi yote hazina ubora stahiki na pia haziendani na maumbo ya wahusika. Jambo hili limesababisha askari kulazimika kuendelea kutumia sare zilizogawiwa mwaka 2014. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutopteka wito wa Serikali kutilia maanani thamani ya fedha dhidi ya huduma au bidhaa wakati wa matumizi ya fedha za umma (*value for money*) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia vyombo husika kufanya uchunguzi wa mchakato wa manunuzi ya sare za jeshi ili kujiridhisha kama manunuzi hayo yamezingatia thamani ya fedha dhidi ya huduma au bidhaa hizo zilizonunuliwa kwa kutumia fedha za walipa kodi. Pia kuna tatizo limeonekana la ununuzi wa magari ya jeshi ambalo nalo tungeomba lifanyiwe uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutumia Jeshi katika shughuli ambazo zinaweza kufanya na sekta binafsi; kwa mujibu wa tovuti ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; mionganoni mwa majukumu msingi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni pamoja na kulinda Katiba na uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kufanya mafunzo na mazoezi ili kuijweka tayari kivita wakati wote; kufundisha umma shughuli za ulinzi na usalama; kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji wakati wa maafa;

kutoa huduma mbalimbali za kijamii; kukuza elimu ya kujitegemea na uzalishaji mali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa na mwisho kabisa kushiriki ulinzi wa amani wa kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja majukumu hayo, imeanza kuzuka tabia ya kulitumia Jeshi la Wananchi katika kufanya shughuli za kawaida za kiraia ambazo zingeweza kufanywa na sekta binafsi na ndipo hapa tunapoongea habari za *PPP*. Jeshi limekuwa likipewa kandarasi za kujenga majengo mbalimbali ya Serikali bila zabuni kushindanishwa. Aidha, lilipewa pia zabuni isiyo na ushindani ya kusafirisha korosho kutoka Mikoa ya Kusini na kupeleka kwenye maghala ya kuhifadhiya korosho hizo ambayo mpaka sasa hivi għarama zake halisi hazijafahamika tunataka Mheshimiwa Waziri anapokuja kumalizia aeleze Bunge lako. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo hicho cha kulipatia Jeshi la Wananchi zabuni zisizo na ushindani, licha ya kuiminya sekta binafsi katika kupata zabuni hizo, lakini pia kimeinyima Serikali fursa za kupata mapato ya kodi na tozo nyininge kutokana na shughuli hizo kwa sababu Jeshi au Serikali inafahamika kwamba hailipi kodi. Tunalitaka Jeshi hili liache kufanya shughuli hizi na zirudi mikononi mwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikishauri wakati wote; Jeshi ndilo linalotakiwa kuwa kisima cha fikra (*think-tank*) cha Taifa na pia kitovu cha fursa mbalimbali kutokana na ugunduzi litakaokuwa linaufanya kutokana na tafiti za kisayansi katika kila sekta. Tofauti na matarajio hayo Jeshi sasa limekuwa linashindana na wananchi katika kugombea fursa ya kuwa chanzo cha fursa kwa wananchi pamoja na kujihusisha na mambo ya kisasia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa changamoto kwa Serikali hii, kulieleza Bunge na taifa kwa jumla kwamba ule uwezo mkubwa wa sayansi na

teknolojia Jeshini ambao ulifikia hatua ya kuvumbua gari aina ya Nyumbu; ambao ulikuwa ni kitovu cha fursa nyngi za kiuchumi kwa sekta binafsi na kwa mwananchi mmoja mmoja umekwenda wapi hadi kufikia hatua ya Jeshi kujingiza katika kazi za sekta binafsi ikiwemo na shughuli za kisiasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu ingawa kuna taarifa kwamba Zanzibar tayari wameshaleta mapendekezo yao, lakini mapendekezo hayo yatakuwa yamechelewa sana hivyo yamechelewesha pia stahiki ya fursa za kisheria ambazo wanajeshi wetu wangeweza stahili kuzipata toka awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ulinzi na usalama mipakani Tanzania; kuna kurasa ambazo hatutazisoma lakini ninaweza kuzisoma kurasa hizo kwa sababu nilikuwa nasisitiza jambo ambalo Mheshimiwa Waziri hapa amelisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri ukurasa wa 14 inasema tishio la ugaidi; ugaidi wa kimataifa umeendelea kuwa tishio la usalama duniani kuendelea kuwepo kwa makundi ya *Al Qaeda* na *Al Shabaab Boko Haram* na mengine mengi ndiyo hasa ulikuwa msisitizo wetu kwenye hotuba yetu ya Kambi ya Upinzani kwenye maeneo ambayo tumeambiwa tusiyasome. Tunaomba Mheshimiwa Waziri ayachukue na kuyafikisha Jeshini aone namna yeye ya kusaldiana sisi watu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ili kuweza kuyafanya mambo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Jeshi; kumekuwa na migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na wananchi ambayo kwa sasa inaanza kuathiri mahusiano kati ya wananchi na Jeshi. Hakuna anayepinga kwamba kuna umuhimu wa kuwa mipaka ya wazi kati ya maeneo hayo na kwamba hakuna mwenye haki ya kuingilia eneo la mwenzake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto iliyopo ni kwamba Jeshi limekuwa likiacha maeneo yake kwa muda mrefu na bila kuweka mipaka iliyodhahiri kiasi kwamba

wananchi wanayatumia bila kujua kama yako chini ya miliki ya Jeshi. Matokeo yake baada ya miaka mingi kuanzia miaka kumi na tano ambapo wananchi wanakuwa wameshaweka makazi yao, ndipo Jeshi linajitokeza na kudai kuwa hilo ni la kwao na hivi karibuni tumeshuhudia mifano mingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na upungufu huo; na pamoja na ukweli kwamba eneo husika linaweza kuwa ni mali ya Jeshi kweli, lakini njia mbazo Jeshi limekuwa likitumia kuwaondoa wananchi hao si njia za kiuungwana. Jeshi linatakiwa kufahamu kwamba ni Jeshi la Wananchi na ardhi linayotaka kuitwaa ni ardhi ya wananchi wa Tanzania chini ya udhamini wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa hiyo ikiwa lina ushahidi kuwa ardhi inayokaliwa na wananchi ilitwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, basi halina budi kuwasiliana na uongozi wa wananchi wa eneo husika ili kutafuta namna bora ya kuwahamisha wananchi bila kuwafanya vitendo vya kinyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mazingira mengine ambayo baadhi ya Wakuu wa Vikosi vya Jeshi wamekuwa wakiwanyang'anya wananchi ardhi kutokana na maslahi yao binafsi kwa mfano maeneo ya Vijiji vya Bugosi kilichopo kata ya Nyamisangura na Kenyambi kilichopo Kata ya Nkende walitwaliwa kwa amri ya Mkuu wa Kikosi cha Jeshi cha Makoko kutokana na tamaa ya fedha kutoka Kampuni ya Simu ya Vodacom iliyokuwa imeingia mkataba na wananchi wa vijiji hivyo kutokana na kampuni hiyo kuweka mnara wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa ulinzi wa amani nje ya nchi; pamoja na ushiriki wetu wa ulinzi wa amani nje ya nchi kupitia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa hususan MONUSCO, UNAMID, UNFL na majeshi mengine, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua tangu utaratibu huu uanze hadi leo hii, ni wanajeshi wangapi wamepoteza maisha wakiwa wanafanya shughuli hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira Jeshini; moja ya sifa za kupata ajira jeshini ni kuwa mwombaji awe amepitia mafunzo

ya JKT au JKU. Hata hivyo, idadi ya wanaopata mafunzo hayo ni kubwa kuliko nafasi halisi za ajira. Kutokana na hali hiyo, wapo vijana wengi wanaofuzu mafunzo ya JKT na JKU wanaobaki mitaani bila kazi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kufahamu athari za vijana hawa waliofundishwa kutumia silaha kubaki mitaani bila kazi ya kufanya. Miaka ya nyuma tumekuwa tukiishauri Serikali kwamba hata kama haiwezi kuwaajiri vijana wote wanaohitimu mafunzo ya JKT au JKU, basi ianzishe programu za ufundi na ujasiriamali kwa kushirikisha vyuo vya *VETA* wakati wa mafunzo ili vijana hao watakapohitimu weweze kupata vyeti vya *VETA* pia ili waweze kupata ajira katika maeneo yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Jeshi la kujenga Taifa katika kuchechua uchumi wa viwanda; kwa takribani miaka kumi iliyopita Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiishauri Serikali kuwekeza katika miradi ya uzalishaji katika Jeshi la Kujenga Taifa ambayo hatimaye itapelekea kukuwa kwa viwanda vidogo vidogo. Pia tulipendekeza kwamba Serikali itumie nguvu kazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga uchumi endelevu nchini na hasa kwa kipindi hiki ambacho mpango wa maendeleo umejikita kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; nahitimisha hotuba yangu kwa kulipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kazi ya utumishi wao uliotukuka wa kulinda nchi yetu kwa gharama ya uhai wao, lakini pongezi hii iende sambamba na stahiki zao wanazostahili kuzipata wanajeshi hao ikiwa pamoja na mishahara, posho zao za chakula, pamoja na *ration* zingine, hii ni kwa majeshi yote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Viongozi Wakuu wa Jeshi kuendelea kuelimisha wananchi walio chini ya kuzingatia maadili yao ya kazi na kamwe wasikubali kutumika kisiasa kwa maslahi ya wanasiasa wachache wanaotaka kutimiza malengo ya kisiasa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kurudia; pamoja na pongezi hizo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa Viongozi Wakuu wa Jeshi kuendelea kuelimisha wanajeshi walio chini yao na hata wenyewe wanajeshi hao kuzingatia maadili yao ya kazi na kamwe wasikubali kutumika kisiasa kwa maslahi ya wachache wanaotaka kutimiza malengo ya kisiasa na hivi karibuni tumeshuhudia kauli ya Mkuu wa Majeshi aliyokuwa anatoa tishio kwa watu wa upinzani. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kabisa kutumia Jeshi kwa shughuli ambazo zinaweza kufanywa katika sekta binafsi na badala yake iwekeze katika sayansi na teknolojia Jeshini ili Jeshi liweze kuwa kitovu cha fikra uwezwapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu Serikali itilie maanani maneno ya Mwanafalsafa Albert Einstein; amani ya kudumu haiwezi kupatikana kwa vitisho, isipokuwa tu kwa jitihada za dhati za kutengeneza mazingira ya kuaminiana na mazingira ya kuaminiana yatajengeka tu kama Serikali na viongozi wenye dhamana ya uongozi wa nchi hii watatenda haki kwa kila mmoja. Daima tukumbuke wosia wa Albert Einstein kwamba hata silaha ziwe na nguvu kiasi gani, haziwezi kulisaidia Jeshi kuleta hali ya usalama kwa Taifa lolote na pia haziwezi kuwa tegemeo la ulinzi kwa uhakika la kuleta amani. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Maliza maliza.

**MHE. CECIL D. MWAMBE - K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa Serikali kutenda haki kwa kuwapa wananchi uhuru kamili wa mawazo, kukusanyika, kuandamana, kukosoa na haki mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii kama njia thabiti ya kudumisha amani ya nchi yetu.

Mwisho kabisabaada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha hotuba yangu na maneno yote yaingie kwenye *Hansard*. Ahsante sana. (*Makofii*)

HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENIKATIKA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA  
TAIFA, KUHUSU BAJETI YA WIZARA HIYO, KWA MWAKA WA  
FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni 99(9) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2016)

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuanza hotuba yangu kwa kunukuu maneno ya mwanafalsafa mashuhuri Albert Einstein aliyesema kwamba: *"A permanent peace cannot be prepared by threats but only by the honest attempt to create a mutual trust. However strong national armaments may be, they do not create military security for any nation nor do they guarantee the maintenance of peace"*
2. **Mheshimiwa Spika**, tafsiri isiyo rasmi ya maneno hayo ni kwamba; Amani ya kudumu haiwezi kupatikana kwa vitisho, isipokuwa tu kwa jitihada za dhati za kutengeneza mazingira ya kuaminiana. Hata silaha ziwe na nguvu kiasi gani, haziwezi kulisaidia jeshi kuleta hali ya usalama kwa taifa lolote na pia haziwezi kuwa tegemeo la uhakika la kuleta amani.
3. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]
4. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]
5. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]
6. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]
7. **Mheshimiwa Spika**, kwa tafsiri isiyo rasmi, ni kwamba ipo sababu ya msingi ya kutenganisha Jeshi na Polisi. Hii ni kwa sababu moja linapambana na kupigana na maadui wa taifa; na jingine linawahudumia na kuwalinda wanachi. Jeshi linapochukuwa majukumu yote; – ya Jeshi na ya Polisi; basi maadui wa taifa hugeuka kuwa wananchi.

**8. Mheshimiwa Spika**, kwa mantiki hiyo, wananchi wanakuwa wahanga wakubwa wa uonevu na ukandamizaji wa kijeshi kwa kuwa huonekana kama maadui wa taifa na pia wanakuwa hawana chombo cha kuwalinda wao na mali zao. Kwa sababu hiyo; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapinga vikali, suala la Jeshi letu kutaka na au kujaribu kuingilia masula ya ndani ambayo kimsingi yako chini ya Jeshi la Polisi.

**B. JESHI LA WANANCHI KAMA KISIMA CHA FIKRA CHA TAIFA  
(NATIONAL THINK TANK)**

**9. Mheshimiwa Spika**, ukiachilia mbali jukumu la kulinda mipaka ya nchi; Jeshi ndio mbadala wa kila kitu nchi inapokuwa kwenye mkwamo (crisis). Mbadala huo hauwezi kutokea,kama Jeshi halijawezeshwa kitaaluma na kuboea katika kila aina ya utaalamu katika sekta zote.

**10. Mheshimiwa Spika**, katika nchi zilizoendelea, Jeshi ni kitovu cha utafiti na ugunduzi wa teknolojia za hali ya juu. Kwa Mfano, Kwa mujibu wa Jarida la "Business Insider" la nchini Marekani lili洛chapishwa mwaka 2014 ni kwamba; Wizara ya Ulinzi ya Marekani inahusika na ugunduzi wa karibu vifaa vyote ki-elektroniki duniani<sup>1</sup> Akitilia mkazo hoja hiyo, mwanauchumi wa Kiitaliano Mazzucato anaeleza kwamba; ili kufikia viwango vya juu vya teknolojia kama vile kwenda mwezini kunahitaji ujasiri wa hali ya juu, uwezo na utayari wa kuwekeza kikamilifu katika maeneo yenye hatari ambayo sekta binafsi huwa na woga wa kufanya hivyo.

**11. Mheshimiwa Spika**, mchumi huyu anamalizia hoja yake kwa kusema kwamba Jeshi la Marekani lilikuwa mara nyingi linawekeza katika maeneo hatarishi (risky areas) jambo ambalo lilipelekea kuvumbuliwa kwa vifaa vya kielektroniki kama vya Apple nk. Matokeo ya jambo hili ni kuzalishwa kwa vifaa vinavyotumika duniani kote ambapo ni vigumu kufikiria dunia hii ingekuwaje bila vifaa hivyo.

**12. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maoni hayo; ukiachilia mbali teknolojia ya kijeshi (military technology) ambayo inatakiwa kuwepo na kuendelezwa nyakati zote ili kuimarisha

uwezo wa Jeshi katika mbinu za kivita; Jeshi pia linatakiwa libobee katika teknolojia nyingine kwa maendeleo ya taifa. Sababu kubwa ya kufanya hivyo ni kama nilivyooleza hapo awali kwamba; Jeshi linatakiwa kuwa na uwezo wa kufanya kila kitu nchi inapokuwa kwenye mkwamo. Ni dhahiri kwamba, halitaweza kufanya kila kitu ikiwa halina utaalamu katika kila sekta.

**13. Mheshimiwa Spika**, swali la msingi hapa ni je, Serikali imewekeza kiasi gani katika shughuli za utafiti na ugunduzi katika Jeshi letu? Je, Bajeti ya maendeleo inayotengwa inakidhi mahitaji ya kufanya tafiti katika sekta mbalimbali ili kuwezesha ugunduzi na uvumbuzi wa teknolojia mpya katika sekta hizo kwa maendeleo endelevu ya nchi?

**14. Mheshimiwa Spika**, ili kupata majibu ya maswali hayo, inabidi kufanya uchambuzi wa bajeti ya Maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT angalau kwa miaka minne iliyopita ili tuone kama kuna jitihada zozote za kulifanya Jeshi letu liwe kisima cha fikra.

**15. Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT kwa miaka minne iliyopita ni kama ifuatavyo:-

i. Mwaka wa fedha 2015/16:

a) Fungu 57 (Wizara); fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa ni shilingi bilioni 220. Fedha iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2016 ilikuwa ni shilingi bilioni 40 sawa na asilimia 18 tu ya bajeti iliyoidhinishwa.

b) Fungu 38 (Ngome); fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa ilikuwa ni shilingi bilioni 8; lakini hadi kufikia mwezi Machi, 2016 hakuna hata senti moja iliyokuwa imetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hii ndiyo kusema kwamba; hadi tunafikia mzunguko wa tatu wa utekelezaji wa bajeti kuu ya Serikali; - bajeti ya maendeleo katika Fungu 38 (Ngome) ilikuwa hajatekelezwa kabisa.

c) Fungu 39 (JKT); lilitengewa shilingi bilioni 4 kutekeleza mradi wa ujenzi na ukarabati wa makambi ya Jeshi la Kujenga Taifa, lakini hadi kufikia Machi, 2016 hakuna hata senti moja iliyotolewa kwa ajili ya mradi huo.

**ii. Mwaka wa Fedha 2016/17**

a) Fungu 57 (Wizara) fedha ya maendeleo iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 230; iliyotolewa hadi kufikia Machi, 2017 ni shilingi bilioni 33.9 sawa na asilimia 14.7 tu ya fedha iliyoidhinishwa.

b) Fungu 38 (Ngome). Fungu hili liliidhinishiwa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya miradi ya maendeleo lakini hadi kufikia Machi, 2017 ni shilingi bilioni 1 ilitolewa. Hii ni sawa na asilimia 10 tu ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

c) Fungu 39 (JKT); Fungu hili lilikuwa limeidhinishwa shilingi bilioni 8 lakini hadi Machi, 2017; ilikuwa imetolewa shilingi bilioni moja sawa na asilimia 12.5 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

**iii. Mwaka wa Fedha 2017/18**

a) Fungu 57 (Wizara) fedha iliyotengwa ilikuwa shilingi bilioni 205 na hadi kufikia Aprili, 2018, shilingi bilioni 169.786 sawa na asilimia 82.82 ya fedha iliyotengwa ilikuwa imeshatolewa.

b) Fungu 38 (Ngome) Fungu hili lilitengewa shilingi bilioni 8 na fedha iliyopokelewa hadi kufikia Aprili, 2018 ilikuwa ni shilingi bilioni 6.793 sawa na asilimia 84.92.

c) Kwa upande wa JKT (Fungu 39) fedha ya maendeleo iliyokuwa imetengwa ni shilini bilioni 6 na iliyotolewa ilikuwa ni shilingi bilioni 5 sawa na asiliimia 83.33

**16. Mheshimiwa Spika**, ukiangalia takwimu hizi utaona kwamba utekelezaji wa bajeti ya maendeleo ya Wizara na mafungu yake yote kwa mwaka wa fedha 2017/18 uliimarika zaidi kuliko miaka miwili iliyotangulia. Hata hivyo, ukiangalia fedha halisi iliyotolewa ni kidogo sana kuweza kufanya mambo makubwa ya tafiti na ugunduzi wa teknolojia za kisasa Jeshini na katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

**17. Mheshimiwa Spika**, utengaji wa bajeti ndogo ya maendeleo sambamba na utekelezaji duni wa bajeti hiyo unairudisha nyuma Wizara na unapunguza ufanisi, ubora na tija ya majeshi yetu. Kambi Rasmii ya Upinzani Bungeni inataka Serikali, kwa kadri ile ile ambayo inalisifu jeshi letu kuwa ni imara, lenye weledi na ufanisi mkubwa, basi sifa hizo zionekane kwenye kutenga bajeti ya kutosha ya maendeleo sambamba na utekelezaji madhubuti wa bajeti hiyo. Vinginevyo itakuwa tunajifurahisha tu kwa maneno kumbe hali halisi ni mbaya sana.

**18. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/19 bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa Wizara ilikuwa shilingi bilioni 220, Ngome shilingi bilioni 8 na JKT shilingi bilini 6. Hata hivyo tofauti na ilivyo desturi ya utoaji wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti; safari hii Wizara nzima ya Ulinzi na JKT pamoja na mafungu yake yote halkutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti hadi kufikia Machi, 2019. Kitendo hiki kinazuia kufanya tathmini kama fedha zimetolewa au hazikutolewa katika kutekeleza miradi ya maendeleo katika mafungu husika.

**19. Mheshimiwa Spika**, hali ya bajeti ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT pamoja na mafungu yake yote – yaani Fungu 38 (Ngome) na Fungu 39 (JKT) inazidi kuwa mbaya. Kwa mfano fedha za maendeleo zinazoombwa kwa Fungu 57(Wizara) ni shilingi bilioni 120; ikiwa ni pungufu ya bilioni 100 kutoka bilioni 220 zilizotengwa mwaka 2018/19. Kwa upande wa Fungu 38(Ngome) fedha za mandeleo zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ni shilingi bilioni 6 ikiwa ni pungufu ya shilingi bilioni 2 kutoka shilingi bilioni 8 iliyotengwa mwaka wa fedha 2018/19. Hali kadhalika bajeti ya maendeleo katika Fungu 39 (JKT) imepungua kutoka shilingi bilioni 6 mwaka 2018/19 hadi kufikia shilingi bilioni 2 kwa mwaka 2019/2020.

**20. Mheshimiwa Spika**, kitendo cha Serikali kutotekeliza bajeti ya maendeleo ya Wizara hii, sio tu kunalifiedhehesha Jeshi letu, lakini pia kinawaweka wananchi katika hali ya hatari kubwa. Kwa mfano wote tunafahamu jinsi matukio ya milipuko ya silaha katika maghala ya silaha za milipuko huko Mbagala na Gongo la Mboto – Dar es Salaam,

yalivyosababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa makazi ya wananchi. Katika kukabiliana na hali hiyo, ilitakiwa fedha ya kutosha ya maendeleo itengwe kwa ajili ya ukarabati wa maghala hayo.

**21. Mheshimiwa Spika**, Kama nilivyoeleza hapo awali, kwamba jeshi ni mbadala wa kila kitu ikiwa nchi iko kwenye mkwamo. Kwa sababu hiyo jeshi linatakiwa kuwa kisima cha fikra (think tank) cha taifa ili kuliondoa taifa kwenye mkwamo ikiwa limekwama. Ili jeshi liweze kuwa na uwezo huo; lazima liwekeze sana kwenye tafiti na kubobeaa katika kila sekta. Kwa vyovypote vile uwekezaji huo hauwezi kuwa wa shilingi bilioni 8 au 6 ambazo tumezoea kutenga. Bajeti hiyo ni ndogo mno kuweza kujenga maabara za kisasa zenyen vifaa vinavyokidhi teknolojia ya kisasa kuwezesha Jeshi kufanya tafiti katika nyanja mbalimbali na kulisiaida taifa kusonga mbele kiuchumi.

**22. Mhehimwi Spika**, kwa kifupi, bajeti ndogo ya maendeleo katika Wizara ya Ulinzi na JKT sambamba na utekelezaji duni wa bajeti hiyo haiendani kabisa na azma ya kulifanya Jeshi kuwa kisima cha fikra wala kuwa la kisasa lenye ufanisi.

### **C. NYONGEZA YA MISHAHARA KWA WANAJESHI**

**23. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo kwa watumishi wengine wa umma, nyongeza ya mishahara ya kila mwaka (annual increment) ni hitaji la kisheria na kikanuni na pia ni kichocheo cha ari ya kufanya kazi kwa bidii zaidi.

**24. Mheshimiwa Spika**, pamoja na uhalisia huo, zipo taarifa kwamba wanajeshi hawajapata nyongeza ya mishahara kwa ngazi zote tangu Serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani. Nyongeza ya mwisho ya mishahara, ilifanyika mwaka wa fedha 2015/2016 wakati wa utawala wa Serikali ya awamu ya nne.

**25. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishatoa angalizo kwa Serikali hii kutoa kipaumbele kwa maslahi ya wanajeshi kwa kuwa ni kada ambayo imejitoa kwa gharama

ya uhai wao katika kulinda mipaka ya nchi yetu dhidi ya adui ye yote kutoka nje na kuhakikisha kwamba Taifa lipo salama wakati wote.

**26. Mheshimiwa Spika**, si vema wanajeshi wakaanza kulalamika kuhusu masuala ambayo ni stahili zao za kisheria. Ni vema Serikali ikatambua hatari ya vyombo vyenye dhamana ya kutunza silaha kuwa sehemu ya walalamikaji. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili, ni lini italipa nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi pamoja na malimbikizo ya nyongeza hizo toka ilipositisha malipo hayo?

**D. POSHO YA CHAKULA KWA WANAJESHI (RATION ALLOWANCE) IMEGEYZWA KUWA ADA YA KULIPIA MAFUNZO KWA WANAJESHI WANAOKWENDA MAFUNZONI**

**27. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka mingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa mstari wa mbele kutetea maslahi ya wanajeshi wetu ikiwemo posho ya chakula (ration allowance). Msingi wa kutetea maslahi ya wanajeshi ni kuwapatia wanajeshi wetu lishe bora na kuwafanya wawe na nguvu ya kuhimili mazoezi na kazi mbalimbali za kiaskari wanazofanya. Aidha, lengo jingine ni kuwafanya wawe na utulivu wa ndani ili waweze kufanya kazi yao ya kulinda usalama wa nchi yetu wakiwa hawana mawazo ya kwamba watakula nini .

**28. Mheshimiwa Spika**, utaratibu uliopo ni kwamba, posho hii ya chakula hutolewa moja kwa moja kwa askari kila mwezi. Askari anayepokea posho hii huwa na uhuru nayo wa kuitumia kwa namna yoyote ile ikiwa ni pamoja na kuitumia na familia yake.

**29. Mheshimiwa Spika**, licha ya posho ya chakula kwa wanajeshi kuwa ndogo kutokana na kupanda kwa gharama za maisha; kumeibuka utaratibu mpya wa kutowalipa moja kwa moja askari wanaokwenda kwenye mafunzo na kozi mbalimbali za kijeshi na badala yake posho hiyo hulipwa moja kwa moja kwenye chuo au taasisi inayotoa mafunzo hayo

kwa ajili ya kugharamia chakula atakachotumia mwanajeshi huyo kwa kipindi chote cha mafunzo.

**30. Mheshimiwa Spika**, hii ni sawa na kusema kwamba wanajeshi hao wanaokwenda mafunzoni wanalipia mafunzo na kozi hizo kwa kutumia posho yao ya chakula jambo ambalo si haki kwao. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua; ni shilingi ngapi katika bajeti ya Maendeleo ya Wizara hii iliyotengwa kwa ajili ya kugharamia mafunzo kwa wanajeshi wetu; na kama fedha za mafunzo zipo ni kwa nini kuwalazimisha wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kulipa ile fedha yao ya chakula katika chuo au taasisi inayotoa mafunzo hayo?

**31. Mheshimiwa Spika**, licha ya wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kutoridhishwa na uamuzi huo wa kulipa fedha zao za chakula kwenye taasisi na vyuo vlnavyotoa mafunzo hayo, bado chakula wanachopewa kwa siku hakiendani na thamani ya shilingi 10,000/= wanayolipa kwa siku kwa ajili hiyo.

**32. Mheshimiwa Spika**, kutokana na madai ya wanajeshi ya muda mrefu ya kuongezewa posho yao ya chakula ili kuweza kumudu gharama maisha ambazo zinaendelea kupanda, na kutokana na malalamiko ya kutoridhishwa na uamuzi wa kulipa fedha za chakula kwenye taasisi na vyuo vya mafunzo badala ya kuwalipa moja kwa moja kama ilivyokuwa desturi; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali; mosi, kuongeza posho ya chakula kutoka shilingi 10,000/= kwa siku ya sasa, hadi kufikia shilingi 15,000/= kwa siku ili waweze kumudu gharama za kununua chakula bora.

**33. Mheshimiwa Spika**, sambamba na nyongeza ya posho hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali vilevile, kusitisha mara moja uamuzi wa kulipa fedha za posho ya chakula kwa wanajeshi kwenye vyuo na taasisi zinavyotoa mafunzo kwa wanajeshi na badala yake fedha hizo zilipwe moja kwa moja kwenye akaunti za wanajeshi husika ili wawe na uhuru wa kutumia fedha hizo wenyewe. Sambamba na hilo, Serikali ilihakikishie Bunge hili kuwa, itakuwa inatenga fedha za mafunzo kwa wanajeshi, na kwamba; itaacha mara

moja kutumia fedha za chakula kwa wanajeshi wanaokwenda mafunzoni kama ada ya kulipia mafunzo hayo.

#### **E. HALI ZA WASTAAFU WA JESHI HAZILINGANI NA UZITO WA KAZI WALIZOFANYA**

**34. Mheshimiwa Spika**, hali za wastaifu wa Jeshi, waliostaifu kati ya mwaka 1985 hadi 2000 ni mbaya sana kulingana na mafao yao ya kustaifu na pensheni zao za kila mwezi hasa kuanzia Private hadi cheo cha Brigedia Jenerali. Ikumbukwe kwamba, mionganoni mwa wastaifu hawa ni wale walioshiriki vita vya Kagera pamoja na vita vya ukombozi Msumbiji.

**35. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali ngumu ya maisha inayowakabili, wastaifu hawa wamekuwa ni walinzi binafsi katika makazi ya watu na taasisi mbalimbali na bado posho wanayoipata ni kama fedheha kwao ukililinganisha na nafasi muhimu walizokuwa nazo katika usalama wa taifa hili.

**36. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rami ya Upinzani inaihooji Serikali; haya ndiyo malipo wanayostahili baada ya kulitumikia taifa hili kwa gharama za maisha yao?

#### **F. MUDA WA SAA ZA KAZI JESHINI BADO UNALALAMIKIWA**

**37. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika mwaka wa fedha 2017/18 ilieleza katika hotuba yake juu ya malalamiko ya wanajeshi kuhusu mabadiliko ya muda wa saa za kazi kutoka saa tisa na nusu alasiri mpaka saa kumi na mbili jioni bila kupewa sababu za msingi za mabadiliko hayo.

**38. Mheshimiwa Spika**, Serikali kuititia Waziri mwenye dhamana na Wizara ya Ulinzi na JKT alisema kwamba; kwa asili ya kazi za jeshi, mwanajeshi anatakiwa kuwa tayari kwa kazi wakati wote. Kambi Rasmi ya Upinzani inatambua kwamba wanajeshi wanatakiwa kuwa tayari kwa kazi muda wote kama kuna dharura au hali ya hatari. Lakini katika mazingira ya kawaida ambapo hakuna dharura au tishio la usalama kuwaweka kazini wanajeshi kwa muda wa ziada ni

kuwachosha kiasi kwamba hata ikitokea dharura unakuta wamechoka. Lakini pia kuwaweka wanajeshi kazini hadi saa kumi na mbili jioni ni kuwanyima fursa na muda wa kufanya shughuli za kijasiriamali kama vile ufugaji, kilimo cha mbogamboga na biashara ndogondogo kujiongezea kipato. Kwa maneno mengine ni kuwaongezea umaskini na msongo wa mawazo kutokana na ukata.

**39. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imefuatilia jambo hilo na kubaini kwamba, muda wa kazi bado haujarekebishwa na kwamba bado kuna malalamiko kuhusu suala la muda wa kazi. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kurekebisha muda huo ili muda wa kutoka kazini kwa wanajeshi uwe saa tisa alasiri kama ilivyokuwa awali. Hii itaondoa manung'uniko mionganoni mwa wanajeshi na hivyo kuongeza ufanisi wa jeshi letu.

#### **G. KUNA MIZENGWE KATIKA UPANDISHAJI WA VYEZO KWA WANAJESHI**

**40. Mheshimiwa Spika**, kupandishwa cheo ni stahili ya kisheria kwa mwanaleshi yeyote aliyeko katika ajira hiyo kwa zaidi ya miaka minne na au aliyefuzu mafunzo au kozi inayomfanya awe na sifa za kupanda kutoka ngazi moja ya cheo kwenda nyingine. Pamoja na uhalsia huo, zipo taarifa kwamba kuna mrundikano wa wanajeshi wanaostahili kupandishwa vyeo kutokana na muda waliokaa jeshini (zaidi ya miaka mine) na wengine wamefuzu kozi zinazowastahilisha kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa vyeo mpaka sasa. Yapo mazingira ambayo, unakuta baadhi ya wanajeshi wamehudumu jeshini kati ya miaka mitano mpaka sita lakini hawapandishwi vyeo.

**41. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inazo taarifa kwamba kulikuwa na wanajeshi 8,000 waliofuzu kupandishwa vyeo mwezi Desemba, 2018 lakini ni 4,000 tu waliopandishwa vyeo. Hii ina maana kwamba, wanajeshi 4,000 waliokuwa na sifa hawakupandishwa vyeo. Mwezi Februari, 2019 wapo wengine waliofuzu na kuwa na sifa za kupandishwa vyeo na

Mwezi Mei wapo wengine watafuzu na hivyo kufanya idadi ya wenye sifa za kupandishwa vyeo kuendelea kuongezeka.

**42. Mheshimiwa Spika**, Ifahamike kwamba, kutowapandisha vyeo maafisa wa jeshi kwa wakati kuna athari za moja kwa moja mosi, kwenye mishahara yao; na pili, kwenye pensheni zao. Kwa hiyo, askari aliypaswa kupandishwa cheo miaka miwili iliyopita halafu akaachwa akaja kupandishwa miaka miwili baadaye anakuwa amepunjwa nyongeza yake ya mshahara ambayo ingetokana na cheo hicho na pia mapunjo hayo yanakwenda pia kuathiri pensheni za akari hao.

**43. Mheshimiwa Spika**, kutokana na utata huo wa kuwapandisha vyeo wanajeshi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili kuna wanajeshi wangapi wenye sifa za kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua kuna tatizo gani linalosababisha wanajeshi wasipandishwe vyeo kwa wakati; na kama jibu ni bajeti finyu. Je Serikali iko tayari kuwaomba radhi wanajeshi ambao wana sifa za kupandishwa vyeo lakini hawajapandishwa na kuwaahidi kuwalipa malimbikizo ya mishahara ya vyeo vipyaa pindi watakapowapandishwa vyeo?

#### **H. MCHAKATO WA MANUNUZI YA SARE ZA JESHI UCHUNGUZWE**

**44. Mheshimiwa Spika**, mionganoni mwa mahitaji msingi ya wanajeshi ni pamoja na sare zao za kazi. Na kutokana pilikapilika za shughuli za kijeshi, sare hizo hazina budi kuendana na maumbile yao; na pia kuwa na ubora wa hali ya juu ili ziweze kudumu kwa muda mrefu.

**45. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inazo taarifa kwamba; tofauti na wakati wa utawala wa awamu ya nne ambapo sare zilikuwa na ubora wa hali ya juu; na pia ziliendana na maumbo ya wahusika; sare zilizogawiwa mwaka huu wa 2019 hazina ubora stahiki na pia haziendani na maumbo ya wahusika. Jambo hili limesababisha askari kulazimika kuendelea kutumia sare za zamani ambazo

zinaonekana kuwa bora kuliko sare mpya. Sare za zamani ziligawiwa mara ya mwisho mwaka 2014.

**46. Mheshimiwa Spika**, kutokana wito wa Serikali kutilia maanani thamani ya fedha dhidi ya huduma au bidhaa wakati wa matumizi ya fedha za umma (value for money) Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia vyombo husika kufanya uchunguzi wa mchakato wa manunuzi ya sare za jeshi ili kujiridhisha kama manunuzi hayo yamezingatia thamani ya fedha dhidi ya huduma au bidhaa zilizonunuliwa kwa kutumia fedha za walipa kodi.

**I. SERIKALI KUTUMIA JESHI KATIKA SHUGHULI AMBAZO ZINAWEZA KUFANYWA NA SEKTA BINAFSI**

**47. Mheshimidwa Spika**, kwa mujibu wa Tovuti ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; mionganoni mwa majukumu msingi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni pamoja na:-

- i. Kulinda Katiba na Uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- ii. Ulinzi wa mipaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
- iii. Kufanya mafunzo na mazoezi ili kujeweke tayari kivita wakati wote.
- iv. Kufundisha umma shughuli za ulinzi wa Taifa.
- v. Kushirikiana na mamlaka za kiraia katika kutoa misaada ya kibinadamu na uokoaji wakati wa maafa
- vi. Kutoa huduma mbalimbali za kijamii.
- vii. Kukuza elimu ya kujitegemea na uzalishaji mali kupitia Jeshi la Kujenga Taifa.
- viii. Kushiriki ulinzi wa amani kimataifa.

**48. Mheshimiwa Spika**, pamoja majukumu hayo; imeanza kuzuka tabia ya kulitumia Jeshi la Wananchi katika kufanya

shughuli za kawaida za kiraia ambazo zingeweza kufanywa na sekta binafsi. Jeshi limekuwa likipewa kandarasi za kujenga majengo mbalimbali ya Serikali bila zabuni kushindanishwa. Aidha lilipewa pia zabuni isiyo na ushindani ya kusafirisha korosho kutoka Mikoa ya Kusini na kupeleka kwenye maghala ya kuhifadhiya korosho hizo.

**49. Mheshimiwa Spika**, kitendo hicho cha kulipatia Jeshi la Wananchi zabuni zisizo na ushindani, licha ya kuibinya sekta binafsi katika kupata zabuni hizo; lakini pia kimeinyima Serikali fursa za kupata mapato ya kodi na tozo nyingine kutokana na shughuli hizo.

**50. Mheshimiwa Spika**, Kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikishauri wakati wote; Jeshi ndilo linalotakiwa kuwa kisima cha fikra (think-tank) cha taifa na pia kitovu cha fursa mbalimbali kutokana na ugunduzi litakaokuwa linaufanya kutokana na tafiti za kisayansi katika kila sekta. Tofauti na matarajio hayo; Jeshi sasa limekuwa linashindana na wananchi katika kugombea fursa badala ya kuwa chanzo cha fursa kwa wananchi.

**51. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa changamoto kwa Serikali hii; kulieleza Bunge na taifa kwa jumla kwamba; ule uwezo mkubwa wa sayansi na teknolojia Jeshini ambaao ulifikia hatua ya kuvumbua gari aina ya nyumbu; ambaao ulikuwa ni kitovu cha fursa nyingi za kiuchumi kwa sekta binafsi na kwa mwananchi mmoja mmoja umekwenda wapi hadi kufikia hatua ya Jeshi kuingilia kazi za sekta binafsi?

#### **J. MABORESHO YA SHERIA YA ULINZI WA TAIFA (THE NATIONAL DEFENCE ACT)**

**52. Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Ulinzi wa Taifa ya mwaka 1966 ni ya zamani sana, na kwa vyovyote vile haikidhi mahitaji ya mazingira ya sasa. Mara kadhaa Serikali imekuwa ikiahidi kuwa itaifanya maboresho Sheria hiyo, ili iendane na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia lakini mpaka sasa ahadi hiyo haijatekelezwa.

**53. Mheshimiwa Spika**, llikuwa ni ahadi ya Serikali kwamba mapendekezo ya upande wa pili wa Muungano (Zanzibar) juu ya sheria hiyo yangetatikana baada ya kusuasua kwa muda mrefu. Ingawa kuna taarifa kwamba Zanzibar tayari wameshaleta mapendekezo yao; lakini mapendekezo hayo yatakuwa yamechelewa sana hivyo yamechelewesha pia stahiki na fursa za kisheria ambazo wanajeshi wetu wangestahili kupata toka awali.

**54. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kulieleza Bunge hilli; ni lini italeta Bungeni muswada wa marekebisho ya Sheria hiyo; ili iendane na wakati?

**55. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**56. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**57. Mheshimiwa Spika**, kulikuwa na tatizo la kuondolewa kwa alama za mipaka (beacons) kati ya nchi yetu na Kenya katika maeneo ya Migori – Kenya na Tarime – Tanzania. Zoezi la kurejesha alama hizo limechukua muda mrefu sasa bila mafanikio. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Wizara husika katika nchi zote mbili ziongeze kasi ya urejeshaji wa alama hizo; sambamba na kuboresha barabara zinazoelekea kwenye vituo teule vya kijeshi (detarcs).

#### L. SERIKALI KUSHINDWA KULIPA FIDIA KWA WANANCHI KWA MAENEKO YALIYOCHUKULIWA NA JWTZ NA JKT

**58. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasikitika kwa kitendo cha Serikali cha kuchukua maeneo ya wananchi kwa ajili ya JWTZ na JKT na kukaa muda mrefu bila kulipa fidia jambo ambalo licha kuchelewesha haki kwa wananchi hao; wamiliki wengine wanakuwa wameshafariki na hivyo kudhulimika kabisa.

**59. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua ni maeneo mangapi ya wananchi yametwaliwa na jeshi na fidia hajjalipwa mpaka sasa. Aidha,

Tungependa kupewa pia mchanganuo wa maeneo hayo kimikoa.

**M. MIGOGORO YA ARDHI BAINA YA WANANCHI NA JESHI**

**60. Mheshimiwa Spika**, kumekuwa na migogoro ya ardhi baina ya Jeshi na Wananchi ambayo kwa sasa inaanza kuathiri mahusiano kati ya Wananchi na Jeshi. Hakuna anayepinga kwamba kuna umuhimu wa kuwa mipaka ya wazi kati ya maeneo hayo na kwamba hakuna mwenye haki ya kuingilia eneo la mwenzake.

**61. Mheshimiwa Spika**, changamoto iliyopo ni kwamba Jeshi limekuwa likiachaa maeneo yake kwa muda mrefu na bila kuweka mipaka iliyodhahiri kiasi kwamba wananchi wanayatumia bila kujua kama yako chini ya miliki ya Jeshi. Matokeo yake baada ya miaka mingi (kuanzia miaka kumi na tano na kuendelea) ambapo wananchi wanakuwa wameshaweka makazi yao, ndipo Jeshi linajitokeza na kudai kuwa hilo ni eneo la Jeshi.

**62. Mheshimiwa Spika**, pamoja na upungufu huo; na pamoja na ukweli kwamba eneo husika linaweza kuwa ni mali ya Jeshi kweli; lakini njia ambazo Jeshi limekuwa likitumia kuwaondoa wananchi hao si njia za kiuungwana. Jeshi linatakiwa kufahamu kwamba ni Jeshi la Wananchi; na ardhi inayotaka kuitwaa ni ardhi ya wananchi wa Tanzania chini ya udhamini wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; kwa hiyo ikiwa lina ushahidi kuwa ardhi inayokaliwa na wananchi ilitwaliwa kwa matumizi ya Jeshi, basi halina budi kuwasiliana na uongozi wa wananchi wa eneo husika ili kutafuta namna bora ya kuwahamisha wananchi bila kuwafanya vitendo vya kinyama.

**63. Mheshimiwa Spika** nasema hivi kwa masikitiko makubwa hasa kufuatia kitendo cha kinyama kilichofanywa na Jeshi la Wananchi cha kuwabomolea makazi na kukata mazao ya wananchi wa maeneo ya Kisopwa, Mloganzila na Kiluvya "B" yaliyopo Wilaya ya Kisarawe na Bungo katika Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani, kwa madai kwamba maeneo hayo yalikuwa ni ya Jeshi.

**64. Mheshimiwa Spika**, hata kama ni kweli maeneo hayo ni ya Jeshi; lakini njia iliyotumika kuwaondoa wananchi hao si ya kibinadamu hasa ukizingatia kwamba kipindi hiki ni cha mvua na kwa hiyo baada ya kubomolewa nyumba zao iliwalazimu wananchi hao waendelee kunyeshewa mvua usiku na mchana na mali zao kuharibiwa.

**65. Mheshimiwa Spika**, Kimsingi wananchi hao wametendewa kama vile ni waasi au wavamizi kutoka nje. Ifahamike kwamba; jambo hili linajenga chuki baina ya wananchi na Jeshi na hivyo halikubaliki!!!. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inatoa rai kwa viongozi wanaohusika; ikiwa ni pamoja na Waziri wa Ulinzi; Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mkuu wa Majeshi kulichukulia jambo hili kwa uzito unaostahili na kutafuta njia bora ya kuwahamisha wananchi ambao inasadikiwa wamevamia maeneo ya Jeshi bila kuwadheru na bila kuwasababishia hasara ya mali zao.

**66. Mheshimiwa Spika**, yapo mazingira mengine ambapo baadhi ya Wakuu wa Vikosi vya Jeshi wamekuwa wakiwanyang'anya wananchi ardhii kutokana na maslahi binafsi. Kwa mfano maeneo ya Vlijiji vya Bugosi kilichopo Kata ya Nyamisangura na Kenyambi kilichopo Kata ya Nkende yalitwaliwa kwa amri ya Mkuu wa Kikosi cha Jeshi cha Makoko kutokana na tamaa ya fedha kutoka kampuni ya simu ya Vodacom iliyokuwa imeingia mkataba na wananchi wa vijiji hivyo kutokana na Kampuni hiyo kuweka Mnara wa mawasiliano katika vijiji hivyo.

**67. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa wananchi wa vijiji hivyo walikuwa wakinufaika kwa malipo ya fedha kutokana na mnara huo kuwa katika maeneo hayo; Mkuu huyo wa kikosi alilingilia kati suala hilo na kudai kuwa eneo hilo ni la Jeshi na hivyo kusababisha fedha hizo kulipwa Jeshini.

**68. Mheshimiwa Spika**, ni jambo la kushangaza kwamba kabla ya Vodacom kuingia mkataba wa malipo na wananchi Jeshi halikua na mgogoro wowote na wananchi; lakini baada ya kuona kuna fursa ya kupata fedha ndipo linadai kuwa eneo

hilo ni la Jeshi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuchunguza ukweli kuhusu mmiliki halali wa maeneo husika ili haki itendeke.

**N. USHIRIKI WA ULINZI WA AMANI NJE YA NCHI**

**69. Mheshimiwa Spika**, pamoja na ushiriki wetu wa Ulinzi wa Amani nje ya nchi kupitia Jumuiya za Kikanda na Kimataifa( hususan MONUSCO, UNAMID, UNFL, MINUSCA, UNMISS n.k.); Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua; tangu utaratibu huu uanze hadi leo hii, ni wanajeshi wangapi wamepoteza maisha na wangapi wamejeruhiwa?

**70. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inasikitishwa na uamuzi wa Serikali kuwapeleka wanajeshi wetu kulinda amani katika nchi zenyе vita kupitia mkakati wa kimataifa wa "kulinda amani" yaani *peace keeping* badala kutumia mkakati wa kutumia nguvu kupambana na waasi yaani "*enforcement keeping*" jambo ambalo limepelekea wanajeshi wetu wengi kuawa katika operesheni hizo. Kwa sababu hiyo; tunaitaka Serikali ilihakikishie Bunge hili na wananchi wote; kwamba ni lini itabadili dhana hiyo ya kulinda amani ambapo wanajeshi wetu wanakuwa na silaha nyepesi na zisizoweza kukabiliana na silaha nzito za kivita za waasi wa nchi hizo na badala yake kutumia mkakati wa nguvu – enforcement strategy ili kupunguza vifo vyaa askari wetu bila sababu za msingi?

**71. Mheshimiwa Spika**, sambamba hilo, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependza kujua vilevile ni kwa nini wajane au wagane wa wanajeshi waliofariki hawatunzwi inavyostahili kuendana na stahili za pensheni kama ambavyo wangepata stahili hizo kwa wenza wao ikiwa wangekuwa hai?

**O. AJIRA JESHINI**

**72. Mheshimiwa Spika**, moja ya sifa za kupata ajira jeshini ni kuwa, mwombaji awe amepitia mafunzo ya JKT au JKU. Hata hivyo, idadi ya wanaopata mafunzo hayo ni kubwa kuliko nafasi halisi za ajira. Kutokana na hali hiyo, wapo vijana wengi wanaofuzu mafunzo ya JKT na JKU wanaobaki mitaani bila kazi.

**73. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Serikali kufahamu athari za vijana hawa waliofundishwa kutumia silaha kubaki mitaani bila kazi ya kufanya. Miaka ya nyuma tumekuwa tukiishauri Serikali kwamba; hata kama haiwezi kuwaajiri vijana wote wanaohitimu mafunzo ya JKT au JKU, basi ianzishe programu za ufundi na ujasiriamali kwa kushirikiana na VETA wakati wa mafunzo ili vijana hao watakapohitimu waweze kupata vyeti vya VETA pia ili waweze kupata ajira katika taasisi nyingine baada ya kufuzu mafunzo ya JKT.

**74. Mheshimiwa Spika**, Lengo la kutoa ushauri huo, lilikuwa ni kutoa fursa mbadala ya ajira kwa vijana wanaohitimu JKT kutokana na nafasi chache za ajira Jeshini ukilinganisha na idadi kubwa ya wahitimu. Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kujua, Serikali imetekeleza pendekozeli hili kwa kiasi gani ili kupunguza changamoto ya ajira kwa vijana wanaohitimu mafunzo ya JKT.

#### **P. NAFASI YA JESHI LA KUJENGA TAIFA KATIKA KUCHECHEMUA UCHUMI WA VIWANDA NCHINI**

**75. Mheshimiwa Spika**, kwa takriban miaka kumi iliyopita, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikiihauri Serikali kuwekeza katika miradi ya kiuchumi ya uzalishaji katika Jeshi la Kujenga Taifa, ambayo hatimaye itapelekeea kukuwa kwa viwanda vidogo vidogo. Tulipendekeza kwamba; Serikali itumie nguvu kazi iliyopo kwenye Jeshi la Kujenga Taifa katika kujenga uchumi endelevu nchini, na hasa kwa kipindi hiki ambacho Mpango wa Maendeleo wa Taifa umejikita kwenye uchumi wa viwanda.

**76. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilipendekeza kuwa; Jeshi la Kujenga Taifa ndio liwe dira na kutoa mwongozo wa namna ya kuendesha uchumi wa viwanda. Tulishauri kwamba Serikali itenye mashamba makubwa ili vijana wa JKT wawapo mafunzoni, wafanye mafunzo kwa vitendo ya kilimo ili nchi iweze kujitegemea kwa chakula lakini zaidi sana kuzalisha ziada ambayo itatumika kwenye viwanda kama malighafi. Kwa sababu hiyo,

tulipendekeza pia kwamba; Serikali iwaagize wakuu wa makambi ya JKT kutengeneza programu maalum za uzalishaji mali katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, viwanda, ufundu, uvuvi n.k. kila mwaka na kwamba; Waziri mwenye dhamana awe anatoa taarifa ya uzalishaji uliofanywa na JKT na mapato (maduhuli) yaliyopatikana kutokana na uzalishaji huo katika kila Bunge la Bajeti.

**77. Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa ushauri huo wa siku nyingi, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupewa mrejesho wa utekelezaji wa ushauri huo. Serikali ilieleze Bunge, JKT imekeleza miradi mingapi ya uzalishaji na imeingiza fedha kiasi gani kutokana na uzalishaji huo, na ina mpango wa kuteleza miradi mingapi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

**Q. NAFASI YA JESHI KATIKA KUPAMBANA NA MATUKIO YA KIGAIDI NCHINI.**

**78. Mheshimiwa Spika**, katika bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilishauri na kupendekeza kwamba; Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, hususan kitengo cha Upelelezi wa Kijeshi (Military Intelligence) kitoe msaada wa kipelelezi kwa Jeshi la Polisi ili kubaini na kukabiliana na vitendo vya kigaidi vilivyokuwa vinafanywa na "Watu wasiojulikana" dhidi ya raia wasio na hatia.

**79. Mheshimiwa Spika**, msingi wa ushauri huo ulitokana na ukweli kwamba, kulikuwa na kila dalili kwamba Polisi walikuwa wamezidiwa mbinu na nguvu ya kukabiliana na magaidi hao. Hii ni kwa sababu kwanza matukio, hayo yalikuwa yanawalenga Askari Polisi wenywewe; lakini pili, hawakuweza kuyadhibiti nyakati yalipotokea. Itakumbukwa kwamba takriban miaka mitatu iliyopita kulikuwa na matukio ya kigaidi ya kuvamiwa kwa Vituo vya Polisi na kupora silaha, kuwauwa Askari Polisi na kuwapora silaha, pamoja na wananchi kuuwawa na hususan viongozi wa Serikali za Mitaa katika Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani.

**80. Mheshimiwa Spika**, Kutokana na Jeshi la Polisi kushindwa kujihami kwa wakati ule; Kambi Rasmi ya Upinzani ilieleza

kwamba yamkini matukio hayo yalikuwa yanafanywa na watu wenye mafunzo ya kijeshi na mbini za kivita ndio maana waliweza kutekeleza uhalifu huo bila kukamatwa na bila kujulikana kwa majina yao, na hata walikoelekea.

**81. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**82. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**83. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**84. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**85. [MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**R. HITIMISHO**

**86. Mheshimiwa Spika**, nahitimisha hotuba yangu kwa kulipongeza tena Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa utumishi wao uliotukuka wa kuilinda nchi yetu kwa gharama ya uhai wao.

**87. Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa viongozi wakuu wa Jeshi kuendelea kuwaelimisha wanajeshi walio chini yao kuzingatia maadili yao ya kazi, na kamwe wasikubali kutumika kisiasa kwa maslahi ya wanasiasa wachache wanaotaka kutimiza malengo yao ya kisiasa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuacha kabisa kulitumia jeshi kwa shughuli ambazo zinaweza kufanywa na sekta binafsi na badala yake iwekeze katika sayansi na teknolojia Jeshini ili Jeshi liwe kitovu cha fikra na ugunduzi na hivyo kuwa chanzo cha fursa mbalimbali za kiuchumi kwa wananchi.

**88. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imebaini pia kwamba, bajeti ya Wizara ya Ulinzi na JKT imekuwa na mserereko wa kushuka na pia ile kidogo inayotengwa haitekelezwi ipasavyo. Tunataka Serikali itambue kwamba; kuchelewesha au kutopeleka kabisa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye Wizara hii ni kuuweka

rehani ulinzi na usalama wa taifa hili. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kutofanya mzaha kabisa na bajeti ya Wizara hii na kwa maana hivyo tunaitaka Serikali itekeleze kikamilifu bajeti itakayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii.

**89. Mwisho Iakini si kwa umuhimu; Serikali itilie maanani maneno ya Mwanafalsafa Albert Einstein kwamba;** Amani ya kudumu haiwezi kupatikana kwa vitisho, isipokuwa tu kwa jithada za dhati za kutengeneza mazingira ya kuaminiana. Na mazingira ya kuaminiana yatajengeka tu kama Serikali na viongozi wenye dhamana ya uongozi wa nchi hii watatenda haki kwa kila mmoja wetu. Daima tukumbuke wosia wa Albert Einstein kwamba; hata silaha ziwe na nguvu kiasi gani, haziwezi kulisaidia jeshi kuleta hali ya usalama kwa taifa lolote na pia haziwezi kuwa tegemeo la uhakika la kuleta amani.

**90. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inatoa wito kwa Serikali kutenda haki kwa kuwapa wananchi uhuru kamili wa mawazo, kukusanyika, kuandamana, kukosoa na haki mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii kama njia thabitii ya kudumisha amani ya nchi yetu.

**91. Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Cecil David Mwambe (Mb)

**Kny:MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI  
KATIKA WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA**

16 Mei, 2019

**MWENYEKITI:** Bado upo hapo Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kwa sababu sasa tunataka kuanza kuchangia, lakini kwa kweli ningependa kupata mwongozo kabla ya uchangiaji haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Msemaji wa Kambi ya Upinzani alipofika kifungu cha 55 anapozungumzia hali ya ulinzi na usalama na mpaka ya nchi na alipofika kifungu cha 56 amezungumzia hali ya kisiasa na hali ya Mgombea Urais wa Kiti cha Urais katika nchi ya Malawi na kuihusianisha na mgogoro wa mpaka kati ya nchi yetu na nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linahusu mahusiano ya kidiplomasia na hatuwezi kuliacha Bunge hili linamaliza kuipokea hotuba hii na kuacha maelezo haya yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani yakihalalisha kile wanachokiamini wao kuhusu nchi nyingine na taratibu za uendeshaji wa demokrasia katika nchi hiyo nyingine na kuoanisha na mgogoro wa kimahusiano ya kidiplomasia na nchi yetu na ukikumbuka Mheshimiwa Rais ni hivi karibuni tu Rais wetu na *delegation* kubwa ya viongozi katika nchi yetu walikuwa kule katika Taifa la Malawi na kudhihirisha kwamba mahusiano yetu kati ya Malawi na Tanzania ni makubwa na yako salama na ni mazuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuondoa jambo hili kwenye hotuba hii ya Kambiya Upinzanitunaweza kabisa kuibua mjadala na mgogoro wa mahusiano ya kidiplomasia ambao utakuwa umechipuka ndani ya Bunge letu. Ninaomba mwongozo wako kama jambo hili linastahili kubaki kwenye hotuba hii ama linatakiwa liondolewe.

**MWENYEKITI:** Ulisema 56?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Aya ya 55 hali ya ulinzi na usalama ambayo inaenda mpaka aya ya 56.

**MWENYEKITI:** Aya ya 56, Makatibu na watu wa *Hansard* aya za 55 na 56 zinaondolewa katika Taarifa Rasmi za Bunge, hiyo ndiyo *rullingi* ya kiti. Spika ni mimi leo, mimi ndio Spika soma Kanuni ya sita, ndio ishatoka. (*Makofii*)

Kwa hiyo, watu wa *Hansard* na Makatibu aya za 55 na 56 ni uchochezi zinatoka wala hazina *interest* ya Taifa, kwa hiyo tumeziondoka.

**MHE.JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Ehee Mheshimiwa *Chief Whip* - Upinzani.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imezuka tabia ya mashangilio huku Bungeni ya kutaja vyama, sasa nimesikia CCM oyeee sasa nauliza, je, mashangilio hayo yanakubalika ili na wengine wakifanya wasije wakachukuliwa hatua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* wa Upinzani mimi sikusikia nitakwenda kwenye *Hansard* kama imesemwa. Ahsante. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza kuchangia muda wetu ni mdogo, tunaanza na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MBUNGE FULANI:** *Peoples...*

**WABUNGE FULANI:** *Power.*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii kwa kuwa mchangiaji wa kwanza katika hotuba ya Waziri wa Ulinzi.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wote wa Wizara hii, mimi naomba nikuombe pamoja na wenzetu, lakini kwa Wabunge wote haipendezi hata kidogo kuzungumzia kuhusu posho, maslahi ya wanajeshi wetu humu ndani kwa kufanya hivyo kwa sababu hawa nao ni wafanyakazi pamoja na kazi nzuri wanazofanya lakini bado tuna Jeshi la Polisi, tuna Jeshi

la Magereza lakini bado kuna wafanyakazi wengine tunaposide kwamba eti hawa waongezewe posho ni kuwagombanisha hawa wanajeshi na Serikali yao.

Niwaombe sana ndugu zangu tusijipendekeze kwa kusema humu ndani eti waongezewe posho naomba sana. Jeshi hili lina utaratibu wake kuhusu maslahi, Jeshi hili lina utaratibu wake namna ya upandishwaji vyeo, hawapandishwi hivi hivi, tuwaachie wenyewe wafanye kufuatana na utaratibu wa kwao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri kwasababu ya kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara hii kupitia Jeshi letu, kupitia *CDF* na JKT wanafanyakazi nzuri sana niwape tu *assurance* kwamba bajeti hii itapita bila matatizo ili muende mkafanye kazi ya kulinda nchi yetu ndani na nje.

Mimi nina maombi mawili; la kwanza ni ushauri lakini pili ni ombi. Ombi langu la kwanza Mheshimiwa Waziri tulipokuwa pale Mlale nilitoa ombi mbele ya Amiri Jeshi Mkuu, mbele ya *CDF*, lakini na Mkuu wa JKT, nilisema hivi Kanda ya Ziwa kwa maana ya Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita, Chato na Singida hakuna Kambi ya JKT na hili ni suala la kisera Mheshimiwa Waziri. Tunaomba sana tunaomba sana Kanda hiyo siyo kwamba imesahaulika hapana, nafikiri ni utaratibu na muda ulikuwa bado haujafika nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri kwa Kanda hii ya Ziwa hebu tupate Kambi ya JKT. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kwimba, Tarafa ya Mwamashimba tunalo eneo la ekari 3750 nina uhakika eneo lile kwa sababu halitumiki kwa sasa, halitumiki vizuri eneo lile najua litatosha kwa ajili ya Kambi yetu ya JKT. Vijana hawa watakaokwenda pale mbali na Kambi najua watafanyakazi ya kilimo, ufugaji kwa kufanya hivyo watapata ajira kupitia ufugaji na kilimo. Niombe sana Mheshimiwa Waziri hili ulibebe kwa sababu nililisema siku ile na leo narudia tena kusema mbele ya viongozi wakuu, hebu mlibebe hili kwasababu Kanda yetu ya Ziwa kwa kweli haina Kambi ya JKT na

nikuombe Mheshimiwa Waziri kama nilivyoomba pale Kwimba Mwamashimba tunalo eneo la ekari 3750. (*Makof*)

La pili hili ni ushauri, vijana waliopitia JKT wanasifa kuu kadhaa ni wakakamavu, ni wachapakazi, ni wazalendo, ni watu wanaojituma, ni watu wenyewe nidhamu na wavumilivu sasa vijana hawa Mheshimiwa Waziri, kwa mwaka 2001 tuliporudisha JKT mpaka 2014 vijana walioenda JKT walikuwa 104,594. Walipomaliza walioajiriwa/waliopata ajira ni asilimia 24 tu katika vijana 104,594. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri hawa vijana hawa wanafundishwa namna ya kutumia silaha za moto kundi kubwa hili la watu/la vijana karibu 76,000 linaenda vijijini, wakija wale ndugu zetu wa nchi zinazotuzunguka wakawashawishi kwa sababu hawana kazi, lakini wamejifunza namna ya kutumia silaha kwa njia moja, sitaki ..., wanaweza kushawishika, lakini nikuombe Mheshimiwa Waziri wanaweza wakashawishika kwenda kujunga na makundi mengine yaliyoko nje.

Sasa ombi langu tunayo maeneo mazuri ya kilimo, madini, uvuvi, mifugo hebu hawa vijana hawa kwa sababu ni wataalam hebu tuwachukue tuwapeleka kwenye maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi. Kwa mfano ukichukua vijana ukawapeleka Kanda ya Ziwa ile kanda yote ile ni ya uvuvi, ukiwapeleka kule watafanyakazi ya kuvua pamoja na kuchakata samaki. Ukiwapeleka maeneo ya mifugo pale Mpwapwa na maeneo mengine watafanya kazi ya kufuga lakini pamoja na kuchakata mazao ya mifugo, hili ni jambo ambalo kuliko kuwaacha tu hawa vijana hawa ambaa ni wengi kila mwaka tunawazalisha, niombe sana Mheshimiwa Waziri vijana hawa wa JKT tunaweza tukawapeleka wakafanyakazi nzuri zaidi kuliko kusubiri ajira, lakini wanaweza wakajiajiri wao wenyewe kutegemea na mafunzo wanayoyapata. Ajira haziwezi kutosha sijui kwenye Mashirika ya Umma wala sio Serikalini, lakini bado wanaweza wakajiajiri kwa kazi ya kulima, kufuga, uvuvi na kwenye madini. Huo ndiyo ulikuwa ushauri wangu.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Fakharia Khamis, ajiandae Mheshimiwa Anatropia Theonest.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na Amiri Jeshi Mkuu wa Jeshi hili na pia sitomsahau Mkuu wa Jeshi la Nyuki Zanzibar ambaye kwa umahiri wa kazi zake anavyozifanya pamoja na viongozi wote wa Jeshi mliokuja hapa Bungeni leo, hongereni kwa Waziri wenu alivyotoa hotuba yake vizuri, hotuba yake ndogo lakini imeeleweka na imefahamika na tumeielewa nya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia nyumba za makazi za wanajeshi Zanzibar. Nyumba ziko chakavu za muda mrefu ukiangalia tuliokuweko Brigedi ya Nyuki pale Zanzibar, tayari ni chakavu za zamani toka Mapinduzi walivyozijenga, ukija Mtoni unakuta hivyo hivyo, ukienda Mwanyanya na kwininge kote, angalau mngezifanya ukarabati zikaridhisha angalau na wanajeshi wakawea kukaa pahala wakatulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiendelea utaangalia kwamba hizo Kambi zenyewe tayari ziko uraiani, ukija Brigedi ya Nyuki imezungukwa mpaka nyuma yake kuna soko, ukija Mwanyanya imezungukwa na raia, ukija Mtoni tena pale ndio imekuwa mashaka maana kuna mtu amejenga ameingia ndani ya Kambi ambaye ni mtu maarufu ambaye tuna wasiwasi mtu maarufu akikaa pahali kama penye Jeshi ni tatizo kwa kweli. Sasa ningeona lazima muweze kujipanga. Sikwambieni muhame kwa sababu nikisema muhame kwa Zanzibar ile mnakwenda wapi, lakini inabidi muweze kutoa elimu ya kutosha kwa wale wanaokaa pale na tuchukulie isije ikatokea kama yale yaliyotokea Mbagala inatakiwa mtoe elimu, muwaeleweshe, muwape mipaka yao wanatakiwa wanafika wapi na wapi ili kuimarisha ulinzi wa Kambi zenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja lingine kuhusu malipo ya fidia ya maeneo yaliyotwaliwa au yaliyochukuliwa na Jeshi, ukurasa wa 30 umeelezea na nimeshukuru kwamba

umesema Kigoma kule tayari mmelipa, na kule Lindi tayari mmelipa ambapo hili ni mwanzo mzuri na hayo mengine waliobakia wanadai fidia zao m jitayarische nao muwalipe kwa sababu mtu akianza uzuri amalizie uzuri na kwa wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali walituarifu kwamba JKT na JKU wataweza kupata ajira ya Jeshi na ninajua hivi karibuni kama nilimsikia Mheshimiwa Rais akilizungumza hilo. Sasa nilikuwa nataka kujua hatua aliyofikia katika ajira hiyo wamefikia hatua gani, tunataka kujua pia na fedha hizo za kuajiri hao vijana wetu wanazo, kwa sababu ukiwaajiri vijana kutoka JKT na JKU unapata vijana wazalendo. Kwa sababu kule Jeshini wanafundishwa somo la uzalendo, ukakamavu na heshima, sasa ukipitia kwenye misingi ya kuwachukua wao unapata watu waliobora na watoweza kuli heshimu Jeshi na kuwa heshimu raia wao na kuheshimu utendaji wao wa kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukija suala la haki za wastaa fu wanaomaliza muda wao wa kazi wanajeshi. Unajua kwa wale waliokuweko Zanzibar wakati wanapomaliza wakistaafu wanapata shida kwenda Bara kufuatilia mafao yao na nilishazungumzia mara nyngi. Kwanza inapendeza unapostaa fu unapewa chako kabisa, *ki-cheque* chako mkononi, unaondoka. Maana hii kumpeleka mara kaenda Bara kufuatilia mara karudi unamtia umaskini, kwa sababu pesa yenewe hana na kwenda na kurudi unamuongezea umaskini.

Sasa Mheshimiwa Waziri nataka akija aniambie ile Ofisi ya Zanzibar itashughulikia pensheni kwa waliokuweko Zanzibar viyi ipo au itaan zishwa au mnachukua hatua gani au bado waendelee kupata usumbufu na kuhangaika kwenda huku na huku? Ningemba na hilo nilijue Mheshimiwa Waziri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja la mwisho mambo ya michezo, michezo ajira, michezo ni afya, michezo maingiliano baina ya upande huu na upande huu na tuna michezo yetu ya aina mbalimbali na ninyi mnao vijana wenu

mahiri wa JKT na JKU, kwa nini hao hamuwafanyi ndio vijana wa Taifa? Kwa sababu tayari wana umahiri, mnawafundisha michezo, wana uwezo ili watakapokuwa mkiwapeleka kwenye Kambi zetu za michezo mpira kitaifa, riadha kwenda mbio, hebu liangalieni na hili badala ya kuokota vijana hatukatai vijana mitaani kuwa mnakuwa nao lakini ingekuwa jicho lenu kubwa mnalenga hawa vijana ambaa mmewasomesha JKT na JKU. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba kuwatangaza wageni wa Mheshimiwa Lusinde ambaa wanatoka Shule ya Sekondari Mvumi wapo wanafunzi 40 na walimu 12, karibuni Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Anatropia dakika tano, ajiandae Mheshimiwa Msabaha dakika tano.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru kwa nafasi, niipongeze hotuba ya Kambi ya Rasmi ya Upinzani Bungeni wamesema dhahiri kwamba Jeshi lifanye kazi ya kulinda mipaka ya nchi na ninarudia Jeshi letu tunalipenda sana liendelee kupambana tunapongeza uzalendo wao watulinde. Mambo ya ndani ya nchi kwa maana mambo ya siasa tuwaacie wanasiada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hoja mbili kwa sababu ya muda, changamoto ya bima ya afya kwa wanajeshi; natambua kwamba wanajeshi wanatibiwa na wanaambiwa watimbiwe kwenye Hospitali ya Jeshi, lakini changamoto inatokea kwamba si kila sehemu ya nchi hii kuna Hospitali ya Jeshi. Wanaopaswa kutibiwa wakati mwengine ni wazazi wa mwanajeshi, ni mwenza wa mwanajeshi na watoto na sio lazima wote wawe wanaishi kwenye eneo la kambi. Nadhani Wizara iangalie na iipe kipaumbele kama ambavyo sisi tunatibiwa na bima za afya na kuchagua ni wapi pa kupata matibabu basi na wanajeshi wazalendo wanaopigania nchi hii wapate haki hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nitaongelea Fungu Namba 39 ambalo ni JKT natambua JKT kwamba inafanya biashara kwa kupitia Shirika lake la SUMA JKT. Lakini kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye SUMA JKT kiasi kwamba wakati mwingine nakuwa napata wasiwasi CDF wanavyokuwa wa busy anafanyakazi au awaza kufanya kazi ya IGP huku SUMA JKT mbona mambo hayaendi sawa? [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT wamekuwa wanajingiza kwenye mikataba ambayo si tu haina tija kwa Taifa lakini inahatarisha hata uhai au afya ya usalama wa ndani ya nchi yetu mfano SUMA JKT waliingia mkataba na Shirika/Kampuni ya Kichina la *Holley* ambayo baadae ikaja kuitwa *Tanzansino* mwaka 2016. Walitaka kuingia kwenye biashara ya kuzalisha madawa mkataba ukavunjika, lakini sehemu ya ubia ya mkataba illkuwa ni ardhi ya jeshi, makubliano yakawa katika kuvunja mkataba na ile sehemu ya jeshi ikatolewe ardhi ikatolewa kati China na Tanzania. Walilazimika kutoa fedha kwa ajili ya kunusuru ardhi ya jeshi, you can imagine watu wanaingia mkataba mpaka kukubali eneo ya jeshi liwe sehemu ya makubliano ya lile eneo ni hatari sana kwa mustakabali wa uhuru wa nchi yetu au mambo ya ndani ya nchi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili hawa hawa SUMA JKT walingia mkataba na *Cami* katika kiwanda chao cha uzalishaji nguo kinaitwa *Cami Suma*. *Cami Suma* walipaswa kuzalisha nguo, walilenga kulisha Afrika Mashariki na Afrika kwa ujumla. Mkataba umevunjika, hakuna kilichoendelea, lakini kinachosikitisha kati ya *Tanzansino* na *Cami Suma* waliendelea kutoa fedha zaidi ya milioni kumi kwa ajili ya ku-service zile mashine, lakini pia na umeme. Unaona kwamba wanaingia kwenye mikataba mibovu, fedha zinatumika na hakuna tija inayopatikana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio huo tu mkataba waliingia pia SUMA JKT na shirika moja linaitwa *Equator Automatic Company* ambayo hii nayo ni ya China, lengo lao lilikuwa kuunganisha magari makubwa, magari ya fire, vifaa vikubwa

kwa ajili ya ujenzi mkataba huo huo ukasuasua. Mkataba sasa hivi upo kwenye *wind up*, wakaingia kwenye mkataba mwingine na Kampuni ya Kichina inaitwa *Chenggong Limited* huo mkataba ambao ni wakuingiza mashine kubwa kubwa kwa ajili ya ujenzi, kukodisha lakini pia na kuza. Mpaka naongea hapa kumekuwa nakusuasua kwa vibali kwa sababu wakati mwingine mashine zinazoingizwa nchini ni kubwa. Huo ni mfano mdogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT ambayo inauza haya matrekta ambayo yote tunayajua ali maalufu kama SUMA iliingia mkataba na Kampuni ya *URSUS SA* kutoka Poland ikiwa ni mkataba wa zaidi ya bilioni 119. Huo mkataba wenyewe masharti hayakutimia mpaka tunavyoongea leo masharti hayakutimia kuna baadhi ya mashine hazikuja na tunavyoongea leo humu ndani kuna zaidi ya Wabunge wanadaiwa millioni 500 hawajalipa, watumishi wa umma wanadaiwa zaidi ya bilioni moja hawajalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajiuliza hiyo SUMA JKT ipo kwa ajili ya kusaidia Taifa kwa kuititia biashara au ipo kwa ajili ya kuangamiza Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, na badala namshauri *CDF* ajikite katika kusaidia hizi taasisi, kwa mujbu wa *CAG* taarifa ya 2015/2016 kumekuwepo na zaidi ya bilioni 1.14 zimetumika bila kufuata matumizi ya manunuzi ikiwa ni pamoja na bila kupita kwenye Bodi ya Wakurugenzi. Kuna changamoto kumbwa sana ambayo kama Jeshi tunalolitegemea litulize...

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Msabaha, ajiandae Mheshimiwa Rehani. (*Makofii*)

### **MWOGOZO WA SPIKA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mwongozo, Mwongozo, Mwongozo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mwongozo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ni jambo la mwongozo ni jambo siwezi kusema ni dogo ama ni kubwa naomba tu nipate mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyejita lakini pia nimeisikia hata kwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani unaona kuna jambo hapa tusipopatiwa mwongozo wa kiti chako na tukaliacha si jambo sawa na sidhani kama tutakuwa tunatendea haki *CDF* ama jeshi letu la ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji aliyejita anasema *CDF* ajikite katika kusimamia suala zima la SUMA JKT, nakubalina na aache kuingilia shughuli za /GP. Sidhani kama mwongozo wa kiti chako utaturuhusu jambo hili liendelee kusemwa semwa hapa ndani si jambo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambu sera yetu ya ulinzi na usalama inayo maeneo ya kipaumbele kati ya maeneo hayo ni pamoja na kulinda mipaka yetu kazi ya Jeshi hili ni pamoja na kutoa msaada kwa vyombo vingine vya ulinzi na usalama na vinapofika kwenye kazi ya kutoa msaada kwa vyombo vingine vya ulinzi na usalama sisi Wabunge ni mashaidi Jeshi la Polisi na Jeshi letu la Wananchi wamefanya kazi nzuri kule Njombe kuokoa mauaji ya watoto. Wamefanya kazi nzuri sana kule Rufiji na Kibiti kukomesha mauaji. Sasa ninaomba mwongozo wako, ni kwa nini jambo hili... (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Chief Whip* nakubaliana na wewe kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(b) tunajadili hoja ambazo zipo mbele yetu na kwa kweli haya maneno, ni maneno ya uchochezi, na wala si maneno ya msingi na nimeyaondoa, pengine utasema kwa kifupi ni vivu tu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Msabaha.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kunitete na nikiwa kwenye swaumu Ramadhani naendelea

salama nimshukuru Mungu. Awali ya yote Mwenyezi Mungu nimuombe aniongoze niongee kauli ambayo itampendaza Mwenyezi Mungu na itapendeza Tanzania kwa ujumla. Niipongeze kwanza Kambi ya Upinzani kwa hotuba waliyoiwasilisha na haya waliyoyatoa namuomba kaka yangu Mheshmiwa Waziri ni mweledi, ni mwerevu na makini, ayachukue na ayafanyie kazi katika Wizara yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita kwanza kauli zinazotolewa na Wakuu wa Majeshi tuangalie, kauli yoyote inayotolewa na Mkuu wa Jeshi ni kauli wananchi, ni kauli ambayo inatakiwa iwe ni kauli ambayo haina ukakasi, iwe ni weledi kwa sababu mwaka 1978 ilikuwa ikitolewa kauli kwenye Jeshi, wananchi wote wanasmama, wanatulia, wanasiliza kauli hii ina kitu gani. Lakini sasa hivi tumeona Jeshi letu linaanza kutanatoa kauli ambazo zina ukakasi, kwa hiyo, nimuombe Mkuu wa Majeshi awe mweledi kwa kutoa kauli ambazo zitaenda na Taifa letu na Tanzania kwa ujumla bila ya kuuingiza siasa ndani yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna wanajeshi wachache wanaochafua jeshi, wanaingia mitaani wakunywa pombe za watu, wanavunjwa vitu vya watu, hawalipi pesa, wengine wanawapa wanawake mimba hawawashughulikii wanawake, hawawapi mahitaji na hata wanavyokwenda kutaka mahitaji yao wanakutana na Wakuu wa Majeshi kwa hiyo sasa inakuwa tunaongeza watoto wa mitaani. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri alifuatilie kwa kina maaskari wote wanajeshi wanapowapa wanawake mimba basi wanawake hawa wapate stahiki zao na walelewe watoto, tutoe punguzo la watoto wa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tulikuwa na kiwanda chetu tulikuwa tunaona wanajeshi wanunuviatu kutoka Bora walikuwa wanavaa viatu vizuri. Lakini sasa hivi viatu hivi vinatengenezwa China, havina umahiri wowote yaani buti likipigwa mara moja tu kiatu kinachanika. Sasa ni kwa nini hivi viwanda vya ndani visiimarike, vikatunzwa, vikatengewa bajeti ya kutosha vikatengeneza sare za wanajeshi na viatu vya wanajeshi. Kama Magereza na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukiangalia pia kwenye masuala ya makazi ya wanajeshi tumeona wamejitalidi kwa kweli wamejenga makazi ya wanajeshi. Lakini kwenye makazi ya wanajeshi tunaona kuna ubadhirifu uliotumika, ni kwa nini sasa wasitumie wakandarasi wa ndani angalau tungepata hata makazi bora na bora zaidi kuliko haya makazi haya yaliyojengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuangalie migogoro ambayo inatokewa kwenye mipaka, maeneo ya Jeshi ambao wananchi wanayavamia niombe Jeshi wafanye uhakiki kwenye mipaka ya Jeshi ili hawa wananchi ambao wanaseoga kwenye mipaka ya Jeshi na kujenga na kuanza kulima mazao kwa baadae wanavyokuja wananchi kuwabomolea wanajenga taswira mbaya na chuki kwa wananchi.

Kwa hiyo, niliombe Jeshi pia wahakiki mipaka yote ya Jeshi na kuhakikisha wananchi ambao wamevamia maeneo ya Jeshi wanatolewa kwa utaratibu unao stahiki kama wengine wanalipwa stahiki zao pia waondoke sio kuharibu mazao ya wananchi, na pale labda wananchi wamelima vitu vile basi angalau wawape muda wakishavuna wawaambie basi waondoke sio kuwapiga. Kwa sababu wananchi wengi wategemea Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tuangalie wastaafu wa Jeshi pia hawajalipwa stahiki zao, wale ambao wanadai stahiki zao zilipwe kwa wakati hizi stahiki zilipwe za wanajeshi kwa sababu imekuwa siku nydingi sana wanavyomaliza basi wanachukua muda mrefu hawapewi stahiki zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Rehani ajiandae Mheshimiwa Malembeka.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii kukushuruku kwa kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kuzungumza mambo mtatu ambayo zaidi ni kushauri katika Jeshi letu hili na hasa kwenye upande wa JKT. JKT kwa sasa tunaweza kusema kwamba ni moja kati tegemeo na nguzo mahiri kabisa ambayo inaweza kututolea vijana ambao wanaweza kushiriki harakati mbalimbali Jeshi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kubwa zaidi tunachotaka hapa ni kuweza kutolewa mafunzo yale ya ueledi zaidi katika Jeshi letu hili la JKT na hasa yale ya kuwafanya vijana wale wakitoka pale waende wakajitegemee. Pamoja na mafunzo yanayotoka sasa hivi, lakini bado hayawajengi wale vijana na kuwapa ile *confidence* ya kumaliza JKT na kuweze kwenda kujitegemea na wengi wao wanakwenda kwa mawazo kwamba hawapati ajira kitu ambacho Serikali haiwezi ku-*afford* kuwapa ajira watu wote ambao wanaweza kwenda katika maeneo haya ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wito wangu kwa nini kusianzishwe programu maalum ndani ya JKT ambazo zitawafanya vijana wale waweze kuwa mahiri hasa kwenye upande wa kilimo, mifugo na uvuvi. Tuna mahitaji mengi vitu sasa hivi katika nchi yetu lakini tuna matishio ya hali mbalimbali za hali ya hewa ambazo zinakabiri mazingira yetu kama tungeweza kuliimarisha Jeshi hili la JKT hasa kwa kuzalisha kwenye kilimo cha umwagiliaji maji wakaweza kuzalisha mazao mengi kabisa hasa na tatizo hili la upungufu wa chakula au tishio la ukame ambalo linatokea katika maeneo yetu mbalimbali tungeweza kulikabili na hii ingekuwa ni sehemu moja ya kuwa na *food reserve* kuliko hali inavyokwenda sasa hivi. (*Makofii*)

Kwa hiyo, wito wangu zaidi ni kulitaka jeshi hili lijitetengeneze upya na kuweza kujitegemea hasa kwa ajili ya chakula na mimi maoni yangu binafsi ningependelea wangeweze kuwa kama walivoambiwa Magereza na wao JKT waweze kujitegemea kwa chakula na sio Serikali iweze kuwalisha siku zote wakiwa makambini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika eneo hili ningeomba JKT kupitia Shirika lake lile SUMA na mashirika mengine yaliyoko katika Jeshi la Kujenga Taifa, Jeshi la Wananchi kuweza kujenga ile bandari ya uvuvi. Jeshi limeweze kulipa eneo lile Ras Mshindo, eneo ambalo ni sahihi kabisa kwa ajili ya kujega bandari ya uvuvi. Bandari ile haitaumika kwa sababu ya uvuvi lakini itatumika kama ni sehemu ya karakana meli mbalimbali ambazo zitakuwepo pale ziwe za kijeshi, ziwe za wananchi, ziwe za nje, za sehemu nyingine mbalimbali ambazo zitatengeneza mazingira mazuri ya fedha na kulifanya Jeshi kuwa na mitaji na miradi ya mikakati zaidi kuliko hali inavyokwenda hapa.

Lakini vilevile itadaia katika eneo lile kuweza kulinda mazingira sasa ya bahari kuliko sasa hivi maeneo yetu ya bahari umekuwa ni mkubwa, lakini Wizara inayohusika na taasisi nyinginezo hazina doria wala udhibiti wowote wa mazingira ya bahari tunalitegemea jeshi hili liweze kuzunguka katika maeneo yetu ya bahari yaweze kyalinda, lakini kudhibiti uchafunzi ambao unafanyika hasa sasa hivi ulioingia utupaji wa takataka za kemikali katika bahari zetu na maeneo yetu mbalimbali ya uzalishaji. Kwa hiyo, ningeomba zaidi Jeshi hili lingejikita katika mwelekeo huo na kuweza kujiimarisha zaidi katika maeneo yetu ya bahari ambayo yana fursa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka nilizungumze ni suala zima ya kuimarisha vikosi vyetu hasa kwenye mambo ya michezo kuna fursa kubwa kupitia Jeshi hili la JKT na Jeshi la Wananchi kuimarisha michezo kama ilivyokuwa zamani inavyoonekana sasa hivi ule mwendelezo hasa na makakati uliokuwepo umepungua nguvu.

Kwa hiyo, nimkumbushe Waziri lakini nimkumbeshe CDF na wenzake ya kuweza kuimarisha michezo na kulifanya Jeshi kuonekana kwamba ndio ramani sasa ya michezo Tanzania kama wanavyotumia wenzetu kwa sababu ukiangalia Marekani, Uingereza na maeneo mengine wanajeshi ndio wanakuwa wameshika hatamu hasa michezo na inakuwa ndio dira na nembo ya Taifa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningemuomba *CDF* kuangalia mbinu na njia gani ya kuimarisha sekta hii ya michezo katika Jeshi ambavyo inaweza kutusaidia kuwafanya wanajeshi wetu kuwa mahiri lakini vilevile na kutunza afya zao kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nakushuru sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Malembeka ajindae Mheshimiwa Kanali Masoud.

**MHE. ANGELINA ADAM MALEMBEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye Wizara hii. Kwanza namshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuniamsha salama. Nitoe pongezi kwa Amiri Jeshi Mkuu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Joseph Pombe Magufuli kwa kuiongoza nchi yetu vizuri na kazi nzuri anazo zifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Waziri mwenye dhamana kwa kazi nzuri, zenye tija zinazoendelea kufanywa kwenye Wizara yake, pongezi hizi pia ziende pia sambamba kwa makamanda na Maafande wote nchi bila kuwasahau watendaji wao katika nafasi zao. Kipekee napenda kuwapongeza vijana wote wanaojitolea katika Jeshi la Kujenga Taifa tunawatambua, tunathamini mchango wao na tunawajali sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania nasema ni salama na usalama huu unatokana baina ushirikiano baina ya Wizara hii, Wizara nyingine pamoja na wananchi na pia niwakumbushe wananchi kwamba usalama wa nchi ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunao vijana wengi ambaeo bado hawajapa ajira japo wamekuwa wakijitolea katika vituo vya JKT hapa nchini. Ninaomba Serikali iangalie upya jinsi gani wataweze kuwa ajiri vijana hao. Lakini pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais ambaye

aliweza kuruhusu ajira zitolewe kwa vijana waliojenga ukuta wa Marerani na waliojenga Mji wa Seriakali hapa Dodoma. Lakini Waziri atakapokuja atuambie Wizara yake imejipangaje kwa ajili ya kutoa ajira kwa vijana hao badala ya kusubiri matamko ya Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze pia SUMA JKT kwa kazi nzuri wanazifanya. Wamekuwa wakifanya kazi nzuri na zenye uhakika na gharama naafuu naomba tuenelee kuwaamini na kuwapa kazi ambazo zinaonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu limekuwa na ushirikiano mzuri na majeshi mengine katika nchi nyingine katika masuala ya ulinzi na amani na usalama kwa ujumla wake, katika kuboresha maslahi ya watendaji katika vyombo vya ulinzi na usalama ningependa kujua kwa jumla Mheshimiwa Waziri wiki nzima hii tumekuwa na *clipau* taarifa ambazo zinatembea kwenye mitandao zikionesha baadhi ya Watanzania na wananchi wa nchi jirani ambao wanasema kwamba wamepigwa Afrika Kusini au wamechomwa moto. Sasa Waziri angetuambia taarifa hizi ni za kweli au ni mitandao tu na kama ni kweli Waziri anatueleza nini kuhusiana na hilo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala la ulinzi na usalama limo katika llani ya Chama cha Mapinduzi 2025 na pia limo katika Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa miaka mitano, 2016/2017 mpaka 2020/2021 na utekelezaji wa majukumu mengine katika Wizara hii, mimi naomba niwashawishi Wabunge wenzangu tukubali na kuipitisha bajeti ya Wizara hii ili waweze kuweka mazingira mazuri ya JKT na kuimarishe mafunzo ya vijana, pia kushirikiana na Umoja wa Mataifa (*UN*) na Umoja wa Afrika katika shughuli za ulinzi na amani. Pia waweze kushirikiana na mataifa mengine katika kupambana na uhalifu unaovuka mipaka ikiwepo ugaidi, uharamia na biashara haramu ya madawa ya kulevyia. Lakini pia kuviwezesha vyombo vya ulinzi na usalama kuviongezea rasilimaliwatu na fedha ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Sambamba na hilo kufanya tafiti mbalimbali zenye maslahi kwa wanajeshi na raia kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono maombi ya bajeti kwa ajili ya Wizara hii, ninaomba Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze ni lini Serikali italipa fidia au kurejesha maeneo ambayo wanajeshi walichukua kutoka kwa raia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi pia limeweza kuwekeza katika maeneo mbalimbali, lakini katika uwekezaji wake ni vizuri aje atueleze ni utaratibu gani unaotumika unaotumika katika uwekezaji unaofanywa na Jeshi bila kuzingatia mipango miji na haiba ya mji. Nikitolea mfano Jimbo la Welezo eneo la Jeshi kuna biashara pale za gereji, za kuuza miti, kuuza vyakula, kuosha magari wote katika eneo moja. Naomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo jeshi limekuwa na kumbi mbalimbali za burudani, nilitegemea kumbi zile zitatumika zaidi na wanajeshi. Sasa hivi kumbi zile zimekuwa zinaingiliwa na raia wa kawaida pamoja na wanajeshi na katika burudani zile mara nyingi ugomvi unatokea na ugomvi huo mara nyingi unahusishwa na pombe pamoja na wanawake na katika vita hivyo siku zote wanaopigwa ni raia wanajeshi wanakuwa ndio washindi. Sasa tunataka watuambie ni lini au ana tamko gani kuhusiana na maeneo hayo ya burudani ili wananchi wetu wasiendelee kupigwa, aidha kutokana na masuala ya pombe au masuala ya mapenzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia vituo vya afya vinavyoendeshwa na Jeshi nikitolea mfano Kituo cha Bububu - Zanzibar, Kituo cha Welezo - Zanzibar, Lugalo - Dar es Salaam pamoja na vituo vingine. Vituo hivi vimekuwa vinafanya kazi nzuri sana na wananchi wanapenda sana kwenda kutibiwa pale kwa sababu kwenye vituo vile wanajali sana wagonjwa, wanatoa huduma nzuri na wana upendo wa dhati, lakini tatizo kubwa pale ni bajeti finyu, wanakuwa na bajeti ndogo ambayo wanashindwa kuwa na dawa za kutosha japo wanatoa huduma nzuri. Ni vizuri basi Serikali waviangalie vituo hivi kwa jicho la huruma ili wananchi

waendelee kupata huduma na nikiamini kwamba Jeshi liotaendelea kuisaidia Serikali katika kutoa huduma kwa wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze tena wanajeshi wetu wote kwa kazi nzuri za ulinzi na usalama zinazofanyika hapa nchini. Maneno madogo madogo yapo, lakini hayo Jeshi wakiamua kunyamaza humu ndani hakukaliki tusidanganyane. Jeshi linafanya kazi nzuri sana na katika 100 mtu akikosea 10 akapata 90 maana yake ndio kashinda kafanya vizuri. Lakini kipekee niwapongeze...

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Kanali Masoud dakika tano, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka dakika tano, halafu Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. KANALI MASOUD ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kuendelea kuliamini sana Jeshi letu katika kuwapa kazi mbalimbali licha ya ulinzi walionao, lakini bado wanaendelea kutekeleza majukumu mengi ya Taifa letu na kupunguzia gharama kubwa ya matumizi ya fedha za hapa nchini. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi tunaochangia tunazungumzia habari ya ulinzi, lakini nafikiri wengine hatuna taaluma ya ulinzi sana ndio maana tuazungumza mazungumzo ambayo hayalingani. Dhima ya Jeshi la Ulinzi wa Wananchi la Tanzania ni kuhakikisha usalama wa Taifa letu na wao wana jukumu la kuhakikisha adui kama yuko ndani, kama yuko nje ni jukumu lao kuhakikisha ulinzi wa Taifa hili. Sasa leo tunapokuja kuwaambia kwamba wao waende tu kule mpakani wakakae huku ndani si kazi yao, hii si sahihi. Lazima ifahamike kwamba ili wao wahakikishe wanalinda Taifa hili lazima wahakikishe adui wa ndani, adui wanje wote ni jukumu lao kwa Taifa. (*Makof!*)

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa. Mheshimiwa Kanali subiri kwanza.

## TAARIFA

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kutoa ushauri huo ni kwa sababu yapo matukio ambayo ni hatarishi yameshindwa kutolewa majibu ambayo tungetegemea kwa weledi...

**MWENYEKITI:** Hiyo ni taarifa au?

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo aelewewe tu kwamba hakuna...

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Masoud endelea

**MHE. KANALI MASOUD ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilifikiri tukisimama hapa tutaendelea kulipongeza Jeshi la Wananchi kwa kazi kubwa wanayoifanya na hili ndio nalofikiria. Lakini leo tunapokuja hapa tukawaambia wamekwenda kuchukua korosho, wameoka shilingi ngapi we chukulia wameokoa shilingi ngapi nchi hii katika kazi hiyo walioifanya, lazima tuwaeleze ukweli wenzetu wanafanya kazi ya kujituma na ya kuhakikisha Taifa liko salama. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uimara wa Jeshi lolote duniani likiwepo la Tanzania kwanza lazima liimarishwe katika baadhi ya nyenzo zake. Kwanza kuimarisha wapiganaji wenye kwa maana ya afya, nidhamu na mafunzo na kadhalika. Pia liimarishwe kwa zana za kisasa za kijeshi ambazo nazo ni gharama pia zinatakiwa zifanyiwe *service, maintenance* na vitu vingine kwa gharama kubwa. Kwa hivyo vyote hivyo viimarishwe lakini pia kuimarishwa kwa maslahi yao wenye askari, pia ni jambo muhimu, vitu vitatu hivi vikichanganywa Jeshi lolote duniani litakuwa imara na litafanya kazi kwa ueledi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulizungumza hapa katika muundo wa majeshi ya duniani katika nchi nyingi duniani ikiwepo Tanzania askari wastaifu wa jeshi pia linakuwa ni Jeshi la Akiba.

Kwa hiyo nilikuwa nataka niiombe Serikali iendelee kuangalia jinsi gani ya kuwawezesha wastaifu, kuwaongezea pensheni yao ili wawe imara ili wakati wowote tukitaka kuja kuwatumia wawe bado wana nguvu zinatosha za kuweza kuwatumia na mifano hai ipo katika vita vya Uganda, wanajeshi waliokuwa wamestaifu walichukuliwa wale ambao walionekana hali zao bado ni nzuri walitusaidia katika vita vile. Naomba Serikali sana iliangularie hili na kuwafikiria wanajeshi wastaifu kuwaongezea pensheni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumza ni mipaka ya kambi yetu ya majeshi bado kumekuwa na malalamiko makubwa sana, uingiliano kati ya raia na wanajeshi na mara nyingi tunapouliza ndani ya Bunge hili tunaelezwa hali halisi kwamba fedha za kulipa fidia na mambo mengine na upimaji wa maeneo bado hazitoshi. Naiomba sana Serikali iendelee kuhakikisha inawasaidia wenzetu Wizara ya Ulinzi kuwapatia fedha za kutosha kuhakikisha wanapima makambi yote na kulipa fidia katika yale maeneo ambayo tayari yamekwishapimwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka kulizungumza ni kuhusu Shirika la Nyumbu na Shirika la Mzinga, tunaamini kama Jeshi ni watu wanaolinda Taifa tu, lakini mimi naamini Jeshi bado linaweza likatoa ajira, pia linaweza likachagia fedha kuititia mashirika haya. Tumeyashududia tumeona wenye kabisu mfano Shirika la Mzinga wana uwezo wa kuzalisha bidhaa ambazo zinahitajika nchi za nje, lakini bado mashine zao, vifaa vyao walivyonavyo ni vya teknolojia ya zamani na vingine ni vimechoka naomba pia Serikali iendelee kuangalia sehemu hizi mbili ili kuwasaidia sasa waweze kuzalisha lakini pia kukidhi mahitaji yao ya ndani ili waweze kufanikisha malengo yao waliyoyokusudia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kuchauka  
ajiandae Mheshimiwa Yussuf Salim, Mheshimiwa Kuchauka  
dakika tano, hayupo Mheshimiwa Salim.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti,  
*Bismilah Ramahan Rahim*, nakushukuru kwa kunipa nafasi na  
mimi nataka nianze leo makatibu angalieni dakika  
mnatukata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza na  
kuunga mkono Hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, lakini  
pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri nilipongeze na Jeshi letu  
kwa kazi ngumu wanayoifanya na nawapa hongera sana  
siwapi pole kutokana na kazi ngumu na ugumu kwa sababu  
mwanajeshi hapewi pole akifanya kazi ngumu ndio kazi yake  
anapewa hongera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kile  
ambacho kinatukwaza sisi kama raia. Juzi nadhani ilikuwa  
siku ya Jumatatu kuna Msemaji wa Jeshi la Polisi sikupata jina  
lake, lakini alikuwa ni Luteni Kanali alikuwa anatoa taarifa  
juu ya *clip* inayoendelea katika mitandao ya jamii ikionesha  
jinsi wanajeshi walivyofyeka mazao ya mtu ambaye  
amevamia katika eneo la Jeshi. Akatoa maelezo, akatoa  
vielelezo na akathibitisha kwamba hilo ni eneo la jeshi ambalo  
limenunuliwa na wale raia wamelipwa, *well* hatuna tatizo  
katika hilo. Kinachotuumiza sisi kama eneo ni la kwenu  
wanajeshi kihalali maana yake nini, maana yake na kilichomo  
ndani ya eneo lile ni cha kwenu. Sasa ninyi mlikuwa  
mumuondoe yule yale mazao myaache kwa sababu mazao  
hayo ni ya kwenu, kwa kweli sisi wakulima na watu wa  
mazingira inatumiza sana tunapoona Jeshi linatumia nguvu  
zake tunaita utemi kufyeka mazao ya kulima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Amiri  
Jeshi Mkuu Awamu ya Pili wa nchi hii Mzee Ali Hassan Mwinyi  
ni mhamasishaji m kubwa wa kilimo cha papai. Leo akikuuliza

Jeshi lako linatumika kufyeka mipapai utamjibu nini? Tunaliomba Jeshi letu kama eneo ni lenu tumieni taratibu na sheria kuhakikisha mnadhibiti maeneo yenu kwa sababu kiusalama ni maeneo yenu, lakini muwe waungwana kwa sababu mazao hayana kosa lolote, tumuogope Mwenyezi Mungu yale mazao ninyi mngeyatumbia mapapai ni lishe bora kabisa kwa nini myafyeke, ile hamtoi picha nzuri tumeambiwa hapa na Kambi ya Upinzani kwamba Jeshi liwe-*think tank* ya Taifa hili, tunataka muwe mfano bora kwa wananchi na vijana wetu. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo labda limewaumiza sasa nawapeni asali kidogo hiyo ilikuwa shubiri kwenu. Wanajeshi wetu wanafanya kazi masaa 24 lakini katika hali ya kawaida *minimum* wanafanya kazi masaa 12 ondoa ule muda wa kusafiri. Sasa kama anafanya kazi masaa 12 kwa nini hawalipwi *overtime* lakini baya zaidi kinachoumiza kwa nini mishahara yao haiwi-*specific* ikawa hii ni tofauti na wafanyakazi wengine. Lakini kwa nini wanajeshi hawa kama halipwi *over time*, hawana mishahara ambayo ni tofauti na wafanyakazi wengine wanaofanya masaa tisa, lakini bado wanaendelea kukatwa kodi ndani ya mishahara yao hii si haki, kama Wabunge tunatakiwa kuisimamia Serikali kuhakikisha kwamba wanajeshi hawa wanalipwa kulingana na namna wanavyofanya kazi, ndio maana wanajeshi hawa anapostaafu anadhalilika sana muda mfupi tu.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri ulisimamie hili kuona kwamba wanajeshi hawa wanapata stahiki kulingana na kazi ngumu wanayoifanya. *Minimum 12 hours* ukimwangalia mtu amesimama pale halafu anakatwa kodi kwenye mshahara wake hii siyo *fair* kabisa kabisa, lazima hili liangaliwe na marekebisho yafanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanajeshi hawa wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, ameligusia Mheshimiwa Anatriopia, limegusiwa hata katika hotuba zote hawana *insurance*, hawana bima ya afya, sasa hili nalo ni tatizo. Tatizo ni nini? Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ihakikishe kuwapatia wanajeshi hawa bima za afya kwa faida yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne ambalo nataka kulizungumzia hili ni lako kama Mwenyekiti wa Kamati hii lakini kama ambaye leo uko kwenye kiti tunaiambia Serikali, Jeshi nilisema hapa na leo naendelea kusema linaweza likawa chanzo kikubwa cha kuiletea mapato Taifa hili na kuingiza fedha nyingi katika pato la Taifa kulikoni Wizara nyingine yoyote. Inaweza ikashindana na Wizara ya Maliasili na Utalii kama Jeshi letu tatalitumia vizuri kuingiza fedha za kigeni katika nchi yetu.

Niombe Serikali kwa nini tunanunua ndege hizi tunazonunua ambazo kwa mujibu wa taarifa toka ziliponunuliwa tunapata hasara kila mwaka kwa nini? Kwa nini fedha hii isitumike kununua ndege na vifaa vyta kijeshi ambapo nchi yetu tumeingia katika *US Missions* vifaa hivi vikatumika kule ambako tunapata fedha moja kwa moja hakuna ujanja wa namna yoyote. Kwa nini isitumike hivyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi kama Bangladesh, Pakistan, India, Rwanda, China, Nigeria, Uruguay na Ukraine zinaendesha nchi zao kwa sababu ya huyu *UN Mission* tu, sisi tunashindwa nini? Kwa mfano katika pale *UN* ukiingia tu unalipwa iwe ni *dry/lease*, iwe ni *wet/lease* unalipwa pesa yako kila baada ya miezi mitatu. Risasi inalipwa, bunduki inalipwa, hanga linalipwa, gari linalipwa, ndege inalipwa sasa kwa nini inashindikana hivyo? Kwa mfano gari moja ukiingiza katika *US Mission* inalipwa dola za Kimarekani 4000 kwa gari moja. Sasa kama tumeingiza gari 100 pale tutakuwa tunapata kiasi gani achalia mbali ndege na hivyo vifaa vingine, kwa hiyo huo ni mfano na *US Mission* wanalipa kila baada ya miezi mitatu hiyo fedha hakuna ujanja ujanja kwamba wamewaambia watu wapake rangi ndege wanakwambia milioni 200 kumbe ni milioni tano.

Kwa hiyo, tunaiomba Serikali badala ya kuelekeza fedha katika miradi ambayo inaleta hasara iwekeze katika Jeshi ili Jeshi litukusanyie hii fedha. Tulishasema kwamba Jeshi likitumika vizuri ni *think tank* na linaendelea Jeshi hili kutuzalishia fedha nyingi za kigeni kadri inavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujulize leo tuna miaka zaidi ya 10 nchi yetu iko katika ulinzi huu wa amani kule Sudan, DRC lakini tumepata nini? Tumepata fedha kiasi gani labda Mheshimiwa Waziri kama unazo *data* unaweza ukatuambia ni fedha kiasi gani, lakini bado tunaishauri Serikali iangalie namna ambayo tutalitumia Jeshi letu kama kitega uchumi na ni kuliwezesha tu tukanunua vifaa hivi badala ya kuingia katika miradi ambayo ukweli haileti tija kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kukizungumzia katika Jeshi, wanajeshi hawa kuna malalamiko makubwa namna ambavyo wanakaa muda mrefu ndani ya Jeshi bila ya kupanda yyeo. Mtu anatumikia cheo kwa miaka 12 hajapanda cheo kingine hii kwa kweli inaumiza wanajeshi wetu, lakini si inawaumiza *personally* inaumiza mpaka na familia zao. Kwa hiyo tunaomba huo muda ambao wanajeshi wanakaa pale jeshini uangaliwe vizuri na isiwe mtu anakaa zaidi ya miaka 12 bila kupanda cheo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine wanapoenda katika mafunzo Serikali ihakikisha kwamba inawapatia stahiki na malipo yao mapema kabla ya kuingia katika mafunzo kwa sababu wanaziacha familia nyumbani, zinahitaji huduma ye ye yupo kwenye mafunzo usipomlipa kwa wakati *concentration* yake itakuwa ni kuangalia familia na kuangalia mafunzo matokeo yake ikija ile akiwa katika mafunzo yale ya hatari ndio unakuta tunapata majeruhi katika mafunzo. Tuiombe Serikali kuhakikisha kwamba inawalipa wanajeshi wetu stahiki zao kwa wakati kabla ya kuanza kwa mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba Jeshi ni kioo katika jamii yetu, Jeshi linatakiwa liwe mfano bora la kufundisha wananchi wote tabia nzuri na mwendo mzuri. Jeshi letu linafanya kazi katika mazingira magumu liongezewe bajeti, lakini hata hii bajeti finyu itoke na itoke kwa wakati ili waweze kufanya kazi zao kwa ukamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kupigiwa kengele kwa sababu nimeweka *stop watch* leo nimeona ni dakika yangu

ya tisa namalizia kwa kusema kwamba nampongeza Mheshimiwa Waziri na wanajeshi kwa kazi ngumu na nawatakia kila la heri, ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo maneno kwa Makatibu wanakuwa *time* yako si kweli, acha mkwara huo, wivu tu huo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Musukuma, Mheshimiwa Mlinga tutamalizia na Getere.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia.

**MWENYEKITI:** Dakika tano.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuuomba mhimili wa Bunge kwamba sisi Wabunge tunapoapishwa kuwa Wabunge ni vizuri sana kama mhimili uone umuhimu wa kuchukua ile miezi mitatu ya mwanzo kutupeleka kwenye Chuo cha Jeshi cha Kunduchi cha *NDC* ili tuweze kujifunza kuzungumza maneno yanayoilinda taifa letu. Chuo hiki ni kizuri na mimi nina imana kama Bunge litakubaliana na mimi kwamba Wabunge tukapate miezi mitatu ya kufundishwa pale, hii migongano ya maneno ya hovyo hovyo yanayotokea humu ndani haitakaa itokee. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni wa leo tu, asubuhi Mheshimiwa Spika ametueleza kuhusiana na Mbunge kijana Mheshimiwa Masele anayetuwalisha kwenye Bunge la *PAP*, kijana huyu pengine angekuwa amefundwa pale Kunduchi haya yote yaliyotokea kule *PAP* yasingetokea. Kwa hiyo, ni muhimu sana sisi kama Bunge tukubaliane twende tukafundishwe. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitazungumzia kidogo tu kuhusu SUMA JKT. Sisi Wabunge tunaotoka kwenye maeneo ya migodi, nilikuwa naishauri Serikali maeneo haya ya migodi na hasa hii migodi mikubwa ni vizuri Serikali malindo yale ambayo yanalindwa na vyombo ulinzi vya nje wangepewa watu wa SUMA JKT. Kwa mfano, kwenye migodi mikubwa kama Geita wanalindwa na Kampuni inaitwa *G4S*, mlinzi mmoja analipwa karibu dola 800 yule mzungu mwenye kampuni na *retired officer* kutoka huko *South Africa*. Lakini vijana wetu wanalipwa shilingi 200,000/300,000 na mimi nimeona SUMA JKT wamefanya vizuri mpaka wametoa na gawio kwenye Serikali. Hizi fedha wangelipwa SUMA JKT wangefanya vizuri zaidi hapa wangetupa gawio kubwa zaidi kwa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kule migodini kwa kuwa hawa watu waliopewa hizo kampuni za ulinzi ni wazungu wa *South Africa*, wanawa-*train* vijana wetu vibaya na nilishazungumza hata humu ndani, ukienda kule Geita kwenye migodi ile kama *GGMna* migodi mingine ya Kahama, wale walini wa kule wakimkamata kijana aliyeenda kule tu hata kuokota mawe wanawapiga, wanawanyanyasa na hata wanawakamata wanawake wanaenda kuwalalisha na mbwa. Sasa ni vizuri walini wale wangepewa walini wetu ambao wamefundishwa na wana maadili mazuri ya Kitanzania, nadhani ingekuwa ni vizuri zaidi na Jeshi letu lingeweza kupata fedha nydingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe tu, kiukweli amezungumza kaka yangu pale kuhusuana na kauli zinazotolewa na wenzetu. Mimi niombe tu kwamba kiukweli maadui huwezi kujua wako ndani ama wako nje. Tukianza kulisema Jeshi kwa ubaya kwamba wakae kimya, mambo yakiharibika mimi natoa mfano tu siku moja humu ndani uliwaka moto, kila mtu alikimbia humu. Hebu lijaribu liripuke bomu humu ndani tuone mtu jasiri wa kuweza kukaa humu ndani.

Kwa hiyo, mimi niombe tu sisi kama Wabunge kwa Jeshi letu hili la mfano linasifikasi kimataifa, Wizara kama hii

siku inayoletwa humu ndani, tusilifananishe Jeshi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama. Ni watu ambao kiukweli muda wao mwingi wanafikiria kutulinda sisi tukae salama na nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa binafsi yangu nikuombe na Wabunge wenzangu, Jeshi linafanya kazi nzuri, ni watu wanaotakiwa kupewa moyo na mimi ningombwa kama tungeweza kupata muda kidogo tukapelekwa Jeshini kama wiki mbili, ukaona ule msoto ulioko kule halafu bajeti inaletwa humu watu wanaanza kuongea mambo ya hovyo hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana ndugu zangu wanajeshi mnafanya kazi nzuri na sisi kama Wabunge tunawaombea endeleeni kuilinda nchi yetu, haya maneno madogo madogo... (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, unga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mlinga ajiandae Mheshimiwa Getere.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, na mimi niungane na Wabunge wenzangu wengi kuwapongeza Jeshi letu la Ulinzi kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Lakini nilikuwa natoa ombi kwa Wabunge na hata Kanuni zetu inabidi tuzibadilishe, inapofika kipindi tunapojadili bajeti ya Jeshi, Wabunge wote tuwe kitu kimoja. Ukitaka ujue ubora na kazi kubwa wanayoifanya Jeshi angalia yaani ukiona majirani zetu wametulia ujue Jeshi wako kazini. Maana kuna kipindi fulani makelele makelele yalikuwa yanasi kika huko lakini sasa hivi yametulia. Kwa hiyo, nikupongeze sana Ndugu Venance Mabeyo kwa kazi kubwa ambayo unaifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nilikuwa napenda kupata majibu, hivi wanajeshi wanapokwenda kwenye

makambi kule kuna vitu gani wanapewa, mbona wakija mtaani wanakuwaga na vurugu sana, kwa sababu mwajeshi akimkuta mtu wa kawaida kavaa nguo inayofanana na Jeshi anamvua, mwajeshi akiwa baa akifanyiwa kitu cha hovyo inakuja kambi nzima baa kuleta vurugu, hivi kuna kitu gani mnawapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la ulinzi wa mipaka. Jukumu la Jeshi letu ni kulinda mipaka ya nchi yetu, sina hofu sana naamini kazi nzuri wanayoifanya, lakini sasa hofu yangu inapokuja ninapoona kwenye makambi ya majeshi na maeneo ya majeshi yanapoingiliwa na wananchi wa kawaida. Wananchi wanalima, wanajenga, wanauziana yale maeneo, sasa najiuliza, hivi kwenye mipaka yetu kukoje? Sina hofu sana, lakini kuna umuhimu wa kufanya ukaguzi kwenye mipaka kwa sababu siku tunaweza tukakagua mipaka ya nchi tukakuta nchi iko nusu tayari watu wameshajigawia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni jambo la matibabu, hili ndiyo jambo kubwa sana ambalo linalalamikiwa na wanajeshi wengi. Tunajua wanajeshi wengi wanaishi kwenye makambi na sina imani kama wake zao na wenye ni wanajeshi. Naamini wake zao wengi wanafanya kazi nydingine na wako maeneo ya nje ya makambi na watoto wao pia wanaishi nje ya makambi kwa sababu wengine ni wanafunzi. Sasa suala la matibabu limekuwa kizungumkuti, wengi wanatibiwa katika zahanati na hospitali za jeshi ambazo ziko kwenye kambi za Jeshi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapata taabu sana wanapopata rufaa, matibabu ambayo hawawezi kutibiwa kwenye kambi zao, mpaka waende Lugalo. Lugalo kuna urasimu wa matibabu, wanajeshi wenyewe vyeo vya chini wanapokwenda pale wakiwa wanaugua wanawekwa *pending* mpaka watibiwe watu wakubwa. Hilo suala mimi nimeshakutana nalo na Waziri analifahamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanashindwa kujiunga na mifuko mingine ambayo wafanyakazi wangine wanatibiwa,

wanasema na hoja ya usiri. Hoja ya usiri ipi, kwenye matibabu hakuna usiri, wanasema wataanzisha mfuko wao wa wanajeshi kwa ajili ya matibabu. Kazi yao walijonayo tu ya kulinda nchi ni ngumu, sasa wanataka kuanzisha kazi nyiningine tena. Changamoto watakayopata, kwanza wana vituo vichache yya matibabu, pili mfumo wa malipo kuandaa ni kazi, tatu kuandaa mfumo kwa ajili ya ukaguzi na kuhakiki madeni hiyo Jeshi hawataliweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nawashauri, Jeshi wangejingga katika mfumo wa matibabu ambao wanaupata majeshi yote ya ulinzi, kama Polisi, kama Jeshi la Magereza, kama Usalama wa Taifa, kama *PCCB*, kwa sababu hata wakistaafu wanajeshi hawathaminiwi tena.

Kwa hiyo, mimi naunga mkono hoja lakini suala la matibabu ya wanajeshi ni muhimu sana wakajingga na mfumo mwengine ambao wanatumia majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hizo dakika ambazo nimepewa. Mimi nimshukuru Waziri wa Ulinzi, Waziri mwenye *TBS* ambaye amekaa Serikalini muda mrefu, lakini anafanya kazi iliyotukuka kwa kweli anapaswa kupongezwa. (*Makofii*)

Niwashukuru Wakuu wa Majeshi, Mkuu wa Majeshi aliyeo *CDF*na wenzake wote wanafanya kazi nzuri. Duniani tunaposema nchi, maana yake ni Jeshi hakuna kitu kingine ambacho kinakuwepo zaidi ya hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumze mambo tu kwamba ukiangalia kwenye maeneo mengi sasa kwenye hizi ukaguzi wa *CAG*, kuna suala la *SUMA JKT*. Mimi nilikuwa nataka kusema kitu kimoja, Jeshi ni jambo, ni kitendo, ni tukio,

ni kitengo ambacho kinatakiwa kuwa kitakatifu cha kutosha, hasa ukija kwenye Jeshi ukakuta kuna vitu vidogo vidogo hivi vinazungumzwa SUMA JKT nimeona hapa ukurasa wa 34/35 kwamba wamekusanya madeni milioni 330, bilioni 1.545, wamekusanya madeni lakini kutoka kwenye deni kubwa lipi? Hapa ni madeni wamekusanya, kutokea deni kubwa lipi sasa? Maana yake tuseme kulikuwa na madeni labda bilioni mbili, wamekusanya bilioni moja tukasema labda wako afadhali. Lakini kitendo ukiangalia kwenye kitabu cha CAG kinaleta kasoro, kwa hiyo, tunaomba SUMA JKT wafanye kazi iliyotukuka kukusanya madeni na waone yale matrektakyanasaidia nini wananchi wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo hapo lipo Kilimo Kwanza, nilenda pale nikafikiri labda kuna matrektakama yanauzwa. Nikaambiya kumbe matrektayale yalisharudishwa Serikalini, yako pale Kilimo Kwanza, yamekusanywa yalikuwa yamerudishwa ili yaweze kulipwawale wenyewe waweze kurudisha madeni yao. Sasa yamekaa pale, ni ya Serikali, hayajaenda kwa wananchi, hayalimi, hayauzwi yapo tu. Sasa nikasema hii maana gani hii, mambo gani haya tunafanya haya. Kwa hiyo, nasema kwamba Mheshimiwa Waziri naomba mkitokahapa bajeti ikipita najua mnaptishwa, mkaangalie utaratibu, yale matrektachukueni. Kama hamuwezi kuyauza yana bei ndogo, warudishieni wakulima waliokopa wakafanya kazi watakuwa wanalipa kidogo kidogo ili waweze kupata hiyo ajira yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo muhimu sana katika nchi yetu, kama JKT na kama Jeshi la Tanzania ambalo lina maeneo makubwa sana katika nchi hii, litatumia vijana wa JKT katika mambo ya kilimo na kuajiriwa tutafanya kazi kubwasana. Nimeenda kwenye eneo moja linaitwa Chita kama unaenda Ifakara, Morogoro, eneo kubwa, bonde kubwa kuna matrektalakini hakuna kazi inayofanyika. Nenda maeneoyote ya makubwa ya JKT, kuna maeneo mazuri, makubwa tunaomba JKT na Jeshi kwa ujumla watumie vijana wetu wale wa JKT kuwapa ajira kwenye maeneo hayo, mbona inawezekana, shida iko wapi? Kwa sababu uwezo

wa kuwapa matrekta tunao, uwezo wa kuwahimili tunao, ....kuwapa tunao, shida iko wapi.

Kwa hiyo, naomba Waziri mwenye *TBS* uhakikishe kwamba vijana wetu wanapata ajira kutokana na maeneo makubwa ya JKT, tunaomba utusaidie namna ya kuyafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze tu kwa ujumla, hatuna namna yoyote ya kulaumu mambo ya Jeshi. Mtu anayezungumza Jeshi labda ana kichaa, kwa sababu hawa ndiyo wanafanya nchi inakuwepo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. LUCIA U. M. MILOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo zimekwenda asilimia ndogo sana, asilimia 18 tu hadi sasa na kipindi kilichobaki ni mwezi mmoja tu kuisha mwaka wa Serikali. Naitaka Serikali ipeleke bajeti iliyosalia kipindi hili kilichobakia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maslahi ya wanajeshi na polisi; kwa kuwa kazi hii ya uanajeshi au polisi ni kazi hatarishi inahitaji motosha, naomba Serikali ihakikishe inawapa motisha na kuongeza maslahi ya wanajeshi na polisi. Mavazi ya wanajeshi yatolewe pale wanapohitaji maana kazi yao inahitaji mavazi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bima ya wanajeshi, wanajeshi hawana bima za afya, naitaka Serikali iwapatie bima za afya wanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kauli za vitisho, kumekuwa na kauli za vitisho kwa wananchi. Wananchi wengi

sasa hivi wamejengwa na woga badala ya Jeshi kuwa kimbilio. Naomba Wakuu wa Majeshi wawe na kauli zinazohamasisha utulivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulipongeza Jeshi letu kwa kazi nzuri wanayoifanya katika maeneo tofauti ndani na nje ya nchi. Katika nchi zilizoendelea duniani, nchi kama Marekani, bajeti ya ulinzi wa nchi hiyo ndiyo inayopewa kipaumbele cha kwanza katika bajeti ya nchi hiyo duniani. Kwa kuzingatia kuwa bila ulinzi na utulivu wa nchi maendeleo endelevu hayawezি kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano, malengo yake ya msingi ni kuifikiha Tanzania kwenye uchumi wa katika ifikapo mwaka 2025 na ikizingatiwa kwa sasa kuna miradi mikubwa ya kimkakati ambayo itachochea uchumi wetu kwa haraka zaidi. Miradi hiyo ni kama ujenzi wa Bwawa la Kufua Umeme Rufiji, Mradi wa Reli wa *SGR*, ununuzi wa ndege mpya (*ATC*) na Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Uganda - Hoima - Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo na nyinginezo, naomba Serikali ingeangalia upya upangaji wa bajeti kwa kuzingatia uhalisia na bajeti hiyo iongezewe maradufu. Jinsi maendeleo yanavyoendelea ndivyo wahalifu na wapinga maendeleo waongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi linahitaji fedha zaidi ili kujumuisha kiteknolojia (kiulinzi), mafunzo mbalimbali, kununuua vifaa vya kisasa, mitambo ya kung'amua uhalifu, mafunzo ya ndani na nje ya nchi, ujenzi wa nyumba za askari, kuazisha viwanda, maslahi ya wanajeshi na mambo mengine ya kijeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT iongezewe fedha ili iweze kuzalisha zaidi kwa kuanzisha viwanda vidogo vidogo katika makambi yake. Hii itasaidia kuwapatia ajira vijana wetu wanaohitimu mafunzo ya JKT.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi liendeleee kuongeza ulinzi kwa maeneo nyeti ya Serikali na pia Jeshi liimarishe zaidi ulinzi kwa viongozi wetu wakuu wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudi kumpongeza sana Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wetu wa Tanzania, *CDF*, Makamanda wote na Wizara ya Ulinzi kwa kazi njema ya kulinda nchi yetu.

Mungu libariki Jeshi la Wannachi wa Tanzania. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100%.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kwa kumpongeza sana mtoa hoja kwa wasilisho zuri asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri katika ukurasa wa 10 anazungumzia kuhusu mpaka wa Mashariki ya Tanzania ambapo tunapakana na Bahari ya Hindi. Ukanda huu wa Pwani wenyе urefu wa kilometra 1,424 ndipo Kisiwa cha Mafia kinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali tete ya usalama katika eneo hili ikiwemo tishio la magaidi kutoka nchi jirani, naleta ombi maalum kwa Serikali pawepo na kikosi cha wanamaji katika Kisiwa cha Mafia ili kujikinga na matishio hayo kwa sasa hapo kikosi kidogo (*detach*) ambacho kina vifaa duni na hawawezi kwenda maeneo ya bahari kuu ambapo uharamia unafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 21 wa kitabu unazungumzia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana. Jeshi limeweka utaratibu mzuri na kila Wilaya kupewa nafasi kwa vijana kujejunga na Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Mafia kila mwaka kumekuwa na tatizo la vijana kutoka nje ya Mafia wanaoletwa kuchukua nafasi hizo. Nia nzuri ya Serikali ni

kuhakikisha Jeshi letu linakuwa na sura ya kitaifa lenye uwakilishi wa kila kona ya Tanzania. Hili sio suala la ubaguzi, ni jitihada za makusudi za Serikali kwa maeneo ya pembezoni kama Wilaya ya Mafia vijana wake mnapata fursa ya kujunga na Jeshi. Ni matarajio yangu Mheshimiwa Waziri ataweka miongozo kukabiliana na hali hii inayoharibu taswira ya Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ni muhimu sana hasa ukizingatia ni Wizara ya Ulinzi wa nchi, mipaka yetu na kulijenga Taifa letu liwe bora na salama. Serikali ione umuhimu ya kutoa fedha zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya kuboresha mfumo wa mawasiliano salama Jeshini chini ya Fungu 57. Hii ni muhimu sana kwa utekelezaji wa mfumo wa mawasiliano ambao utasaidia katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya utunzaji wa zana, magari na mitambo katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaitaka Serikali kulipa madeni ya kimkataba kwa kutenga fedha zaidi kwenye miradi ya maendeleo Fungu 57. Tunaitaka Serikali kutoa nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi wetu. Kwani hili ni hitaji la kisheria na kikanuni na pia ni kichocheo cha ari ya kufanya kazi kwa bidii zaidi. Serikali itoe kipaumbele kwa maslahi ya wanajeshi kwa kuwa ni kada ambayo imejitoa kwa gharama ya uhai wao katika kulinda mipaka ya nchi yetu dhidi ya adui yoyote kutoka nje na kuhakikisha kwamba lipo salama wakati wote. Kwa hiyo, si vizuri wanajeshi kuanza kulalamika kwa suala hili ambalo ni stahiki yao ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isifanye suala la kisiasa ama ubabaishaji katika kuwapandisha vyeo wanajeshi. Tunaitaka Serikali iwapandishe vyeo wanajeshi wote wanaostahiki kulingana na sheria, sio nusu

wapandishwe na nusu hawapandishwi, huo si uadilifu. Kuna malalamiko kwamba wanajeshi 8,000 waliofuzu kupandishwa vyeo mwezi Desemba, 2018; lakini ni 4,000 tu waliopandishwa na ilhali sifa wanazo. Je, Serikali ituambie ni lini watawapandisha vyeo wanajeshi hao?

**MHE. SUZANA C. MGONUKULIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutohana na uzito wa Wizara ya Ulinzi, Serikali itoe fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa ajili ya Fungu 38 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ili kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa na Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amani tunayoiona hapa nchini ni kwa sababu mipaka yetu inalindwa vizuri, kwa kutotoa fedha za maendeleo kutasababisha Wizara hii isitimize wajibu wake kiurahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kulipa fidia kwa wananchi kwa maeneo yaliyochukuliwa na JWTZ na JKT na kutoa muda mrefu bila kulipa fidia jambo ambalo licha ya ucheleweshaji haki hadi wamiliki wameshafariki na hivyo kudhulumika. Ifike wakati Serikali isiwanyanyase wananchi kwa kiasi hicho. Kwa maeneo yote ambayo hadi leo fidia haijalipwa basi kwa bajeti ya mwaka 2019/2020 ilipe fidia zote.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Mchango wangu nitajikita juu ya utendaji kazi wa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wameonesha uadilifu katika utendaji kazi zao katika maeneo mbalimbali. Tukichukulia uadilifu na uharaka walioonesha katika ujenzi wa nyumba za wafanyakazi na ofisi za Mji Mpya wa Serikali, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapa *tender* za ujenzi wa nyumba na ofisi za Serikali

kutokana na ubora wa majengo yao wanayoyajenga na pia uharaka wa kuyakamilisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijana ambao wapo katika Kambi za JKT vikosi mbalimbali ambao wako tayari kutekeleza litakaloamrishwa. Je, kwa nini badala ya kuweka walinzi katika aidha Ofisi za Serikali, majumbani na nyumba za watu binafsi kuajiri walinzi ambao siyo waaminifu na wengine hawajulikani makazi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini tusitumie vijana wetu wa JKT kufanya kazi hizo ili kuinua vipato vyao na pia Serikali kupata fedha? Mfano hawa *Security Groups* wanapolinda aidha nyumbani wanadai shilingi 300,000 kwa mwezi, yule mlinzi analipwa shilingi 60,000, sasa hii inapelekea mlinzi kutokuwa mwadilifu katika kazi yake. JKT wakipewa hii tender watalinda kwa uadilifu na vilevile mfano hizo shillingi 300,000 anaweza akapewa mlinzi shilingi 150,000 na 150,000 ikaingia katika mfuko wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni kuhusu wanajeshi wetu, wanajeshi hawa wanaendelea kuonesha uaminifu wao kwa nchi na Serikali kwa ujumla. Basi Serikali ione umuhimu wa kuwapa stahili zao vilevile na upandishwaji wa vyeo. Hawa ni watu muhimu katika ulinzi wa amani ya nchi yetu, lazima tuwathamini na kuonesha umuhimu wa Serikali kwao, tusiwakatishe tamaa.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nchi ya amani na utulivu wakati kuna nchi nyingine tuko jirani nazo hawalali wala kufanya kazi kwa amani kutokana na vurugu za mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaenzi wanajeshi wetu na tuwathamini kwa kazi zao nzito wanazofanya.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali bajeti itakayopitishwa na Bunge itolewe kwa wakati ili kuweza kusaidia Wizara kutekeleza miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kutekelezwa. Serikali imshauri Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano pindi anapofanya uteuzi wa Maafisa wa Jeshi katika ngazi mbalimbali, angalau azingatie jinsia, maana takribani maafisa wa juu wote wa Jeshi ni wa jinsia ya kiume, takribani 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ione umuhimu wa kuwapatia bima ya afya wanajeshi wetu wote hapa nchini pamoja na familia zao kuliko kutegemea kupata matibabu katika hospitali za kjeshi maana wakati mwengine wanajeshi hawa hulazimika kutumia gharama (fedha zao) kugharamia matibabu katika hospitali ambazo siyo za Jeshi. Hivyo bima ya afya ni muhimu kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwa wale wanajeshi ambao wamepata mafunzo au kozi ambayo itawawezesha kupandishwa vyeo kutohana na mafunzo hayo, wapewe haki yao ya kupandishwa vyeo hivyo. Serikali iwajengee nyumba za kutosha Maafisa wa Jeshi, pia wanajeshi wetu ili wawe na makazi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mipaka upya katika maeneo yote ya Jeshi nchini ili kuondoa migogoro ambayo inaendelea baina ya Jeshi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namuomba Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema na umri mrefu Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Mbunge na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ili aweze kuendelea kutekeleza majukumu yake yote katika Wizara hii.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, kulingana na umuhimu wa Wizara hii na mambo ya ugaidi yanayoendelea nchini na duniani kote, nitakwenda kuchangia mambo kadhaa ili kushauri Wizara hii ambayo ni muhimu kwa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazoidhinishwa na Bunge zipelekwe na kutolewa kwa wakati, naishauri Serikali kuzingatia maazimio ya Bunge ili kuleta ufanisi kwa Jeshi letu pia ufanisi wa utendaji kazi wa Jeshi lenyewe na kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya wanajeshi na wananchi, kumekuwa na malalamiko makubwa kutoka kwa wananchi hususani wale wanaozunguka maeneo ya Jeshi kunyang'anywa maeneo yao kwa nguvu na kuwatesa wananchi wanaozunguka maeneo ya Jeshi, hali sio nzuri wala haileti sura nzuri kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho ya chakula kwa wanajeshi ni vyema Serikali kulipa jambo hili umuhimu mkubwa ili kuleta motisha kwa wanajeshi wetu na familia zao, kwani wanajeshi wakiwa na manung'uniko ni hatari kubwa hasa kwa kuangalia umuhimu wao katika masuala ya ulinzi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pesa za mafunzo kwa wanajeshi kumekuwa na utaratibu mbaya sana kwa wanajeshi wa nchi yetu wanapotaka kuijendeleza kimasomo, wengi wao wanajitegemea wenyewe. Suala hili linaweza kuondoa utendaji bora, kwani pesa ambayo alitakiwa kusaidia familia zao ndiyo analipa masomo, inawakatisha tamaa wanaotaka kuendelea na masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandishwaji wa madaraja, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wanajeshi waliokidhi vigezo vya kupandishwa madaraja, nashauri Serikali kufuatilia jambo hili kwa busara kubwa na kumalizatizo hili ili kuleta motisha ya kazi kwa wanajeshi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi waliopata mafunzo na baadaye kuachwa mitaani bila kazi kuna athari kubwa sana kwani vijana hawa wanapewa baadhi ya mafunzo ambayo ni ya kijeshi ambayo kwa kubaki kwao mitaani inaweza kuwa hatari kubwa zaidi kwa nchi yetu, ni vyema Serikali ikabadilisha utaratibu ili kulinda nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iwe inawaandalia kazi za kufanya baada ya kutoka kwenye mafunzo.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, ningependa kupata majibu ya Serikali kuhusu mahusiano ya ujirani mwema kati ya Kata ya Mngeta – Kijiji cha Ikule na Kikosi cha Chita JKT. Mimi Mbunge bado napata malalamiko toka kwa wananchi ambao walikuwa wanafanya shughuli za kilimo maeneo ambayo walikuwa wanaamini kuwa ni maeneo yao tangu enzi za mababu zao na ndio maana kuna makaburi na mazao ya kudumu ambapo Chita JKT inasema ni maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa wapo wazee wanasema Jeshi halijawahi na hakuna kumbukumbu zozote za miutasari ya kijiji ya kukubali ugawaji wa ardhi toka kijijini hapo, lakini pamoja na wananchi hao kunyang'anywa maeneo ya mashamba yao, bado walikuwa tayari kukaa pamoja na kufanya mazungumzo ili kupata namna bora ya wakazi hao kupata mashamba ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa nilipoongea na Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Mwinyi aliahidi kushirikiana na wananchi kwa kupeleka vifaa vya kilimo cha kisasa Jeshini Chita na kufanya uzalishaji mkubwa na wananchi watashirikishwa kwa kupewa mashamba na kupata ujuzi wa kilimo bora ili wazalishe kwa wingi na kuondoa umaskini wa kipato kwa wananchi hao, kuwa wakulima wa nje (*out growers*). Tangu tuongee na mkakati huo ni miaka miwili sasa imepita, je, ni lini mpango huo utatekelezwa? Ahsante.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuchukua fursa hi kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kufika mahali hapa na mimi nichangie hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ya mwaka 2019/2020.

Aidha nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri, hotuba hii inakwenda kutekeleza ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kama ilivyoainishwa hasa katika masuala mazima ya ulinzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kuvipongeza vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kufanya kazi kubwa katika kuhakikisha hali ya amani, usalama na utulivu inaimarika. Katika mwaka 2018/2019 Serikali imelitumia Jeshi la Wananchi wa Tanzania kusaidia mamlaka za kiraia katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali kama vile uokoaji wa watu na mali zao pamoja na ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Mtumba, Dodoma, hatua nzuri sana na ya kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalipongeza Jeshi la Wananchi wa Tanzania kwa kuendelea kushiriki kwenye misheni za kulinda amani chini ya mwamvuli wa Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa. Misheni hizo ni *MINUSCA* huko Jamhuri ya Afrika ya Kati (*CAR*); *MONUSCO* Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (*DRC*); *UNAMID* nchini Sudan; *UNFIL* nchini Lebanon; *UNISFA* huko Abyei na *UNMISS* nchini Sudan Kusini. Ushiriki wa Jeshi letu pamoja na vyombo vingine vya usalama katika misheni hizo za amani umeendelea kuvipatia uzoefu, kuongeza maarifa na mbinu mbalimbali za kijeshi na kiintelijensia. Aidha, vyombo vyetu vimeendelea kujifunza matumizi ya vifaa vya kisasa na kuanzisha au kuimarishe mahusiano ya kijeshi na nchi nyingine zinazoshiriki kwenye misheni hizo. Jambo zuri ni katika kuimarishe usalama wa raia na mali zao, Serikali imeendelea kudhibiti hali ya ulinzi na usalama nchini kwa kuboresha mazingira ya kuishi askari na kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuendelea kufanya juhudhi kubwa kwa Jeshi letu, katika mwaka 2019/2020 Serikali imeendelea kuimarishe hali ya ulinzi na usalama, kuendelea kutoa fursa za mafunzo kwa vyombo vya ulinzi na usalama, kuvipatia vifaa na zana za kisasa na

kuendelea kushirikiana na Jumuiya ya Kimataifa katika kupambana na makosa yanayovuka mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kuhusu mipaka, Jeshi limekuwa linapiga na kuvunja na kubomoa nyumba za wananchi, kuchukua sheria mkononi kwa Jeshi siyo kitu sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia za wananchi kwa maeneo yao ina suasua kabisa na ikibidi kama ikishindikana warudishiwe maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda Jeshini, kuingia uchumi wa viwanda ni vyema tukawekeza katika viwanda viliyoanza vya Jeshini kwani ni nguvu kazi iliyotayariki na ya uhakika lakini ukosefu wa fedha na kuwarudisha nyuma vifaa chakavu vinakwamisha ufanisi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa mipaka, Jeshi lipatiwe vifaa na pesa zaidi ili kuhakikisha mipaka yetu inakuwa salama kama uwepo wa boti za doria na helkopta za ulinzi, ujenzi wa madaraja ya kuitisha vifaa vizito nyakati za dharura ni muhimu sana.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya tuonayo katika hali halisi kwa usimamizi uliotukuka wa Waziri na ushirikiano wa makamanda wake. Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli ambaye ni Jemadari Mkuu mwenye upendo wa Jeshi na nchi yake kwa ujumla na ndiko kunakopelekea amani kuimarika na kudumu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za maendeleo zinazopangwa na kuidhinishwa na Bunge ziweze kutolewa katika ukamilifu wake, kwani mwaka 2018/2019 hadi Machi, 2019 zimetolewa asilimia 41.8 ambazo hazitendi haki kwa Jeshi kwani kazi yao ni ngumu na hali hiyo wanahitaji kubadili na

kuboresha maeneo yao ipasavyo ili wawe wepesi na katika mazinigira mazuri ya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utafiti ni muhimu sana kwani utatuwezesha kufanya mambo yetu kwa ufanisi na tija, kwenye mashirika yetu (Nyumbu na Mzinga) ya Jeshi kuendelea kuwapatia kipaumbele chao. Hivyo tunaomba pesa inayoidhishwa ikatolewa kwa asilimia 85 kuliko hii hali ya asilimia 10 hadi sasa haina mshiko kwa Jeshi letu (2028/2019).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa wananchi na Jeshi letu la wananchi katika kutwaliwa maeneo na ulipaji wa fidia ni kizungumkuti kwa sasa. Mgogoro huu hauwezi kuwa wa kudumu hapa nchini kwani unatatatulika hivyo unaweza ukatoweka kabisa, kutokutoa pesa inayoidhinishwa kwa ukamillifu na wakati illi waweze kutathimini maeneo hayo na kuyalipia fidia ambayo haiwi na manung'uniko kwa wanaolipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya mwaka 2018/2019 hayakuweza kulipwa kwa wahusika na Jeshi halikufanya kazi kwa wahusika kutokana na asilimia 14.32 ya bajeti iliyotolewa. Tunaomba bajeti ya mwaka 2019/2020 kutolewa kwa ukamillifu ili maeneo ya Jeshi yatambulike na wananchi wasiwe na manung'uniko yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikitishwa sana na makazi ya wanajeshi wetu hapa nchini na kazi yao ngumu waifanyao na hawana muda maalum wa kazi yaani wapo mchana na usiku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tukiona bajeti ya Fungu 57 inatolewa kwa 1.47% ya mwaka 2018/2019 hadi sasa inasikitisha kwani dalili hii haioneshi kama tuna nia njema ya kuboresha makazi ya wanajeshi tukimuunga mkono Raisi wetu. Tunaomba pesa ya Fungu 57 itolewe kwa nia njema kwa asilimia kubwa zaidi tuwatolee tatizo hili la mazingira mabovu ya makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii. Pili, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wote kwa kuendelea na kuiwasilisha kwa ufasaha mkubwa hotuba hii. Hii ni Wizara muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ajira katika Jeshi letu, naipongeza Wizara kwa kuendelea kuchukua vijana wa nchi hii kwa mujibu wa uwezo na sheria ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika suala hili ni kuitahadharisha Wizara iendeleze umakini wa kuwapembua na kuwafahamu vyema vijana ambao wanawaajiri. Nchi yetu imezungukwa na nchi jirani ambazo baadhi yao zina matatizo yao na kukimbilia katika nchi yetu, vijana wa nchi hizi wanapokimbilia katika nchi yetu huwa wanajiingiza (wanaweza kujilingiza) katika jamii ya Watanzania na kuweza kujipenyeza kuweza kujunga na Jeshi letu. Hivyo Wizara naionomba iendeleee kuwa makini sana katika kuwachukua vijana na kujunga jeshini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya Jeshi la Wananchi; Jeshi letu limekuwa na kazi ya kulinda na kuhakikisha usalama wa mipaka yetu lakini Jeshi hili pia linapaswa kuangalia maeneo mengine ya kuweza kusaidia wananchi hasa katika nyanja za kiuchumi. Mfano maeneo yafuatayo yanaweza kusaidia kwa kutoa elimu ya kiuchumi kwa wananchi kama Kiwanda cha Ushonaji, Kiwanda cha Samani Chang'ombe ambacho hutengeneza samani, ufugaji wa samaki katika mabwawa na uvuvi. Maeneo hayo niliyoyaorodhesha nashauri Jeshi lipeleke ujuzi wake kwa wananchi ili na wao waweze kutumia ujuzi wa maeneo hayo kuweza kujikwamua kiuchumi .

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mimi na Watanzania wote afya njema. Na pia nawatakia waislam wa Tanzania na duniani kwa ujumla mfungo mwema wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JWTZ na JKT ni majeshi yetu ya ulinzi wa nchi yetu ya Tanzania na kwa muda mrefu yamekuwa yakifanya kazi katika mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yao. Kwa kuwa Tanzania bado ni nchi maskini na bajeti yetu hajitosheleri na tunategemea sehemu ya bajeti yetu toka kwa nchi wafadhili ambapo fedha haziletwi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu pia linatumika vizuri wakati wa majanga mbalimbali kama mafuriko, tetemeko la ardhi, ujenzi wa madaraja na barabara wakati wa athari za mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya ardhi kati ya JWTZ na wananchi; jina la Jeshi letu linajieleza kuwa ni la wananchi wa Tanzania lakini katika siku za karibuni kumekuwa na migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi, na katika kitabu cha hotuba ya Waziri imezungumzia ukurasa wa 29 hadi 30 imeeleza kuwa limedhibiti maeneo ya Jeshi kwa kuboresha mazingira kwa kupanda miti na kusimika nguzo na pia kulipa fidia maeneo ya Ras Mshindo (Lindi) shilingi 3,005,697,801.00 na Kakonko (Kigoma) shilingi 550,000,000.00, napongeza hatua hii. Lakini katika Jiji letu la Tanga upo mgogoro wa Jeshi na wananchi katika Kata za Masiwani Shamba na Tangasisi, naiomba Wizara imalize mgogoro huu kwa kulipa fidia wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi Na. 4 (1999) inasema; "*whether you have title deed or not so long you have been there for long time, customary law recognizes you as the owner of the land.*" Naomba kuititia sheria hii na Wizara wawalipe wananchi fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano na majeshi mengine duniani; napongeza ushirikiano mzuri uliopo kati ya Jeshi letu na majeshi mengine katika nchi za Bara la Afrika, Ulaya, Marekani na Jumuiya za Kimataifa kama *NATO* na *United Nations*. Vyema tukatoa kila aina ya ushirikiano katika mafunzo na mazoezi mbalimbali kwani Jeshi letu pia huvuna uzoefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafao kwa wanajeshi wastaafu; kumekuwa na tabia wanajeshi wetu wanapostaafu au wanapopandishwa vyeo kucheleweshewa malipo yao ya kustaafu na malipo ya kupandishwa vyeo. Naiomba Serikali ihakikishe wanajeshi wanalipwa stahiki zao kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora; katika Jeshi linazungumzwa suala la utawala bora lakini mara kadhaa Jeshi linahusishwa na mambo ya kisiasa kwa kuegemea upande wa Chama Tawala (CCM). Nashauri Jeshi letu lisijhusishe na masuala ya kisiasa kabisa.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ubia wa SUMA JKT na *Holleywa* kununua hisa za milioni 744 mwaka 2007 na kutengeneza *Tanzansino* kwa lengo la kuzalisha dawa na bidhaa za madawa. Wabia hawa hawakuelewana, mkataba ukavunjika na kugawana mali na sehemu ya ardhi ya Jeshi ilikuwa sehemu ya mkataba. SUMA JKT wakalazimika kulipa fidia ya fedha kunusuru eneo la Jeshi kuwaangukia mkononi. Swali, ipi ilikuwa nia ya SUMA JKT kuingia ubia wa biashara ya namna hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa SUMA JKT na CAMI ukiitwa CAMISUMA ukiwa na lengo la kuzalisha nguo na kusambaza (*CAMISUMA Garments*) 2006; SUMA 3% na CAMI 61%. Jeshi lilllipa milioni 10 kwa ajili ya umeme na huduma mbalimbali kwenye hivyo viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT na *Equator Automatic Co. Ltd*; SUMA 30% na *Equator* 70%. Kuunganisha magari makubwa, basi, mashine za kilimo, magari ya

zimamoto *etc.*, mkataba umevunjika na mchakato wa ku-*windup* unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA JKT na *Chenggong Ltd.*; Tanzania 80% na *Chenggong Ltd.* 20%. Lengo ni kukodisha, kuuza vifaa na mitambo mikubwa ya ujenzi, *bulldozer*, *caterpillar* *etc.* Mkataba uliingiwa mwaka 2015 ila upembuzi yakinifu ulifanyika 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa matrekt ya SUMA JKT (2015) na Kampuni ya Ursus SA kutoka Poland wenye thamani ya bilioni 119.9; lengo kuuza matrekt na vipuri vyake na huduma nyinginezo. Mkataba huu pia haukukamilika, swali, kuna shida gani JKT?

Mheshimiwa Mwenyekiti, manunuzi mbalimbali yamefanyika bila kufuata taratibu au bila kupitishwa na bodi. Manunuzi yenye thamani ya 1,114,565,015 kwa mujibu wa *report* ya CAG 2015/2016 katika Fungu 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi kupewa bima ya afya; hiki kiwe kipaumbele kwa kuwa huduma ya matibabu kwenye hospitali ya jeshi haijasambaa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umri wa miaka mitatu hadi sita kabla ya mwanajeshi kuo ni mrefu mno kiasi cha kupelekea vijana hawa kujilingiza katika uasherati au wanawake kuchelewa sana kupata watoto ukizingatia kuwa umri wa kuzaa huwa unapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda vyeo/ madaraja na mshahara; Jeshi liendelee kuhimiza uzalendo huku Serikali ikitimiza wajibu wake wa nyongeza ya mishahara na madaraja.

**MHE. MUHAMED AMOUR MUHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ni vyema tukamshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kunipa uhai na uzima na kuniwezesha kuchangia mada iliyopo mezani ya Wizara ya

Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Nianze kwa kuzungumzia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kuhusu maeneo yaliyochukuliwa na JWTZ kutoka mikononi mwa wananchi; kwa miaka mingi sasa baadhi ya maeneo hayo wananchi hawajafidiwa, kwa mfano kule Zanzibar sehemu inayoitwa Kiongwe Jeshi limechukua eneo ambalo wananchi walikuwa wakilima na kufugia wanyama wao, lakini pia hili eneo ni mali yao. Kwa miaka mingi tunavyozungumza wananchi hawajapata fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iwaonee huruma wananchi hawa kukatwa fedha katika mafao yao baada ya kustaaifu. Kupitia awamu hii askari wastaifu wamekuwa wakikatwa asilimia 20, hii ni hatari, niiombe Serikali ifikirile tena hali ya kuwabakishia wastaifu hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo cha Bahari, hapa napo pana mazonge makubwa, JWTZ linatumia *force* kubwa sana ya kutisha kupambana na wavuvi wetu ambao pia ni raia wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, suala la */license* haieleweki dhahiri hasa ni */license* ya aina gani inayotakiwa na hapa wavuvi kutoka Zanzibar wamekuwa wakisumbuliwa kwa aina ya */license* inayohitajika. Aidha, baadhi ya nyakati hupigwa na kuumizwa vibaya. Niiombe Serikali iliangalie hili kwa huruma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua majukumu makubwa ya Wizara hii katika ujenzi wa Taifa, usalama wa nchi kupitia mipaka ya nchi na usalama wa raia. Malalamiko ya wananchi kwa Jeshi hususani katika maeneo yaliyopakana na Jeshi kwa kigezo cha Jeshi kutokuwa na umiliki halali na wananchi kuingilia maeneo hayo kwa kupewa na Manispaa au Halmashauri na baadae kuleta migogoro ya wananchi kupigwa na wanajeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu Wizara ya Ardhi bado inashughulikia mipaka na maeneo hayo yaliyoingiliana na wananchi. Ni kwa nini Jeshi linachukua hatua ya kuwapiga, kuchoma nyumba, kubaka kina mama, kuwapa mateso yasiyoelezeka wananchi ambao kimsingi walipewa maeneo hayo kupitia Halmashauri? Ni kwa nini Jeshi linafanya unyama huu na huku Serikali ikiangalia unyama huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro uliopo katika Kata ya Misunkumilo kuhusu mpaka wa Jeshi jambo hili lipate ufumbuzi. Pia katika Jimbo la Kibamba ambalo Jeshi linaendelea na unyanyasaji kwa raia ni nini suluhisho?

**MHE. JOYCE J. MUKYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ndogo; kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Serikali ilitenga fedha za maendeleo katika Fungu 38 - Ngome kiasi cha shilingi billioni nane tofauti na shilingi billioni mbili kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo kwa bajeti hii imetengewa shilingi billioni sita kama nilivyoeleza hapo juu ni pungufu ya shilingi billioni mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Jeshi la Kujenga Taifa, Fungu 39 fedha za maendeleo iliyokuwa imetengwa ni shilingi billioni sita na iliyotolewa ilikuwa shilingi billioni tano sawa na asilimia 83.33.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kutotekeleza bajeti ya maendeleo ya Wizara hii siyo tu kunafedhehesha Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania (JKT) lakini pia kunawaweka wananchi katika hali ya hatari kubwa. Hili nalisema hivi kwa kuwa yanapotoka matukio ya ghafla ya uharibifu hata wanaopelekwa kwa ajili ya kuweza kutoa msaada wa haraka ni Jeshi la Kujenga Taifa. Mfano, kufanya huduma za ujenzi mara tu yatokeapo majanga kama mafuriko yanapoharibu miundombinu kama vile madaraja, majengo ya Serikali kuharibika, ni hawa hawa wanajeshi ndiyo wanaitwa kwa haraka kufanya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo cha kutopandisha vyeo Maofisa wa Jeshi kwa wakati kuna athari za moja kwa

moja ikiwa ni pamoja na katika mishahara yao na pia katika *pension* zao, kwa hiyo askari aliyetakiwa kupandishwa cheo miaka miwili iliyopita halafu akaachwa akaja kupandishwa miaka miwili baadae atakuwa amepunjwa nyongeza yake ya mshahara ambapo ingetokana na cheo hicho na pia mapunjo hayo yanakwenda kuathiri *pension* za askari hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo napendekeza Serikali ilieleze Bunge hili kama tatizo gani linasababisha wanajeshi wasipandishwe vyeo kwa wakati na kama ni bajeti finyu? Je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa askari hawa wanaotumikia nchi kwa moyo huku mahitaji yao yanapotekeliza kwa wakati?

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hotuba hii sehemu mbili; kwanza kwa kuwa vita vya Kagera historia yake hajjawekwa vizuri ili vizazi vijavyo viweze kujua jinsi Jeshi letu la Ulinzi liliyopigania nchi hii na kumwaga damu yao ili kutetea nchi yetu kutoka kwa Nduli Idd Amin, naomba kushauri kwamba historia ya vita hivi iandikwe na kuwekwa kwenye nyumba zetu za makumbusho na pia kwenye *library* za vyuo vyote vya elimu ya juu. Nakumbuka kazi hii ya uandishi iliashaanza na Mwenyekiti wake akiwa Spika Mstaifu, Pius Msekwa na Katibu wake alikuwa Luteni Kanali Livingstone Kaboyoka kwa vile hawa wote wawili wako bado hai ningeshauri mawasiliano yafanyike ili wasaidie kutoa taarifa muhimu ya vita hivi vya Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa *TARURA* inafanyakazi za matengenezo ya barabara mijini na vijijini, ningeshauri Jeshi la Kujenga Taifa lisaidie kuunda vikosi vya vijana hasa vijijini wakiwapa mafunzo ya ukakamavu na kuwasaidia wapate mafunzo ya kutengeneza barabara hasa vijijini ili badala ya kutoa pesa nyingi kwa wakandarasi ambao wakiondoka wanaacha barabara zikiharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT ingeweza kufanyakazi na *TARURA* na kuunda *Road Building Brigades* ambao wanatokana na maeneo husika. Hizi *brigades* zingeweza

kupatiwa *basic equipments* kama sururu, majembe, mapanga, mabeleshi na *wheelbarrows* ili kila mara wakarabati maeneo wanamoishi. Malipo yao yanatokana na michango ya wananchi na magari/pikipiki zinazotumia barabara hizo. Tuna mifano Tanzania ambapo enzi za ukoloni kulikuwa na vituo vya matengenezo ya barabara kila maeneo ya barabara. Kambi hizo zilikuwa zinajulikana kama PWD. Ahsante

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikikumbusha mara nyingi sana hapa Bungeni kwa njia ya maandishi na kuhutubia kwa mdomo suala la migogoro ya mipaka kati ya Kambi ya Jeshi ya JKT iliyopo Itaka, Mbozi na wananchi wanaozunguka maeneo ya Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vilivyoathirika na mgogoro huu ni Itewe, Sasenga na Mboje, zaidi ya kaya 800 zimeathirika kwa kuwa wameambiwa waache maeneo yao ambayo wamekuwa wakiyatuma tangu uhuru. GN na ramani zote zinaonesha kwamba wananchi wa vijiji nilivyovitaja awali kwamba maeneo hayo ni mali yao. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na JKT ashughulikie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na Bajeti ya Wizara; ninapenda kuishauri Serikali kuongeza bajeti ya Wizara hii kwani imeshindwa kufanya shughuli zake kwa ufanisi. Mfano, Mkoani Pwani, Wilaya ya Kibaha kuna Kambi ya Nyumbu na Msangani. Matatizo ya Msangani na Nyumbu ni tangu enzi za awamu ya kwanza za mwasisi wa Taifa hili, ndiyo barabara inayoelekea kwenye kambi hizo ilitengenezwa, ni mbovu na ni shida kiasi hata wanaofanya au watoa huduma katika majeshi hayo hupata shida kufika huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi la Nyumbu; enzi za Mwalimu, Nyumbu iliweza kutengeneza mpaka gari kwani Nyumbu ina mashine na mitambo ambayo iliwezesha kufanya kazi kwa ufanisi lakini leo hii Nyumbu tuliyoitaraja kuleta mapinduzi ya viwanda majeshini imepotea. Hali hii imesababisha wananchi na vijana waliokuwa wamepata vibarua kukosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la migogoro ya mipaka na raia; nitoe ushauri Serikalini kuhakikisha inafuatilia mipaka hiyo na maeneo yote ya Jeshi yapimwe na kupata haki za umiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira Jeshini ni tatizo, kuna vijana walioahidiwa kuajiriwa baada ya kujenga Mererani na pia wapo wa Operesheni Kikwete walioahidiwa kuajiriwa lakini mpaka sasa wapo mitaani na tunajua wanajua matumizi ya silaha, hivyo kuwaacha mtaani ni hatari. Operesheni Magufuli nao wapo mtaani, je, hii si hatari kubaki na vijana bila kupewa shughuli za kufanya?

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri sana wanayoifanya ya ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara ni kwamba watengeneze *products* nzuri sana na kutoa *services* ambayo kama itafanyiwa *marketing* ya kutosha itaongeza kipato kwa Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na vijana wengi wanaomaliza shule na kubaki wakizagaa mtaani. Jeshi lingewachukua na kuwapatia ujuzi ili wanaporudi mitaani kwanza wawe wakakamavu, nidhamu na ujuzi wa kuweza kujiajiri. Lakini wakati huo huo Jeshi linakuwa na akiba ya kutosha yanapotokea matukio kama vita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine maslahi ya wanajeshi yazingatiwe sana ili kujenga uaminifu na kujiepusha na matukio yasiyofaa. Lakini pia wapewe motisha ya kuwafanya

wafanye kazi kwa furaha maana kazi yao ya *risk* sana kwa maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wanajeshi wangekuwa wanakatiwa bima ya maisha maana tayari wameyatoa maisha yao kwa ajili ya Taifa. Wakati wowote wapo katika *risk* ya kupoteza maisha na wengi wanategemewa na siyo kupoteza maisha tu, hata ulemavu wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kitendo cha kuwazuia wanajeshi wapya wasioe mpaka baada ya muda fulani sioni kama ni busara, na pia kunachochea maambukizi ya ugonjwa wa UKIMWI na msongo wa mawazo kwa wanajeshi wetu, kitu ambacho ni hatari sana kwa watu wanaohusika na ulinzi wa nchi yetu.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kidogo kwenye Wizara hii nyeti, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana kati ya Jeshi la Wananchi Mikumi na wananchi wa Kitongoji cha Vikweme. Nilishalifikisha jambo hili kwa Mheshimiwa Waziri na nilishauliza swali hili mara kadhaa hapa Bungeni bila mafanikio, Mji Mdogo wa Mikumi wapo tayari kabisa na wameshatenga eneo kwa ajili ya kuwapa Jeshi ili wakafanyie huko mazoezi, lakini Jeshi letu limekataa na kuendelea kuling'ang'ania eneo la Vikweme ambalo wananchi wengi wa Jimbo la Mikumi wanalitegemea kwa kilimo na pia kuna nyumba za wananchi kwa makazi, shule, nyumba za ibada na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuomba sana Waziri aweze kulitatua hili na pia afanye ziara jimboni Mikumi kama alivyoniahidi wakati akijibu swali langu Bungeni.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia Wizara hii muhimu kwa ulinzi wa mipaka ya nchi yetu dhidi ya adui wa nje, Jeshi la Wananchi la Tanzania lipo kuhakikisha linamlinda Mtanzania dhidi ya

mataifa mengine na pale kunakuwa na utawala dhalimu basi Jeshi hushika hatamu. Ni kwa masikitiko makubwa Awamu hii ya Tano tumeshuhudia wanajeshi wakishushwa hadhi hadi kufikia kusafisha Jiji la Dar es Salaam, kupiga picha zilizo na mantiki wala taswira nzuri na Wakuu wa Mikoa hasa wa Dar es Salaam. Enzi nakuwa niliamini wanajeshi ni watu wenye mosi, kujitokeza kwa nadra sana mbele ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sote tunakumbuka hata wakati wa *operation UKUTA* ya CHADEMA tulishuhudia wanajeshi nao wakijiandaa kukabiliana na raia ilhali Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ipo kuhakikisha usalama wa raia na mali zao, na kama kuna uhalifu wowote ichukue hatua. Hii ni sawa kuona Jeshi la Wananchi likifanya mambo kwa matakwa ya mtawala na hili limedhihirishwa dhahiri kwa kauli aliyoitoa Mkuu wa Majeshi Jijini Dodoma wakati wa uzinduzi wa Ofisi za Serikali kuwa wanafuatilla kauli za uchochezi na viashiria vyake na kuwa wapo tayari kuvidhibiti. Hii si sawa na wala si kazi ya JWTZ. Na hili linabidi likemewe kwa nguvu zote na kila mzalendo anayelitakia mema Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuchangia kwenye hilo napenda sana Mheshimiwa Waziri atuambie wananchi wa Bugosi na Kenyambi ni lini watalipwa fidia zao stahiki kwa sababu wanajeshi walivamia lile eneo inasemekana ni baada ya kuvutiwa na mnara ambao Ndugu Thobias Ghati alikuwa ameingia mkataba na Kampuni ya Vodacom huku wakiacha kambi yao iliyopo Kata ya Nyandoto ambayo mosi ipo nje ya mji na mahali stahiki kwa wao kukaa maana miundombinu ya barabara na madaraja sasa imeimalika si kama awali. Lakini kama wameshindwa kulipa fidia kwa wakati wananchi wangu wanaomba wanajeshi wawapishe na warudi kwenye kambi yao, maana hili nimekuwa naliongelea tangu Bunge la Kumi na kila siku Waziri anaeleza watalipa mwaka wa fedha uliopo lakini hawalipi mwaka wa tisa huu sasa nikilisemea hili bila utekelezaji wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hivi wananchi hawa wamewakosea nini Serikali ya Chama cha

Mapinduzi tangu mwaka 2008 wanashindwa kuyaendeleza maeneo wala kufanya shughuli za maendeleo maana wamezuiwa, hii si haki kabisa. Jana Tarehe 15 Mei, 2019 Waziri akijibu swali la Mheshimiwa Masoud alisema zile shilingi bilioni 20 zilizotengwa na Bunge tayari wananchi walifanyiwa tathmini wamelipwa shilingi bilioni tatu, nauliza Tarime tulishafanyiwa tathmini kwa zaidi ya mara tatu bila malipo na hata juzi walikuwa huko, ni lini sasa tutalipwa? Naomba kupewa majibu yanayokidhi haja na yenye matumaini kwa wananchi wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia niombe wanajeshi hao waliovamia maeneo ya Bugosi na Kenyambi ambayo yapo katikati ya mji basi iwapo mtalipa fidia wasizidi kujiongezea maeneo maana Tarime Mji hatuna maeneo ya kutosha na inakuwa na muingilio mkubwa kati ya Jeshi na raia. Mwisho wa siku kwa *principle* za Jeshi unakuta wananchi wangu wanapitia dhoruba nydingi na mateso ya kijeshi pale wanapotumia *public services* zilizopo kwenye maeneo waliochukua na kibaya zaidi mnachelewesha fidia huku wanajeshi wamewazuia wananchi kuendeleza maeneo yao ila wao wanakodisha hayo maeneo waliopoka kwa raia na fedha wanazichukua, hii si sawa na inahitaji uvumilivu wa hali ya juu. Kama kiongozi nimekuwa nikiwasihii wananchi wavumillie lakini uvumilivu una mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa Waziri utuhakikishie, kumbuka hata wale wananchi waliokuja mwaka juzi kkuona toka Tarime wengine ni wazee wanafariki kabla ya kupata haki yao si sawa kabisa.

Mwisho naomba kujuu kama Wizara inapata mapato ya ule mnara uliopo Bugosi ambao ulikuwa na mkataba kati ya Ndugu Thobias Ghati na Vodacom na baada ya wanajeshi kujichukulia maeneo yale waliamuru Vodacom walipe Mkuu wa Kikosi cha Makoko kinyume na sheria maana bado yule mwananchi hajafidiwa, hivyo ule mkataba ulitakiwa kuendelea mpaka pale watakopolipa fidia. Maana hapa si sawa na kuamuru mojawapo ya nyumba yenye wapangaji kuwa wale wapangaji walilipe Jeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Ndugu Thobias Ghati tunapenda kujua hizo fedha za mnara zimekuwa zikila Wizarani na kama ndivyo ni kiasi gani cha fedha kwa miaka yote hiyo? Na kama haziji ni hatua gani itachukuliwa sambamba na ukaguzi wa kina kwenye hilo suala la mnara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndio maombi na mchango wangu kwa leo ambayo ni Jeshi la kulinda mipaka ya nchi na sio kuingilia mambo ya ndani ya nchi. Pili fidia kwa wananchi wangu wa Mtaa wa Kenyambi, Kata ya Nkende na Bugosi Kata ya Nyamisangura pamoja na mapato ya mnara uliopo kwenye eneo la Ndugu Thobias Ghati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Jeshi kutumika kisiasa, wakati wa uzinduzi wa Makao/Ofisi za Serikali Dodoma Mkuu wa Majeshi alinukuliwa akisema kuwa Jeshi linafuatilia kauli tata zinazoashirika uvunjifu wa amani. Sio kazi ya Jeshi la Polisi kushughulikia au kupeleleza kauli tata za kuashiria uvunjifu wa amani, ni vyema Jeshi likafanya kazi yake ya kulinda mipaka ya nchi na sio kuingilia Wizara ya Mambo ya Ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uimarisaji mipaka ya nchi, Jeshi la Ulinzi lipo lakini idadi ya wahamiaji haramu kuititia njia ya panya katika mipaka ya nchi jirani yanaogezeka siku hadi siku, kwa nini hatua zaidi zisichukuliwe na hii imebainika hasa kwenye mapango ya Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya mipaka kati ya wananchi na Jeshi la Ulinzi, ipo migogoro mingi kama Pangawe, Kizuka, Mzinga na Kilombero ambayo imesababisha hata mauaji kwa askari na wananchi, iko haja mipaka ya Jeshi ikahakikiwa upya kwa kuwashirikisha wananchi walio kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia kwa askari wanaopoteza maisha wakiwa kwenye vita nchi za nje

ikilinganishwa na nchi zingine za Afrika Mashariki ni ndogo na zinalalamikiwa na ndugu, pia ipo shida ya urasimu katika kulipa fidia za wajane waliopoteza waume zao wakati wa vita.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja hii katika suala la mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa kwa vijana kwa mwaka 2018/2019 jumla ya vijana 19,895 wa mujibu wa sheria walipatiwa mafunzo kwenye kambi mbalimbali. Aidha vijana 21,966 wamepata mafunzo kwa kujitolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hawa wakimaliza mafunzo hawapati ajira na huku wamepata mafunzo hata ya kivita. Ningombaa Serikali iweze kuona athari za vijana hawa waliofundishwa kutumia silaha kubaki mitaani bila kazi ya kufanya. Nlnashauri Serikali hata kama haiajiri waweke utaratibu au kuanzishwe programu wakishirikiana na *VETA* ili wawatumie vijana hawa kupata kozi anuai ambazo zitawasaidia kujajiri na kuweza kukuza uchumi binafsi na wa Taifa, kwa mfano yanaweza kuwepa mashamba na wakapewa mitaji ya kuzalisha malighafi zinazoweza kutumiwa katika viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi, ninaiomba Serikali iwape nyongeza za mishahara wanajeshi kama kada nyingine zinavyotakiwa kwani hawajapata nyongeza zao tangu Serikali hii ya Awamu ya Tano imeingia madarakani. Tuwape kipaumbele kwa maslahi yao kwa kuwa kada hii imejitoa kwa gharama ya uhai wao katika kulinda mipaka ya nchi yetu ili iwe salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo kadhaa nataka majibu ya Serikali. Majeshi yetu kupelekwa Darfur na Congo DRC, kwa nini mpaka leo majeshi yetu yanapelekwa Darfur na Congo DRC? Malipo yake kwa Taifa hili kwa sasa ni shilingi ngapi? Fedha

za malipo zinachangia bajeti kiasi gani? Ukombozi wa Afrika umekwisha, Watanzania wengi wameuawa sana, hakuna malipo kutoka kwa nchi tulizokomboa mfano South Africa, Namibia, Zimbabwe, Mozambique na nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanza kupeleka Watanzania wengi kuuawa bila malipo kwa muda mrefu, sasa hivi imefika wakati wa nchi kuomba malipo kwanza kabla ya kupeleka vijana wetu kuuawa, Congo kwa mfano kuna madini mengi na wanajeshi wetu wanauawa huko kila siku. Naomba watulipe fedha au madini ili tujenge uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani sasa hivi hakuna nchi inapeleka watu wake vitani nchi nyingine bila malipo makubwa. Serikali ituambie wale wanajeshi waliouawa mwaka jana na mwaka juzi Congo DRC fidia imelipwa kiasi gani? Leo kuna wanajeshi wanapelekwa Darfur miaka mitatu wakati Omar Al-Bashir amefukuzwa, hakuna amani, nani anatulipa? Umoja wa Mataifa inalipa kiasi gani kwa thamani ya watu wetu wanaenda kuuawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka tulienda kumuondoa Mohamed Bakar kule Comoro kwa maslahi ya Wacomoro tulillipwa bei gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Rwanda tunaisifia kuwa iko juu kiuchumi na kwamba Kagame anajenga uchumi wake. Kazi yake amepeleka majeshi Congo DRC anachochea vita, wanateka maeneo ya madini, wanachimba na kuuza *thenwanajenga* uchumi wa Rwanda. Sisi Jeshi letu tunapeleka kuuawa bure bure tu, haikubaliki.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi; hongera sana kwa Wizara, Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake wote Wizarani. Pia hongera kwa Jeshi letu kwa upana wake ikijumuisha uongozi wa ngazi zote. Hongera sana kwa kazi iliyotukuka, sio tu kwa kuendelea kulinda mipaka yetu, bali pia kwa kuendelea kuingilia katikati kazi na majukumu mbalimbali ya kijamii na kiuchumi

kama vile ujenzi/urudishaji wa huduma za dharura kufuatia maafa, kuharakisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali Kuu, zoezi la ukusanyaji korosho na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, teknolojia zilizopitwa na wakati; nimesoma changamoto hii katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri (hotuba ya bajeti) katika vifaa, mitambo, vitendea kazi na kadhalika, ni jambo la kuendelea kuishauri Serikali kuendelea kuboresha bajeti ya Wizara ya Ulinzi, lakini kwa upande mwingine nashauri Wizara iboreshe mpango wa elimu endelevu kwa wataalam waliopo (*Continuing Professional Development (CPD)*) na kuzalisha wataalam kulingana na mahitaji. Hii itasaidia uendelevu (*sustainability*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka; katika mpaka wa Kusini wenye jumla ya kilometra 1,536 Wilaya ya Tunduru ni sehemu yake (eneo la kandokando ya Mto Ruvuma), kutokana na ishara za kukua kwa changamoto za kiulinzi katika mpaka nashauri Kambi ya Jeshi iliyokuwepo katika eneo la Kitanda, nje kidogo ya Mji wa Tunduru irejeshwe na kuboresha kwa kuondoa changamoto zilizosababisha kambi hiyo kufungwa siku za nyuma.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kumshukuru Mungu kwa kuniamsha salama na kuendelea kunijalia uhai na kunipa uwezo wa kujadili hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii pamoja na wakuu wote wa majeshi yetu yote. Kwa kweli, kazi inayofanywa na majeshi wanastahili pongezi na heshima iliyotukuka kwa kuilinda nchi yetu ndani na nje ya mipaka yetu. Askari wetu wanafanya kazi kwa weledi mkubwa, nasema hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuacha kuwaingiza kwenye mfumo wa Bima ya Afya (*NHIF*) askari wetu sio jambo jema. Familia za askari wetu zinahangaika sana na masuala ya afya kwani hakuna hospitali bora kwenye vikosi/makambi ya

majeshi yetu na zipo pia familia zinazokaa uraiani mbali na Kambi za Jeshi, hivyo wanapopata uhitaji wa matibabu wanapata shida sana. Serikali ione umuhimu wa kuwaingiza askari wetu kwenye utaratibu wa bima ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko pia tatizo la malipo ya posho za maaskari wetu. Wako maaskari wengi wanaodai posho mbalimbali kama vile posho za likizo, posho za madaraka na mengine kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili kwa majeshi yetu ni muda wa kuingia na kutoka kazini. Ili askari awahi kuingia kazini inamlazimu kutoka nyumbani saa 11:00 alfajiri au saa 10:30 na jioni wakitoka saa 11:00 wanafika nyumbani zaidi ya saa 03:00 usiku. Hawa ni wale wanaokaa nje ya makambi ya majeshi yetu, hivyo kuwafanya askari wetu kukosa utulivu wa kikazi maana muda mwingsi wanashinda kwenye daladala, hasa kwa askari wanaoishi Dar es Salaam.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru kwa michango mizuri na niwapongeze kwa michango mizuri lakini nimpongeze..., nimeona kwenye mchango wa Mheshimiwa Anatropia kazungumzia kuhusu masuala ya afya. Ukienda kwenye ukurasa wa 50 wa hotuba ya Waziri, anasema Wizara inaendelea na utaratibu wa kuanzisha matibabu kupitia bima ya afya.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hongera sana na nampongeza Mheshimiwa Rais juzi tumemuona na Balozi wa Ujerumani kuboresha Hospitali ya Lugalo ambacho ni chombo muhimu kwa afya ya wanajeshi wetu pamoja na makamanda, *CDF* na wengine. (*Makofii*)

Kwa hiyo tunachukua nafasi hii kuwapongeza, siyo kila kitu cha Jeshi kitakuja humu ndani nataka niwaambie, kuna mambo mengine hayazungumzwi humu ndani, lakini Wajumbe wa Kamati wanajua namna Kamati inavyoshughulikia masuala na maslahi ya wanajeshi, Serikali jioni mjiandae kujibu kuanzia saa kumi.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 10:00 jioni.  
*(Makof)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilitishwa hadi saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudi)*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na  
Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Mmejipanga vipi huko? Mheshimiwa Mwakyembe.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa mimi naunga mkono hoja na nataka nitamke mapema kabisa kwamba kama kuna taasisi hapa nchini yenye rekodi ndefu iliyotukuka ya nidhamu, maadili, weledi na utendaji wa hali ya juu basi taasisi hiyo ni Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili za Jeshi kuwa mfano bora wa kuigwa nchini ilijitokeza mapema tu baada ya uhuru, wakati wa uhuru ambapo Baba wa Taifa alimkabidhi Luteni Alexander Ngwebe Nyirenda, bendera na mwenge wa uhuru akauweke juu ya Mlima Kilimanjaro, kitendo ambacho Baba wa Taifa alikielezea kishairi shairi kwamba mwenge huo utamulika ndani nan je ya mipaka yetu ili ulete matumaini

pale ambapo hakuna matumaini, ulete upendo mahali penye chuki na heshima mahali palipo na dharau na kwa hakika mwenge ultusaidia kuona mapema kabisa baada ya uhuru kwamba kuna dhuluma ndani ya Bara la Afrika na ndiyo maana Tanzania tukawa ngome kuu ya mapambano ya harakati za kupigania uhuru katika Bara la Afrika na ndiyo maana mwaka 1963 nchi yetu ikapewa heshima kuwa ndiyo Makao Makuu ya Kamati ya ukombozi wa Bara la Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mwaka 2011 nchi yetu ikapewa heshima kubwa kuwa ndiyo Kituo Kikuu cha Kumbukumbu ya Historia ya Harakati za Ukombozi wa Bara la Afrika na ukiongelea harakati za ukombozi kwa kweli tunapata hiyo heshima kutokana na Jeshi letu la Wananchi wa Tanzania. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nduli Iddi Amin alipojaribu kuleta jeuri hiyo jeuri ilizimwa na majeshi yetu, tunawapongeza sana. Na kwenye vurugu popote pale duniani vijana wetu wakienda wanaacha alama ya heshima na ndiyo maana leo hii ukienda Kinshasa, Lubumbashi unatembea kifua mbele kama Mtanzania kutokana na kazi kubwa ambayo akina Jenerali Mwakibolwa waliifanya hao wote ndiyo JWTZ. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema nalipongeza sana Jeshi letu hasa kwa upande wa michezo. Hawajaanza jana hawa. Akina Filbert Bayi wakiwa jeshini ndiyo Mtanzania wa kwanza kutuletea sifa hapa mwaka 1974 baada ya kuvunja rekodi ya dunia ya mita 1,300 Christchurch – New Zealand, hiyo JWTZ. Sio huyo tu, tunae mweznake Juma Ikangaa mwanajeshi mweznake ambaye alikuw abingwa wa mbio za New York za *marathon* mwaka 1988, JWTZ hiyo, sio huyo tu, tuna Samson Ramadhan, mshindi wa *marathon* Melbourne – Australia mwaka 2006 ni JWTZ.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ni ndefu sana, nisimsahau kijana wetu Simbu, mshindi wa medali ya dhahabu *Mumbai Marathon* na vilevile medali ya shaba *London Marathon*...

**MWENYEKITI:** Ikangaa.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ikangaa nimemtaja ndiye mshindi wa *marathon* ya New York, kuna wengi. Tuna akina Cecilia Panga bingwa wa *Beijing International Marathon*, Emmanuel Gisamoda, *Shanghai International Marathon*. Kwa kweli jeshi letu limetupa heshima kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona muda wangu umekwisha, naomba tu niseme naunga mkono hoja na kwakweli Jeshi letu linastahili heshima kutoka kwa kila Mtanzania. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kupata nafasi hii na mimi mkono hoja. Nampongeza na Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri wanayofanya. Nawapongeza sana Jeshi la Wananchi kwa kazi kubwa wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo amesema Mheshimiwa mchangiaji Dkt. Mwakyembe, Jeshi limekuwa sehemu ya kimbilio sana. Tunapokuwa tunapata majanga makubwa katika nchi hao ndiyo watu ambao kwakweli wanakuwa *multipurpose* wanafanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa, lakini vilevile tunapopata mafuriko maeneo mbalimbali wanashiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia hivi karibuni ukiacha shughuli kubwa ambayo wanafanya hata nje ya nchi kujenga heshima na utashi wa Tanzania na uzalendo uliotukuka, wamekuwa wakitumwa katika maeneo mbalimbali kwakweli hatujawahi kupata malalamiko kutoka huko ambako wanafanya kazi, maana yake wanabebe uzalendo, wanawakilisha nchi yetu vizuri sana na kupeleka sura chanya ya Jeshi letu nje ya mipaka ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na kwamba Jeshi wanafanya kazi lakini amewapa nafasi kubwa wamefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa nyumba za Serikali, sasahivi wanajenga majengo hapa ya Mji Mpya wa Serikali pale Mtumba, lakini wamekabidhiwa majengo kule kwetu Ukonga, Jimbo la Ukonga pale tunashukuru sana, lakini kubwa zaidi ni kitendo cha ushujaa Mheshimiwa Rais aliona ambacho alikuwa anafanya yule Ndugu Charles Mbuge na akampandisha kuwa *Brigadier General/jambo* kubwa sana kwa kazi kubwa anayofanya. Hii maana yake aatia nguvu wanajeshi ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa sana. Tunawathamini, tunawaheshimu waendelee kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema namna hiyo, nashukuru sana naunga mkono hoja. Nawapongeza sana wanajeshi na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya. Ahsante sana. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii nimpongeze sana sana Waziri mwenye dhamana ya Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Kwakweli tunapongeza sana Dkt. Mwinyi kwa kazi nzuri anayofanya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mkuu wetu wa Majeshi nchini, mmeona kabisa kwa siku hizi zote za karibuni nilisema hapa asubuhi, Sera yetu ya Ulinzi na Usalama imejikita katika maeneo kadhaa kama manne hivi. Ukiangalia la kwanza ni ulinzi wa mipaka yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Waheshimiwa Wabunge hatutakuwa na moyo wa shukrani kama siku hii ya leo hatutalipongeza Jeshi letu la Ulinzi kwa ulinzi mkubwa

unaofanywa kwenye mipaka ya nchi hii na hiyo imesababisha nchi yetu kuendelea kubaki ni nchi pekee sisemi kwenye mataifa mengine, sijui kinachoendelea huko, lakini mmeona ulinzi wa Taifa letu kwenye mipaka yetu ni imara kweli kweli na tuko salama kweli kweli. (*Makofi*)

Kwa hiyo, ni lazima kwakweli siku hii ya leo ilikuwa ni siku yetu sisi Wabunge wote kwa pamoja kuungana kwanza kulishukuru Jeshi letu la Ulinzi na kulipongeza kwa kiasi kikubwa na kiasi cha kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera yetu ya Ulinzi na Usalama inasema Jeshi hili la Ulinzi na Usalama katika hali moja ama nyngine litashirikiana na raia katika masuala mbalimbali. Mmeshuhudia Jeshi hili, tulipopata m aafa kwenye kivuko, Jeshi letu la Ulinzi na Usalama na Jeshi la Polisi walifanya kazi kubwa kweli kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mmeona nilisema hapa asubuhi sitaki kurudia yale yaliyokuwa yanasewma lakini pale ilipotokea kuna umuhimu wa Jeshi letu la Ulinzi na Usalama na Jeshi letu la Polisi kufanya kazi kwa pamoja wamefanya kazi nzuri Njombe, wamefanya kazi nzuri kule Kibiti na maeneo mengi tu wamefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kwakweli nasimama hapa kulipongeza Jeshi letu la Ulinzi na Usalama, lakini tumeona kabisa kwamba Jeshi hili lina kazi na limeendelea kurithi maono na maoteo mazuri ya Baba wa Taifa kudumisha ushirikiano na mahusiano mema na nchi nyngine na hasa katika Bara la Afrika. Mmeshuhudia Wanajeshi wetu wakijitoa kweli kweli kwenye ulinzi na usalama hata kwenye mataifa mengine nje ya Taifa letu na hiyo ndiyo Sera yetu ya Ulinzi na Usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunachokisema hapa tunampongeza kwanza Amiri Jeshi Mkuu, Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu kama leo wote sisi Wabunge tunakubaliana na kuungana mkono kwamba kazi nzuri inafanywa na Jeshi letu la Ulinzi na Usalama

ina maana Amiri Jeshi Mkuu anafanya kazi yake sawa sawa kulisimamia Jeshi letu. Kwa hiyo ni lazima na yeze tumpongeze. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa sisi tunachokichukua kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge ni ushauri ambao, ushauri mwema, ushauri wenyewe msingi ambao Bunge linatushauri Serikali namna nzuri ya kuliboresha Jeshi letu, ya kuhakikisha Jeshi letu linaendelea kufanya kazi yake vizuri tena kwa weledi mkubwa na hiyo hatuna shaka, tumekuwa tukishuhudia lakini tunaendelea kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanaungana mkono na Jeshi letu na wanaendelea kutoa ushirikiano wa kutosha kwa Jeshi letu ili liendelee kuwa Jeshi la mfano na liendelee kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema haya ambayo hata ungeniamsha kwenye usingizi ningeyasema tu, ninaomba nichukue nafasi hii kuunga mkono hoja, kumpongeza Waziri, kulipongeza Jeshi letu na kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu Dkt. John Pombe Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mtoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuja kuhitimisha hoja yangu jioni ya leo. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha, kutupa afya njema ili kuweza kuhitimisha majukumu ya Wizara yangu kama ambavyo ilivyo ada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza na kwa maandishi. Waliochangia kwa maandishi idadi yao ni 29 na waliochangia kwa kuzungumza idadi yao ni 15 ukiwajumuisha Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Waitara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kujibu hoja kwa hoja za Kamati; kwa kiwango kikubwa Kamati imejielekeza katika kuiombea Wizara ya Ulinzi iweze kupata fedha za kutosha kutekeleza majukumu yake. Tunashukuru kwa hilo na hatuna shaka yoyote kwamba kadri hali ya uchumi inavyoimarika Serikali inaona umuhimu wa kuongeza fedha kwa Wizara yetu ili majukumu yetu ambayo ni ya msingi kabisa ya ulinzi wa nchi yaweze kufanyika kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo Kamati ya NUU (Nje, Ulinzi na Usalama) imeshauri kuongezwa kwa ukomo wa bajeti ya Wizara ya Ulinzi, Serikali ione umuhimu wa kuongeza kasi ya ulipaji madeni ya kimkakati kwa kutenga fedha zaidi kwenye miradi ya maendeleo, Serikali itoe fedha za maendeleo zilizoidhinishwa kwa Fungu 38 kwa mwaka wa fedha unaoisha, Serikali ione umuhimu wa kuongeza fedha za maendeleo zilizotengwa, Serikali itoe fedha zote zilizoidhinishwa kwa ajili ya kugharamia mafunzo na usalama na utambuzi, Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya utunzaji wa zana, magari, mitambo na Serikali itoe fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya kuboresha mfumo wa mawasiliano salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla karibu hotuba nzima ya Kamati ilijikita katika uona umuhimu wa kuweza kupata bajeti stahili ya kutekeleza majukumu yetu na sisi tunasema ahsanteni sana na Serikali kwa kweli nia hii ipo, kadri uwezo unavyoongezeka na Wizara hii inaweza kupata mgao unaostahili kwa majukumu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hao, naomba sasa niingie kwenye hoja za Kambi ya Upinzani na nianze kwa kusema leo nimesikitishwa sana kwa kauli zilizokuwa zinatolewa kuhusu Jeshi letu. Tumezoea kusikia kwamba ndani ya Bunge hili kila mtu anaunga mkono kazi nzuri zinazofanya na Jeshi letu. Yanapotokea maneno aidha ya kukashifu au kukejeli kwa kweli huwa napata taabu sana kwa sababu Waheshimiwa Wabunge, sisi sote ni mashahidi juu ya kazi nzuri inayofanywa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tuangalie tu majirani zetu wapi kuko salama kama tulivyo sisi. Sasa tusichukulie kwamba amani hii tuliyokuwa nayo ipo tu imekuja yenyewe, kuna watu wanafanya kazi usiku na mchana. Kwa hivyo, naomba niwasih sana ndugu zangu katika suala la ulinzi wa nchi tusiingize sana siasa. Tukiingiza siasa tutaharibu kwa sababu ulinzi ndio kila kitu. Bila ya ulinzi, bila ya amani hamuwezi kufanya kingine chochote. Kwa hiyo, bila shaka tutarekebisha kauli zote zilizotolewa ambazo kwa kweli hazikuwa na sababu ya kutolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la hali za wanajeshi wastaa fu hususan cheo cha *private* hadi *Brigadier General*/hazilingani na uzito wa kazi wanazofanya. Niseme tu Serikali inathamini kwa kiwango kikubwa kazi zinazofanya na zilizofanya na wanajeshi wastaa fu. Serikali imehakikisha wanalipwa mafao yao ya kustaafu kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo za utumishi wa JWTZ. Aidha, Serikali imeendelea kupitia upya mafao ya wanajeshi wastaa fu wote ili aweze kuendelea kulipwa kwa kuzingatia hali ya uchumi ilivyo kwa lengo la kuboresha maslahi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleze Bunge lako tukufu kwamba mpango wa kuboresha maslahi kwa wanajeshi wanaostaafu upo na tunaenda hatua kwa hatua, Jeshi hili ni kubwa. Huwezi kufanya watu wote wapate mara moja. Ilianza ngazi ya *Major General*/mpaka Jeneral, itafuata ngazi nyininge na hatimae tutakamilisha Jeshi lote lakini maadam nia na dhamira ipo, hali ya uchumi ikitruhusu jambo hili litatekelezwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja kutoka Kambi ya Upinzani kwamba nyongeza ya mishahara kwa wanajeshi, wao waliita *annual increment* haipo kwa maana walisema wanajeshi hawapati *annual increment* kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaeleze kwamba *statement* hiyo sio kweli, Serikali inaendelea kutoa *annual increment* kila mwaka kwa ngazi za vyeo husika. Serikali

imekuwa ikitoa nyongeza za mishahara kwa maana *annual increment* kwa kipindi chote cha Serikali ya Awamu ya Tano na inaendelea kufanya hivyo. Aidha, hakuna malimbikizo yoyote ya *annual increment* ambayo hayajalipwa au wanajeshi wanadai. Pia hakuna posho zilizofutwa, bali zilizopo zimeendelea kuboreshwa zaidi mfano, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 posho za wanajeshi zimeboreshwa kwa asilimia 15 ikilinganishwa na posho za mwaka uliopita. Kwa hiyo, hapa tunachozungumzia ni kwamba kila mwaka kwa kila cheo kuna *increment* wanayopata kwenye mishahara yao. Lakini vilevile posho zinazotolewa kwa mfano *Ngome Allowance* ile ya makazi fedha za maji, fedha za umeme, fedha za taaluma zote zimekuwa zikipata *increment* na kama nilivyosema kwa kiwango cha asilimia 15.

Kwa hiyo, ningeomba sana kwamba hizi *statement* zinazotolewa pengine ni vyema watu wakathibitisha kabla ya kuzisema ndani ya Bunge lako. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu posho ya chakula kwa wanajeshi yaani *ration allowance*, Kambi ya Upinzani imesema imegeuzwa kuwa ada ya kulipia mafunzo katika shule na vyuo vya kijeshi kwa wanajeshi wanaokwenda mafunzoni. Nataka niwaeleze ndugu zangu kwamba *ration allowance* ni fedha zinazotolewa kwa ajili ya kumlisha mwanajeshi na kila mwanajeshi anapata fedha hizo kuititia kwenye akaunti yake pamoja na mshahara wake. Kwa hiyo ukisema kwamba umepewa fedha za chakula halafu umekwenda kwenye mafunzo unataka ulishwe, hiyo sio sawa. Cha msingi hapa ni kwamba kuna maeneo machache ambayo watu wanaopata *ration allowance* bado wanapewa na chakula, nayo ni katika *operations*, siyo kwenye mafunzo ya kawaida. Kwa hiyo, *operations* na kazi za mipakani, kule wanalishwa na wanapata *ration allowance*, lakini kwa wengine wote wanatakiwa wajilishe kwa sababu fedha hizo wameshaingiziwa kwenye akaunti zao. (*Makofi*)

Kuhusu suala la JWTZ kuingilia utendaji wa kazi za Jeshi la Polisi, mimi nadhani tu niliweke sawa hili ili Waheshimiwa

waelewe, vyombo hivi nya ulinzi na usalama haviwezi vikafanya kazi kila kimoja peke yake, hiyo itakuwasiyo kazi ya ulizi. Kazi ya ulinzi inataka vyombo vishirikiane, kwa sababu matishio ni tofauti. Unaposema kwamba jeshi la wananchi libaki mipakani, wakati kuna ugaidi, unategemea itakuwaje. Inapokuwakuna suala la ugaidi lazima Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, Usalama wa Taifa na vyombo vingine nya ulinzi na usalama vishirikiane, ndicho kinachoanyika. (*Makofii*)

Kwa hiyo, JWTZ na Jeshi la Polisi ni Vyombo nya Ulinzi na Usalama ambavyo vimeundwa kwa sheria na mipaka ya majukumu yao ya kiutendaji ipo wazi, na hakuna mwingiliano wowote. JWTZ itanedelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria za nchi yetu na bila kuingilia mamlaka ya vyombo vingine nya ulinzi na usalama, ni masikitiko na bahati mbaya sana kwa Kambi ya Upinzani kudiliki kusema, kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi anaingilia Mamlaka ya Jeshi la Polisi, hii siyo sahihi, hata kidogo na tunaikataa kwa nguvu zote, kwa sababu kwanza tutambue kwamba Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, ndiyo Mwenyekiti wa Kamati ya Vyombo nya Ulinzi na Usalama. Kwa hiyo, Mkuu wa Majeshi anayo haki kuzungumzia vyombo vyote kwa ujumla wake, akiwa kama Mwenyekiti. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nadhani hoja hii siyo sahihi na tuendelee kuamini kwamba bila ya kuwa na Jeshi kushirikiana na vyombo vingine, kuna baadhi ya kazi zitashindikana kufanyika! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna hoja ya kwamba Serikali haiwekezi kwenye shughuli za ugunduzi na utafiti katika JWTZ. Nataka niwaeleze ndugu zangu kwamba ukienda Nyumbu, ukienda Mzinga, utakuta kuna baadhi ya tafiti zinafanyika hadi leo, ni kweli tunakiri kwamba fedha za kuwawezesha kufanya tafiti kubwa bado hazijapatikana, lakini hii haikuwakatisha tamaa, wamekuja na mpango mkakati, taasisi zote mbili hizi; Nyumbu, wao wamekuja na mpango wa miaka 10, wenye bajeti ya shilingi bilioni 227 na kwa miaka mitano ya kwanza bilioni 105. Fedha hizi zikipatikana kuitia bajeti zetu kwa sababu sasa hivi hili suala

liko katika majadiliano Serikalini, Shirika hili litawenza kufanya kazi zake za utafiti inavyotakiwa na vilevile Mzinga wana mpango wa miaka mitano, wenyewe bajeti ya shilingi bilioni 152 ambaao na wenyewe fedha hizi zikianza kutiririka katika bajeti zao kwa miaka inayokuja, wataweza kufanya tafiti kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mchakato wa manunuzi ya sare za Jeshi, kwamba uchunguzwe. Walisema Kambi ya Upinzani, kwamba taratibu za ununuzi wa mavazi ya Jeshi hufuata taratibu kwamba hauendi, yaani una walakini, lakini pia wanajeshi wanavaa mavazi ambayo hayawatoshi, kwamba kuna mavazi madogo au makubwa wanapewa. Sasa tuweke sawa kwanza kuhusu mchakato wa manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utata wowote katika utaratibu wa manunuzi ya mavazi ya Jeshi. *Tender zinatolewa* kama kawaidia, watu wanashindanishwa kama kawaida na wanaoleta mavazi hayo basi wanakuwa wamweshinda kitaratibu zinazohusika, sasa sijui Kambi ya Upinzani wanalitoa hili wapi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusu mavazi kutowatosha wavaaji, nalo ni maelezo ambayo yana kasoro. Niseme tu kwamba mavazi yote ya Jeshi, yote, wanajeshi kila mtu anapimwa isipokuwa kombati, kwa hiyo, ukiwaonaleo wanajeshi wote wamevaa mavazi yanayowatosha, kwa sababu wanapimwa. Kombati peke yake ndiyo zinaletwa kwa *size mbalimbali*, kuna ndogo, *medium*, *large* na *extra-large*. Sasa kuna mtu yeye ni *size yake* ni *small* amepewa *extra-large*, kunahaja gani ya kulalamika, si kurudisha tu ili aweze kupewa kwa *size yake*. (*Makofii*)

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa, ndugu zangu Kambi ya Upinzani, msiyachukue maneno haya kijumlajumla, haya ni maneno yenye lengo la kugombanisha, nadhani si sawa sisi tukayabeba kwa ujumla namna hiyo. Mimi sioni tatizo lolote, kama *size zipo* kuanzia *small* mpaka *extra-large*, kwa

nini usipate size yako, kama umepewa siyo, ni kiasi cha kubadilisha tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Sheria ya Ulinzi wa Taifa; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inaendelea kufanya majadiliano ya ndani yenye lengo la kuboresha Sera ya Ulinzi na kama tulivyo sema siku za nyuma, hatimaye tume pata mapendekezo au tuseme maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na vilevile baada ya kupitiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na wenyewe wametoa maoni yao, kazi inayofanyika sasa hivi ni kutayarisha rasmu ya kwenda kwenye Balaza la Mawaziri ili hatiye hii sera iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya ulinzi na usalama kwenye mipaka yetu ya nchi; Wizara inasema zoezi la kurejesha alama za mipaka kimataifa llnahitaji fedha na utayari wa nchi husika. Hapa hoja ilikuwa ni kwamba mipaka hakuna alama na kwamba Wizara husika hazijashughulikia tatizo la mipaka kwa maana ya *beacons* na kadhalika. Mheshimiwa Masoud hili suala amekuwa akilizungumza kila mwaka, lakini tushukuru tu na niseme kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa na katika mpaka wetu wa Kenya kazi hii imefanyika, katika mpaka wetu wa Uganda, kazi hii imefanyika na katika mpaka wetu wa Burundi kazi hii imefanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka mingine tutaendelea kwa kadri fedha zinavyopatikana na mtambue tu, kwamba kazi hii ni kazi ya Wizara nyingi, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Mambo ya Nje, Wizara ya Ulinzi na kadhalika. Kwa hiyo, ni vyema tushukuru kwamba hatua zimeanza kuchukuliwa na tumeanza sasa kuboresha mipaka yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maeneo ya wananchi yaliyochukuliwa na Jeshi Serikali kushindwa kulipa fidia; hii imekuwa ni hoja kwa siku nyingi sana, na naomba nieleze kidogo kuhusu hoja hii kwamba Serikali inatambua umuhimu wa kuhakikisha kwamba wananchi wote wanalipwa fidia kwa kadri uwezo unavyopatikana. Mwaka

huu tunaomaliza, tulitenga bajeti ya shilingi bilioni 20.9 kwa ajili ya kulipa fidia katika maeneo mbalimbali. Tumeshafanikiwa kulipa eneo moja la Kilwa, lakini tumeanza kulipa Kakonko kule, na tumeanza vilevile kulipa maeneo kadhaa.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapani kwamba, sasa hivi Wizara ya Fedha imeshaweka/imeshatenga shilingi bilioni 16 ili tuendelee kulipa maeneo mengine yaliyobaki. Tathmini, uhakiki ulishafanyika katika katika baadhi ya maeneo, samahani, tathmini ilishafanyika, lakini uhakiki ndiyo unaoendelea sasa. Kwa hiyo, kuna eneo la Ilemela kule, maeneo mawili katika Wilaya ile, lakini vilevile kuna maeneo ya Tarime, kuna maeneo ya Makoko, kuna maeneo kadhaa ambayo yanafanyiwa uhakiki, ili fedha zile zianze kulipwa kwa wahuksika.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tuvute subira wakati mchakato huu wa uhakiki wa fedha zilizofanyiwa uthamini unaendelea ili tuweze kukamisha ulipaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi baina ya wananchi na Jeshi, kama vile kubomolewa nyumba, kukatwa mazao ya wananchi na kadhalika; yamezungumzwa sana humu ndani, lakini mimi napenda niseme mambo mawili; kwanza tutambue kwamba maeneo ya jeshi ni maeneo ambayo wananchi wakiambiwa wasikae karibu ni kwa maslahi yao wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na ningekuwa nayasema haya bila ya matukio yaliyotokea siku za nyuma, pengine ningonekana nasema tu, lakini tuna mifano hai, yalitokea pale Gongo la Mboto, yalitokea pale Mbagala, kwa nini wananchi waendelee kukaa katika maeneo haya.

Sasa watu tunatofautiana, kuna watu unaweza ukawaambia mnatakiwa kuhamza wakahama, kuna watu wengine hawaelewi lugha hiyo, kwa hiyo, lazima hatua zichukuliwe, na ndiyo maama hatua zinapochukuliwa, basi

tusiwe tunapiga kelele ni kwa sababu ya maslahi yao wenyewe, haya maeneo mengine ni hatari kwa watu kukaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa zaidi ni kuangalia nani mwenye haki, unapokuwa umevamia katika eneo la Jeshi liliopimwa, lenye mipaka. Kuna njia gani zaidi ya kuzungumza zaidi ya kumwambia mtu atake asitake lazima aondoke, kwa hiyo, ndicho kinachofanyika. Kwa hiyo, sioni kama hili suala tulichukulie kisiasa, tulichukulie kwamba watu wameonewa, watu hawajaonewa, na mpaka haya yametokea, wameshapewa *warning* mara kadhaa, kila aina ya juhudhi zinafanyika na nimwambie tu ndugu yangu aliyezungumia suala hili la kukatwa hii mipapai, ni kwamba Serikali za Mitaa ile, za Vijiji vile, zilitumika kuwashawishi, kuwaambia wananchi wahame, lakini baada ya mbinu zote kushindikana, basi lazima tutumile njia hizi, hakuna njia nytingine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa amani nje ya nchi, Waheshimiwa Wabunge kwenye upande wa Upinzani walitaka kujua idadi ya wanajeshi waliopoteza maisha na vilevile na stahili wanazopaswa kupewa endapo wanapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanajeshi anapoumia au kufariki akiwa katika ulinzi wa amani huwa anapewa malipo ya sehemu mbili, sehemu ya kwanza anapata malipo ambayo yanatolewa na Umoja wa Mataifa na sehemu ya pili hutolewa na Seikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuzingatia kanuni zilizowekwa za pensheni kwa Majeshi ya Ulinzi.

Kwa hiyo, hakuna utata katika mafao ya wanaopoteza masiha wakiwa katika ulinzi wa amani, fedha hizo zinatolewa kwa pande zote mbili na niseme tu malipo yanayotolewa na Umoja wa Mataifa ni dola za kimarekani 70,000 na fedha za rambirambi ambazo hutolewa na Mkuu wa Majeshi ikiwa ni mishahara ya miezi sita na familia zinasafirishwa pamoja na mizigo kwenda nyumbani. Kwa hiyo,

hakuna utata kabisa katika eneo hili na mara zote yanapotokea maafa ya kupoteza watu katika maeneo hayo, Serikali imekuwa ikitoa taarifa na taarifa ziko wazi za idadi ambao wamepoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili nizungumzia pia wajane wa wanajeshi waliofariki, hoja ilikuwa ni kwamba hawatunzwi, ni kwamba wajane wa hawa waopoteza maisha, Serikali imekuwa ikihakikisha kuwa wanatunzwa, wajane na mayatima na kuwapa stahiki zao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya jeshi katika kupambana na matukio ya kigaidi nchini; Kitengo cha Usalama na Utambuzi (*Military Intelligence*) kitumike kusaidia Jeshi la Polisi kubaini na kukabiliana na vitendo vya kigaidi vinavyofanywa na watu wasiojulikana, mfano kutekwa kwa watu ambao wamewataja. Sasa niseme tu, ni Kambi hii hii ya Upinzani katika hoja yao walisema Jeshi lisiingilie kazi za Polisi, halafu Kambi hii hii inasema, *military intelligence* isaidie Polisi. Sasa tunachoweza kusema hapa ni kwamba vyombo hivi lazima vifanye kazi kwa pamoja. *Military Intelligence* lazima iasaide jeshi la polisi katika masuala ya ugaidi, masuala ya uharamia, masuala ya usafirishaji haramu wa watu na kadhalika, hizo kazi lazima zifanywe kwa pamoja, kwa hiyo, msione kwamba jeshi linaingilia kazi wa vyombo vingine, ni wajibu wao kufanya kazi hizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Jeshi la Kujenga Taifa katika kuongeza uchumi wa viwanda nchini. Hili linatambulika, Jeshi la Kujenga Taifa linafanya kazi ya viwanda, linafanya kazi ya kilimo, ufugaji na kadhalika. Nia na madhumuni ni kwamba tuhakikishe wanachangia katika ukuaji wa uchumi na wana viwanda kadhaa kama ambavyo nimevitaja katika hotuba yangu vikiwemo Kiwanda cha Mahidi - Ruvuma, Kiwanda cha Kutengenezea Bidhaa za Ngozi - Dar es Salaam, Kiwanda cha Kokoto, Kiwanda cha Kutengeneza Samani - Chang'ombe, Kiwanda cha Maji - Dar es Salaam na kadhalika. Kwa hiyo, viwanda viko vingi, wanaendelea kufungua na biashara mbalimbali, ikiwemo

ulinzi na kadhalika, ili tuweze kuchochaea uchumi kupitia Jeshi letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ajira Jeshini, wanasema vijana wengi wa JKT kutoajiriwa na Jeshi, nadhani hii niitolee ufanuzi kidogo. Tunachukua vijana wa kujitolea wengi, kwa mwaka wanaweza wakafika 20,000; hatuvezi kuwaajiri vijana wote hawa, na ieleteke kwamba anayeingia katika Jeshi la Kujenga Taifa, si kwa madhumuni ya kutafuta ajira, ni kwa madhumuni ya kupata stadi za kazi, ni kwa madhumuni ya kupewa stadi za ulinzi wa nchi yake, na hili ni Jeshi la Akiba. Kwa hiyo, hawa huwa wanapewa mafunzo yale ya kijeshi, lakini baadaye wanapewa mafunzo ya stadi za kazi. Wanaobahatika kuajiriwa wanaajiriwa na ambao hawabahatiki wanatakiwa wakajajiri baada ya kupata stadi za kazi hizo.

Kwa hiyo, vijana wengi wamekuwa wakilalamika lakini nataka ieleteke, kwamba ukijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa, siyo kwamba unaingia kwenye ajira, ni kwamba unakuja kuoata mafunzo ya stadi za kazi na ukakamavu za uzalendo, ili hatimaye uweze kuwa jeshi la akiba kwa ajili ya nchi yako. Kuna baadhi ya nchi ni watu wote lazima wapiti huko. Kwa hiyo, ilie hoja ya kwamba mnawafundisha kutumia dhana za kivita halafu hamuwapi ajira, wala siyo hoja, kwa sababu kuna nchi, kwa mfano Israel, kila mtu, lazima apate mafunzo hayo. Madhumini yake ni nini, madhumuni yake ni kwamba hili ni Jeshi la Akiba, wanapohitajika wakati wa vita, lazima watu hawa wawe wana ujuzi wa kutumia silaha ili waweze kuisaidia nchi yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wa saa za kazi jeshini bado unalalaikiwa, Waheshimiwa Wabunge, mimi nadhani tusiingie huku, wanajeshi wanatakiwa wawe kazini, wawe tayari masaa 24, jeshini hakuna suala la saa za kazi, saa 24 uwe tayari. Ukiwa una mapumziko ni kutokna na kitengo ambacho upo au maeneo ya kazi ambayo unafanya au una majukumu maalum, lakini kwa mara zote inatakiwa masaa 24 watu wawe kazini. Kwa hiyo, hili suala la kulalamikiwa kwa masaa 12, mimi nadhani wala siyo la msingi na tusiingilie kama

wanasiasa, tuwaache wenyewe kwa kanuni zao na taratibu zao za kijeshi watekeleze majukumu yao. (*Makof*)

Mimi nadhani haitakuwa busara twende na vile mnavyotaka kwamba watu saa tisa wasiwepo, limetokea tatizo, itakuwa sisi wa kwanza kulaumu kwamba Jeshi halikutekeleza wajibu wake, ndiyo maama watu wote wanatakiwa wawe kazini muda wote na tumwachie Mkuu wa Majeshi apange taratibu za kazi kwa wanajeshi wake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upandeshwaji vyeo kwamba kuna mizengwe, kuna nini, mimi nadhani hizi kauli tujiepushe nazo, hakuna mizengwe, kuna taratibu. Taratibu kupandishwa vyeo JWTZ au tuseme Jeshi kwa ujumla, utaratibu wa kupandisha vyeo maafisa na askari unazingatia mambo yafuatayo; kufanya kazi, kufanya kozi kwa cheo husika, tabia na mwenendo mzuri, utendaji kazi mzuri na kujituma, tabia yake kiusalama, nafasi katika muundo kama ikama ipo, kutimiza muda wa kukaa na cheo kimoja. Sasa haya yote yanafuatwa, asitokee mtu akaja kwa Mbunge akasema kwamba mimi sjapandishwa cheo na kozi nimefanya, kozi siyo kigezo pekee, nimetaja vigezo vingapi hapo, kuna vigezo vingi! (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tujiepushe na kuchukua maneno haya kutoka kwa vijana hawa au kwa watu ambao hawalitakii mema Jeshi. Mimi nataka nikupeni ushahidi wangu, kwa kipindi nilichokaa katika Wizara hii, watu wamepanda vyeo ninawaona kila wakati. Watu wamepanda vyeo kila wakati kwa sabbu jeshi hili linaendeshwa kwa taratibu na kanuni zinazotakiwa na ndiyo maana tuko vizuri, hata ulinzi wetu uko vizuri, kama ingekuwa kuna matatizo hayo simgeona kuna migomo na vitu kama hivyo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingie kwenye hoja za Waheshimiwa Wabunge wengine, Mheshimiwa Richard Ndassa alitaka Kambi ya JKT Kanda ya Ziwa, hili limepokelewa

litafanyiwa kazi na bila shaka na sisi tunataka hilo litokee.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Fakharia alitaka nyumba za wanajeshi ziboreshw, ni kweli, tunatambua kwamba tuna changamoto ya kuchoka kwa nyumba nyingi za Jeshini, na ndiyo maana tukawa tuna ule mradi wa nyumba mpya. Nyumba mpya zile zimejengwa zaidi ya 6,000, hazitoshelezi, nyumba za zamani kuna bajeti ndogo Wizarani, kuna bajeti ndogo Ngome kwa ajili ya kukarabati nyumba zile, lakini kwa sababu ya upungufu wa bajeti, hatuwezi kufika kote zikawa nzuri kwa wakati mmoja. Tunaomba tuvumilie wakati utaratibu unaendelea awamu kwa awamu kuboresha nyumba na ukarabati wa nyumba za wananchi.

Kuhusu suala la fidia kwa wanaodai, hili nimeshalizungumza, fidia za ardhi, suala la ajira, lini watapata ajira kama alivyosema Mheshimiwa Rais, tunalifanyia kazi liko katika mchakato wa kupanga wale ambao Mheshimiwa Rais alisema wapatiwe ajira, watapata ajira hizo kama ilivyoagizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki za wastaifu kusumbuliwa, hili Mheshimiwa Fakharia naweza nikasema kwamba tumelipokea, tunaona ugumu wa mtu ambaye amestaifu hajapata mafao kwenda Makao Mkuu kila mara kunaweza kukamgharimu sana. Tutatafuta utaratibu mzuri zaidi wa *documents* zote kuwekwa sehemu moja pale Zanzibar ili wazijaze na baadae baada ya kukamilisha mchakato huo zipelekwe Makau Makuu ndipo muhusika atakiwe kwenda kule ili kumalizia mchakato.

Mheshimiwa Anatropia alizungumzia bima ya afya, na sisi tunakubaliana kwamba ni muhimu tupate bima ya afya kwa wanajeshi na mchakato wa kuanzisha bima ya afya kwa wanajeshi unaendelea. Sisi kama Wizara tunataka bima ya afya ya wanajeshi itayoendeshwa na wanajeshi na hili tunasababu ya kutaka kufanya hivyo, kwa sababu fedha zitakazopatikana tutaweza kuboresha vituo vyetu, kujenga vipyta na kutumia na hospitali nyingine kutoa huduma. Kwa

hiyo watu wasiwe na wasiwasi kwamba labda mna vituo vichache hapana, vituo vingine vitatumika ambavyo siyo vya jeshi tukiwa na bima ya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, SUMA kujiingiza kwenye mikataba mibovu, hili lilishazungumzwa *Tanzansino, Cami SUMA, Equatorwote* hawa tulishatolea ufanuzi katika bajeti zilizopita, mikataba hii imesitishwa kwa sababu haikuwa mizuri na ni nia ya Serikali kuondoa mikataba yote mibovu na sasa hivi mikataba mingine yote tunayoingia tunahakikika inakwenda vizuri ilituweze kupata masilahi kutokana na mikataba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ile Kampuni ya URSUS, Mheshimiwa Anatropia nikueleze tu kwamba URSUS haifanyi kazi na SUMA JKT, inafanya kazi na *NDC*, wanakwenda vizuri matreka tunayaona wanaendelea kama kawaida. URSUS hawapo upande wa SUMA. (*Makofii*)

Mheshimiwa Maryam Msabaha, kuhusu viatu kwamba havina viwango vinavyotakiwa; nieleze tu kwamba viatu sasa vinanunuliwa nchini humuhumu, SUMA JKT wana kiwanda kidogo cha viatu, lakini kuna kampuni zinazozalisha ndani zinanunuliwa humu ndani. Kwa hiyo siyo kweli kwamba tunaendelea kununua kutoka China vyenye kiwango kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uhakiki wa mipaka nilishalitolea maelezo Mheshimiwa Rehani anataka mafunzo ya JKT yawajenge vijana kujitegemea, hili ndiyo tunalolifanya, tunawafundisha stadi za kazi ili waweze kujitegemea na kuna programu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya uwezeshaji. Ni matumaini yetu kwamba tukiziunganisha hizi baada ya kupata stadi za kazi na kuwezeshwa vijana hawa wataweza kujitegemea wao wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, JKT lijitegemee kwa chakula ndiyo nia yetu, ni kweli tunayo maeneo makubwa ya kilimo na ufugaji, tunataka tuwawezeshe JKT kifedha kwa maana kibajeti ili waweze kulima, waweze kufuga wajitegemee wao wenywewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Ras Mshindo kwamba ijengwe karakana na bandari ya uvuvi, hilo liko katika nia yetu kuweza kuweka karakana pale nzuri kwa ajili ya meli za kijeshi na meli za kiraia, vilevile ikiwezekana kuweka bandari ya uvuvi ili kuweza kupata kipato kwa ajili ya kuendesha Jeshi na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malembeka Serikali iangalie jinsi ya kuajiri vijana wa JKT, hili nilishalitolea ufanuzi Waheshimiwa Wabunge vijana hawa ni wengi, hatuwezi kuwachukua wote, lakini vyombo vyote vya ulinzi na usalama vimetakiwa kuchukua kutoka JKT.

Kwa hiyo, baada ya kuchukuliwa na vyombo vyote vya ulinzi na usalama bado wanabaki wengi ni lazima watafutiwe njia nyingine za kujajiri.Kwa hiyo wasitegemee kwamba wote watapata ajira katika vyombo vya ulinzi na usalama.

Kuhusu Waziri atoe taarifa ya kupigwa watu kule Afrika ya Kusini, hili lilihatolewa ufanuzi na Waziri wa Mambo ya Nje kwamba atalitolea maelezo yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Jeshi Welezo kwamba haliendani na mandhari ya pale na vitu vinavyofanyika siyo vizuri, hili limeshazingatiwa na limefanyiwa kazi kwa kweli yale mambo ambayo yalikuwa yanaharibu taswira pale yameshaondolewa.

Mheshimiwa Kanali Masoud, Serikali iongeze pensheni kwa wastaafu; hili liko katika mkakati kama nilivyosema awamu kwa awamu, mipaka fedha nyingi za upimaji na fidia hazitoshi Serikali iongeze, tunakubaliana na kadri bajeti itavyoruhusu tutaendelea kupima ili kuondoa migogoro ambayo kila mara inajitokeza.

Kuhusu Nyumbu na Mzinga yaboreshwe, nimeshatoa ufanuzi kwamba wana mipango mikakati sasa ili kuweza kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Salim Jeshi limetumika kiutemi kufyeka mipaka nilishalisemea. Wanajeshi hawalipwi *overtime*, hakuna Jeshi duniani wanaolipwa *overtime*, Jeshi dunia nzima wanafanya kazi muda wote. Kwahiylo hakuna suala la *overtime* jeshini, wanakatwa kodi kwenye mishahara ndivyo utaraibu, Serikali inajientesha kwa kodi za watu wote, hakuna upendeleo katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mishahara haina tofauti na watumishi umma, hii siyo kweli wana viwango vyao ni tofauti, hawana bima za afya ndiyo kama tulivoyzungumza kuhusu bima ya afya na fedha zitumike kwenye *piece keeping* ili kupata fedha. *Piece keeping* tunafanya na hizo *re-embracement* tunazipata, na tunaweza kuboresha Jeshi kuititia *re-embracement* hizo.

Mheshimiwa Musukuma ametaka Wabunge wapate mafunzo pale *NDC*, ni wazo zuri na mimi ninashauri kwa kila mwenye nafasi na atakayependa anaweza ku-*apply* pale *NDC* aweze kupata mafunzo kwa kweli itabadilisha taswira au uelewa wa ulinzi katika nchi yetu.

SUMA JKT wapewe ulinzi wa migodi watafanya kazi ya kwenda kushawishi migodi iwave kazi kwa sababu ni uwamuzi wao kumpa wanaemtaka lakini SUMA JKT watafanya kazi hii.

Kuhusu bima ya afya, Mheshimiwa Mlinga tulishaitolea ufanuzi, Mheshimiwa Getere alitaka matreka ya SUMA JKT pale kilimo kwanza yaondolewe au wakulima warudishie, hili limepokelewa na Mkuu wa JKT atalifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo linaondoka kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo hoja nytingine kuhusu maeneo mengi ya Jeshi kuvamiwa na wananchi kuanzia sasa au tumeshatoa utaratibu wa kwanza kupima maeneo ya Jeshi ili kuweka mipaka. Nadhani hii ndiyo itaondoa tatizo lote, kwa miaka mingi Jeshi lilikuwa lina maeneo ambayo hayajapimwa hiyo ilitoa nafasi kwa watu kuyavamia, lakini

sasa yatapimwa na yatapewa hati miliki, ili kuondoa utata huu wa kuvamiwa mara kwa mara na kuleta migogoro.

Vilevile tutaweka mapango kwa sasa wakati utaratibu huo wa kutafuta fedha za kupima na kupata hati miliki mapango yatawekwa, miti itapandwa ili kuondoa utata wa mipaka ilipo na wananchi waache kuyavamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakuu wa Vikosi wamepewa maelekezo ya kufanya doria mara kwa mara ii watu wasiachiwe wanajenga wanamaliza halafu ndiyo wanakuja kubomolewa, hii iwe inafanyika pale wanapoanza ili kuondoa malalamiko yanayotokana na watu ambao wameshajenga au wameshawekeza vyatutu kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za mikataba kwamba Serikali itenye fedha za kutosha katika fungu la maendeleo ili kulipa madeni ya mikataba. Hii imekuwa ikifanyika awamu kwa awamu, fedha zote karibu zote ambazo zinawekwa katika bajeti yetu ya maendeleo madhumuni yake ni hayo kulipa mikataba ambayo tumeingia, si rahisi kuilipa yote kwa kipindi kimoja na ndiyo maana kila mwaka tumekuwa tunafanya hivo awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mzinga na Nyumbu, nilishatolea ufanuzi kwamba mashirika haya yana mipango mikakati ili yavezeshwe na yakiwezeshwa yatafanya kazi nzuri zaidi kuliko ambavyo inafanyika sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za chakula kwa wanajeshi kwamba Serikali itenye fedha za kula za kutosha na ziongezwe kiwango, hii hoja imepokelewa, tunaendelea mazungumzo na Hazina ili kuona uwezekano, bila shaka hili linategemea na mapato ya Serikali, lakini kila mapato yakiongezeka na uwezekano ukipatikana kwa sababu tumetoka mbali, hatukuanzana hii fedha ambayo inatolewa sasa hivi tulianza shilingi 3,000 ikaja shilingi 5,000, ikaja shilingi 8,000 sasa shilingi 10,000. Kwa hiyo, bila shaka Serikali itaendelea kuboresha hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sera ya Ulinzi ya Taifa, nimeshalitolea maelezo kwamba mchakato wake sasa umefika hatua nzuri sana na muda si mrefu tutafikisha katika mamlaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Serikali itenye fedha kwa ajili ya shughuli za Jeshi ikiwemo barabara, vikosini na barabara za mipakani; kwa kweli mpaka sasa hivi hakuna sera maalum ya barabara za mipakani na fedha hizo haziji katika Wizara ya Ulinzi, fedha hizo bado zinapelekwa Halmashauri, ni wajibu wa halmashauri kuhakikisha kwamba wanaziboresha barabara hizo.

Waheshimiwa wengi walichangia kuhusu vijana wa JKT kuwezeshwa ili waweze kujajiri. Niseme tu kwamba JKT linaendelea kutoa mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana wakujitolea, kupitia shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, ufugaji na ufundu. Aidha, kupitia mashamba darasa yaliyopo makambini vijana wanajifunza utaalim mbalimbali wa kilimo na ufugaji utakaopelekea kuwezakujitegemea mara wanapomaliza mkataba.

Vilevile JKT ililingia mkata na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ikilenga kuwafundisha elimu ya ujasiliamali wakufunzi wanaotoa mafunzo kwa vijana wa JKT; mafunzo hayo yameongeza uwezo vijana kupata elimu iliyo boresha ya stadi za kazi na ujasiri amali. Pamoja na hatua hizo JKT ipo katika mpango wa kujenga *Vocational Training Center*, Kongwa, Dodoma ili kuweza kuongeza uwezo wa mafunzo ya stadi za kazi kwa vijana ili waweze kujajiri wenye baada ya kuhitimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mkazo tuweke hapa kwamba hawa vijana wawezeshwe baada ya kupata stadi za kazi wajajiri kwa sababu si kweli kwamba wote wanaweza kuajiriwa na Jeshi na sasa hivi imekuwa malalamiko mengi, lakini ni kutojua pale wanapojiunga kwamba si wote watakaopata ajira na bila shaka wakiwezeshwa kimafunzo wataweza kujitegemea wao wenye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kero ambazo zilielezwa hapa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu kumbi za burudani katika Kambi za Jeshi kutumiwa na wananchi badala ya wanajeshi na kuwa chanzo cha ugomvi kati ya wanajeshi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tueleze tu kwamba mwanajeshi anapokuwa nje ya kazi akifanya makosa anashtakiwa kwa mujibu wa sheria bila kujali kwamba yeze ni mwanajeshi.

Kwa hiyo isichukuliwe kwamba kwa kuwa ni mwanajeshi basi anaweza akavunja sheria anavyotaka hilo halipo na tunaweza kueleza hapa kwamba mara nyingi yaktitea matatizo kama haya hata Jeshi lenyewe linachukua sheria, linachukua taratibu za kinidhamu dhidi yao na bila shaka taarifa zilitolewa basi utaratibu wa kisheria na kikanuni utachukuliwa dhidi ya wanaovunja maadili ya kijeshi wanapokuwa nje ya maeneo ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mbunge alitaka wanajeshi kwamba walipwe mishahara maalum; jibu ni kwamba wanajeshi wote wanapoandikishwa kwa ajili ya ulinzi wa Taifa hulipwa mishahara maaum yaani *specific salary* na Serikali kila mwezi kwa kuzingatia cheo na muda wa kukaa na cheo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mengi nitakuwa nimeyatolea maelezo ya ujumla na yale ambayo sijayatolea maelezo moja moja basi kama kawaida yetu tutayapanga ili Waheshimiwa Wabunge waweze kupata maelezo ya maandishi kwa kila hoja ili waweze kujiridhisha na majibu yetu kwa wale ambao pengine majibu yao maswali yao nitakuwa sijaweza kuyatolea ufanuzi wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii na baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA'A NA MICHEZO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iliamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono, Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA-KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 57 - Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa**

Kif.1001 - *Administration and Human Resources Management...* Sh.17,308,432,190

**MWENYEKITI:** Kama kawaida yetu majina ya mshahara yameshakuja, nitamuita Mheshimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi hii, sikusudii kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameeleza vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri hasa upande wa ajira kwa vijana wetu wanaomaliza JKT amesema kwamba kila mwaka zaidi ya vijana 20,000 wanahitimu mafunzo ya JKT, najua JKT siyo kazi yao wala siyo wajibu wao kuajiri.

Sasa hii ni kwa Serikali na bahati nzuri Waziri wa Ajira yuko pale kwa sababu kama unaweza ukatoa vijana 20,000, lakini wanaopata ajira ni vijana 5,000; hawa vijana 15,000 wamakwenda mtaani na vijana hawa wamefundishwa namna ya kukamata silaha au kutumia silaha.

Sasa ombi langu kwa Serikali Mheshimiwa Waziri wa Ajira na Serikali kwa ujumla hili lione kwa sababu kama ni baada ya miaka mitano, 15,000 mara miaka mitano ina maana kutakuwa na vijana 75,000 wako mtaani hawana kazi na wanajua namna ya kutumia silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelezo lakini sina sababu ya kutoa shilingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika maelezo yangu ni kwamba pamoja na hayo mafunzo ya kijeshi wanapewa stadi za kazi, lengo ni hilo hilo kwamba watakapotoka waweze kujiajiri wao wenyewe au aje ajiriwe na sekta binafsi pamoja na sekta nyingine za Serikali siyo lazima vyombo vya ulinzi na usalam.

Pia nimeeleza vilevile katika maelezo kwamba upo mkakati wa kuwawezesha vijana hawa kupitia lile Baraza la Uwezeshaji la Taifa ili waweze kujiajiri wao wenyewe wanapokuwa katika maeneo yao, hakuna njia nyingine. Kama nilivyosema nilitoa mfano wa nchi ya Israel kwamba watu wote wanapita kwenye Jeshi na lengo ni nini; lengo kwamba watu wote wale wanauwezo wa kusadia nchi yao inapotokea vita. Na sisi vilevile tunawahesabu vijana hawa kwamba ni Jeshi la Akiba. (*Makofii*)

Kwa hiyo wanahitajika na nchi kwa hivo ni lazima tuendelee na programu hizi lakini waelewe tu kwamba wanapoingia Jeshi la Kujenga Taifa siyo maana yake ni ajira maana yake ni kwamba waweze kupata hizo stadi na waweze kujiajiri wao wenyewe na wachache wataajiriwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Almas Maige.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana pia na mimi nichangia kuhusu kukamata mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ni rafiki yangu ndugu yangu lakini suala hili ninalotaka kulisema ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuongelea mashirika ya kimkakati Shirika la Nyumbu na Shirika la Mzinga. Mashirika haya yana umuhimu mkubwa sana katika nchi hii katika

maendeleo na katika nchi nyingine mashirika haya ya majeshi ndio yanayoleta maendeleo katika teknolojia, mashirika haya yote yametelekezwa hayana uwezo mkubwa kifedha, hayana mtaji, yanatumia fungu namba 38 la Ngome kuyaendesha na hela hakuna.

Naomba nielezwe Serikali inasema nini kuhusu kuyawezesha mashirika haya na kama majibu yatakuwa siyo mazuri nakusudia kukamata shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza katika maelezo yangu na ipo katika kitabu changu cha hotuba kwamba mashirika haya yana mpango mkakati na nimeeleza kwamba kila mmoja mpango mkakati wake una bajeti ambao sasa hili unazungumzwa Serikalini kwa madhumuni ya kuwawezesha. Nyumbu ina mpango mkakati wa miaka 10, Mzinga ina mpango mkakati wa miaka mitano. Hakuna shaka kwamba Serikali itakapomaliza mchakato wa kupitisha mipango mikakati hii na bajeti zake, mashirika haya yatafanya kazi nzuri kama inavyokusudiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amejieleza vizuri sana na tutahakikisha kwamba kuna *commitment* ndani yake kwamba mashirika haya baadae yataonekana yanafanyakazi kama ambavyo ilikusudiwa ilipoanzishwa, basi nimsamehe shilingi yake Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera na mkakati wa ulinzi kuwaenzi, kuwatanza mashujaa wetu walioshiriki vita katika

shughuli nzima za amani na Mheshimiwa Waziri utakumbuka kwamba mashujaa wetu walioshiriki vita vya Kagera na kule Msumbiji hali zao za maisha pamoja na kwamba tayari wamestaafu lakini hali zao za maisha ni mbaya na hata pale ambapo wengine waliofariki wajane hali zao za maisha ni mbaya.

Ningependa kupata mkakati za ziada kuina kwamba wastaafu hawa ambao wengine ni walemovu mnawaenzi kwa kiasi gani na wajane ambao waume zao walishiriki vita hivyo mtawatunza kiasi gani na kama sikuridhika sina haja ya shilingi yako, lakini nataka kujua tu mkakati ukoje. Naomba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimjibu Mheshimiwa Masoud kwamba kwanza tuelewe wakati wa vita hivyo vya Kagera wapo wanajeshi kwa maana waliokuwa kwenye ajira ya Jeshi waliokwenda vitani na wako ambao walikwenda wakiwa siyo wanajeshi, wamechukuliwa kutoka kwenye taasisi nyiningine na utaratibu ni ule ule wa *pension*. Mimi taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba baada ya vita vyenyewe kilitolewa kifuta jasho kwa wote na kwa maana hiyo kilichofuata baada ya pale ni taratibu za *pension* kwa mujibu wa mtu taasisi yake alipotokea kwahiylo kwa Wanajeshi ni kwa mujibu wa *pension* za wanajeshi na wale wengine kwa mujibu wa *pension* za kule ambako walikuwa wakifanyiakazi.

Kwa hiyo, siyo rahisi kuwatunza au kuwalipa posho au mishahara wote wale kwa sababu kwanza idadi yao ni kubwa, lakini uwezo huo kwa Serikali haupo.

**MWENYEKITI:** Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa

Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja dogo la mwisho kwamba Serikali kama haina uweo wa kuwatunza kwa sababu idadi hii hamna. Je, Serikali itupe *commitment*

kwamba mna mkakati gani na Waziri sasa wa kuweza kuwatambua kwa sababu wengine ni walemavu na tayari mmewaacha ni hilo tu, sina haja ya shilingi yako, najua fedha zako kaa nazo mwenyewe. *Commitment* ya Serikali namna gani ya kuweza kuwatambua hawa na kujua angalau stahiki zao zitakuwa ni zipo kwa sababu hali zao ni mbaya, wajane wanateseka, watoto wao wanateseka, sina haja ya shilingi yako kaa nayo mwenyewe Ramadhani hii ukafuturu vizuri tu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimueleze Mheshimiwa Masoud kwamba hili suala na sisi tumeliona na kuna wakati tulikwenda kujifunza kwa wenzetu (*war veterans*), kwa mfano, Afrika ya Kusini, kuna nchi kadhaa ambazo zina utaratibu fulani wa kuwatunza hawa wanajeshi wastaaifu wa siku nyingi waliosaidia nchi zao, kwa hiyo nasisi tumeenda kujifunza kwa madhumuni ya kuleta mkakati au sera ya jinsi gani ya kusaidia wanajeshi wastaaifu. Kwa hiyo, hii ikikamilika bila shaka Serikali itakuja na utaratibu maalum. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kama sitaridhika na majibu nitagawana mshahara na Waziri, nitatoa shilingi, najua, najua... (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya nchi iko wazi juu ya ulipaji wa fidia, lakini ni siku za hivi karibuni tumeona kuwepo na malalamiko ya wanajeshi kuvamia maeneo ya raia au wanajeshi kuingia kwenye maeneo ya raia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri ameeleza hapa kwamba katika mwaka wa fedha uliopita wamelipa takribani shilingi billioni tatu lakini kwenye bajeti yao walikuwa na takribani shilingi billioni 20, ni mwaka huu tunaona wanaomba shilingi milioni 100.

Sasa swali langu naijuliza hizi fedha zitaweza kulipa fidia na je, wana mkakati gani mahsus ikuhakikisha kila wanaodai walioingiliwa kwenye maeneo yao wanalipwa kwa sababu mifano iko wazi maeneo ya wananchi yamevamiwa na Jeshi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu Mheshimiwa Anatropia kama ifuatavyo:-

Kwanza nadhani lugha nzuri tuseme yametwaliwa na Jeshi kwa manufaa ya Taifa, siyo yamevamiwa. Tuelewe kwamba Jeshi linapochukua ardhi ni kwa manufaa ya Taifa siyo kwa manufaa ya mtu binafsi, kwa hiyo lugha nzuri ni kwambani kweli kwamba Jeshi limetwaa baadhi ya maeneo kwa ajili ya ulinzi wa Taifa. (*Makofii*)

Sasa nimeeleza katika maelezo yangu na naomba sasa hivi nitoe maelezo ya ziada; ni kwamba mwaka huu tunaomalizia tulitenga shilingi bilioni 20.9, shilingi bilioni tatu zilishalipwa Kilwa, shilingi bilioni 16 ziko katika utaratibu wafanyakaji wa uhakiki kutoka Hazina wameshakwenda katika maeneo ambayo yameshafanyiwa uthamini ili tuweze kulipa na maeneo hayo ni haya yafuatayo:-

- (i) Kilima cha Loserwai (*Tanganyika packers*) shilingi bilioni 2.2;
- (ii) Kiteule cha Kilima cha Illemela (Mwanza) shilingi bilioni 3.8;
- (iii) Kiteule cha Tarime, Nyamisangura na Nyandoto shilingi bilioni 1.5;
- (iv) Kambi ya Makoko (Musoma) shilingi bilioni 1.1;
- (v) Kambi ya Viteule, Kakonko (Kigoma) shilingi bilioni 2.3; na
- (vi) Ras Mshindo kama nilivyosema Wilayani Kilwa shilingi bilioni 3.6

Kwa hivyo, tuliweza kulipa fedha hizi bila shaka kwa sehemu kubwa tutakuwa tumeondoa tatizo hili. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, nakushukuru. Nadhani Kanuni za ulipaji wa fidia ziko wazi lakini pia *interval*/ya lini fidia zinapaswa kulipwa iko wazi.

Sasa swalii langu, zitalipwa ndani ya muda huu wa mwezi mmoja? Kwasababu pia hazijawa *reflected* kwenye vitabu vyake. Mimi nitaomba watu wajadili kwa maana ya tuweze kuwa na uhakika kwamba hizo fedha zitalipwa kwa ajili ya hiyo ardhi iliyotwaliwa kwa manufaa ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyeekiti, nitaomba nitoe hoja.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono kweli? Wachangiaji: Mheshimiwa Sophia, Mheshimiwa Mwambe, Mheshimiwa Matiko, Mheshimiwa Haonga, Mheshimiwa Magereli, Mheshimiwa Upendo, Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Alberto, Mheshimiwa Msigwa bado? Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Kangi, Mheshimiwa Mwigulu, Mheshimiwa Ghasia, Mheshimiwa Waitara, Mheshimiwa Bonnah, Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Mattar, Mheshimiwa Chumi, Almasi, Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Nyongo, na Mheshimiwa Jacqueline. Kule nani kule, Mheshimiwa Mtulia? Na Mheshimiwa Rehani, tunaanza na Mheshimiwa Rehani. Mheshimiwa Rehani.

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti wewe pumzika unaumwa shingo. (*Kicheko*)

**MHE. SALUM MWINYI REHANI:** Mheshimiwa Mwenyeekiti, ahsante.

Mimi nimuombe swahiba wangu Mheshimiwa Anatropia juu ya suala hili la ulipaji wa fidia kwamba aweze kurudisha hiyo shilingi kwa sababu mimi kama Makamu Mwenyekiti wa hii Kamati, *commitment* ya Serikali pamoja na watu wa Wizara ya Fedha ilishatolewa na tulijadili, tukakubaliana na mwongozo ukawa umetoka kuhakikisha kwamba hizi pesa zinakwenda kwa wakati. Sasa labda lilitobaki hapa pengine tu Waziri wa Fedha aseme lini lakini kwa kweli hizi pesa zinamalizika ndani ya kipindi hichi cha awamu hii yaani ya mwaka huu wa fedha kabla ya kuingia mwaka mwagine. Kwa hiyo naona haina haja ya kuweza kushikilia shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninamuunga mkono Mheshimiwa Anatropia kwa sababu tunachotaka hapa, tunataka *commitment* ya Serikali kuzitoa hizo pesa. Ninyi Wabunge wote ni mashahidi mara nyingi tumepitisha pesa kama Bunge lakini hizo pesa haziendi kwenye Wizara husika, kwa hiyo tunapozungumza kwamba pesa ziko kwenye makaratasni kweli lakini Wizara hii itapata hiyo pesa lini? Ni mara nyingi tumetoa pesa, pesa hazifiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia wananchi hawa ni kweli wametoa ardhi yao kwa ajili ya Serikali yetu na wanajeshi wetu wafanyakazi vizuri lakini tukmbuke Wananchi hawa ni maisha walikuwa wanaishi hapo na sasa wanahitaji kuondoka na kwenda kujenga wanakokwenda.

Je, ni lini Seroikali itatoa hizi pesa kuhakikisha hawa wananchi wanapata stahiki yao kwa sababu malalamiko yamekuwa ni mengi na ni kweli mimi niko kwenye Kamati pesa zitatoka lakini lini? Tunaomba Waziri wa Fedha aji-*commit* hapa na kusema lini hizo fedha zinatoka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, namuomba Mheshimiwa Anatropia aendelee kushika shilingi mpaka *commitment* ya Wizara iseme lini pesa inatoka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi migogoro ya ardhi Tanzania hasa zaidi kwenye maeneo yanayomilikiwa na majeshi iko eneo kubwa sana na sisi Wabunge karibu wote hili tatizo lipo kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Jeshi la Magereza kuna baadhi ya maeneo wanamiliki na yenye ni kinyume cha utaratibu, lakini bahati mbaya kabisa hawalipi fidia kwa wakati kama ambavyo iko kwenye Jeshi la Ulinzi kama ambavyo tumeomba. Sisi tunachoiomba Serikali, nia ya kushika shilingi ni kutaka kuonesha msisitizo wa jambo hili, mpeni hela Mheshimiwa Mwinyi hata yeye hatamani hawa watu waendelee kukaa kwenye hayo maeneo na kuyakalia ili waweze kulipa fidia. Mwaka jana aliomba hela, mwaka juzi aliomba hela, mwaka huu tena anaomba hela halafu bado wanasema pesa yenye ni kidogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri hapa amelalamika pesa haifiki kwake kwa wakati, lakini hata yeye anatamani na ardhi hili ni muhimu, Jeshi hili ni mambo ya siri siyo kila mtu anatakiwa akae karibu na maeneo ya Jeshi na majeshi mengi sasa hivi ukija kwa mfano, Masasi sisi tuna Kambi kubwa pale lakini tayari iko katikati kabisa ya Mji. Walipeni hawa watu fidia watoke, wawaache wanajeshi wafanye shughuli zao pale ndani mbalimbali lakini vinginevyo hii itakuja kuleta shida hata kwenye jamii zetu kwa sababu watoto, hata watu, magaidi wanaweza wakaona shughuli mbalimbali za kijeshi kwenye maeneo yao kwa sababu wamezunguka sana haya makambi. Kwa hiyo, tuiombe Serikali na Mheshimiwa Waziri...

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:**...bahati nzuri amesimama hapa apeleke pesa kwa Mheshimiwa Mwinyi amalize hili tatizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe kabisa Mheshimiwa Anatropia, mtani wangu huyu kwamba ni dhamira na nia njema ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi ambao ardhi yao imetwaliwa kwa ajili ya ulinzi wa Taifa hili wanalipwa fidia yao na ndiyo sababu Jeshi hili la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania ni jeshi la wananchi wenyewe, ni jeshi ambalo lina mapenzi na nia njema na wananchi wake na Mheshimiwa Waziri hapa ameeleza nia njema na dhamira na ameonesha namna ambavyo Serikali tumeendelea kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilikuwa kwenye Kamati hii kabla sijateuliwa kuwa Waziri, tulihakikisha tunaisimamia Serikali na hasa lile eneo la Kilwa ambalo leo Mheshimiwa Waziri amesema shillingi billioni tatu zimeshalipwa. Huu ni ushahidi kwamba Serikali inaendelea kuwajali na kuwalipa wananchi wake. Tunaomba Wananchi wawe na subira, Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania liko pamoja nao na kulinda amani yao na usalama wa nchi hii. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwigulu.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Waziri mtoa hoja ameelleza na amefafanua kwa kina, Jeshi la Wananchi na Wizara wameendelea kulipa madai haya ya fidia na kwa kuwa bahati nzuri sana maeneo haya ya Jeshi la Wananchi pamoja na wananchi wanaouzunguka siyo maeneo yenye mgogoro, ni maeneo ambayo tayarimyako kwenye makubaliano, liliokuwa linasubiriwa ni malipo na tayari malipo yameendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe tu ndugu yangu asikie *commitment* ya Waziri, arudishe shilingi na tuwaache wazee wa kazi wakaendelee na kazi tusiendelee kuwachelewesa hapa kwa sababu kwa kweli kazi yao ni kubwa na jambo hili siyo jambo la mgogoro, lingekuwa jambo la mgogoro tungenesema migogoro imalizwe haraka. Haya ni

mambo ambayo yamenyooka kama Waziri alivyosema na fedha zimeendelea kutoka na Bajeti ilikuwepo na fedha zilikuwepo na *commitment* imeshatoka kwamba utaratibu huo utaendelea na Waziri amesema kabisa, ametaja na maeneo kwamba atakapokuwa amekamilisha migogoro yote hiyo wala hata haitasikika.

Kwa hiyo, tumuachie Waziri akamalizie kazi hiyo kwa sababu ametubainishia hata maeneo ambayo migogoro hiyo itakuwa imemalizika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante sana na mimi nimwambie tu Mheshimiwa Anatropia arudishe ile shilingi kwa sababu *commitment* ya Mheshimiwa Waziri inajitosheleza kwa maana pesa zipo, kinachofanyiwa sasa hivi siyo tathmini, ni uhakiki tu wa ile tathmini iliyofanywa ili kuhakikisha kwamba wanaolipwa wanastahili na siyo vinginevyo. Kwa hiyo, hakuna zaidi ya *commitment* kwamba *commitment* ni kumaliza kuhakiki ndipo pesa zilipwe.

Mheshimiwa Mwenyeiiti, ahsante, Anatropia amrudishie Mheshimiwa Waziri pesa yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alberto.

**MHE. ALLY SALEH ALLY:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, ahsante. Wakati anaanza hotuba yake Mheshimiwa waziri hapa alisema amesikitishwa sana na *contribution* ya upande wa Upinzani kuhusiana na hotuba yake, lakini nataka nimhakikishie Wapinzani ni wananchi na ni wazalendo na ndio maana sasa hivi tunasimama kutetea hili jambo limalizike ili Jeshi letu lifanye kazi kwa uzuri na kwa salama. Tuna nia njema kama ambavyo wengine wana nia njema sisi Wapinzani na nchi hii.

Sasa Mheshimiwa Waziri tunachotaka sisi kama alivyosema mtoa hoja tunataka *commitment*. Muda mrefu tunaepuka migogoro isitokezee, watu wakiondoka haraka

ina maana Jeshi lita-settle haraka katika hayo maeneo ili taratibu za kiulinzi ziendelee, tukichelewa ndiyo tunachelewa migogoro ile ambayo umeitaja inatokezea inhabidi mtumie nguvu kuondoa watu.

Sasa mimi nasema katika kiswahili kuna msemo unasema; "kata pua, unga wajih." Tumekata pua mara nyingi kufanya mambo makubwa mengine kwenye *Stiegler's*, kwenye ndege, kwenye *train* na hapa tukate pua, tumalize tatizo hili. Tulimalize *for good*, Serikali *iji-commit* kumaliza tatizo hili *once and for all* ili mwakani tena tusije tena tukaja tena kuomba hapa ikawa bado watu hawajahama, watu wanakatiwa mipapai, watu wasasukumwa sukumwa, hilo lisitokezee. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Anatropia kwamba Serikali itupe *commitment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwangu Tarime nashukuru Waziri ametaja kwamba wanalipa *1.3 billion*. Tangu mwaka 1981 wale wanajeshi wa Nyandoto tulifanya kuwakaribisha baada ya kukatika kwa daraja, mawasiliano yalivyorudi bado waliendelea kuhodhi yale maeneo na kuongeza mengine ambako ni ndani ya mji kabisa.

Sasa Mheshimiwa Waziri nimekuwa nikiongea hili nikiwa Mbunge wa Viti Maalum, nikiwa Mbunge sasa hivi na wewe mwenyewe umekuja mpaka hapa wakakuona na kwingine kote Tanzania, tunataka *commitment* umesema zimetoka shilingi bilioni tatu, bado shilingi bilioni 16 kweli ndani ya mwezi mmoja tulio baki kumaliza mwaka wa fedha utuambie sasa hivi shilingi bilioni 16 zitatoka kwenu na wataenda kulipa hawa wananchi ili tumalizane na hili, kwa sababu tunaona pale ambapo wananchi wanaingia kwenye Kambi ya Wanajeshi wanakuwa-*harrased*, wanakatiwa migomba, wanabomolewa nyumba, sisi tunavumilia miaka 20; Heche ajazaliwa mpaka leo nyumba huwezi ukajenga,

huwezi ukaendelea na chochote kile umekaa tu, nyumba inabomoka huruhusiwi kujenga, sio haki kabisa kwa wananchi wetu. Kwa hiyo, tunataka *commitment* ambayo kweli tuwaambia wananchi kwamba kufikia Julai kutakuwa wameama na wanajeshi wameyachukua yale maeneo, wananchi wamelipwa stahiki yao ili nao waende wakajiendeleze huko kwингine. Ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi letu ni Jeshi la Wananchi na sisi Wabunge tuko hapa kama wawakilishi wa wananchi, tunawasemea wananchi.

Ninaomba Mheshimiwa Waziri asione kwamba hili jambo tunamwambia yeye wala tunaliambia Jeshi, tunaiambia Serikali kwamba hili jambo sasa lifike mwisho na niseme sisi Kambi ya Upinzani na mimi nasema kama Kiongozi wa Kambi anayelibeza Jeshi bila shaka atakuwa amepungukiwa , sisi tunalipenda Jeshi letu na tunapenda Jeshi lisiwe linasemwa hovyo hovyo, sasa haya mambo yanafanya wananchi wanalisema Jeshi hovyo na matokeo yake ile heshima kwa Jeshi inapungua. Kwa hiyo, ili heshima ya Jeshi iendelee kudumishwa haya mambo yanayofanya wananchi walisemeseme hovyo hovyo Jeshi letu lazima Serikali muangalie uwezekano wa kukata pua na kuunga wajihii kama alivyosema Mheshimiwa Ally Saleh, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilitaka nimuomba Mheshimiwa Anatropia aweze kuachia shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati, lakini tumeshapitia maeneo yote ambayo yanatakiwa kulipwa na ameshakutana na wananchi ambao wanadai hayo maeneo, lakini tayari wako kwenye mkakati wa kuwalipa hao wananchi, kama alivyosema Mjumbe mmoja aliopita kwamba

wameshaangalia ni wananchi gani wanatakiwa kulipa na sasa hivi kinachofanyika ni uhakiki, kwa hiyo, tuko kwenye hatua ya uhakiki, kwa hiyo namuomba sana Mheshimiwa Anatropia aweze kumuachia Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili mambo mengine yaweza kuendelea. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niombe kama ni *commitment* kama alivyosema Mheshimiwa Esther Matiko kwamba Mheshimiwa Waziri alifika hadi katika eneo lake, hiyo ni sehemu ya *commitment* kwamba wako *serious* kulipa, lakini pia unaona kabisa katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri wana *information* za kutosha, wanajua wapi nani anadai na ninadaiwa kiasi gani, lakini kwa kumalizia kabisa unaona kabisa kwamba dhamira lko wazi, utashi upo, nia ipo.

Kwa hiyo, mimi naomba kwa Mheshimiwa Anatropia waswahili wanasema subira yavuta kheri, tuwe na subira na kwa *commitment* ambazo Mheshimiwa Waziri amezisema hapa na kwa umakini alio nao mimi ninaamini kabisa, lakini kama vile haitoshi sisi wenyewe kama Bunge kulinda maslahi ya wananchi tulipitisha sheria hapa kwamba uthamini ukifika muda fulani kama haawajalipwa unafanyika upya, kwa hiyo, Serikali haiwezi kuwa tayari kuingia gharama kufanya tena uthamini upya. Kwa hiyo mimi naona wazi *commitment* ipo, rejesha shilingi Mheshimiwa Anatropia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mattar.

**MHE. MATTAR ALI SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nimuombe sana Mheshimiwa Anatropia amrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli Serikali imeshaanza kazi, Serikali hii siku Mheshimiwa Waziri siku, ameelewa, ameshaanza kulipa, dada yangu nikuombe sana mrejeshee Mheshimiwa Waziri shilingi yake kwa uhakika aliokuwa nao Mheshimiwa Mwinyi anaweza kuchapa kazi na madeni yote

ninawahakikisha atalipwa, nikuombe hebu mrejeshee shilingi yake, aende akafanya kazi ili uhakikishe wapiga kura wetu wawewe kulipwa pesa zao kwa uhakika na kwa wakati, ukizua Mheshimiwa Anatropia shilingi ya Mheshimiwa Waziri itakuwa kazi haifanyiki, nikuombe sana ndugu yangu, Mheshimiwa Waziri wetu yule msikivu na mchapa kazi, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuomba sana mdogo wangu Mheshimiwa Anatropia aachie hiyo shilingi, mimi nakwambia mambo ya uhakika kwamba historia ya nyuma ni kweli walikuwa hawalipwi au hela zilikuwa hazipatikani, lakini kuanzia mwaka huu tumeona maeneo makubwa yalikuwa yanadaiwa hela yamelipwa, wananchi wamepokea hela zao na wameondoka kupisha maeneo makubwa, Jeshi hili ni letu, huduma hii tunaitaka sisi wote.

Mheshimiwa Anatropia tafadhali muachie Mheshimiwa shilingi ili Mheshimiwa Waziri afanye kazi yake, ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na mimi niungane na wengine tunalipenda sana Jeshi la Wananchi tunaliheshimu, lakini sisi kama wawakilishi wa wananchi tunayo haki ya kulisifu, kulikosoa pale linapokwenda kinyume.

Mheshimiwa Waziri tunakusaidia wewe, Serikali lazima iwajibike, ili Jeshi letu lisichafuliwe ni lazima Serikali itoe hela *iji-commit* itoe hela wananchi wale ambao wanapata taabu wako kwenye mazingira ya hovyo na kama kweli tunalipenda Jeshi hii ndio kazi ya Bunge tunawawakilisha wananchi wetu, haya mambo ya kusema sijui tunaombwa urudishe shilingi wakati wananchi wanateseka huku, kwa kufanya hivyo tunalipenda Jeshi la Wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili Jeshi lisichafuliwe Serikali itoe hela na ipo Serikali kwa ajili ya kuhakikisha Jeshi linapata hela ili likae na utengamano na wananchi wake, wananchi wajivunie Jeshi lake, sasa tusifike mahali hapa tukaona kama sisi tunavyotetea Jeshi tunakuwa maadui wa Jeshi la Wananchi, maslahi ya wananchi ndio haya ya kuhakikisha Jeshi linapata pesa. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa, legeza hiyo mishipa ya shingo usi....

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niinue shingo, namaliza unanikatisha.

**MWENYEKITI:** Haya maliza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema hiki tunachokifanya wapinzani ndio kulipenda Jeshi, Serikali itoe pesa mko kwa ajioi ya kutoa pesa Jeshi lifanye kazi vizuri, lakini tusiseme tunalipenda Jeshi halafu tunalizibia kupata hela. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante umeelewaka, Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi, mimi niseme tu kwamba wengi wamezungumza na mambo yenye we waliyozungumza yanaelewaka, Mheshimiwa Waziri aliyoeta *commitment* anaelewaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikumbushe jambo moja tu ambalo watu wengine wanasema kila wakati nasikia *commitment*, bajeti tuliyonayo ni *cash budget* maana yake unakusanya ndio unatumia, hasa *sometimes* tunaposema *commitment* mtu anasema *commitment* unaweza ukakusanya fedha zisifike kwenye kiwango. Lakini Mheshimiwa Waziri amesema sio kesi bajeti aliyonayo tayari ana hela ya kufanya hiyo kazi, anachosubiri hapa ni tathimini ifanyeka alipe hala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naona wakati fulani Mheshimiwa Anatropia mrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri pia na wewe unaposhika shilingi ya watu uwe unaangalia sura za kushika shilingi, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana ninaomba niseme kwamba Serikali inawezekana kabisa ndio inayojenga chuki kati ya Jeshi letu na wananchi kwenye maeneo yetu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haonga kaa chini huna mchango. Mheshimiwa Magereli.

**MBUNGE FULANI:** Fitna mkubwa wewe.

**MHE. LUCY S. MAGERELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, Jeshi la Wananchi ni kati ya vyombo muhimu sana kwa ajili ya ustawi na mustakabali wa maisha ya Watanzania na niungane na mtoa hoja kwamba Serikali itoe *commitment* kwamba itatoa fedha za fidia kwa wakati kwa ajili ya kufidia maeneo ambayo wanajeshi wameyatwaa.

Mimi nina changamoto hii katika eneo la Kijaka pale Kimbiji, Kigamboni. Suala hili la miaka zaidi ya 10 mpaka leo wananchi wa eneo lile hawajafidiwa tayari leo nimemsikia Mheshimiwa Waziri anaorodhesha maeneo mengine wakati na eneo hili ya Kijaka Kimbiji bado fidia hajapatkana, kwa hiyo tunapodai ya kwamba fedha zitolewe ili wananchi walipwe, hao wanajeshi tunasafiri nao kwenye daladala, tunaishi nao vijjjini tunataka wakitokea vijjjini tusalimiane, tuhudumiane, tuzikane sio tukiwaona tusijae hasira wapeni fedha wafidie wananchi waachie maeneo yao maisha yao yaendelee, ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Waziri husika amesema vizuri sana kwamba haya maeneo yanatwaliwa kwa manufaa ya Taifa na manufaa hayo ya Taifa nadhani ni vizuri yasiwatese hawa wananchi ambao wanatoka katika hayo maeneo.

Sasa suala lililopo ni kwamba katika maeneo ambayo Serikali imechukua hayo maeneo wameweka ulinzi kiasi kwamba wananchi hawaruhuswi kufanya shughuli yoyote ile ya kimaendeleo pamoja na kwamba wanacheleweshwa miaka hadi miaka kulipwa fidia. Sasa mtu hana maendeleo kwenye eneo lake, lakini bado pia vilevile fidia halipwi ili kuondolewa katika hilo eneo, kwa hiyo maana yake ni kwamba tunawafanya watu wazorote kwenye umaskini waendelee kukaa hapo kwenye maeneo bila shughuli yoyote wanayofanya, hawawezi kujenga nyumba nzuri, hawaweze kulima kiasi hicho, kwa hiyo kimsingi tunatesa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hapa ni kwamba Waziri hapa atatuambia lakini wanaaotoa *commitment* kihalisa ya pesa ni watu wa Wizara ya Fedha, kwa hiyo kwa sababu hapa ndani tuna Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha watuambie kama je, inapofika mwisho wa mwaka huu wa fedha hiyo hela itapatikana ama la, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri atatuambia kwamba mipango imeshafanyika mpaka sasa lakini je, hiyo hela itatoka ama haitatoka ni watu wa fedha kutupa hayo majibu. Kwa hiyo ifike mahala sasa tuheshimu hawa wananchi na tuache ili wasiteseke na tupate hiyo *commitment* kutoka kwa Serikali, ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ninamuomba Mheshimiwa Anatropia Theonest amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi kwa sababu tatu; moja, hata Mheshimiwa Rais mwenyewe ameliona hili na hakupenda migogoro hata Kamati ya Mawaziri wanane aliounda ameelekeza pia kuangalia

migogoro ya majeshi ili wasigombana na wananchi, kwa hiyo wanalitambua.

Lakini la pili, Mheshimiwa Waziri amesema hapa fedha anazo na ametaja ameenda mbali zaidi kutaja angalau kila eneo na kiwango cha fedha ambacho kinatakiwa, hoja hapa ni uhakiki ili watu wote waweze kulipwa, ni kweli kwamba hatupendi migogoro, lakini ameshaonesha njia na fedha zinapatikana ili akalipe fidia. Sasa ili tusimkwamshe, tumrudishie shilingi yake afanye kazi na tuunge mkono ili jambo hili liweze kuisha, nakushukuru sana. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nimwambie dada yangu Mheshimiwa Anatropia kama amefuatilia vizuri Sheria ya Masuala ya Fidia wala hakuna haja ya kulilia *commitment* kwa sababu *commitment* ipo kisheria, mtu akifanyia *evaluation* tumeona sisi hata kwenye madini ndani ya miezi sita aliyefanyiwa *evaluation* na ikawa imehakikiwa na imekubalika anatakiwa alipwe na baada ya miezi sita asipolipwa anatakiwa alipwe na *disturbance allowance* yaani kunakuwa kama ni *interest* ndani ya miaka miwili, baada ya miaka miwili ile *evaluation* inakuwa ime-expiry.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali hatuwezi kukubali hayo yatokee. Mheshimiwa Waziri ameshaonesha *commitment* ya kulipa, tayari kuna watu wameshalipwa na bado yale maeneo mengine ambayo hayajalipwa ameshataja na kiwango cha fedha kimeshajulikana. Nimuombe Mheshimiwa Anatropia wala asililie kuomba *commitment*, ipo kisheria, kwa hiyo naomba tu umrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri aendelee na kazi yake. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimuombe mdogo wangu Mheshimiwa Anatropia amrudishie Mheshimiwa Waziri shilingi yake ili aweze kutekeleza majukumu yake kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameshatoa *commitment* na kwamba Serikali yetu hii ya Awamu ya Tano ni Serikali sikivu, ikiahidi inatekeleza, kwa hiyo, mimi niseme pasipo na mashaka *commitment* iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri itatekelezwa. Kwa hiyo nimuombe tu kwamba amrudishie shilingi ili Mheshimiwa Waziri aende kutekeleza majukumu yake, asiwe na kikwazo. Mheshimiwa Anatropia tafadhalii rudisha shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwijage.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru naelewa *concern* ya *Awonyesiga* Anatropia, vijiji vya Visole, Itoju, Bugasha, Mayondwe eneo lake lilichukuliwa na Jeshi miaka 41 iliyopitaliakini *Awonyesiga* mimi nimeongea na Mheshimiwa Waziri hata *CDF* pale amesimama kabisa kanipigia saluti, akasema anatuma watu kwenda Kaboya wanakwenda kuititia eneo la Kaboya ingawa kwenye orodha haikutajwa wakirudi na sisi tutalipwa, kwa hiyo mrudishie shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtulia.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama waliotangulia wenzangu wengi wamemuomba Mheshimiwa sana dada yangu, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Dar es Salaam Mjini kwa wajanja na anajua umuhimu wa Jeshi letu. Lakini tunakubaliana ya kwamba *commitment* imeshatolea na imetolewa ufanuzi kwa wajumbe waliotangulia ya kwamba pesa tayari zimeshatengwa kwenye bajeti, pesa tayari zimeshafanyiwa..., watu wamefanyiwa uhakiki tayari kabisa tathimini imeshafanyiwa, kwa hiyo kilichobaki hapa dada yangu Mheshimiwa Anatropia rudisha shilingi na ukirudisha shilingi maana yake Mheshimiwa Waziri anaenda kukaa sasa kufanya kazi na bahati nzuri Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yupo na wao wote wamekubaliana na Mheshimiwa Waziri kwa maelezo

ya Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Fedha imemtihibitishia kabla mwaka huu kuisha pesa hizo zitapatikana na watu watalipwa, kwa msingi huo shilingi irejeshwe, dada yangu chonde chonde rejesha shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante niungane na Wabunge wenzangu kumuomba Mheshimiwa Anatropia arudishe hiyo shilingi ili Mheshimiwa Waziri aweze kuendelea na mipango aliyonayo.

Kwanza kabisa kama Serikali tulisikia kilio cha Wabunge hawa kuhusiana na madai ya fidia katika maeneo mengi mbali na haya ya Jeshi na Serikali ilivyokuwa *serious* iliunda ile Kamati ya Mawaziri nane, baadhi ya migogoro iliyoangaliwa ilikuwa ya fidia pia ambayo ni ya majeshi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria yenye we iko wazi, Sheria Namba Saba ya mwaka 2016 ambayo ni Sheria ya Uthamini na Usajili Wathamini ambayo imeweka bayana kwamba sasa hivi mtu hawezi kuchukua eneo kama hana fidia, kwa hiyo lazima kama Wizara ya Ardhi tunafuatilia na katika hili linaloendelea sasa Wizara ya Ardhi inashirikiana na karibu sana na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhakikisha kwamba maeneo yote yaliyokuwa na migogoro ya ardhi hususani fidia yanafanyiwa uthamini ili waweweze kulipwa haki yao, kwa sababu mengine yalifanyiwa zamani na ndio maana sasa hivi uhakiki unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimuombe sana Mheshimiwa Anatropia kwa sababu kwa sasa hivi kipindi hiki pesa zilizotengwa zaidi ya shilingi bilioni 16 zinakwenda kulipa wale ambao tayari wameshaainishwa na tuna imani kwamba migogoro yote ambayo ipo na inadai fidia Serikali imeamua kwamba lazima sasa migogoro yote iishe na

hatutaruhusu tena kuingiza migogoro mingine mipya ya fidia baada ya hii iliyopo.

Kwa hiyo shera itazingatiwa na haya yote yanakwenda kufanyika, rai yangu niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge tumrudishie ili ile mipango iliyopo ikamilike na tuendelee pia kulinda maeneo yetu kwa kusimamia sheria na hawataweza tena kuanzisha migogoro mipya ya fidia. Nimuombe arudishe kwa sababu Serikali *commitment* yake iko wazi na ndio maana tukatii maoni yenu, tukaweka sheria ambayo sasa itakuwa inaangalia muda, miezi sita hujalipa unalipa na *interest*, baada ya miaka miwili hakuna tena uthamini unaanza upya hautahesabu kama ni mali yako na hii haiwezi kutokea tena, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata fursa hii ya kulisemea jambo hili na naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu dhamira njema ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayasema haya kwa sababu dhamira ya kuhakiki ilikuwa ni njema kwa ajili ya wananchi wenyewe, nitolee mfano mmoja Jimboni kwa Mheshimiwa Matiko, Tarime thamani iliyokuwa imeletwa ya ardhi ile ilikuwa ni ndogo sana kulingana na ardhi yenyewe baada ya uhakiki na sasa hivi timu ya uhakiki imepata fedha leo, moja ya eneo wanalokwenda kurudia ni Tarime ili wananchi hawa walipwe fedha yao halali kulingana na ardhi yao. Mheshimiwa Matiko hata haujanisikia, pole. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na niseme lingine ambalo ilikuwa linachelewesa malipo haya ilikuwa ni Mthamini Mkuu alikuwa hajasaini taarifa yake ya uthamini ambayo ameisaini jana na leo imefika Wizara ya Fedha, napenda kuliambia Bunge lako tukufu kwamba ndani ya kesho Ijumaa na Jumatatu maeneo yafuatayo yanakwenda kulipwa, eneo la Ilemela shilingi bilioni 3.5 inakwenda kulipwa kwa sababu

taarifa yake imesainiwa, eneo la Arusha Jiji shilingi bilioni 3.5 fedha yake inakwenda kulipwa taarifa imesainiwa na eneo la Musoma shilingi bilioni 1.1 fedha yake inakwenda kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yaliyobaki kama nilivyo sema ilikuwa taarifa ile haioneshi uhalisia. Mfano mwingine wa Serikali ya Awamu ya Tano kuona kwamba inatenda kwa ajili ya wananchi wake, eneo la Kakonko lilitakiwa ilipwe shilingi bilioni 2.2 lakini taarifa iliyokuja ilikuja alipwe mtu mmoja wakati eneo lile kuna watu wengine. Serikali inayojali wananchi wake tukasema hapana tunarudi na jana tumelipa shilingi milioni 50 kwa Mthamini Mkuu ili aende Kakonko aweze kujiridhisha, wananchi wote wapate haki yao. Hiyo, ndio Serikali inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha sidhani kama ninahitaji kusema zaidi. Nilichoeleza mimi ni kwamba *commitment* ya Serikali ipo ndio hiyo kwa takwimu kwamba hatukusema tu hewani na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha amethibitisha kwamba kinachofanyika sasa hivi ni uhakiki na kule ambako uhakiki umeshafanyika wanaenda kulipwa, sasa *commitment* gani zaidi ya hiyo Mheshimiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mheshimiwa Waziri tunampenda sana na mmeonesha mnavyompenda sana na sisi tunajaribu kumsaidia ili kila siku asiwe anajibu maswali yaleyale ya kulipa fidia kwa sababu, sheria za fidia ziko wazi...

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Anatropia hapa wewe...

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...ninakubali kumpa *benefit of doubt* kwa sababu tutarudi tutaona kama ametekeleza au hajatekeleza. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Na sio *benefit of doubt* na Naibu Waziri wa Fedha ameshatoa *commitment* na hoja hii ipo tayari kwenye Kamati ya Bajeti kwa Kanuni ya 98 toka mwezi wa tatu na ahadi ya Serikali ilikuwa pesa hizi zinalipwa. Kwa hiyo, nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo mengi niliyotaka kuyatoa kwenye hoja hii yametolewa. Nashukuru niachie hali hiyo. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana, na mimi kama sitaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri nitatoa shilingi yangu, mimi sitaiachia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *Standing Orders* za nchi, za utumishi, watumishi wanapohamishwa wanatakiwa walipwe usafiri, walipwe mizigo na *allowance* nyingine karibu kwa siku saba. Kumekuwa na wanajeshi ambao wamehamishwa kutoka Dar es Salaam wameletwa Dodoma, wanajeshi hawa wengine wako Ihumwa, hamjawalipa *allowances* zao, hamjawalipa za mizigo, hizi pesa zote wanajeshi hawajalipwa hawa ambao mnasema mnawapenda sana na mnasema tusiwaguse; ni kweli, hatutakiwi kuwagusa, hawajalipwa pesa zao.

Mheshimiwa Waziri ni lini hawa wanajeshi waliotoka Dar es Salaam watalipwa pesa zao, ili waitumikie nchi yetu bila kuwa na matatizo? Wameacha familia zao kule Dar es Salaam wako hapa, ili wafanye kazi yao ya ulinzi vizuri, watulinde vizuri, tuwe na Taifa kama ambavyo limetengamana, ni lini watalipwa pesa zao? Kama sitapata majibu ya kuirdhisha natoa shilingi. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wafanyakazi wakihamishwa kama ambavyo sasa hivi watu wameletwa huku Makao Makuu wanapaswa na wanastahili kulipwa. Pengine utaratibu wa jeshi ni tofauti kidogo na hii ni *special case* kwa sababu uhamisho jeshini uko mwingi, unaweza ukatolewa kambi moja ukapelekwa kambi nyngine, nao ni uhamisho na mara nyngi unatetegemea na uwepo wa fedha kwa kipindi hicho, lakini mara zote wanaohamishwa bila kulipwa palepale inahesabika kwamba ni deni watakuja kulipwa fedha zinapopatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana hata hivyo niseme tu kwamba hii ya kuhamia Dodoma ni *special case*, lakini uhamisho wa kawaida Jeshini kwa kiwango kikubwa umesimamishwa kwa sababu ya madeni yaliyokuwepo ni mengi na tunatafuta nyenzo za kuweza kuwalipa kadri tunavyowahamisha, ili watu wasiendelee kulimbikiza madeni.

Kwa hiyo, hili la Dodoma upande wa Wizara watu wote wamelipwa, lakini upande wa Jeshi, naomba Mheshimiwa Mbunge unipe nafasi ya kwenda kufanya uhakiki kujithibitishia hali ilivyo, lakini nataka nikuhakikishie kwamba itakuwa *priority* kwa Serikali kuwalipa wote waliohamishiwa Makao Makuu. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu naliheshimu Jeshi na Mheshimiwa Waziri amesema, lakini ninachotaka kusema wanajeshi hawawezi kusema kwa sauti, lakini tunapata malalamiko yao kama wananchi na kama wawakilishi, lakini kwa heshima ya Waziri na kwa sababu naheshimu Jeshi naomba Waziri hilo jambo mlifanyie kazi, ili hawa wanajeshi walipwe pesa zao waweze kutulinda vizuri. Naachia shilingi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Kifungu hiki kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts Unit</i> .....	Sh. 252,712,300
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning Unit</i> .....	Sh. 401,640,000
Kif. 1004 – <i>Internal Audit Unit</i> .....	Sh. 186,034,000
Kif. 1005 – <i>Procurement Management Unit</i> .....	Sh. 66,773,200
Kif. 1006 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Sh. 69,137,200
Kif. 1007 – <i>Government Communication Unit</i> ....	Sh. 96,700,000
Kif. 1009 – <i>Independent Telecommunication Network</i> .....	Sh.149,584,000
Kif. 2001 – <i>Industries Constructions and Agriculture</i> .....	Sh. 323,989,000
Kif. 2002 – <i>Military Research and Development</i> ..	Sh. 223,908,110
Kif. 2003 – <i>Building Consulting Unit</i> .....	Sh. 59,260,000
Kif. 2004 – <i>Estate Management and Development Unit</i> .....	Sh.136,840,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 38 – Defence**

Kif. 1001 – <i>National Defense Headquarter (NDHQ)</i> .....	Sh. 1,397,869,208,475
Kif. 1006 – <i>Defense Forces Headquarter Command</i> .....	Sh. 1,566,906,400
Kif. 1007 – <i>Land Forces Command</i> .....	Sh. 2,394,362,086
Kif. 1008 – <i>Air Defence Command</i> .....	Sh. 2,147,414,744
Kif. 1009 – <i>Navy Command</i> .....	Sh. 1,203,488,495
Kif. 1010 – <i>Military Hospitals</i> .....	Sh. 1,545,527,400

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 39 – National Service**

Kif. 1001 – *The National Service Force*.....Sh. 300,035,425,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **KITABU CHA NNE - MATUMIZI YA MAENDELEO**

#### **Fungu 38 – Defence**

Kif. 1001 – *National Defense*  
Headquarter (NDHQ).....Sh. 6,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

#### **Fungu 39 – National Service**

Kif. 1001 – *The National Service Force*.....Sh. 2,000,000,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

### **Fungu 57 – Ministry of Defence and National Service**

Kif. 1003 – *Policy and Planning Unit*.....Sh. 400,000,000

Kif. 1009 – *Independent Telecommunication Network*.....Sh. 1,000,000,000

Kif. 2001 – *Industries Constructions and Agriculture*.....Sh. 3,500,000,000

Kif. 2002 - *Military Research and Development*.....Sh. 115,000,000,000

Kif. 2003 - *Building Consulting Unit*.....Sh. 0

Kif. 2004 - *Estate Management and Development Unit*.....Sh. 120,000,000,000

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.  
*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa Hoja. *(Makofî)*

## TAARIFA

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 104(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba Kutoa Taarifa kwamba Bunge lako likikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba sasa Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.  
*(Makofî)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Naafiki. *(Makofî)*

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwambe vipi, unaunga mkono hoja, nini? *(Makofî)*

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti).*

**MWENYEKITI:** Aah, nikisimama mimi wewe huwezi kusimama, mimi nikisimama wewe unakaa, kaa chini.

Sasa nitawahoji; kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwanza nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri na imeonekana ile *spirit* ya Wabunge wote kuheshimu mamlaka za Jeshi na mamlaka za Jeshi, Jeshi hili ni kubwa sana katika Afrika, sio Jeshi la mchezo, linatambulika, wanafanya kazi katika mazingira, lakini ni Jeshi ambalo linaheshimika. (*Makofi*)

Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, lakini nichukue nafasi kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa namna alivyojitoa na kutaka kuimarisha vyombo hivi vya ulinzi nchini mwetu. Majeshi yetu sasa hivi yako vizuri na yote sababu kiongozi wetu, Amiri Jeshi Mkuu ameahidi kuyashughulikia na mambo yote haya yanashughulikiwa, kwa hiyo muwe na subira tu. (*Makofi*)

Nampongeza Katibu Mkuu, *CDF, Chief of Staff*, Makamanda wote, wapiganaji wote kwa kazi nzuri ambazo mnafanya. Hongereni sana. (*Makofi*)

Na mwisho kabisa napongeza Klabu ya Simba ambayo imeshinda leo, maana wengine wamekwenda Zaire kutafuta vitu vya kubanabana. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.54 Jioni Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,  
Tarehe 17 Mei, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*